# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI YA MASHIRIKA YA UMMA



## MWAKA WA FEDHA 2021/22

MACHI 2023

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli Dodoma. Simu ya Upepo: "Ukaguzi", Simu: +255(026)2161200, Tarakilishi: +255(026)2117527, Baruapepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

**Kumb.Na.CGA.319/421/01B** **29 Machi 2023**

Mh. Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
Chamwino,
**40400 DODOMA.**

**YAH: RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418, ninayo furaha kuwasilisha kwako ripoti ya mwaka ya ukaguzi wa mashirika na taasisi zingine za umma kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Ninawasilisha,

Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania**

## Mamlaka

Majukumu na wajibu wa kikatiba wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu Na. 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi, Sura ya 418.

## Dira, dhima na kaulimbiu

**01 — Dira yetu**

Kuwa taasisi yenye Kuaminika na ya kisasa katika ukaguzi wa umma inayotoa huduma za ukaguzi za viwango vya juu zinazoimarisha imani kwa umma.

**02 — Dhima yetu**

Kutoa huduma za ukaguzi zenye kiwango cha juu kwa njia za kisasa zenye kuimarisha uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma.

**03 — Kaulimbiu yetu**

Kuwa taasisi yenye kuaminika na ya kisasa katika ukaguzi wa umma.




**Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo**

Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo.

**Kufanya kazi kwa ushirikiano**

Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje.

**Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo**

Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi stahiki.

**Kufanya kazi kwa utaalam**

Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora.

**Kufanya kazi kwa uadilifu**

Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadili na sheria katika utoaji wa huduma za ukaguzi.

**Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi**

Tunahimiza, kuvumbua, na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwa ajili ya kuboresha huduma za ukaguzi



# SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti ya ukaguzi ya mashirika na taasisi zingine za umma kwa mwaka wa fedha 2021/22. Ripoti hii inatoa tathmini huru ya utendaji wa taasisi hizo na kutoa ushauri kwenye maeneo muhimu yanayohitaji uangalizi na uboreshaji katika usimamizi wa utendaji wa mashirika na taasisis zingine za umma.

Ripoti hii inaangazia mapungufu katika mifumo ya udhibiti wa ndani, usimamizi wa fedha na miundo ya uendeshaji wa mashirika na taasisi zingine za Umma. Masuala yaliyoangaziwa yamejumuisha mapungufu katika usimamizi wa manunuzi na mikataba, usimamizi wa mapato na fedha, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa bajeti na pia usimamizi unaohusiana na taratibu za kodi. Ripoti hii vile vile imebainisha mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa mashirika na taasisi zingine za umma hususani katika sekta ya afya, sekta ya utalii, mamlaka za maji, taasisi za elimu ya juu, mafunzo, na utafiti, benki na mifuko ya hifadhi za jamii, pamoja na utendaji wa bodi za mazao na sekta ya uziduaji.

Ili kukabiliana na masuala haya, nimetoa mapendekezo ya maboresho ambayo nashauri uongozi wa taasisi hizo kuyatekeleza. Lengo langu ni kuhakikisha mashirika na taasisi zingine za umma zinazingatia sheria, kanuni, na sera na kupelekea kufikia utendaji wa ufanisi  katika kutoa huduma kwa umma.

Ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Serikali, mashirika ya umma, na wadau wengine waliotuunga mkono wakati wote wa ukaguzi huu. Pia ningependa kutambua kujitolea kwa dhati na bidii ya timu yangu, ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa katika utayarishaji wa ripoti hii.

Kwa kumalizia, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, ripoti hii ni kiungo muhimu cha kukuza uwazi, uwajibikaji na utawala bora ndani ya sekta ya umma.

Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikal**

## YALIYOMO

ORODHA YA MAJEDWALI ........ v
MUHTASARI ........ viii
SURA YA KWANZA ........ 1
UTANGULIZI ........ 1
SURA YA PILI ........ 3
HATI ZA UKAGUZI ........ 3
SURA YA TATU ........ 7
MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA ........ 7
SURA YA NNE ........ 10
UTENDAJI WA KIFEDHA WA MASHIRIKA YA UMMA ........ 10
SURA YA TANO ........ 24
UFANISI WA MASHIRIKA YA UMMA KATIKA KUIMARISHA MAZINGIRA YA KIBIASHARA 24
SURA YA SITA ........ 42
USIMAMIZI WA MAPATO NA FEDHA KATIKA MASHIRIKA YA UMMA ........ 42
SURA YA SABA ........ 52
USIMAMIZI WA MATUMIZI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA ........ 52
SURA YA NANE ........ 64
USIMAMIZI WA BAJETI KATIKA TAASISI ZA UMMA ........ 64
SURA YA TISA ........ 72
USIMAMIZI WA MIKATABA NA UNUNUZI ........ 72
SURA YA KUMI ........ 95
TATHIMINI YA UDHIBITI WA MIFUMO YA NDANI, RASILIMALI WATU NA UTAWALA .. 95
SURA YA KUMI NA MOJA ........ 114
USIMAMIZI WA KODI KATIKA MASHIRIKA NA TAASISI ZINGINE ZA UMMA ........ 114
SURA YA KUMI NA MBILI ........ 132
MWENENDO WA BENKI ZINAZOMILIKIWA NA SERIKALI NA TAASISI ZA KIFEDHA.... 132
SURA YA KUMI NA TATU ........ 144
**MAPITIO** KATIKA SEKTA YA UTALII TANZANIA ........ 144
SURA YA KUMI NA NNE ........ 157
UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI ........ 157
SURA YA KUMI NA TANO ........ 167
TATHMINI YA UTENDAJI WA TAASISI ZA MAFUNZO, UTAFITI NA ELIMU YA JUU ... 167
SURA YA KUMI NA SITA ........ 180
UFANISI WA MAMLAKA ZA UDHIBITI KATIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAO ........ 180
SURA YA KUMI NA SABA ........ 191
UFANISI WA TAASISI ZA UMMA KATIKA SEKTA YA AFYA ........ 191
SURA YA KUMI NA NANE ........ 206
MAZAO NA BODI ZA MAZAO ........ 206
SURA KUMI NA TISA ........ 218
UFANISI KATIKA SEKTA YA MADINI, GESI NA MAFUTA ........ 218
VIAMBATANISHO ........ 244

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 1: Mwenendo wa hati za ukaguzi ..... 5
Jedwali Na. 2: Mwenendo wa hati za ukaguzi kwa asilimia ..... 5
Jedwali Na. 3: Mwenendo wa mahitimisho ya uzingatiaji wa sheria ya ununuzi ya umma .. 6
Jedwali Na. 4: Muhtasari wa aina za Hitimisho ya uzingatiaji wa sheria ya bajeti ..... 6
Jedwali Na. 5: Utekelezaji wa Mapendekezo ya Miaka Iliyopita ..... 8
Jedwali Na. 6: Taasisi zilizopata hasara au nakisi kwa miaka miwili ..... 11
Jedwali Na. 7: Orodha ya mashirika yaliyopata faida 2020/21 yakapata hasara 2021/22 ... 12
Jedwali Na. 8: Taasisi zenye mitaji hasi ..... 15
Jedwali Na. 9: Taasisi zenye uwiano wa ukwasi chini ya moja ..... 17
Jedwali Na. 10: Taasisi za umma zenye madeni zaidi ya mtaji ..... 20
Jedwali Na. 11: Orodha ya mashirika yaliyokusanya mapato nje ya mfumo ..... 44
Jedwali Na. 12: Akaunti zilizositishwa zinazosimamiwa na Taasisi za Umma. ..... 47
Jedwali Na. 13: Mashirika yenye matumizi yasiyokuwa na tija ..... 53
Jedwali Na. 14: Mashirika ya umma yenye matumizi yasiyostahili ..... 54
Jedwali Na. 15: Mashirika yenye masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu ..... 58
Jedwali Na. 16: Mashirika ya umma yaliyochelewesha michango ya kisheria ..... 59
Jedwali Na. 17: Kiasi cha ruzuku ambacho hakikutolewa na serikali kwa mashirika ..... 65
Jedwali Na. 18: Mashirika yenye mapungufu katika matumizi ya mfumo wa bajeti ..... 68
Jedwali Na. 19: Utekelezaji usioridhisha katika majukumu ya kamati za bajeti ..... 69
Jedwali Na. 20: Mashirika yaliofanya matumizi zaidi ya kiwango cha bajeti idhinishwa .... 71
Jedwali Na. 21: Orodha ya taasisi zilizochelewa kukamilisha miradi ..... 73
Jedwali Na. 22: Taasisi zilizochelewa kupokea bidhaa ..... 74
Jedwali Na. 23: Orodha ya magari yaliyonunuliwa lakini hayajapokelewa ..... 76
Jedwali Na. 24: Mikataba iliyosainiwa kabla ya kuhakikiwa ..... 79
Jedwali Na. 25: Taasisi zenye mapungufu katika malipo ya utangulizi ..... 80
Jedwali Na. 26: Mashirika yenye Mapungufu Katika dhamana za utendaji ..... 82
Jedwali Na. 27: Ununuzi ambao gharama za mkataba imezidi bajeti ilipitishwa ..... 88
Jedwali Na. 28: Orodha ya taasisi zilizochelewa kufanya malipo ..... 89
Jedwali Na. 29: Taasisi zilizofanya manunuzi nje ya mfumo wa TANePS ..... 90
Jedwali Na. 30: Mashirika ya umma bila bodi za wakurugenzi ..... 96
Jedwali Na. 31: Mashirika ya umma yenye Matumizi yasiyoridhisha ya mpango mkakati.... 99
Jedwali Na. 32: Mashirika ambayo hayajafanya menejiment ya vihatarishi ipasavyo...... 100
Jedwali Na. 33: Mashirika ambayo hayana nyaraka za miongozo ya kuendesha kazi zake 102
Jedwali Na. 34: Maofisa wanaokaimu katika nafasi zao zaidi ya miezi sita ..... 105
Jedwali Na. 35: Taasisi zenye upungufu wa watumishi ..... 107
Jedwali Na. 36: Orodha ya taasisi ambazo hazitumii GAMIS ..... 112
Jedwali Na. 37: Riba na adhabu zilizotozwa kwenye Mashirika ya Umma ..... 115
Jedwali Na. 38: Kodi mbalimbali ambazo hazikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kati ya siku 56 hadi miaka tisa ..... 116
Jedwali Na. 39: Ucheleweshaji wa kuwasilisha kodi Mamlaka ya Mapato ..... 118
Jedwali Na. 40: Migogoro ya kodi kati mashirika ya umma na TRA ..... 119
Jedwali Na. 41: Malipo kwa waajiriwa na watoa huduma ambayo hayakutozwa kodi ..... 121
Jedwali Na. 42: Kutofautiana kwa mapato kati ya taarifa za fedha na mrejesho wa kodi 123
Jedwali Na. 43: Kuchelewa na kutokujaza marejesho ya kodi ..... 129
Jedwali Na. 44: Malipo yasiyoambatanishwa na risiti za kodi za kielektroniki ..... 130
Jedwali Na. 45: Taarifa za rejesho kutokana na uwekezaji ..... 142
Jedwali Na. 46: Maeneo ya uwekezaji yanayofanya kazi kwa muda mlefu kwa mfululizo 151
Jedwali Na. 47: Mwenendo wa upotevu wa maji ..... 160
Jedwali Na. 48: Upungufu wa uzalishaji maji katika miji ..... 163
Jedwali Na. 49: Madai ya Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira ..... 165

Jedwali Na. 50: Malengo ya udahili dhidi ya idadi ya wanafunzi waliodahiliwa ............ 174
Jedwali Na. 51: Utendaji usioridhisha Kiwanda cha Uchapaji Chuo Kikuu cha Dar es Salaam... 176
Jedwali Na. 52: Madai yaliyokataliwa na Mfuko wa Bima wa Afya............................ 193
Jedwali Na. 53: Uwezo wa viwanda vya Bodi ukilinganisha na uzalishaji halisi............. 208
Jedwali Na. 54: Uwezo wa maghala kuhifadhi dhidi ya kiwango halisi cha kuhifadhi...... 208
Jedwali Na. 55: Mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya biashara kwa tani .................. 211
Jedwali Na. 56: Uwezo wa ukusanyaji wa pato la ndani dhidi ya uwezo wa kulipa gharama za uendeshaji........................................................................... 212
Jedwali Na. 57: Mwenendo wa mabadiliko ya bei za mazao ya chakula (bei ya jumla) ... 214
Jedwali Na. 58: Mwenendo wa hali ya upatikanaji wa mbolea nchini ....................... 215
Jedwali Na. 59: Malengo ambayo hayakutekelezwa ............................................ 219
Jedwali Na. 60: Ankara za gesi ambazo muda wake unaenda zaidi ya ukomo wa mkataba221
Jedwali Na. 61: Mwenendo wa mapato na uzalishaji ........................................... 223
Jedwali Na. 62: Shughuli Zilizochelewa kwenye mradi wa Buhemba......................... 225
Jedwali Na. 63: Bei za gesi zinazotozwa na TPDC na kampuni ya PAET ..................... 235

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. I: Hati za ukaguzi na mahitimisho ya uzingatiaji wa Sheria ya ununuzi na Kanuni zake na Sheria ya bajeti na Kanuni zake kwa mwaka wa fedha 2021/22 ........... 244
Kiambatisho Na. II: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa Miaka Iliyopita 251
Kiambatisho Na. III: Ulipaji wa gawio kwa mashirika na taasisi zingine za Umma.......... 296
Kiambatisho Na. IV: Asilimia 15 ya Mcahngo katika Mfuko Mkuu wa Serikali (Sh. milioni) 297
Kiambatisho Na. V: Mashirika ambayo hayaja changia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali... 299
Kiambatisho Na. VI: Taasisi zenye madeni yasiyolipwa......................................... 301
Kiambatisho Na. VII: Taasisi zenye madeni makubwa hadi tarehe 30 Juni 2022............ 303
Kiambatisho Na. VIII: Makusanyo pungufu yatokanayo na vyanzo vya ndani ................ 306
Kiambatisho Na. IX: Taasisi zilizokutana na changamoto katika matumizi ya MUSE ....... 308

## MUHTASARI

Ripoti hii ina sura 19 zinazotokana na ukaguzi wa mashirika ya umma na taasisi zingine za umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2022. Maeneo yafuatayo yamejadiliwa kwa kina katika ripoti hii:

### Hati za ukaguzi

Nimekamilisha ukaguzi wa hesabu kwa mashirika ya umma 206 na kutoa hati za ukaguzi 203. Kati ya hati za maoni 203 nilizotoa, 196 ni hati zinazoridhisha, tano ni hati zenye shaka na nilishidwa kutoa maoni kwa mashirika mawili na hakuna hati mbaya iliyotolewa. Nimeshindwa kutoa taarifa za ukaguzi kwa mashirika matatu ambayo yemefanya shughuli zake bila Bodi ya Wakurugenzi kwa zaidi ya miezi 12 hivyo taarifa zake za fedha na ukaguzi hazikuweza kusainiwa.

Pia, nilifanya ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria ya ununuzi ya umma na kanuni zake; na sheria ya bajeti na kanuni zake kwa mashirika ya umma 203 na kuhitimisha kuwa mashirika ya umma 128 yalikidhi uzingatiaji sheria ya ununuzi ya umma na kanuni zake na 75 yalikidhi japo yalibainika kuwa na mapungufu kadhaa, kwa upande wa sheria ya bajeti na kanuni zake, mashirika ya umma 151 yalikidhi uzingatiaji wa sheria ya bajeti na kanuni zake; na 52 yalikidhi japo yalibainika kuwa na mapungufu kadhaa.

### Utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita

Katika ripoti yangu ya mwaka wa fedha 2020/21, nilitoa mapendekezo 126 ya ukaguzi. Mapendekezo 53 (asilimia 42) yalitekelezwa kikamilifu; mapendekezo 63 (asilimia 50) yapo kwenye hatua za utekelezaji; mapendekezo tisa (asilimia 7) hayakutekelezwa na mapendekezo moja (asilimia 1) yamepitwa na wakati

Pia nilipitia utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi za miaka ya nyuma 2020/21 kwa kila shirika la umma na taasisi zingine za umma na kubaini kuwa kati ya mapendekezo 6146,mapendekezo 2195 (asilimia 36) yalitekelezwa kikamilifu; mapendekezo 1064 (asilimia 17) hayakutekelezwa. Mapendekezo 2611(asilimia 42) yapo kwenye

hatua mbalimbali ya utekelezaji wakati mapendekezo 276 (asilimia 4) yamepitwa na wakati.

Vile vile, nilifuatilia utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa mashirika ya umma katika mwaka wa fedha 2021/22 na nilibaini, kati ya maelekezo 163, maelekezo 70 (asilimia 43) yalitekelezwa; maelekezo 92 (asilimia 56) yapo kwenye hatua ya utekelezaji na elekezo moja (asilimia 1) halikutekelezwa.

### Utendaji wa kifedha wa mashirika na taasisi zingine za umma

Nimekagua udhibiti wa kifedha wa mashirika ya umma na taasisi nyingine 206 na kubaini kuwa, mashirika 45 yamepata hasara kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo wakati mashirika 16 yaliyopata faida kwa mwaka wa fedha 2020/21 ila yamepata hasara kwa mwaka wa fedha 2021/22. Mapungufu au hasara hizo zilichangiwa zaidi na utendaji usioridhisha, ukosefu wa vyanzo mbadala vya mapato na hivyo kutegemea kwa kiwango kikubwa cha fedha kutoka Serikali kuu; na pia udhaifu katika usimamizi wa matumizi na mapato.

Vilevile, nilibaini kuwa mashirika 24 yalikuwa na kiasi kikubwa cha mikopo kuliko mitaji, wakati mashirika 10 yalikuwa na mitaji hasi, na mashirika 45 yaliyokuwa na kiasi kikubwa cha madeni ya muda mfupi kuliko mali zao za muda mfupi. Kutokana na changamoto za kifedha zinazoyakumba mashirika ya umma na taasisi zingine zinahitaji msaada wa Serikali ili kuweza kutimiza dhumuni la uanzishwaji wake.

Aidha, nilibaini mashirika 18 hayajalipa gawio serikalini na mashirika mengine 58 hayakuweza kuchangia katika mfuko mkuu wa Serikali kama inavyotakiwa na kifungu cha 12(3) cha Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2020).

### Ufanisi wa mashirika ya umma katika kuimarisha mazingira ya biashara

Ukaguzi wangu ulibaini maeneo yanayohitaji uboreshaji katika taasisi za umma za mkakati na miradi ya kimkakati yenye jukumu la kujenga mazingira mazuri ya biashara. Nilibaini Kampuni ya Ndege Tanzania iliingia gharama zisizobadilika za shilingi bilioni 5.27 na

kupata hasara ya mapato yanayotarajiwa ya shilingi bilion 20.35 kutokana na ndege kutofanyakazi, Shirika la Reli Tanzania nilibaini jumla ya ajali 795 ambazo zilizosababisha kuahirishwa kwa safari za treni. Shirika la Umeme Tanzania nilibaini kuchelewa kwa Kampuni ya IPTL kutimiza wajibu wa mkataba kufuatia uamuzi wa mahakama wa Serikali kulipwa dola za Marekani milioni 148.4.

## Usimamizi wa mapato na fedha katika taasisi za umma

Ukaguzi wangu wa usimamizi wa mapato na fedha ulibaini masuala kadhaa yanayohitaji kushughulikiwa katika taasisi mbalimbali, mapato mengine yaliyopatikana nje ya mifumo ya malipo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania yenye thamani ya shilingi bilioni 13.5, huduma za uchimbaji zilizofanywa na Shirika la Madini la Taifa hazikuwa na uthibitisho wa kazi iliyofanyika zenye thamani ya shilingi bilioni 13.30, ukusanyaji wa mapato nje ya mfumo wa malipo ya kielektroniki wa Serikali yenye thamani ya shilingi bilioni 3.32, kutokufanyika kwa mapitio na idhini ya malipo ya kodi kwa wapangaji katika Shirika la Nyumba,Shirika la Reli na Shirika la Mawasiliano Tanzania, Akaunti za benki zilizositishwa zenye kiasi cha shilingi bilioni 20.65, Uwepo wa watumishi waliohamishwa kwenye taasisi zingine lakini waliendelea kuwa waidhinishaji wa akaunti za benki ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na madeni yasiyothibitishwa na yasiyoweza kurejeshwa shilingi bilioni 7.51 katika Shirika la Mawasiliano Tanzania.

## Usimamizi wa matumizi katika mashirika ya umma

Ukaguzi wangu kuhusu usimamizi wa matumizi katika mashirika ya umma kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022 ulibaini kuwa taasisi 12 ziliingia gharama zisizokuwa na tija za jumla ya shilingi bilioni 63.77 zilizotokana na riba na adhabu kwa kucheleweshwa kwa malipo ya wadai mbalimbali, taasisi 21 zilifanya matumizi yasiyo sahihi ya shilingi bilioni 77.75 ambayo yalifanywa ama pasipo kuzingatia kanuni za matumizi, kutokuwa na vielelezo vya kutosha kubainisha usahihi wa matumizi hayo, au kulipwa kwa wadai na wafanyakazi wasiostahili. Katika Hifadhi za Taifa Tanzania nilibaini jumla ya malipo ya shilingi bilioni 1.95 ambayo hayakuwa na viambatanisho, na pia malipo ya posho ya wafanyakazi ya shilingi milioni 38.72 yaliyolipwa zaidi ya viwango vilivyoidhinishwa.

Aidha, nilibaini matumizi ya kiasi cha shilingi bilioni 195.99 yaliyofanyika kutoka mfuko wa miundombinu ya reli kinyume na matumizi ya mfuko huo yalioainishwa katika kifungu cha 68 (9) cha Sheria ya Reli, Sura 170.

Pia, nilibaini mashirika ya umma 99 yenye madeni ya muda mrefu shilingi trilioni 7.65, mashirika 31 yenye masurufu ambayo hayajarejeshwa shilingi bilioni 3.51, na taasisi 11 zilichelewesha kutuma michango yao ya kisheria kwa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya jumla ya shilingi bilioni 131.80 kwa kipindi cha kuanzia mwezi mmoja hadi zaidi ya mwaka.

### Usimamizi wa bajeti katika mashirika ya umma

Nilibaini kuwa Serikali haikutoa shilingi bilioni 161.88 za ruzuku kwa mashirika 18. Mashirika 50 hayakuweza kukusanya jumla ya mapato ya shilingi bilioni 174.63 zilizopangwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani. Mashirika 13 yalikuwa na changamoto ya ufanisi katika kutumia mfumo wa bajeti wa PlanRep katika kuandaa bajeti; Pia nilibaini Mashirika saba yalitumia bila idhini jumla ya shilingi bilioni 118.04 zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa.

### Usimamizi wa mikataba na ununuzi

Katika mapitio ya usimamizi wa mikataba na ununuzi kwa mashirika ya umma na taasisi zingine, nilibaini taasisi saba ziliingia mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 45.71 na dola za Marekani milioni 7.75 bila kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Afisa sheria wa shirika husika. Katika Shirika la Magazeti Tanzania nilibaini ununuzi wenye thamani ya shilingi bilioni 7.49 na dola za Marekani 48,480 yaliyotolewa kwa wauzaji bidhaa na watoa huduma bila kufuata taratibu zozote za ununuzi. Pia, katika Bohari Kuu ya Dawa nilibaini mipango iliyo kinyume na taratibu za ununuzi katika utekelezaji wa mkataba na kusababisha hasara ya dola za Marekani 821,958.36 (sawa na shilingi bilioni 1.89). Aidha Bohari Kuu ya Dawa na Hospitali ya Mloganzila walifanya jumla malipo ya shilingi bilioni 61.99 kwa watoa huduma pasipo kuwa na mkataba wa makubaliano unaoelekeza ulipaji wa malipo hayo.

### Tathimini ya udhibiti wa mifumo ya ndani, rasilimali watu na utawala

Nilibaini Mashirika ya umma 13 hayakuwa na Bodi za wakurugenzi; Mashirika 42 yalikuwa na changamoto katika utumiaji wa mfumo wa MUSE; Mashirika 15 hayakutumia mipango mikakati yao ipasavyo; Mashirika 14 yana watumishi wanaokaimu nafasi zao kwa muda wa kati miezi sita mpaka miaka saba na mashirika 12 yalikuwa na jumla ya upungufu wa watumishi 4,547. Mfuko wa taifa wa bima ya afya ulitoa mikopo ya shilingi bilioni 41.42 kwa wafanyakazi bila ya kutumia mfuko unaojulikana kama Revolving fund.

### Usimamizi wa kodi katika mashirika ya umma

Nilibaini migogoro ya kodi katika mashirika matano ya umma kiasi cha shilingi bilioni 126.95 iliyopo katika bodi na mahakama za usuluhishi, riba na adhabu zilizotozwa kwenye mashirika na taasisi zingine za umma sita kutokana na kutofuata sheria za kodi shilingi bilioni 123.32, kodi mbalimbali ambazo hazijawasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kiasi cha shilingi bilioni 46.83, kodi zilizochelewa kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kiasi cha shilingi bilioni 5.09, kodi ya mapato na kodi ya zuio ambazo hazikukatwa kwenye malipo kiasi cha shilingi bilioni 4.12 na malipo yaliyofanyika bila risiti za kielektroniki kiasi cha shilingi milioni 556.83.

### Mwenendo wa benki zinazomilikiwa na serikali na taasisi zingine za kifedha

Mwaka 2022 Benki ya Maendeleo ya TIB iliendelea kupata hasara kabla ya kodi ya shilingi bilioni 131.07, wakati huohuo faida ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilipungua kwa shilingi milioni 390 ambapo uwiano wa mikopo chechefu ya Benki ya Maendeleo ya TIB, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na Benki ya Azania ilikuwa kati ya asilimia 5.86 hadi asilimia 20.32. Pia, benki hizo zote zilikuwa na jumla ya mikopo chechefu ya shilingi bilioni 278.93 ikilinganishwa na shilingi bilioni 430.61 za mwaka 2021 na kupelekea mikopo ambayo iliainishwa aidha kuwa chini ya kiwango, mashaka au hasara ipatayo shilingi bilioni 357.80 iliyotolewa kwenye vitabu vya fedha. Kwa upande mwingine mwaka 2021 Benki ya Biashara ya Tanzania

ilikuwa na uwiano wa mikopo chechefu ya asilimia 9.87, kinyume na kiwango kinachokubalika na Benki Kuu ambacho ni asilimia 5, huku benki hiyo ikiwa na mikopo chechefu ya shilingi bilioni 70.06.

Pia nilibaini kuwa Serikali inaendelea kudaiwa na mifuko ya hifadhi za jamii mikopo iliyoiva ipatayo shilingi trilioni 1.49. Vilevile, mifuko ya hifadhi ya jamii inakabiliwa na changamoto za urejeshwaji wa mikopo ambapo mwaka 2021/22 vikundi vya ushirika vya akiba na mikopo havikurejesha shilingi bilioni 27.30.

Halikadhalika, nilibaini kuwa mapato ya uwekezaji umeshuka kwa shilingi bilioni 2.07 sawa na asilimia 45 kwa kipindi cha miaka mitano kutoka 2018 hadi 2021. Pia nilibaini utendaji na usimamizi usioridhisha wa kampuni tanzu tatu zinazosimamiwa na mifuko ya hifadhi za jamii.

## Mapitio ya sekta ya utalii Tanzania

Mradi unaotekelezwa wa kuwabadilishia makazi jamii za watu wanaoishi ndani ya eneo la hifadhi ya Ngorongoro kwenda nje ya eneo hilo unakabiliwa na changamoto ambazo zinaweza kukwamisha kukamilika kwa mradi huo; Mwaka 2021/22 kulikuwa na uhaba mkubwa wa maji uliozikabili mbuga za wanyama na kusababisha vifo vya wanyamapori wapatao 135 katika eneo la hifadhi ya Ngorongoro, na kupelekea wengine kuvamia maeneo ya makazi ya watu kutafuta maji na malisho hali iliyoongeza migogoro ya wanyamapori na binadamu.

Pia kutoanza kazi kwa kituo cha kidijitali cha kutangaza utalii ni mojawapo ya changamoto zinazokwamisha ufanisi wa Bodi ya Utalii kutangaza utalii ili kukuza sekta hiyo, na kukatika mara kwa mara kwa huduma za mtandao wa intaneti katika maeneo ya vivutio vya utalii kunazorotesha juhudi za kutoa huduma bora kwa watalii katika Mamlaka za Hifadhi za Taifa.

## Utendaji wa mamlaka za maji

Katika mapitio ya utendaji wa Mamlaka za Maji nilibaini upungufu wa maji kati ya asilimia 10 hadi 80 ya mahitaji ya maji katika mamlaka za maji 25. Mamlaka za maji 23 zilipata hasara ya shilingi bilioni 162.14 kutokana na upotevu wa maji katika mwaka 2021/22.

Pia, nilibaini kiwango kisichoridhisha cha ukusanyaji wa madeni katika Mamlaka za Maji 28, ambapo jumla ya madeni yasiyolipwa hadi tarehe 30 Juni 2022 yalikuwa shilingi bilioni 127.07 (2021: Shilingi bilioni 129.59). Aidha kulikuwa na upungufu katika utekelezaji wa miradi ya maji katika Mamlaka za Maji mbalimbali yenye thamani ya shilingi bilioni 56.27.

### Tathmini ya utendaji wa taasisi za elimu ya juu, mafunzo na utafiti

Mapitio yangu ya Taasisi za Elimu ya Juu, Mafunzo na Utafiti, nilibaini kuwa walimu wa ufundi stadi waliteuliwa kwa muda kama wasimamizi na wahandisi wa kusimamia miradi ya ujenzi ambayo ilikuwa inatekelezwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi bila ya kuwa na mbadala wa walimu wa kufanya kazi zao za kufundisha kwa kipindi cha hadi miezi 33. Pia, vituo 12 vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi vilisajili wanafunzi na kuanza mafunzo bila kusajiliwa kwa vituo. Katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, nilibaini mapungufu katika utoaji mikopo kwa programu za kipaumbele, ambapo asilimia 21 tu ya mikopo ilitolewa kwa programu maalumu badala ya asilimia 51 ya mikopo yote. Pia, nilibaini usimamizi usioridhisha wa utafiti na ushauri na utendaji duni wa kampuni tanzu na vituo vingine vilivyofanywa na taasisi hizo.

### Ufanisi wa mamlaka za udhibiti katika kutekeleza majukumu yao

Katika ukaguzi na mapitio ya ufanisi wa mamlaka za udhibiti nilibaini mapungufu kadhaa kama vile: mapungufu kwenye mifumo inayotumiwa na mamlaka tisa za udhibiti katika kutoa huduma kutochukua hatua madhubuti za udhibiti dhidi ya wadau wanaokiuka sheria, kanuni na miongozo; mapungufu katika taratibu na hatua zinazochukuliwa kushughulikia malalamiko; kutofanya ukaguzi kwa uthabiti na udhaifu katika utoaji wa leseni, usajili na taratibu za uthibitisho na uhakiki zilizotumiwa na Mamlaka za Udhibiti.

### Ufanisi wa taasisi za umma katika sekta ya afya

Ukaguzi wangu ulibaini Mfuko wa Bima ya Afya ulikataa madai ya kiasi cha shilingi bilioni 8.84 kati ya madai yote ya shilingi bilioni 92.44 yaliyotozwa na hospitali za umma. Aidha, Mfuko wa Bima ya

Afya ulirekodi nakisi kabla ya kodi inayofikia shilingi bilioni 189.65 (2021: shilingi bilioni 93.68). Bohari Kuu ya Dawa ilitoza bei kubwa zaidi kiasi cha shilingi bilioni 1.01 kwa vituo vya afya tofauti na bei zilizoidhinishwa, pia kulikuwa na ongezeko la bidhaa zilizopokelewa zikiwa zimebakiza chini ya 80% ya muda wa kuisha au miaka miwili kabla ya muda kuisha Katika Bohari Kuu ya Dawa shilingi bilioni 295.76; na utoaji wa huduma za mikopo bila mkataba halali katika Hospitali ya Taifa Muhimbili shilingi bilioni 16.73.

### Mazao na bodi za mazao

Wakati wa ukaguzi wa bodi za mazo nilibaini mapungufu kadhaa kama vile; Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kujiendesha chini ya uwezo wa viwanda vyake vya kuzalisha na chini ya uwezo wa maghala yake kuhifadhi; uwezo mdogo wa kuzalisha mbolea nchini ambapo wastani wa asilimia saba tu ya mbolewa inazalishwa nchini; kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya biashara; Bodi za mazao ya biashara kutokuwa na uwezo wa kuendesha shughuli kutoka kwenye mapato ya ndani yanayotokana na shughuli mama. Kwa mfano; uwezo wa Bodi ya Pamba, Bodi ya Pareto, na Bodi ya Mkonge kujiendesha kwa fedha za mapato ya ndani yanayotokana na kazi zao mama ni chini ya asilimia 5.

### Utendaji katika sekta ya uziduaji

Tathmini yangu ya ufanisi wa sekta ya uziduaji, nilibaini maeneo kadhaa ambayo yanahitaji kuzingatiwa ili kuboresha utendaji kwa ajili ya kuleta manufaa kwa umma na kukuza uchumi. Kuchelewa kutekeleza mradi wa umeme wa makaa ya mawe ya Kiwira Megawati 200; Kuchelewa kulipia gesi ambayo haikutumika kwa wakati ambayo muda wa matumizi yake unazidi ukomo wa mkataba inayohusisha shilingi bilioni 30.41; Migogoro ya muda mrefu kuhusu gharama zilizotumiwa na makampuni ya gesi kiasi cha dola za Marekani milioni 386.34 ; Bei kubwa ya gesi inayotozwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kwa kwa Shirika la Umeme Tanzania; Kutoanzishwa kwa mfumo na mikakati ya matumizi ya rasilimali za ndani katika kukuza technolojia kwenye sekta ya mafuta na gesi ; Kutekelezwa Mradi wa ujenzi wa mtambo wa CNG bila kuwepo makubaliano kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Wakala wa mabasi yaendayo haraka.




# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Muktadha

Ripoti hii inatoa matokeo na mapendekezo yaliyobainishwa wakati wa ukaguzi wa mashirika ya umma na taasisi zingine kwa mwaka wa fedha ulioishia mwaka wa fedha 2021/22.

Ripoti hii inajumuisha masuala mbalimbali, ikiwa ni pamoja na maoni ya ukaguzi, utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita, uzingatiaji wa sheria ya ununuzi, usimamizi wa mapato na fedha taslimu, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa bajeti, pamoja na uzingatiaji wa sheria na miongozo ya kodi. Zaidi ya hayo, ripoti hii inabainisha haja ya taasisi za udhibiti kuboresha shughuli zao na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Pia Ripoti hii inaangazia maeneo kadhaa ya mapungufu, ikiwa ni pamoja na kutokuwepo kwa utenganisho wa kutosha kati ya majukumu ya usimamizi na uangalizi, kucheleweshwa kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, na uwekezaji katika miradi isiyo na tija na kusababisha upotevu wa fedha za umma. Aidha, ripoti hii inatoa ufahamu muhimu kuhusu utendaji wa kifedha na uendeshaji wa mashirika ya umma na taasisi zingine na itatumika kama chanzo muhimu kwa wadau wanaopenda kuboresha uwajibikaji na uwazi.

## 1.1 Malengo ya ukaguzi

Ukaguzi ulilenga kutoa maoni huru iwapo taarifa za fedha ziliandaliwa kwa mujibu wa mfumo wa taarifa za fedha unaokubalika, kwa kuzingatia mambo yote muhimu. Aidha, ulilenga kutathmini mashirika ya umma na taasisi zingine zinafuata sheria na

kanuni za ununuzi, pamoja na sheria,kanuni na mwongozo wa bajeti. Ukaguzi pia ulilenga kutathmini ufanisi wa mashirika ya umma katika kusimamia fedha na kutoa huduma kwa umma.

## 1.2 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi ulijumuisha mapitio ya taarifa za fedha na ukaguzi wa kufuata sheria na kanuni kwa mashirika ya umma ya taasisi zingine 206, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa mapato, usimamizi wa matumizi, usimamizi wa ununuzi na mikataba, usimamizi wa mishahara na rasilimali watu, utendaji wa kazi katika sekta ya elimu, na afya, na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Ukaguzi pia ulijumuisha tathmini usimamizi wa hatari, udhibiti wa ndani, na mifumo ya utawala ya mashirika ya umma na taasisi zingine.

## 1.3 Methodolojia ya ukaguzi

Ukaguzi ulifanyika kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAI) vilivyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi (INTOSAI) na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA).

Methodolojia ya ukaguzi iliyotumiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilijumuisha njia,mbinu na taratibu mbalimbali, kama vile ukaguzi wa kumbukumbu na nyaraka, mahojiano na ziara za maeneo mbalimbali yaliyokaguliwa. Ukaguzi pia ulihusisha kupima mifumo ya udhibiti wa ndani ya mashirika na taasisi zingine na kutathmini jinsi taasisi zilivyozingatia sheria, kanuni, na sera husika.




# SURA YA PILI

# HATI ZA UKAGUZI

## 2.0 Utangulizi

Hati za ukaguzi hutolewa kwa kuzingatia tathmini ya hitimisho yanayotokana na ushahidi wa ukaguzi uliopatikana kuhusiana na iwapo taarifa za fedha kwa ujumla wake zimetayarishwa kwa njia zote muhimu na kwa mujibu wa mfumo unaotumika wa kuripoti taarifa za fedha, kama vile Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IFRS) au Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu katika taasisi za umma (IPSAS). Hati za Ukaguzi hutolewa kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi Na. 1200. Hili linafanikiwa kwa kuandaa ukaguzi kwa njia ambayo itamuwezesha mkaguzi kupata uhakika wa kuridhisha kulingana na tathmini ya matokeo dhidi ya kipimo kilichowekwa.

Pia, maoni ya ukaguzi yanajumuisha mahitimisho juu ya uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi ya Umma na kanuni zake, na Sheria ya Bajeti na kanuni zake.

## 2.1 Aina za hati za ukaguzi

Kuna aina nne za hati za ukaguzi ambazo ni:

**Hati inayoridhisha:** Hii hutolewa wakati mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango na mfumo unaokubalika wa utoaji wa taarifa za fedha.

**Hati yenye shaka:** Hii hutolewa pale hesabu zinapoonekana zimeandaliwa kwa usahihi isipokuwa baada ya kupata vielelezo vya kutosha, mkaguzi anahitimisha kuwa makosa kwenye hesabu ama likiwa moja au yakiwekwa pamoja yana athari, lakini hayaathiri maeneo yote katika taarifa za fedha. Mkaguzi anaposhindwa

kupata uthibitisho wa kutosha kumwezesha kuhitimisha ukaguzi lakini athari zinazotokana na kukosa uthibitisho huo kwa ujumla wake haziathiri maeneo yote ya taarifa za fedha.

**Hati mbaya:** Hii hutolewa pale mkaguzi anapokuwa amepata vielelezo vya kutosha kuonesha kuwa taarifa za fedha kwa kiasi kikubwa zina makosa; na zikiangaliwa kwa ujumla wake zinakuwa hazikufuata viwango vinavyokubalika vya uandaaji wa taarifa za fedha.

**Kushindwa kutoa hati:** Hali hii hutokea pale mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu taarifa za fedha ambazo ni msingi wa kutoa hati, hivyo mkaguzi kuhitimisha kuwa athari za makosa yanayoweza kuwa kwenye hesabu ambayo hayakubainika yanaweza kuwa makubwa na yenye athari kwa sehemu zote za hesabu hizo.

Mkaguzi huwa anashindwa kutoa hati katika mazingira ya nadra sana yanayohusisha mashaka; hivyo, kuhitimisha kuwa, licha ya kupata ushahidi wa kutosha wa ukaguzi katika maeneo yenye shaka kwenye taarifa ya fedha, haitawezekana kutoa hati kuhusu taarifa za fedha kwa kuwa kuna viashiria vya mashaka vyenye madhara kwenye taarifa za fedha.

## 2.2 Aya yenye masuala ya msisitizo kwenye ripoti za mkaguzi

Kama nitaona kuna umuhimu wa kuwaarifu watumiaji wa taarifa za fedha kuhusu suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za fedha, kwa mtazamo wangu suala hilo ni muhimu na la msingi kwa ajili ya kuleta uelewa wa taarifa hizo, nitaiweka aya hii kwenye taarifa ya ukaguzi. Aya hii itawekwa pale tu ambapo nimepata vielelezo vya kutosha kuwa taarifa za fedha hazijakosewa; na inapaswa itokane na suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za fedha.

## 2.3 Masuala muhimu ya ukaguzi

Aya ya masuala muhimu ya ukaguzi hutoa taarifa za ziada kwa watumiaji wa taarifa za fedha ili kuwasaidia kuelewa masuala ya kitaaluma ya mkaguzi ambayo yalikuwa na umuhimu mkubwa katika ukaguzi wa taarifa za fedha za taasisi husika. Uwasilishaji

wa masuala muhimu ya ukaguzi huongeza thamani na uwazi kwenye taarifa za ukaguzi.

## 2.4 Hati za ukaguzi zilizotolewa mwaka huu

Katika mwaka wa fedha 2021/22, nimekamilisha ukaguzi wa hesabu za fedha kwa mashirika ya umma 206 na kutoa hati za ukaguzi kwa mashirika 203. Kati ya hati za ukaguzi 203 nilizotoa, 196 zilikuwa ni hati zinazoridhisha, tano ni hati zenye shaka na nilishindwa kutoa maoni ya ukaguzi kwa mashirika mawili. Mashirika matatu yaliyobakia sikuweza kutoa taarifa ya ukaguzi wangu kwa kuwa hayana Bodi ya Wakurugenzi kwa zaidi ya miezi 12 hivyo taarifa zake za fedha na ukaguzi hazikuweza kusainiwa.

Taarifa za hati za ukaguzi kwa kila shirika zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na. I**

## 2.5 Mwenendo wa hati za ukaguzi

Mwenendo wa hati za ukaguzi kwa miaka mitano mfululizo kwa mashirika ya umma na taasisi zingine kutoka 2017/18 hadi 2021/22 umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 1** na **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa hati za ukaguzi**

| Aina ya Hati ya Ukaguzi | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|
| Inayoridhisha | 121 | 147 | 162 | 185 | 196 |
| Yenye shaka | 1 | 0 | 3 | 8 | 5 |
| Kushindwa kutoa Maoni | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Mbaya | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **122** | **148** | **165** | **195** | **203** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa taarifa za fedha zilizokaguliwa*

**Jedwali Na. 2: Mwenendo wa hati za ukaguzi kwa asilimia**

| Aina ya Hati ya Ukaguzi | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|
| Inayoridhisha | 99 | 99 | 98 | 95 | 97 |
| Yenye shaka | 1 | 0 | 2 | 4 | 2 |
| Kushindwa kutoa Maoni | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Mbaya | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **100** | **100** | **100** | **100** | **100** |

## 2.6 Hitimisho katika uzingatiaji wa sheria na kanuni manunuzi na bajeti

Kwa mwaka wa fedha 2021/22, ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria na kanuni ulijikita katika maeneo mawili, ambayo ni uzingatiaji wa sheria ya ununuzi wa umma na kanuni zake pamoja na uzingatiaji wa sheria ya bajeti na kanuni zake. Maeneo haya ndiyo niliyatolea hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni husika.

### 2.6.1 Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria na kanuni za ununuzi wa umma

Katika mwaka wa fedha 2021/22, nimekamilisha ukaguzi wa hesabu za fedha kwa mashirika ya umma 206 na kutoa hitimisho kwa mashirika 203. Kati ya mashirika 203, mashirika 128 yalikidhi uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake. Wakati mashirika 75 yalikidhi ijapokuwa yalibainika kuwa na baadhi ya mapungufu. Taarifa za mahitimisho kwa kila shirika zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na. I** na kwenye **Jedwali Na. 3**

**Jedwali Na. 3: Mwenendo wa mahitimisho ya uzingatiaji wa sheria ya ununuzi wa umma na kanuni zake**

| Aina za hitimisho uzingatiaji | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|
| Yaliyokidhi | 115 | 128 |
| Yaliyokidhi na kubanika kuwa na baadhi ya mapungufu | 79 | 75 |
| Kushindwa kutoa hitimisho | 1 | 0 |
| **Jumla** | **195** | **203** |

**Chanzo:** Uchambuzi wa taarifa za fedha zilizokaguliwa

### 2.6.2 Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya bajeti na kanuni zake

Katika mwaka wa fedha 2021/22, nimekamilisha ukaguzi wa hesabu za fedha kwa mashirika ya umma 206 na kutoa mahitimisho kwa mashirika 203. Kati ya mashirika 203, mashirika 151 yalikidhi uzingatiaji wa sheria ya bajeti na kanuni zake, wakati mashirika 52 yalikidhi japo yalibainika kuwa na kasoro kadhaa.

Taarifa za mahitimisho kwa kila shirika zimeoneshwa katika **Kiambatisho na I** na kwenye **Jedwali Na. 4.**

**Jedwali Na. 4: Muhtasari wa aina za hitimisho za uzingatiaji wa sheria ya bajeti na kanuni zake**

| Aina ya hitimisho | 2021/22 |
|---|---|
| Yaliyokidhi | 151 |
| Yaliyokidhi na kubanika kuwa na baadhi ya mapungufu | 52 |
| **Jumla** | **203** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa taarifa za fedha zilizokaguliwa*



# SURA YA TATU

## MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA

### 3.0 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti za ukaguzi za miaka iliyopita na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na maafisa masuuli katika utekelezaji wa mapendekezo yangu yaliyotolewa kwa menejimenti na utawala.

Ninapenda kutambua juhudi zilizofanywa na maafisa masuuli katika kujibu na kuandaa mpango wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwa mashirika ya umma

Pia, kama sehemu ya majukumu yake ya usimamizi, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Umma mara kwa mara hufanya vikao na ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na Maofisa masuuli wa Taasisis za Umma wanachukua hatua stahiki za kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi na maagizo ya kamati

### 3.1 Tathmini ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo kwa kipindi kilichopita katika ripoti ya mwaka

Kifungu cha 40 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418 kinanitaka kujumuisha hali ya mpango wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi unaoandaliwa na maafisa masuuli na kujumuishwa pamoja na Mlipaji Mkuu wa Serikali katika taarifa ya ukaguzi ya mwaka. Kwa kufuata sheria hiyo. Serikali kupitia Mlipaji Mkuu wa Serikali alijibu na kuwasilisha kwangu mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti yangu ya mwaka wa fedha 2020/21.

Kati ya mapendekezo 126 ya ripoti yangu ya mwaka uliopita, mapendekezo 53 (asilimia 42) yametekelezwa; mapendekezo 63 (asilimia 50) yapo kwenye hatua za utekelezaji; mapendekezo 9 (asilimia 7) hayakutekelezwa; na pendekezo 1 (asilimia 1) limepitwa na wakati. Tathmini ya utekelezaji inaonesha hali inayoridhisha. Maelezo ya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo na mwaka husika ni kama yanavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na II** na **Jedwali Na. 5**

**Jedwali Na. 5: Utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita**

| Mwaka wa Fedha | Yame tekelezwa | Yanayo tekelezwa | Hayaku tekelez wa | Yamepitwa na muda | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **2017/18** | 16 | 26 | 20 | 1 | 63 |
| **2018/19** | 25 | 36 | 52 | 3 | 116 |
| **2019/20** | 34 | 51 | 11 | 1 | 97 |
| **2020/21** | 53 | 63 | 9 | 1 | 126 |

*Chanzo: majibu ya hoja za ukaguzi kutoka kwa mlipaji mkuu wa serikali*

## 3.2 Tathmini ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo kwa kipindi kilichopita katika mashirika na taasisi zingine za umma

Kati ya mapendekezo 6146 niliyoyatoa katika ripoti ya mwaka uliopita kwa mashirika ya umma 206, mapendekezo 2195 (asilimia 36) yametekelezwa; mapendekezo 2611 (asilimia 43) yapo kwenye hatua za utekelezaji; mapendekezo 1064 (asilimia 17) hayakutekelezwa; na mapendekezo 276 (asilimia 4) yamepitwa na wakati. Tathmini ya utekelezaji inaonesha hali inayoridhisha.

Ucheleweshaji wa utekelezaji wa mapendekezo yangu unamaanisha kuwa mapungufu niliyobainisha hayakushughulikiwa na kuna uwezekano wa kujirudia, hivyo kuyaweka mashirika katika hatari ya udanganyifu, uzembe na kushindwa kutekeleza majukumu yao. Hivyo, ninasisitiza menejimenti kutekeleza kikamilifu mapendekezo yote ambayo hayajatekelezwa.

## 3.3 Tathmini ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa Mwaka 2021/22

Tathmini ya hali ya utekelezaji wa maagizo ya kamati hadi mwaka 2021/22 ilibainisha kuwa kati ya maagizo 163 yaliyotolewa na kamati kwa mashirika ya umma 37, Maagizo 70 (asilimia 43) yalitekelezwa, maagizo 92 (asilimia 56) yalikuwa katika hali ya utekelezaji, na agizo moja (asilimia 1) halikutekelezwa.



# SURA YA NNE

# UTENDAJI WA KIFEDHA WA MASHIRIKA YA UMMA

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inatoa tathmini ya utendaji wa kifedha; uhimilivu, uendelevu na ustawi wa utoaji huduma; na viwango vya ukwasi wa aina mbili– mashirika na taasisi zingine za kibiashara katika sekta ya umma na mashirika na taasisi zingine zisizo za kibiashara katika sekta ya umma kulingana na taarifa zao za fedha kwa mwaka 2021/22 ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopta. Mashirika na taasisi zingine za kibiashara zinalenga kupata faida na hazitegemei fedha za ruzuku kutoka serikalini, wakati mashirika na taasisi zingine zisizo za kibiashara yameanzishwa ili kutoa huduma kwa umma bila kufanya biashara na hutegemea fedha za Serikali, ada na michango ili kujiendesha. Mapitio ya utendaji wa kifedha katika sura hii hayajumuishi benki zinazomilikiwa na Serikali, mifuko ya hifadhi ya jamii, na taasisi zinazosimamia soko la mitaji na dhamana zinazouzwa.

## 4.1 Mashirika ya umma yaliyopata hasara au kuwa na nakisi kwa mwaka wa fedha 2021/22

Ukaguzi wangu wa utendaji wa kifedha kwenye mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2021/22, ulibaini mashirika na taasisi zingine za umma 45 zilipata hasara au nakisi kwa miaka miwili mfululizo kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.6**. Kati ya mashirika hayo, 14 yalikuwa ni mashirika na taasisi zingine za kibiashara katika sekta ya umma na 31 ni mashirika na taasisi zingine zisizo za kibiashara katika sekta ya umma. Mashirika na taasisi zingine zisizo za kibiashara yalipata nakisi ambayo kwa kiasi kikubwa ilisababishwa na ukosefu wa ruzuku ya Serikali na

vyanzo mbadala vya mapato. Mashirika na taasisi zingine za kibiashara zilipata hasara hasa kutokana na utendaji usioridhisha kwa uwekezaji uliofanyika, uendeshaji wa biashara, na udhibiti usiofaa wa matumizi na mapato.

**Jedwali Na. 6: Taasisi zilizopata hasara au nakisi kwa miaka miwili**

| Na | Jina la Taasisi | 2020/21 (Sh. Milioni) | 2021/22 (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|
| **Mashirika ya kibiashara** | | | |
| 1 | Kampuni ya Ndege Tanzania | (36,182.50) | (35,238.36) |
| 2 | Shirika la Reli Tanzania | (22,872.19) | (31,295.27) |
| 3 | Kampuni ya Mkulazi | (5,870.87) | (14,395.65) |
| 4 | Shirika la Taifa la Maendeleo | (26,367.79) | (11,921.64) |
| 5 | Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL | (166.26) | (7,839.54) |
| 6 | Kiwanda cha Kimataifa cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro | (2,233.16) | (4,996.90) |
| 7 | Kiwanda cha kibaiolojia cha kuzalisha viuadudu vya kuangamiza mazalia ya mbu (TBPL) | (5,152.92) | (3,615.68) |
| 8 | Benki ya TIB Rasilimali | (292.28) | (838.02) |
| 9 | Kampuni ya Uendelezaji wa Joto-ardhi Tanzania | (618.69) | (791.68) |
| 10 | Kampuni ya Kuzalisha Nguzo za Umeme za Zege Tanzania (TCPM) | (1,187.03) | (703.95) |
| 11 | Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha | (1,741.71) | (505.21) |
| 12 | Soko la Bidhaa Tanzania | (1,449.06) | (323.27) |
| 13 | Kampuni ya Uwekezaji ya PPF na DCC | (158.46) | (60.35) |
| 14 | Kampuni ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam | (95.65) | (2.28) |
| **Mashirika yasiyo ya kibiashara** | | | |
| 15 | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya | (109,713.24) | (204,654.34) |
| 16 | Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba | (8,306.33) | (19,406.06) |
| 17 | Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila | (13,408.21) | (19,028.78) |
| 18 | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam | (3,703.44) | (15,324.80) |
| 19 | Chuo Kikuu cha Dodoma | (11,698.91) | (10,274.08) |
| 20 | Mamlaka ya Elimu Tanzania | (943.18) | (5,261.38) |
| 21 | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira | (1,045.80) | (3,910.77) |
| 22 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kigoma/Ujiji | (2,732.83) | (3,196.11) |
| 23 | Baraza la Mtihani la Taifa | (5,265.19) | (3,161.65) |
| 24 | Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania | (3,507.08) | (3,067.88) |
| 25 | Tume ya Ushindani | (2,347.98) | (2,085.54) |
| 26 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya | (2,980.69) | (2,039.00) |
| 27 | Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania | (2,443.78) | (1,945.21) |
| 28 | Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam | (144.93) | (1,460.85) |
| 29 | Mamlaka ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje | (721.51) | (1,260.54) |
| 30 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Singida | (1,478.98) | (1,259.74) |
| 31 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga | (1,266.65) | (903.71) |

| Na | Jina la Taasisi | 2020/21 (Sh. Milioni) | 2021/22 (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|
| 32 | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima | (727.47) | (848.17) |
| 33 | Kituo cha Uwekezaji Tanzania | (1,043.42) | (731.06) |
| 34 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga | (278.99) | (797.85) |
| 35 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Geita | (904.73) | (677.32) |
| 36 | Mfuko wa Dhamana ya Kuendeleza Sekta ya Korosho | (1,262.20) | (497.74) |
| 37 | Bodi ya Pamba Tanzania | (164.39) | (481.31) |
| 38 | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania | (52.72) | (424.82) |
| 39 | Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari | (473.64) | (323.50) |
| 40 | Baraza la Taifa la Ujenzi | (72.89) | (309.87) |
| 41 | Balaza la Sanaa Tanzania | (150.39) | (245.94) |
| 42 | Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini | (348.82) | (194.16) |
| 43 | Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma | (87.81) | (32.17) |
| 44 | Baraza la Rufaa za Kodi | (47.94) | (21.32) |
| 45 | Bodi ya Pareto Tanzania | (47.30) | (12.76) |

***Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za fedha za mwaka 2020/21 na 2021/22***

Aidha, nilibaini mashirika ya umma 16 yaliyopata faida katika mwaka wa fedha 2020/21 lakini yamepata hasara/nakisi kwa mwaka wa fedha 2021/22 kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na.7**

**Jedwali Na. 7: Orodha ya mashirika yaliyopata faida 2020/21 ila yakapata hasara/nakisi 2021/22**

| Na | Jina la Taasisi | 2020/21 (Sh. Milioni) | 2021/22 (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|
| **Mashirika ya biashara** | | | |
| 1 | Shirika la Mawasiliano Tanzania | 517.00 | (15,563.00) |
| 2 | Kampuni ya Huduma za Meli | 28,489.17 | (9,417.38) |
| **Mashirika yasiyo ya kibiashara** | | | |
| 3 | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 6,631.05 | (5,441.50) |
| 4 | Bodi ya Pamba Tanzania | 151.52 | (1,169.95) |
| 5 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi Wa Mazingira Bukoba | 2,015.04 | (594.04) |
| 6 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea | 23.00 | (633.46) |
| 7 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama | 10,118.70 | (416.55) |
| 8 | Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli | 6,569.23 | (355.95) |
| 9 | Baraza la Ushindani | 103.93 | (234.57) |
| 10 | Tasisi ya Utafiti Wa Misitu Tanzania | 236.58 | (184.65) |
| 11 | Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi Tanzania | 84.95 | (145.16) |
| 12 | Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania | 573.88 | (68.01) |
| 13 | Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania | 415.88 | (82.57) |

| Na | Jina la Taasisi | 2020/21 (Sh. Milioni) | 2021/22 (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|
| 14 | Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 135.07 | (59.09) |
| 15 | Bodi ya Maziwa Tanzania | 25.70 | (51.79) |
| 16 | Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika | 287.97 | (30.82) |

***Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za fedha za mwaka 2021/22***

Pia, nilibaini mashirika mbalimbali na taasisi zingine za umma zilipitia changamoto mbalimbali katika uendeshaji uliosababisha kutofanya vizuri katika uwekezaji na uendeshaji wa biashara, hivyo kupelekea shirika au taasisi husika kupata hasara/nakisi. Sababu za kupata hasara/nakisi kwa baadhi ya taasisi hizo ni kama ifuatavyo;

(i) Kampuni ya Ndege ya Tanzania imekuwa ikipata hasara kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo. Pamoja na Serikali kutoa ruzuku ya shilingi bilioni 30.63 kwa mwaka wa fedha 2021/22, kampuni bado iliripoti hasara ya shilingi bilioni 35.23. Serikali isingetoa ruzuku hiyo, kampuni ingepata hasara ya shilingi bilioni 65.86. Hii inaonesha changamoto ambazo Kampuni ya Ndege Tanzanaia inakabiliana nazo katika soko kwa sasa. Hivyo, Kampuni ya Ndege Tanzania itathmini upya mbinu na mikakati ya uendeshaji ili kupunguza gharama na kuongeza mapato.

(ii) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) uliripoti hasara ya shilingi bilioni 204.65 kutokana na ongezeko la gharama za mafao ya matibabu na gharama za huduma kwa wanachama ambazo hazikulingana na mapato yaliyoongezeka.

(iii) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiliripoti nakisi ya shilingi bilioni 15.32 kutokana na kupungua kwa mapato yanayotokana na ruzuku za wafadhili kwa ajili ya shughuli za kufanya tafiti mbalimbali na mapato ya ushauri.

(iv) TANOIL haikufanya vizuri kutokana na kukosa mtaji wa uendeshaji kutoka kwa kampuni mama ya Shirika la Maendeleo ya Petroli nchini; kutokuwapo kwa bodi ya usimamizi; na changamoto ya upatikanaji wa kiasi kikubwa

cha dola za Marekani ndani ya muda mfupi ili kusaidia upatikanaji wa barua ya dhamana ya mkopo (Letter of Credit) kwa ajili ya kuagiza mafuta na kupelekea kampuni kulipa adhabu na gharama kubwa za kuifadhi mafuta kwa Taasisi ya Ununuzi wa mafuta kwa Pamoja (PBPA) na muuzaji mtawalia.

(v) Hospitali ya Taifa Muhimbili ilipata nakisi ya shilingi bilioni 45.44 kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya jumla ambayo hayakuendana na ongezeko la mapato, gharama ambazo zinajumuisha msamaha wa malipo ya huduma shilingi bilioni 19.15 na marejesho ya bima yaliyokataliwa shilingi bilioni 1.99.

(vi) Mapato ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli yalipungua kwa kiasi kikubwa kutokana na kupungua kwa ruzuku ya Serikali na ruzuku kutoka kwa wafadhili, hivyo mamlaka ikapata nakisi ya shilingi milioni 355.95;na

(vii) Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ilipata nakisi ya shilingi milioni 68.01 kutokana na kuongezeka kwa malipo ya mishahara na adhabu za kutolipa kodi kwa wakati; Kampuni ya Mawasiliano Tanzania (TTCL) iliripoti hasara kutokana na kufanya vibaya kwa bidhaa na huduma zake katika soko; Bodi ya Korosho Tanzania ilipata hasara kutokana na kupungua kwa ruzuku kutoka Serikalini na kupungua kwa michango ya wakulima; na Mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira ya Bukoba ilikuwa na nakisi iliyosababishwa na kupungua kwa mapato na kuongezeka kwa matumizi.

**Ninapendekeza kuwa:**

a) **Mashirika na taasisi zingine za umma ziboreshe ufanisi wa utendaji ili kuongeza ukusanyaji wa mapato na kutekeleza mikakati ya kupunguza gharama za uendeshaji. Aidha, taasisi zianzishe na kuimarisha mikakati ya kubadilisha mwelekeo wa uwekezaji na uendeshaji wa biashara zisizofanya vizuri, kufanya uwekezaji wenye tija na endelevu ili kuongeza mapato.**

b) **Serikali ihakikishe kuwa mashirika yanaendeshwa na watumishi wenye weledi na waliobobea katika uendeshaji wa biashara, ili kuongeza ufanisi. Watumishi wa kariba hiyo wanaweza kutoka serikalini ama kutoka katika sekta binafsi.**

c) **Serikali iimarishe usimamizi wa taasisi kwa kuteua wajumbe wa bodi wenye taaluma na ujuzi katika sekta na stadi za biashara. Ikiwa ni muhimu, nafasi za ujumbe wa bodi zitangazwe ili kupata wajumbe wenye sifa stahiki; na**

d) **Serikali ianzishe na kutekeleza mfumo wa motisha unaotegemea matokeo ya utendaji kazi wa watumishi utakaoenda sambamba na ufanisi na faida zinazopatikana kwa taasisi.**

## 4.2 Mashirika ya umma yenye mitaji hasi

Ukaguzi wangu wa utendaji wa kifedha wa mashirika na taasisi za umma ulibaini mashirika 10 yaliyokuwa na mtaji hasi kwa mwaka wa fedha 2021/22. Kati ya taasisi hizo, taasisi tano zilikuwa ni za kibiashara na taasisi nne zilikuwa siyo za kibiashara. Sababu hasa za mtaji hasi zilikuwa ni malimbikizo ya muda mrefu ya hasara na mikopo iliyochukuliwa na taasisi hizo kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za taasisi husika **(Jedwali Na. 8).**

**Jedwali Na. 8: Taasisi zenye mitaji hasi**

| Na | Jina la Taasisi | Jumla ya Mali (Sh.Milioni) | Jumla ya madeni (Sh.Milioni) | Mitaji (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|---|
| **Mashirika ya kibiashara** | | | | |
| 1 | Kampuni ya Ndege ya Tanzania | 330,927.28 | 488,643.99 | (157,716.72) |
| 2 | Kampuni ya STAMIGOLD | 58,207.90 | 69,882.52 | (11,674.62) |
| 3 | Kampuni ya Uchapishaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam | 34.29 | 1,677.80 | (1,643.51) |
| 4 | Benki ya TIB Rasilimali | 1,483.08 | 1,852.43 | (369.35) |
| 5 | Kituo cha Kompyuta Chuo Kikuu cha Dar es Salaam | 1,165.38 | 1,329.51 | (164.14) |

| Na | Jina la Taasisi | Jumla ya Mali (Sh.Milioni) | Jumla ya madeni (Sh.Milioni) | Mitaji (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|---|
| **Mashirika ya kibiashara** | | | | |
| 6 | Kampuni ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam | 1,563.50 | 1,602.20 | (38.70) |
| **Mashirika yasiyo ya kibiashara** | | | | |
| 7 | Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba | 109,019.13 | 131,294.07 | (22,274.94) |
| 8 | Bodi ya Pareto Tanzania | 605.59 | 1,940.62 | (1,335.03) |
| 9 | Bodi ya Maziwa Tanzania | 64.15 | 166.16 | (102.01) |
| 10 | Bodi ya Katani Tanzania | 1,117.46 | 1,191.31 | (73.85) |

***Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za fedha za mwaka 2021/22***

Kwa mfano, Mfuko wa Maendeleo ya Pamba uliripoti ongezeko la asilimia 525 katika malimbikizo ya hasara kutoka shilingi bilioni 3.70 katika mwaka wa fedha 2020/21 hadi shilingi bilioni 23.10 katika mwaka wa fedha wa 2021/22, hasa kutokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na kiasi cha madeni yasiyokusanyika. Kampuni ya madini ya STAMIGOLD ilikuwa na malimbikizo ya hasara yanayofikia shilingi bilioni 58.44 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 iliyopunguza mtaji wa kampuni. Hasara hii ilisababishwa na kupungua kwa uzalishaji wa madini kutokana na upungufu wa vifaa vya uchimbaji kutoka kwa mkandarasi

Kuwa na mtaji hasi kunatia shaka ikiwa taasisi hizi zitaweza kudumu kwenye utoaji wa huduma na kutekeleza majukumu yao ipasavyo katika siku zijazo.

**Ninapendekeza kuwa mashirika na taasisi zingine za umma (a) zifanye uchambuzi wa kina kuhusu hali yao ya kifedha, kutambua sababu kuu za mtaji hasi na kuandaa mpango madhubuti wa kushughulikia sababu zilizopelekea kuwa na mtaji hasi. Hii inaweza kujumuisha hatua za kupunguza gharama, kuboresha ufanisi, kuongeza mapato, kurekebisha madeni, kuweka mazingira rafiki ya ulipaji, au kuuza mali zisizo za muhimu; na (b) ziombe msaada wa Serikali ili kuongeza mtaji au kuwekeza katika biashara mpya ili kuwa na mapato ya kutosha kulipa madeni na kukuza mitaji ya taasisi.**

## 4.3 Taasisi za umma zisizo na uwezo wa kulipa madeni ya muda mfupi

Ukaguzi wangu ulibaini taasisi 45 ambazo nilizifanyia tathmini na kubainika kuwa na madeni ya muda mfupi zaidi ya mali za muda mfupi, taasisi 15 ni za kibiashara, na taasisi 30 siyo za kibiashara.

Nilibaini kuwa uwiano wa ukwasi wa muda mfupi (jumla ya mali za muda mfupi/jumla ya madeni ya muda mfupi) wa taasisi hizi ulikuwa kati ya 0.02 hadi 0.99 badala ya uwiano chini unaohitajika wa moja **(Jedwali Na.9)**. Idadi ya taasisi hizi imeongezeka mwaka huu ikilinganishwa na taasisi za umma sita zinazofanya biashara zilizoripotiwa katika ripoti yangu ya mwaka uliopita 2020/21.

Nimaoni yangu kuwa taasisi hizi haziwezi kulipa madeni ya muda mfupi yanapoiva. Tatizo la ukwasi wa taasisi hizi lilichangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la gharama za mikopo, kuongezeka kwa fedha za ruzuku zenye masharti bila kutumika kwa wakati katika miradi iliyokusudiwa na ufinyu wa fedha uliosababisha madeni hayo yasilipwe kwa wakati.

**Jedwali Na. 9: Taasisi zenye uwiano wa ukwasi chini ya moja**

| Na | Jina la Taasisi | Jumla ya Mali za Muda Mfupi (Sh Milioni) | Jumla ya Madeni ya Muda Mfupi (Sh.Milioni) | Uwiano |
|---|---|---|---|---|
| | **Taasisi za kibiashara** | | | |
| 1 | Kampuni ya Uchapishaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam | 34.28 | 1,677.80 | 0.02 |
| 2 | Kampuni ya Ndege ya Tanzania | 116,651.65 | 364,819.96 | 0.32 |
| 3 | Shirika la Taifa la Maendeleo | 51,802.03 | 121,477.35 | 0.43 |
| 4 | Shirika la Umeme Tanzania | 1,351,523.00 | 3,144,357.00 | 0.43 |
| 5 | Kampuni ya STAMIGOLD | 24,356.11 | 51,469.58 | 0.47 |
| 6 | Shirika la Posta | 35,203.51 | 69,089.83 | 0.51 |
| 7 | Kiwanda cha kibaiolojia cha kuzalisha viuadudu vya kuangamiza mazalia ya mbu (TBPL) | 2,156.40 | 4,014.26 | 0.54 |
| 8 | Kituo cha Kompyuta Chuo Kikuu cha Dar es Salaam | 726.75 | 1,313.05 | 0.55 |
| 9 | Shirika la Mawasiliano Tanzania | 186,436.00 | 300,879.00 | 0.62 |
| 10 | Benki ya TIB Rasilimali | 1,223.68 | 1,473.58 | 0.83 |
| 11 | Kampuni ya Ranchi za Taifa | 9,285.04 | 11,194.02 | 0.83 |
| 12 | Kampuni ya Magazeti Tanzania | 20,176.23 | 22,509.51 | 0.90 |
| 13 | Kampuni ya Mbolea Tanzania | 14,703.58 | 15,922.01 | 0.92 |

| Na | Jina la Taasisi | Jumla ya Mali za Muda Mfupi (Sh Milioni) | Jumla ya Madeni ya Muda Mfupi (Sh.Milioni) | Uwiano |
|---|---|---|---|---|
| 14 | Kampuni ya Chuo cha Tekinolojia Dar es Salaam | 1,558.95 | 1,602.20 | 0.97 |
| 15 | Kampuni ya Gesi Tanzania | 23,728.00 | 24,359.00 | 0.97 |
| **Taasisi zisizo za kibiashara;** | | | | |
| 16 | Bodi ya Pareto Tanzania | 117.90 | 1,940.62 | 0.06 |
| 17 | Bodo ya Maziwa Tanzania | 13.14 | 166.16 | 0.08 |
| 18 | Balaza la Sanaa Tanzania | 58.29 | 492.94 | 0.12 |
| 19 | Baraza la Taifa la Biashara Tanzania | 68.11 | 404.14 | 0.17 |
| 20 | Bodi ya Katani Tanzania | 207.73 | 1,189.61 | 0.17 |
| 21 | Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila | 5,988.71 | 19,024.42 | 0.31 |
| 22 | Baraza la Ushindani | 24.91 | 69.20 | 0.36 |
| 23 | Taasisi ya Mifupa Muhimbili | 12,936.21 | 34,631.47 | 0.37 |
| 24 | Mamlaka ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje | 3,030.27 | 7,623.84 | 0.40 |
| 25 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga | 1,983.66 | 3,964.75 | 0.50 |
| 26 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kigoma/Ujiji | 1,956.24 | 3,860.79 | 0.51 |
| 27 | Mamalaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Nzega | 838.34 | 1,434.63 | 0.58 |
| 28 | Bodi ya Pamba Tanzania | 2,787.32 | 4,741.98 | 0.59 |
| 29 | Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari | 616.52 | 989.44 | 0.62 |
| 30 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi | 916.71 | 1,460.65 | 0.63 |
| 31 | Baraza la Rufaa za Kodi | 42.87 | 62.46 | 0.69 |
| 32 | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 60,883.82 | 83,895.90 | 0.73 |
| 33 | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania | 1,356.17 | 1,770.75 | 0.77 |
| 34 | Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | 288.58 | 373.02 | 0.77 |
| 35 | Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania | 5,577.04 | 6,956.61 | 0.8 |
| 36 | Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba | 108,393.53 | 131,294.07 | 0.83 |
| 37 | Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania | 4,671.88 | 5,565.09 | 0.84 |
| 38 | Bodi ya Korosho Tanzania | 14,085.72 | 16,775.61 | 0.84 |
| 39 | Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania | 1,980.38 | 2,175.65 | 0.91 |
| 40 | Shirika la Madini la Taifa | 26,330.00 | 28,874.00 | 0.91 |
| 41 | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira | 5,441.10 | 5,964.46 | 0.91 |
| 42 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | 182,462.95 | 196,862.52 | 0.93 |
| 43 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Makambako | 137.45 | 146.32 | 0.94 |
| 44 | Bodi ya Tumbaku Tanzania | 471.83 | 501.94 | 0.94 |
| 45 | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima | 3,329.11 | 3,359.84 | 0.99 |

*Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za fedha za mwaka 2021/22*

**Ninapendekeza kuwa mashirika na taasisi zingine za umma (a) ziongeze vyanzo vya mapato na kutumia vyanzo hivyo kutengeneza mtiririko mzuri wa kifedha, na (b) zijadiliane na**

**wadeni wao ili kuweka masharti mazuri ya malipo ya madeni yanayolingana na mtiririko wa kifedha unaotarajiwa ili kuepuka kulipa riba na adhabu za malimbikizo ya madeni.**

## 4.4 Mashirika na taasisi zingine za umma zinazoendeshwa kwa kutegemea madeni au mikopo

Matumizi ya fedha za mikopo au kuwa na madeni kwa taasisi za umma ni utamaduni wa kawaida, lakini mikopo na madeni yanaweza pia kuongeza hatari za kifedha. Kiwango cha "gearing ratio", uwiano wa madeni kwa mtaji, ni kipimo muhimu kinachotumiwa kupima kiwango ambacho kampuni inategemea mikopo na madeni ikilinganishwa na mtaji wake. Kiwango kikubwa cha uwiano wa mikopo na madeni  kwa mtaji zaidi ya asilimia 100, kinaonesha kuwa taasisi hizo zimejitwika mizigo mikubwa ya madeni na zinaweza kuwa hatarini wakati wa hali mbaya ya kiuchumi au mabadiliko katika biashara.

Ukaguzi wangu wa mitaji ya mashirika na taasisi zingine za umma kwa mwaka wa fedha 2021/22, nilibaini kuwa taasisi 24 zilikuwa na uwiano mbaya wa deni na mikopo kwa mtaji" (jumla ya madeni /jumla ya mtaji) wa zaidi ya asilimia 100, ikiashiria kuwa taasisi hizi zinategemea sana mikopo au madeni kuendesha shughuli zao, hivyo kuwa hatarini zaidi kutokana na gharama kubwa za mikopo na madeni hayo. Hali hii imetokana na sababu mbalimbali kama vile; kuwa na kiwango kikubwa cha mapato ya ruzuku ya mtaji ambao haujatumika; taasisi kuwa na mikopo au madeni mengi na ongezeko la gharama za mikopo na madeni kutokana na kuchelewa kulipa sehemu ya madeni/mikopo na riba. Taasisi zenye madeni au mikopo zaidi ya mitaji zimeainishwa katika **(Jedwali Na.10)** hapa chini.

**Jedwali Na. 10: Taasisi za umma zenye madeni zaidi ya mtaji**

| Na | Taasisi | Kiasi kwa Sh. (Milioni) | | Uwiano wa Mtaji na Madeni (%) |
|---|---|---|---|---|
| | | Jumla ya madeni | Jumla ya mtaji | |
| **Mashirika ya Kibiashara** | | | | |
| 1 | Shirika la Reli Tanzania | 9,243,214.61 | 392,416.12 | 2355.46 |
| 2 | Kampuni ya MCB | 1,986.47 | 427.19 | 465.01 |
| 3 | Shirika la Umeme Tanzania | 15,628,428.00 | 3,949,106.00 | 395.75 |
| 4 | Shirika la Uwekezaji Watumishi | 5,434.46 | 1,495.34 | 363.43 |
| 5 | Kampuni ya Mbolea Tanzania | 21,326.30 | 12,852.48 | 165.93 |
| 6 | Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme | 42,989.24 | 26,466.62 | 162.43 |
| 7 | Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania | 24,673.91 | 15,306.41 | 161.20 |
| 8 | Shirika la Mawasiliano Tanzania | 349,920.00 | 227,884.00 | 153.55 |
| 9 | Mamlaka ya Bandari Tanzania | 2,055,327.40 | 1,492,921.84 | 137.67 |
| 10 | Shirika la Taifa la Maendeleo | 123,007.91 | 94,101.93 | 130.72 |
| 11 | Kampuni ya Ushauri Elekezi ya Uzalishaji Chuo cha Ufundi Arusha | 721.08 | 562.76 | 128.13 |
| **Mashirika Yasiyo ya Kibiashara** | | | | |
| 12 | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania | 23,161.58 | 1,883.44 | 1229.75 |
| 13 | Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania | 3,837,157.00 | 360,599.00 | 1064.11 |
| 14 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha | 418,653.34 | 56,609.50 | 739.55 |
| 15 | Bodi ya Tumbaku Tanzania | 601.94 | 81.97 | 734.34 |
| 16 | Baraza la Ushindani | 69.14 | 15.85 | 436.14 |
| 17 | Ofisi ya Taifa ya Takwimu | 101,820.14 | 25,306.75 | 402.34 |
| 18 | Bodi ya Rufaa za Kodi | 268.06 | 90.86 | 295.03 |
| 19 | Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere Cha Kilimo na Teknolojia | 17,812.70 | 7,593.46 | 234.58 |
| 20 | Chama cha Hakimiliki Tanzania | 543 | 239.89 | 226.35 |
| 21 | Taasisi ya Mifupa Muhimbili | 42,894.95 | 20,380.00 | 210.48 |
| 22 | Baraza la Ushauri la Watumia Huduma za Mawasiliano | 114.37 | 63.84 | 179.14 |
| 23 | Bohari Kuu ya Dawa | 497,304.81 | 367,366.93 | 135.37 |

| Na | Taasisi | Kiasi kwa Sh. (Milioni) | | Uwiano wa Mtaji na Madeni (%) |
|---|---|---|---|---|
| | | Jumla ya madeni | Jumla ya mtaji | |
| 24 | Hospitali ya Taifa ya Muhimbili | 84,545.03 | 64,344.30 | 131.39 |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Fedha, 2020/21 & 2021/22*

**Ninapendekeza kuwa (a) ni muhimu kwa taasisi hizi kufuatilia kwa karibu utendaji wao wa kifedha na kutathmini athari zinazoweza kutokea kutokana na mabadiliko yoyote katika soko au uchumi na kuathiri uwezo wao wa kulipa madeni yao; (b) ziombe msaada wa serikali ili kupata mitaji ya ziada na kuwekeza katika vyanzo vipya vyenye mapato ya kutosha kulipa madeni wanayodaiwa, na (c) zifanye tathmini upya ya muundo wao wa mitaji na malipo ya mikopo au madeni ili kuepuka riba inayotokana na kuchelewesha malipo ya mikopo au madeni.**

## 4.5 Kutolipwa na kushuka kwa ulipaji wa gawio kwa mashirika na taasisi zingine za umma

Ukaguzi wangu wa mashirika ya umma 24 ya kibiashara nchini ulibaini kuwa, mashirika 12 yalipata faida katika kipindi cha mwaka 2021/22. Kati ya Mashirika hayo, sita yalichangia na kulipa gawio kwa Serikali, jumla ya shilingi bilioni 6.8.

Taasisi sita zilizobaki zenye faida hazikulipa gawio kwa Serikali ikijumuisha Benki nne ambazo zilipata faida lakini hazikuweza kulipa gawio kutokana na kuwa na ukwasi wa mtaji kwa ajili ya kukuza uwekezaji. Taasisi mbili zenye faida (Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania) zilipendekeza malipo ya gawio lakini zilikuwa zikisubiri uidhinishwaji na wanahisa katika mkutano mkuu wa mwaka. Taasisi zingine mbili ambazo ni Shirika la Madini la Taifa na UTT-AMIS zililipa kiasi kidogo kuliko kiasi kilichopendekezwa.

Taasisi 12 zilizoripoti hasara katika kipindi hicho hivyo, hazikuweza kulipa gawio. Uwiano wa malipo ya gawio wa taasisi zenye faida

ulishuka kwa asilimia 64 ukilinganisha na mwaka uliopita 2020/21. (**Rejea Kiambatisho Na III).**

**Ninapendekeza taasisi zenye faida zitafute uwiano kati ya kuwekeza upya faida kwa ajili ya ukuaji na kutoa malipo ya gawio kwa wanahisa. Benki za kibiashara za Serikali zinapaswa kuzingatia kuboresha uwiano wa utoshelevu wa mtaji ili kuhakikisha faida ya baadaye.**

## 4.6 Mapungufu yaliyobainika katika uchangiaji wa asilimia 15 ya mapato ghafi kwenda mfuko mkuu wa Serikali

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kutofautiana na mapungufu katika uchangiaji wa asilimia 15 ya mapato ghafi kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mashirka ya umma. Kati ya taasisi 54 **( Kiambatisho Na IV**) zilizopitiwa, ni taasisi sita zilizochangia zaidi ya kiasi kinachohitajika, wakati taasisi 48 zilichangia chini ya kiasi kinachohitajika. Aidha, mashirika matano ya kibiashara katika sekta ya umma yalipaswa kutangaza na kulipa gawio kwa wanahisa kutokana na faida ya mwaka lakini yalichangia katika mfuko wa Serikali kinyume na matakwa ya Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348.

Ukaguzi zaidi wa mashirika 58 ya umma na taasisi zingine **(Kiambatisho Na. V)**, ulibaini kuwa taasisi 29 hazikuchangia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa kipindi cha miaka miwili mfululizo, kinyume na Kifungu cha 12(3) cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348. Kushindwa kutoa michango kunaikosesha serikali mapato yanayohitajika katika utoaji wa huduma kwa Umma.

Matokeo haya yanaonesha ukosefu wa ufuatiliaji na utekelezaji sahihi wa Sheria ya Fedha za Umma na. 348.

**Ninapendekeza kuwa mamlaka husika (a) zichukue hatua madhubuti za kuimarisha ufuatiliaji na utekelezaji wa sheria, ikiwa ni pamoja na kuweka adhabu kwa taasisi za umma ambazo hazifuati Sheria hiyo, (b) kupitia upya vigezo vya kuamua taasisi ambazo hazitakiwi kuchangia katika Mfuko**

**Mkuu wa Serikali ili kukuza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma; na (c ) kupitia kiwango cha asilimia 15 kilichowekwa na Sheria ya Fedha za Umma kwani kinaweza kuwa kikubwa, na kuweka uwezekano wa kusababisha changamoto za kifedha kwa mashirika na taasisi nyingi za umma, inaweza kuwa muhimu kupitia upya kiwango cha michango ili kuhakikisha uthabiti wa kifedha kwa taasisi hizi wakati zikifikia malengo na mahitaji ya mapato kwa Serikali.**




# SURA YA TANO

## UFANISI WA MASHIRIKA YA UMMA KATIKA KUIMARISHA MAZINGIRA YA KIBIASHARA

### 5.0 Utangulizi

Kwa miaka kadhaa sasa, Serikali ya Tanzania imekuwa ikichukua hatua muhimu za kuendeleza miundombinu yake, na kutekeleza miradi mbalimbali yenye lengo la kukuza uchumi na kuboresha maisha ya wananchi wake.

Pia, sura hii inaainisha maeneo ya kuboresha katika uendeshaji wa taasisi saba za umma za kimkakati, ambazo ni Kampuni ya Ndege Tanzania, Shirika la Umeme Tanzania, Shirika la Reli Tanzania, Shirika la Mawasiliano Tanzania, Mamlaka ya Bandari Tanzania, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo, na Shirika la Nyumba la Taifa. Mapungufu haya yanajumuisha kuchelewa kukamilika kwa miradi, kutokuwepo kwa udhibiti wa kutosha wa upotevu wa nishati, ufanisi mdogo katika kutumia rasilimali, na changamoto zingine zinazohitaji kutatuliwa ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji.

## 5.1 Kampuni ya Ndege Tanzania

Ukaguzi wangu wa ufanisi wa Kampuni ya Ndege Tanzania ulibaini mapungufu yafuatayo:

### 5.1.1 Ndege zisizotumika zimesababisha gharama za zisizobadilika shilingi bilioni 5.27 na ukosefu wa mapato yaliyotarajiwa shilingi bilioni 20.35

Nilibaini ndege mbili za Airbus A220-300 (5H-TCH & 5H-TCI) na Bombardier Q400 zilikuwa hazifanyi kazi kwa muda wa siku 2 mpaka 220 kuanzia tarehe 1 Julai 2021 hadi 30 Juni 2022 kwa sababu ya utendaji duni wa ndege ya Airbus A220-300 na huduma dhaifu za baada ya mauzo za kuhakikisha ndege inafanya kazi kama vile huduma za kwenye injini

Uchambuzi wa kifedha umeonesha kuwa ndege zisizotumika zimesababisha kampuni kuingia gharama zisizobadilika kutokana na kukodi na bima jumla ya shilingi bilioni 5.27 na kukosa mapato ya shilingi bilioni 20.35 ambayo yangepatikana endapo ndege ingefanya kazi kwa mwaka mmoja tangu 1 Julai 2021 hadi 30 Juni 2022 . Hali hii imeathiri sana ukwasi na sifa ya kampuni, pia kuongezeka kwa idadi ya ratiba za safari za ndege zilizofutwa kunaathiri uaminifu wa wateja juu ya usafiri wa Kampuni ya Ndege Tanzania.

**Ninapendekeza Serikali iiongezee uwezo kwa kuangalia upya shughuli za sasa za Kampuni ya Ndege Tanzania na kufanya matengenezo na ukarabati wa ndege mara kwa mara ili kuepuka ndege kukaa muda mrefu bila kufanya kazi.**

### 5.1.2 Matumizi yasiyoridhisha ya ndege ya Boeing 787-8 dreamliner yaliyosababisha hasara ya shilingi bilioni 24.9 na gharama za kudumu za matengenezo shilingi bilioni 5.06

Wakati wa mapitio yangu ya utendaji kazi na matumizi ya ndege, nilibaini ndege ya Boeing 787-8 ilizalisha mapato ya jumla ya shilingi bilioni 45.67 na kuwa na gharama ya shilingi bilioni 70.57

ambayo ilisababisha hasara ya jumla ya shilingi bilioni 24.9. Kukosekana kwa ufanisi wa uendeshaji kulisababishwa na idadi ndogo ya abiria na idadi ndogo ya safari za kimataifa, kwani ni safari 9 kati ya 18 za kimataifa zilifanyika kutokana na kusimamishwa kwa baadhi ya safari kwa sababu ya vikwazo vya udhibiti wa ugonjwa wa UVIKO-19.

Zaidi, ukaguzi ulibaini ndege hizo zilisababisha gharama zisizobadilika za shilingi bilioni 5.06 kama gharama za matengenezo ambazo hazikuwa na mapato yanayolingana kutokana na kutofikia masaa ya ndege yanayoweza kutozwa kiwango cha chini. Hii inapelekea ongezeko la madeni ya kampuni ambayo yanaathiri uwezo wa kifedha wa kampuni.

**Ninapendekeza Kampuni ya Ndege Tanzania kufanya kampeni za kina za masoko ili kuukuza ufanisi wa safari za ndege za kitaifa na kimataifa ambazo hazifanyi vizuri.**

### 5.1.3 Gharama za ziada za shilingi bilioni 19.11 zilizotumiwa na Kampuni ya Ndege Tanzania kutokana na Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania kutotekeleza majukumu ya kimkataba

Ndani ya mwaka 2021/22 Kampuni ya Ndege Tanzania ilikodi ndege 11 kutoka kwa Wakala wa Ndege za Serikali ya Tanzania, hivyo kutozwa gharama za matengenezo za dola za Marekani 496 kwa saa moja kwa utendaji kazi wa injini na dola za Marekani 360 kwa maisha ya injini ya mzunguko wa ndege, na kwa mwaka 2021/22 zilifikia shilingi bilioni 25.39 (2020/21 shilingi bilioni 18.56) kiasi hicho kinakusudiwa kwa matengenezo ya ndege wakati zinaharabika na ankara hiyo ilikuwa ni kwa mujibu wa masharti ya mkataba. Katika mapitio yangu ya gharama za uendeshaji, nilibaini kuwa, Kampuni ya Ndege Tanzania iliingia gharama ya shilingi bilioni 19.11 kwa ajili ya matengenezo ya ndege katika mwaka huo,ambayo ni sehemu ya akiba ya matengenezo chini ya mkataba wa Wakala wa Ndege wa Serikali ya Tanzania.

Katika kiasi hicho, shilingi bilioni 17.51 zilitumiwa kwa matengenezo ya ndani yaliyofanywa na Kampuni ya Ndege Tanzania kwa kutumia ujuzi na uwezo wa wataalamu wake, wakati shilingi bilioni 1.6 zilizobaki zilitumika kwa matengenezo ambayo hayakufanywa na Kampuni ya Ndege Tanzania, yalikuwa chini ya makubaliano ya programu ya usimamizi wa injini wa PW1524G. Hatahivyo, gharama zote mbili zilizolipwa na Kampuni ya Ndege Tanzania ni sehemu ya mkataba wa matengenezo yanayotakiwa kugharamiwa na Wakala wa Ndege za Serikali ya Tanzania.

Ni maoni yangu kuwa gharama hizi zilizoingiwa mara mbili zimesababishia kuongezeka kwa hasara kwa Kampuni hii. Kwakuwa, ulipaji mara mbili wa gharama ambazo ni shilingi bilioni 19.11 kwa watoa huduma na shillingi bilioni 25.39 kwa Wakala wa Ndege wa Serikali ya Tanzania,hasara iliyotokea mwaka huu ingeweza kupungua kutoka shilingi bilioni 35.24 mpaka shilingi bilioni 9.85 (ambayo tumetoa malipo kwa Wakala wa Ndege wa Serikali ya Tanzania)

**Ninapendekeza Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi iharakishe mchakato wa kupitia makubaliano kati ya Kampuni ya Ndege Tanzania na Wakala wa Ndege za Serikali ya Tanzania. Mapitio hayo yalenge kufafanua tatizo la malipo mara mbili kwa huduma za matengenezo, ambazo huongeza gharama na madeni kwa Kampuni ya Ndege Tanzania.**

### 5.1.4 Ndege za abiria za kampuni ya Ndege Tanzania kuchelewa kuondoka kwa wastani wa asilimia 25

Kati ya lengo lililowekwa chini ya mpango mkakati wa Kampuni ya Ndege Tanzania ni kufikia kiwango cha asilimia 92 cha ndege kuondoka kwa wakati ifikapo 2021/22, na kuruhusu kiwango cha kuchelewa kilichokubalika sawa na asilimia nane. Mapitio yangu ya ripoti ya utekelezaji wa mpango mkakati nilibaini kuwa kutokana na matatizo ya kiufundi, na mahitaji ya usalama kulingana na mwongozo wa uendeshaji na matengenezo uliopo wa mwaka 2019, pamoja na idadi ndogo ya ndege kulingana na

ratiba za ndege kulisababisha ndege kuchelewa kuondoka kwa asilimia 25 (3,990 / 15,820) ya safari ndani ya mwaka. Kuchelewa huku kulikuwa kati ya dakika 11 hadi masaa manne na dakika 33.

Nina mashaka kuwa, kuna usimamizi usioridhisha wa kutatua changamoto za ndege kuondoka kwa wakati, ambao unaweza kusababisha shirika kupoteza wateja na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji baada ya ndege kuchelewa ikiwemo kuwarejeshea wateja fedha zao.

**Ninapendekeza kuwa Kampuni ya Ndege iimarishe uratibu na shughuli zake za usafirishaji ili kuwezesha ndege kuondoka kwa wakati na kupunguza kuchelewa kwa safari hadi kufikia kiwango kinachokubalika.**

### 5.1.5 Asilimia 96 ya tiketi za ndege za Kampuni ya Ndege Tanzania zilibatilishwa na mawakala

Tiketi iliyobatilishwa ni tiketi ambayo imefutwa na kuwa batili na Kampuni ya Ndege au wakala wa usafiri aliyetoa tiketi hiyo. Tiketi inapofutwa humaanisha muamala umefutwa na kama kuna malipo yoyote yaliyofanywa kwa ajili ya tiketi hiyo yanarejeshwa kwa abiria. Hii inaweza kutokea kwa sababu mbalimbali kama vile abiria kuomba kufuta tiketi yake, makosa yaliyofanyika wakati wa kufanya maombi ya tiketi, mabadiliko katika ratiba za ndege au njia, kutokulipa kwa tiketi na kukosea majina ya abiria.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa kulikuwa na jumla ya tiketi 38,455 zilizofutwa katika mwaka 2021/22, ambapo asilimia 4 zilifanywa na Kampuni ya Ndege Tanzania na asilimia 96 zilifanywa na mawakala. Pia nilibaini kulikuwa na tiketi 479 zilizofutwa baada ya tarehe ya kutumika tiketi hiyo kinyume na ilivyoelezwa katika Miongozo ya Shirikisho la Kimataifa la Usafiri wa Anga.

Nina mashaka kuwa idadi kubwa ya tiketi zilizofutwa zinapelekea kupoteza mapato kwa sababu wakati mwingine wateja hawawezi kupata tiketi kwani mfumo huonesha kuwa ndege zimejaa wakati kiuhallisia ndege zinakuwa bado zina nafasi. Nina mashaka kuwa

hali hii inasababishwa na mawakala kwasababu ya kutokuwepo kwa kikomo cha kubatilisha tiketi zinazosababisha hali kuwa mbaya.

**Ninapendekeza kuwa Kampuni ya Ndege Tanzania iboreshe mifumo ya udhibiti ya ndani kuhusu utaratibu wa kufuta tiketi ikiwa ni pamoja na kuweka masharti na ukomo wa kufuta tiketi kwa mawakala wa safari.**

## 5.2 Shirika la Umeme Tanzania

Ukaguzi wangu wa Ufanisi wa Shirika la Umeme Tanzania ulibaini mapungufu yafuatayo;

### 5.2.1 Mapungufu ya mfumo wa kufuatilia upotevu wa nishati ya umeme

Mita ni vifaa vinavyotumika kupima nguvu inayosambazwa kutoka kwenye kituo ambacho umeme unapokelewa kutoka kiwanda cha uzalishaji. Laini ya umeme ni mtandao wa kuhamisha nishati kutoka vyanzo vya umeme hadi kwenye vituo vya usambazaji au watumiaji. Mapitio yangu ya mita katika laini za umeme yalibaini yafuatayo:

Kati ya mita 1,803 za vituo vya umeme vilivyopo katika mikoa 29, taarifa za mita 1,638 (asilimia 90.8) hazikuoneshwa katika mfumo wa usomaji mita moja kwa moja kwa mwaka mzima, na kuongezea mita 52 zilikuwa na usomaji wa nishati iliyopokelewa pekee, wakati mita 80 zilikuwa na usomaji wa nishati iliyosafirishwa pekee. Suala hili ni kinyume na Kanuni Na. 45(1) ya kanuni za sheria ya umeme (Huduma za Ugavi) za mwaka 2019.

Pia, nilibaini ugumu wa kufuatilia usomaji wa mita kwa mitambo ya kulisha umeme na usambazaji wa umeme (ikiwa ni pamoja na watumiaji wakubwa wa nishati) kutokana na upungufu wa maelezo kuhusu mitambo ya kulisha umeme au vituo vidogo vya umeme katika mfumo wa usomaji mita moja kwa moja.

Uongozi wa shirika ulielezea sababu kuu za udhaifu huu ni matatizo ya mtandao na mita zilizoharibika kwenye vituo vya umeme. Kwa maoni yangu, ufungaji wa mita katika mitambo ya umeme haukuakisi thamani ya fedha, na kuna uwezekano kuwa baadhi ya mita au mitambo ya umeme imefanyiwa udanganyifu au kughushiwa, hivyo kusababisha wizi wa nishati unaofanywa na wateja (hasa watumiaji wakubwa wa nishati) kwa kushirikiana na wafanyakazi wasio waaminifu.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania lifanye tathmini ya mfumo wa usomaji mita moja kwa moja na mita za umeme zinazowekwa ziendane na mazingira ya sasa ya uendeshaji ili kuzuia upotevu wa nishati.**

### 5.2.2 Mita za umeme 874,019 kutothibitishwa na Wakala wa Vipimo

Katika mwaka wa fedha 2021/22, Shirika la Umeme Tanzania lilinunua na kutumia jumla ya mita 874,019 zenye thamani ya shilingi bilioni 115. Lakini hazikuthibitishwa na Wakala wa Vipimo kitu ambacho kinaweza kusababisha hasara kwa mteja au Shirika. Hii ni kinyume na Kanuni ya 22(1) ya Kanuni za Uzani na Vipimo za mwaka 2019 zinazoelekeza kuwa hakuna mita itakayoruhusiwa kutumiwa na mkandarasi au mnunuzi kwa madhumuni ya kupima umeme au gesi inayotolewa au kutumika kwake isipokuwa imethibitishwa kwa mujibu wa Sheria za Umeme Na.10 ya 2008 (Sura.131).

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania litekeleze matakwa ya Kanuni za Uzani na Vipimo za Mwaka 2019, ili kuhakikisha mita zinapimwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo kabla ya kutumiwa na wateja.**

### 5.2.3 Malipo ya kutunza vyura wa kihansi katika bustani ya wanyama ya Marekani kwa shilingi milioni 612

Mwaka 2000 Tanzania ilisafirisha vyura 500 kwenda bustani ya wanyama ya Bronx na Toledo iliyopo Marekani ili kuepuka hatari ya kupotea kwa vyura ambayo ilitokana na utekelezaji wa mradi

wa umeme wa maji wa Kihansi mnamo mwaka 1994. Ingawa haiwezekani kubainisha idadi kamili ya sasa ya vyura vinavyosimamiwa nchini Marekani, Shirika la Umeme Tanzania linagharamia dola za Marekani 130,000 kwa mwaka kwa ajili ya kutunza vyura hao, ambapo inakadiriwa takribani ya dola za Marekani milioni 2.86 zilitumika kwa miaka yote 22 ya kuhudumia vyura. Katika mwaka 2020/21 na 2021/22 ilifanya malipo ya shilingi milioni 611.92 (sawa na dola za Marekani 260,000).

Nimebaini kuwa mkataba kati ya Tanzania na bustani za wanyama za Marekani ulimalizika mnamo Juni 2020 na kuongezewa muda wa miaka miwili hadi Juni 2022. Japokuwa hakukuwa na mpango wowote wa kurudisha vyura hao Tanzania ikizingatiwa kuwa tayari miaka 22 imepita tangu vyura 500 wapelekwe kwenye bustani za wanyama za huko Marekani.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania kupitia Wizara ya Nishati na Wizara ya Maliasili na Utalii iweke mpango mkakati wa kurudisha vyura wa Kihansi ili kuepuka gharama kwa Shirika la Umeme Tanzania.**

### 5.2.4 Ongezeko la riba kwa kucheleweshwa malipo ya madai ya kampuni ya Pan Africa Energy Tanzania shilingi bilioni 113.84

Mkataba wa uuzaji wa gesi kati ya Shirika la Umeme Tanzania na Kampuni ya Pan African Energy Tanzania ambao unatumia kwa uzalishaji wa umeme katika Ubungo I, Ubungo III na Tegeta uliotiwa saini tarehe 17 Juni 2011 na unatarajia kumalizika Juni 2023, unabainisha riba itaongezeka kwa kiwango cha asilimia 4 zaidi ya kiwango cha LIBOR kila mwaka iwapo Shirika la Umeme Tanzania halitalipa kiasi kinachodaiwa kwa Kampuni na Pan African Energy Tanzania.

Katika ukaguzi wangu wa wadeni wa Shirika la Umeme Tanzania, nilibaini kuwapo kwa ankara za Kampuni ya Pan African Energy Tanzania ambazo hazijalipwa kwa miaka 10 (kuanzia 2012/13 hadi 2021/22) zenye thamani ya shilingi bilioni 246.74 ambayo inajumuisha riba ya malipo yaliyocheleweshwa ya shilingi bilioni

113.84. Hii imechangiwa na ukosefu wa fedha za kutosha kuwalipa watoa huduma, na kusababisha gharama kuongezeka kwa taasisi.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania, kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati litafute njia mbadala za ufadhili ili kuhakikisha malipo ya ankara za kila mwezi yanafanyika kwa wakati na kufanya mazungumzo na kampuni ya Pan African Energy Tanzania (PAET) ili isitishe tozo ya riba kwa malipo yanayofuata.**

### 5.2.5 Kampuni ya IPTL kuchelewa kukamilisha malipo kwa Serikali baada ya Serikali kushinda kesi - dola za Marekani milioni 148.4

Mwaka 1995, Kampuni ya Independent Power Tanzania (IPTL) na Shirika la Umeme Tanzania walitia saini Mkataba wa Kununua Nishati ya Umeme kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha umeme. Wakati wa usambazaji wa umeme, kulikuwa na mgogoro wa kiwango cha malipo ambao ulisababisha kufungua akaunti ya escrow mwaka 2006 kwa ajili ya kulinda malipo. Mwaka 2012 Shirika la Umeme Tanzania na Kampuni ya Independent Power Tanzania walimaliza mgogoro huo na kiwango cha fedha kutoka akaunti ya escrow zilipelekwa kwa Kampuni ya Pan African Power Solutions Tanzania ambaye ni mmoja wa wanahisa wa kampuni ya Independent Power Tanzania.

Kampuni ya Independent Power Tanzania ilikuwa na mkopo Benki ya Standard Chartered Hong Kong ambao kwa upande wao wanadai kuwa kampuni ya Pan African Power Solutions Tanzania walitumia baadhi ya fedha kutoka kwenye akaunti ya escrow kulipa hisa za kampuni ya VIP katika Kampuni ya Independent Power Tanzania, badala ya kutimiza wajibu wa malipo wa Shirika la Umeme Tanzania chini ya PAP na kulipa mkopo. Kwa sababu hiyo, mwaka 2016 Kituo cha Kimataifa cha Kutatua Migogoro ya Uwekezaji kiliamua kuwa Shirika la Umeme Tanzania lazima liilipe Benki ya Standard Chartered Hong Kong dola za Marekani milioni 148.4 pamoja na riba. Kufuatia uamuzi

huo, mnamo mwaka 2018 Serikali iliwasilisha kesi ya madai katika Mahakama Kuu ya Tanzania dhidi ya kampuni ya Independent Power Tanzania ili kutekeleza hati ya fidia iliyotiwa saini tarehe 27 Oktoba 2013 ambayo inalinda hatua ya Serikali kutoa fedha kwenye akaunti ya Escrow kutokana na madai ya wahusika wa nje. Uamuzi wa tarehe 1 Machi 2021 ulikuwa kwa upande wa Serikali na kampuni ya Independent Power Tanzania ilikubali kuilipa Serikali dola za Marekani milioni 148.4 mnmo tarehe 01 Machi 2021, hata hivyo hadi wakati wa ukaguzi, mwezi Disemba 2022, IPTL hawakuwa wamelipa kiasi kinachodaiwa.

Ni maoni yangu, ikiwa Serikali italipa madai ya Benki ya Standard Chartered Hong Kong kufuatia uamuzi wa Kituo cha Kimataifa cha Kutatua Migogoro bila kupata kiasi hicho kutoka kwa kampuni ya IPTL, itakuwa imefanya malipo mara mbili kwa kuwa malipo ya umeme tayari yalifanywa kwenye akaunti ya escrow, na kampuni ya IPTL ilitoa ahadi kupitia hati ya kulinda madai ambayo iliiondolea Serikali madai yoyote ya Benki ya Standard Chartered Hong Kong.

Nina mashaka kuwa kuchelewa kwa kampuni ya IPTL kulipa deni lake kunasababisha Serikali kuchelewa kupata fedha za kuilipa Benki ya Standard Chartered Hong Kong. Hali hii inapelekea kuongezeka kwa mkopo kwa sababu ya riba inayoongezeka hivyo kuchafua sifa ya nchi yetu katika jukwaa la kimataifa.

**Ninapendekeza kuwa, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umeme Tanzania, ichukue hatua kuhakikisha kampuni ya Independent Power Tanzania inakamilisha malipo ili kuepuka ongezeko la riba ya mkopo.**

### 5.2.6 Upungufu wa fedha unaoathiri utekelezaji wa mradi wa NGOZI uliopo chini ya kampuni ya Maendeleo ya Joto-ardhi Tanzania (TGDC)

Kampuni ya Maendeleo ya Jotoardhi ya Tanzania inaendeleza Mradi wa Joto-ardhi wa Ngozi Kusini Magharibi mwa Tanzania kwa kushirikiana na Mfuko wa Kupunguza Hatari za Joto-ardhi (GRMF)

na Serikali ya Tanzania. Sehemu ya pili ya mradi, ambayo inahusisha kuthibitisha rasilimali ya joto-ardhi, imeanza mnamo 05 Julai 2019 inatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 17.3 ambapo Mfuko wa GRMF umejitolea kuchangia shilingi bilioni 6.11 (dola za Marekani milioni 2.6), wakati Serikali ya Tanzania ilichangia shilingi bilioni 3.49 kati ya kiasi kinachotakiwa kuchangiwa cha shilingi bilioni 10.92 na hivyo kusababisha upungufu wa shilingi bilioni 7.43 kwenye mradi unaoendelea.Ni maoni yangu kuwa, kampuni ipo katika hatari ya kutokuwa na fedha za kukamilisha mradi na hivyo kupelekea mradi kutokamilika kwa wakati na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Ninapendekeza kuwa, TGDC iwasiliane na kampuni mama (Shirika la Umeme Tanzania) ili itafute fedha kutoka vyanzo vya ndani au nje ya nchi kuhakikisha mradi unakamilika, pamoja na kuepuka kuongezeka kwa gharama za mradi kutokana na riba kutoka kwa mkandarasi na mkandarasi mshauri kutokana na kuchelewa kwa mradi.**

## 5.3 Shirika la Reli Tanzania

Ukaguzi wangu wa ufanisi wa Shirika la Reli Tanzania ulibaini mapungufu yafuatayo;

### 5.3.1 Matukio ya ajali yanaathiri usafiri wa reli

Kuharibika kwa miundombinu ya reli ya zamani kunasababisha kutokea kwa ajali kubwa. Mapitio yangu ya ripoti za ajali kutoka 2019/20 hadi 2021/22 yalibaini kuwa kulitokea ajali kubwa 795 na sababu kuu zikiwa ni majanga ya asili kama mvua kubwa, na kuchelewa kufanya marekebisho makubwa ya miundombinu ya reli.

Nilibaini kutokana na ripoti za ajali, shirika limeingia gharama ya shilingi bilioni 1.70 kwa ajili ya kufanya marekebisho baada ya ajali, pia shirika lilipoteza mapato ya shilingi bilioni 4.36 kwa kusimamisha uendeshaji wa treni kwa takribani masaa 18,221.8 kama ilivyoripotiwa katika Ripoti za ajali za kampuni. Kusitisha

ratiba za treni kunaathiri taswira ya shirika na kusababisha usumbufu kwa wateja.

**Ninapendekeza kuwa, Shirika la Reli Tanzana liongeze hatua za usalama katika uendeshaji wa treni na kufanya marekebisho na matengenezo ya miundombinu yanayohitajika mara kwa mara ili kuepuka hatari za kutokea kwa ajali siku zijazo.**

### 5.3.2 Shirika la Reli Tanzania kuchelewa kuanza mradi wa ujenzi wa reli ya kusini

Moja ya malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa 2021/22 – 2025/26, ni pamoja na Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati na kuendelea kubadilika kuwa nchi ya viwanda yenye maendeleo ya juu ya binadamu au kiwango cha juu cha maisha. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa wa 2021/22-2025/26, unaainisha ujenzi wa Mradi wa Reli ya Kusini kama mradi mkuu unaolenga kufungua Ukanda wa Kusini kwa kuongeza kasi ya usafirishaji wa nje na kuwezesha ukuaji wa uchumi.

Kampuni ya Reli Tanzania (TRC) kama wakala wa utekelezaji wa mradi, iliingia makubaliano na mkandarasi mshauri kwa mkataba Na. PA/003/2013-13/C/15 kwa ajili ya upembuzi yakinifu na muundo wa awali wa ujenzi wa reli ya Mtwara - Songea - Mbambabay na matawi ya reli za Liganga na Mchuchuma. Upembuzi yakinifu na muundo wa awali ulikamilika mwezi Januari 2016, ambao unaonesha urefu wa njia ya mradi ya kilometa 997 na gharama za ujenzi zilizokadiriwa kuwa dola za Marekani bilioni 4.74. Hata hivyo, tangu mwaka 2016 ujenzi wa mradi huo bado haujaanza kutokana na kutopatikana kwa vyanzo vya fedha za kufadhili mradi huo wakati Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa umebakiza miaka mitatu kabla ya kukamilika ifikapo 2026.

**Ninapendekeza Shirika la Reli Tanzania liwasiliane na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mpango ili kubuni mpango wa ufadhili wa mradi wa reli ya**

**kusini ili kufanikisha ujenzi wa reli kwa gharama nafuu na kuendeleza usafiri endelevu kwa ukanda wa kusini.**

## 5.4 Shirika la Mawasiliano Tanzania

Ukaguzi wangu wa ufanisi katika uendeshaji wa Shirika la Mawasiliano Tanzania nilibaini mapungufu yafuatayo;

### 5.4.1 Vikwazo katika utekelezaji wa malengo ya mkakati ya Shirika la Mawasiliano Tanzania

Shirika la Mawasiliano Tanzania limekumbana na changamoto kadhaa katika kufikia malengo yake ya kimkakati. Shirika la Mawasiliano (kanda ya kati ya Dar es salaam) limeshindwa kufikia malengo ya kupata wateja 112,324 sawa na asilimia 73 ya lengo lililowekwa na shirika la kutakiwa kufikia wateja 152,950 kutokana na ukwasi.

Zaidi ya hayo, Shirika la Mawasiliano liko nyuma ya watoa huduma wengine wa simu za mkononi katika kukidhi viashiria muhimu vya utendaji 44 (asilimia 62.9) ikilinganishwa na viashiria muhimu vya utendaji 70 (100%) vya kimasoko na kushughulikia malalamiko ya wateja kufikia hadi siku 405 ambazo ni zaidi ya siku saba zinazohitajika. Malalamiko hayo yanaweza kusababisha kutofurahishwa kwa wateja na hasara. Masuala haya yanatokana na juhudi hafifu kuboresha biashara ya Shirika la Mawasiliano Tanzania, kuongeza  na kuwatunza wateja.

Aidha, ukaguzi wa bidhaa nane za Shirika la Mawasiliano Tanzania unaonesha kuwa bidhaa nne zilizopata faida, wakati bidhaa zingine nne zilipata hasara na kusababisha faida ya jumla kuwa aslimia 4  chini ya lengo la asilimia 5.1. Hii imetokana na kuwa na sehemu ndogo ya soko, gharama za kudumu, na ukosefu wa fedha za kutosha kuendana na  mabadiliko ya technolojia na mazingira ya biashara kwa sekta ya mawasiliano.

**Ninapendekeza Shirika la Mawasiliano Tanzania lijikite katika kuboresha mikakati ya kuongeza  na kuhifadhi wateja kwa**

**kuelekeza rasiliamali za kutosha kuboresha biashara. Shirika linapaswa pia kufanya uchambuzi madhubuti wa athari za biashara ili kuboresha ufanisi wa utendaji na kushughulikia malalamiko ya wateja kwa wakati.**

## 5.5 Mamlaka ya Bandari Tanzania

### 5.5.1 Kiwango kisichoridhisha cha ukaaji wa Meli, kugeuza Meli na muda wa kupakua mizigo katika bandari ya Dar es Salaam

Katika ripoti yangu ya mwaka 2020/21, niliripoti kuhusu kushindwa kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania kupunguza muda wa kusubiri na kuondoka kwa mizigo. Katika ukaguzi wangu kwa mwaka 2021/22 nilibaini kiwango kisichofaa kwa; ukaaji wa meli, kugeuza meli na muda wa kupakua mizigo ulikuwa juu ya lengo la siku 1.58, wakati muda wa kugeuza meli ulikuwa karibu mara mbili ya lengo, wakati kiwango cha nafasi ya bandari kwa kituo cha mafuta kimekuwa juu kidogo kuliko lengo lililowekwa, ikionesha msongamano na mizigo ya jumla ikiwa chini ya asilimia 50.

Hali hii imechangiwa na sababu mbalimbali kama mizigo ya miradi ya kimkakati kuchukua muda mrefu kutolewa bandarini kutokana na muda mrefu wa kufuatilia vibali kutoka kwenye mamlaka za Serikali kama vile, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Shirika la Viwango Tanzania. Sababu zingine zinajumuisha, eneo la kuhifadhi mizigo hutumiwa na wateja wakubwa wanaotumia eneo la bandari kama kituo salama cha kuhifadhi mizigo yao na kusababisha ucheleweshaji wa kutoa mizigo hiyo; muda mrefu wa msamaha uliotolewa kwa baadhi ya nchi; kuharibika mara kwa mara wa vifaa; na uhaba wa waendeshaji hasa waendeshaji wa matrekta ya kituo, hali ambayo imesababisha ongezeko la gharama za bandari kwa kampuni za usafirishaji na wateja.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Bandari ya Tanzania kuchukua hatua stahiki ikiwemo kuboresha mitambo na vifaa vya bandarini, kuongeza ushindani, na kuwezesha bandari kavu ya**

**Kwala kufanya kazi ili kupunguza msongamano wa mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam.**

### 5.5.2 Kutoanza kazi kwa mradi wa bandari ya Nyamirembe wenye thamani ya Shilingi bilioni 4.13

Ukaguzi wangu wa miradi iliyotekelezwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania kwenye bandari za Ziwa Victoria, nilibaini kukamilika kwa ujenzi wa gati, ghala la mizigo, jengo la abiria, ukuta na uzio pamoja na miundombinu mingine katika Bandari ya Nyamirembe mnamo tarehe 29 Novemba 2019 iliyopo Mkoa wa Geita chini ya mkataba Na. AE/016/2017-18/CTB/W/19 uliosainiwa tarehe 24 Agosti 2018 kwa gharama ya shilingi bilioni 4.13 pamoja na kodi ya ongezeko la thamani.

Hata hivyo, nilipotembelea eneo la mradi tarehe 03 Agosti 2022 nilibaini hakukuwa na shughuli zozote za biashara zinazofanyika katika Bandari ya Nyamirembe na hili lilisababishwa na kutofanyika kwa upembuzi yakinifu wa kina kabla ya utekelezaji wa mradi huo.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Bandari Tanzania (a) kuhakikisha kuwa upembuzi yakinifu unafanyika kwa kila mradi ili kuisaidia Mamlaka kufanya maamuzi sahihi na (b) kuweka mikakati ya kuhakikisha bandari ya Nyamirembe inafanya kazi kikamilifu na kuleta faida kwa Mamlaka na Taifa.**

### 5.5.3 Kuchelewa kutekelezwa kwa mradi wa kituo cha pamoja cha kupokelea mafuta

Mradi wa kituo cha kupokelea mafuta kwa pamoja ulibuniwa baada ya sekta ya mafuta kukabiliwa na changamoto ya bei iliyochangiwa na ucheleweshaji wa kupakuwa mafuta kutoka kwenye meli na kupelekea gharama za kuhifadhi mafuta bandarini kuongezeka hivyo kuongeza bei ya mafuta nchini. Wadau wa sekta ya mafuta walipendekeza kuanzishwa kwa kituo kimoja cha kupokelea mafuta kwa lengo la kupunguza gharama za kuagiza na kusambaza mafuta ya petroli, kuboresha

uwajibikaji kwa watendaji, kupunguza upotevu na udanganyifu, na kupunguza gharama za muda wa kukaa bandarini.

Mpango wa mradi ni kujengwa matanki 15 ya kupokelea mafuta yenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya mita za ujazo 600,000 kwa makisio ya shilingi bilioni 177.47 na ujenzi wa gati kwa makisio ya shilingi bilioni 140.36 katika eneo la Mbwamaji Kigamboni. Hadi wakati wa ukaguzi wangu Juni 2022, mchakato wa kupata ardhi ulikuwa bado unaendelea.

Kwa maoni yangu kuchelewa kuanzisha kituo cha pamoja cha kupokelea mafuta kunachelewesha kufikiwa kwa malengo na faida zilizolengwa ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama kwa makampuni ya mafuta na kushuka kwa bei ya mafuta.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Bandari Tanzania ifanye mawasiliano na Wizara ya Ardhi kuhakikisha upatikanaji wa ardhi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.**

## 5.6 Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo

Mapitio yangu katika Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) nilibaini mapungufu yafuatao:

### 5.6.1 Ukarabati usioridhisha wa majengo na miundombinu ya viwanda 467 vya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO)

Wakati wa ukaguzi wangu, nilibaini kuwa majengo 467 ya Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo yako katika hali isiyoridhisha, huku majengo 443 yakitumika. Uongozi wa Shirika ulifanikiwa kukarabati majengo matatu kati ya manne yaliyopangwa katika mwaka wa fedha 2021/22 kwa gharama ya shilingi milioni 730.48. kutokana na ukosefu wa fedha za ukarabati majengo 24 hayatumiki, hivyo shirika kupoteza kiasi cha shilingi milioni 118.64 kwa mwaka kama kodi kwani inabidi shirika likapange kwenye majengo mengine .

### 5.6.2 Kupungua kwa fedha za mikopo kwa biashara ndogo na za kati kwa asilimia 43

Wakati wa ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022, nilibaini kuwa shirika lilitoa aslimia 57 kati ya maombi 4,745 ya mikopo yaliyowasilishwa, kutoka wa viwanda vidogo na wajasiriliamali wadogo kwa kiasi cha shilingi bilioni 6.41 na kuacha asiliamia 43 kutohudumiwa mpaka kufikia Juni 2022. Hali hiyo ilisababisha ongezeko la mahitaji ya mkopo kwa wajasiriliamali wadogo ikilinganishwa na uwezo wa mfuko.

### 5.6.3 Ukarabati usioridhisha wa vituo vya maendeleo ya teknolijia kwa ajili ya kukuza teknolojia ya viwanda nchini:

Ripoti ya menejimenti ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kwa kipindi cha 2021/22 inaonesha kuwa shirika lilipanga kufufua vituo vya maendeleo ya teknolojia katika kila mkoa ili kukuza teknolojia na maendeleo ya viwanda. Hata hivyo, hadi tarehe 30 Juni 2022, SIDO ilikuwa na vituo saba tu vya maendeleo ya Teknolojia vinavyofanya kazi katika mikoa saba tu, huku mikoa 19 ikiwa na vituo visivyofanya kazi kutokana na kutokidhi mahitaji ya mitambo; vifaa vya uzalishaji vilivyopitwa na wakati, upungufu wa rasilimali watu, na mtaji mdogo wa uendeshaji hivyo kuweka kizingiti katika uzalishaji wa bidhaa mpya na uundwaji wa michakato mipya ya uzalishaji.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo liandae mkakati wa kukusanya fedha na kuwasiliana na serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya viwanda na miundombinu inayokadiriwa kugharimu shilingi bilioni 25.5; kuhudumia wafanyabiashara wengi wenye uwezo wa kutoa mikopo; na kufufua vituo vya Maendeleo ya Teknolojia vilivyopo katika mikoa 19 iliyosalia.**

## 5.7 Shirika la Nyumba la Taifa

### 5.7.1 Usimamizi usioridhisha wa mkataba wa ubia kati ya Kampuni ya Al-Karimo Investment na Shirika la Nyumba la Taifa

Mwaka 2004, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) liliingia ubia na kampuni ya Al-Karimo Investment Limited kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ghorofa 10 la kibiashara na makazi, Dar es Salaam kwenye viwanja viwili vya NHC kwa faida ya kibiashara na madhumuni mengine kama yalivyokubaliwa kwenye mkataba na Mbia anaefadhili mradi huo. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi, kasoro kadhaa zilibainika ikiwa ni pamoja na: mradi kutokamilika kwa zaidi ya miaka 17; Mbia alijumuisha kiwanja chake kwenye mradi bila ridhaa ya NHC, na ujenzi ulifanyika kwenye viwanja vitatu badala ya viwili vilivyotolewa na Shirika.Pia, nilibaini mbia alitumia kiwanja chake kuchukua mkopo katika Benki ya Kimataifa ya Biashara (ICB) kwa ajili ya ujenzi wa mradi lakini alishindwa kulipa mkopo huo, deni likifikia kiasi cha dola za Marekani milioni 2.35 sawa ( sawa na shilingi bilioni 5.47).

**Ninapendekeza Shirika la Nyumba (a) lifanye usimamizi na ufuatiliaji wa kutosha na wa mara kwa mara katika uwekezaji wake wote wa ubia, na (b) liwasiliane na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupata ushauri kutokana na mapungufu yaliyojitokeza katika utekelezaji wa mkataba huu wa ubia na hatima yake kwa maslahi mapana ya taifa.**



# SURA YA SITA

# USIMAMIZI WA MAPATO NA FEDHA KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

## 6.0 Utangulizi

Usimamizi wa mapato na fedha ni muhimu kwa mashirika ya umma na taasisi zingine ili kufikia malengo yao. Inahusisha taratibu zote muhimu za kupanga na kudhibiti mapato kwa ufanisi. Usimamizi mzuri wa mapato kupitia upangaji sahihi wa mapato ni muhimu kwa mashirika ya umma na taasisi zingine kwani inahakikisha ukusanyaji wa kutosha wa fedha za kukidhi majukumu ya kifedha ya muda mfupi na mrefu.

Sura hii inaangazia sehemu mbalimbali za usimamizi wa mapato katika mashirika ya umma na taasisi zingine. Pia inaangazia mapungufu katika usimamizi wa mapato ikiwa ni pamoja na mapungufu katika sera na mifumo isiyoridhisha ya usimamizi wa kifedha, pamoja na ukusanyaji wa mapato usiyoridhisha.

## 6.1 Mapungufu katika ukusanyaji na usimamizi wa mapato

Usimamizi na ukusanyaji wa mapato unajumuisha kuwapo kwa mifumo ya uthibiti na utekelezaji wa taratibu zilizowekwa katika ukusanyaji wa mapato. Mapitio yangu yalibaini mapungufu katika ukusanyaji na usimamizi wa mapato katika mashirika ya umma na taasisi zingine:

### 6.1.1 Tozo za bandari zilizofanyika nje ya mifumo ya bili katika Mamlaka ya Bandari Tanzania shilingi bilioni 13.5

Mamlaka ya Bandari Tanzania hutoa ankara/bili kupitia mfumo wa kuhudumia shehena unaojulikana kama (TOS) na mfumo wa

maombi unaojulikana kama (POAs) ili kufanya malipo ya huduma za bahari na mizigo. Hata hivyo, nilibaini ankara/bili huandaliwa kupitia mifumo ambayo haijaunganishwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kuwezesha kujua kiasi cha kodi ya ongezeko la thamani kinachopaswa kukusanywa. Kwa mwaka wa fedha uliopita, Mamlaka ya Bandari Tanzania iliripoti kiasi cha shilingi bilioni 13.5 ambacho ankara zake zilitengenezwa nje ya mfumo. Katika mahojiano na menejimenti nilibaini kuwa mifumo hiyo ilikuwa imeundwa kwa mapato ya uendeshaji tu wa Mamlaka ya Bandari, na siyo kwa mapato mengine yoyote.

Ninaamini kuwa, kuna hatari ya upotevu wa mapato kutokana na makosa yanaweza kutokea kutokana na uandaaji wa ankara nje ya mfumo.

**Ninapendekeza kuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania ihakikishe kuwa utoaji wa ankara za mapato yote ya uendeshaji zinatolewa kupitia mfumo wa bili wa malipo na pia mfumo huu utengamanishwe na mifumo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kuweza kuhakiki kodi inayostahili kulipwa.**

### 6.1.2 Huduma za uchimbaji ambazo hazina uthibitisho wa hati ya kazi zilizofanyika zenye thamani ya shilingi bilioni 13.30

Kwa mwaka wa fedha 2021/22, mashine za uchimbaji za Shirika la Taifa la Madini (STAMICO) zilizalisha mapato ya shilingi bilioni 30.85 (asilimia 41) ya jumla ya mapato ya kampuni ya shilingi bilioni 75.35.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa Shirika la Taifa la Madini lilitoa huduma za uchimbaji kwa mgodi wa dhahabu wa Geita unaojulikana kama Geita Gold Mine zenye thamani ya shilingi bilioni 22.30, ambapo huduma za uchimbaji zenye thamani ya shilingi bilioni 13.30 zilithibitishwa tu kwa ankara na risiti za malipo, hata hivyo, kulikuwa hakuna hati zinazoonesha kiasi cha kazi kilichofanywa na mashine hizo, ambapo ni kinyume cha kifungu cha 29 cha mkataba wa kazi kati ya pande mbili.

Maoni yangu ni kuwa, kuna mapungufu katika kudhibiti na kupitia kazi zilizofanywa na ankara zilizotolewa kutokana na kutokuwepo kwa cheti cha kazi chenye maelezo ya kina.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Taifa la Madini liimarishe udhibiti wa huduma za uchimbaji ambao utahakikisha ankara zinatolewa baada ya uhakiki wa kazi iliyofanywa pamoja na cheti cha kazi kilichothibitishwa kwa undani na kusainiwa na pande zote mbili kwenye mkataba.**

### 6.1.3 Ukusanyaji wa mapato nje ya mfumo wa malipo ya kielektroniki ya serikali shilingi bilioni 3.32

Mwongozo wa Msajili wa Hazina Na. 3 wa 2017, pamoja na Mwongozo wa Utendaji wa Kawaida wa mfumo wa malipo ya kielektroniki ya Serikali toleo 1.1 la Novemba 2019, uliotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango, unahitaji pesa zote za umma kukusanywa kupitia mfumo wa malipo ya kielektroniki ya Serikali.

Katika ukaguzi wangu wa udhibiti na usimamizi wa ukusanyaji wa mapato, nilibaini mashirika matano yaliyoorodheshwa kwenye **Jedwali Na. 11** yalikusanya mapato yenye thamani ya shilingi bilioni 3.32 nje ya mfumo wa malipo ya kielektroniki ya Serikali kinyume na Mwongozo wa Msajili wa Hazina Na. 3 wa mwaka 2017.

**Jedwali Na. 11: Orodha ya mashirika yaliyokusanya mapato nje ya mfumo**

| S/n | Jina la Taasisi | (Sh. Milioni) |
|---|---|---|
| 1 | Kituo cha Ushauri cha Taasisi cha Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam | 2,870.00 |
| 2 | Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Dawa | 232.16 |
| 3 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kyela | 183.22 |
| 4 | Bodi ya Korosho Tanzania | 33.71 |
| 5 | Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania | 2.27 |
| **Jumla** | | **3,321.36** |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa taarifa za fedha zilizokaguliwa, 2021/22*

Aidha, nilibaini kuwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Kyela iliiomba kufungua akaunti za ukusanyaji wa mapato katika benki ya NMB na CRDB kwa barua zenye kumbukumbu namba UWAS/MB/F.362/44 na UWAS/MB/F.362/44 za tarehe 29 Disemba 2021. Barua inaeleza kuwa akaunti hizo zingeweza kurahisisha ukusanyaji wa mapato kupitia mfumo wa malipo ya kielektroniki wa Serikali. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi mwezi Februari 2023, akaunti hizo hazikufunguliwa hivyo makusanyo ya mapato yalifanyika nje ya mfumo wa malipo ya kielektroniki ya serikali.

Ninaamini kuwa, kushindwa kukusanya mapato kupitia mfumo wa Malipo ya Kielektroniki wa Serikali kunaathiri ufanisi wa udhibiti wa mapato. Kwa hivyo, taasisi zote za serikali na biashara lazima zitumie mfumo wa Malipo ya Kielektroniki wa Serikali ili kuongeza ufanisi.

**Ninapendekeza kuwa taasisi za umma zilizotajwa zihakikishe kuwa mapato yote yanakusanywa kupitia mfumo wa Malipo ya Kielektroniki wa Serikali.**

### 6.1.4 Kutokufanya mapitio na kutoidhinishwa kwa kiwango cha kodi ya wapangaji

Wakati wa ukaguzi wangu wa Shirika la Nyumba la Taifa, Shirika la Reli Tanzania na Shirika la Mawasiliano Tanzania, nilibaini kuwa mashirika haya hayakufanya utafiti wa soko ili kuhuisha viwango vyao vya kodi. Hali hii inapelekea kutoza kodi kwa kiwango cha chini na kupoteza mapato.

Kiwango cha sasa cha Shirika la Nyumba la Taifa kinachotumika kiliidhinishwa mwaka 2011 na hakijafanyiwa mapitio kwa kuzingatia mabadiliko ya kiwango cha mfumuko wa bei na hali ya soko kwa miaka 10 iliyopita. Vivyo hivyo, nilibaini kuwa Shirika la Reli Tanzania liliripoti mapato ya kodi ya pango ya jumla ya shilingi bilioni 1.4 kwa mwaka wa fedha 2021/22, ambapo mapato ya kodi ya shilingi milioni 783 (asilimia 56) yalikusanywa bila sera ya upangishaji. Kwa kesi ya Shirika la Mawasiliano

Tanzania, nilibaini kuwa kiwango cha kodi kwa mwaka wa fedha 2021/22 kilitofautiana na kiwango kilichotozwa katika 2020/21. Hata hivyo, hakukuwa na idhini ya bodi kwa mabadiliko ya viwango hivyo.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Nyumba la Taifa, Shirika la Reli Tanzania, na Shirika la Mawasiliano Tanzania wafanye utafiti huru wa soko ili kubaini kiwango cha sasa cha kodi ya soko. Pia, wanapaswa kupata idhini ya bodi kabla ya kutumia viwango vipya ili kuepuka kutoza kodi chini ya kiwango cha soko la sasa na kupunguza mapato ya shirika.**

## 6.2 Usimamizi wa Fedha

Usimamizi wa fedha unajumuisha kuzingatia udhibiti wa msingi na taratibu za ukusanyaji na upatanishi wa akaunti za benki. Ukaguzi wangu katika eneo hili, ulibaini yafuatayo:

### 6.2.1 Fedha zisizotumika katika benki shilingi bilioni 7.35 katika Bohari Kuu ya Dawa

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2022 katika Bohari Kuu ya Dawa, nilibaini akaunti tatu za benki kwenye benki ya NMB na akaunti mbili katika benki ya TCB zilizowekwa pesa ili kurahisisha malipo ya mkopo kwa wauzaji mbalimbali wa vifaa vya matibabu kutoka nje kama inavyohitajika na mikataba ya ununuzi.

Ukaguzi ulibaini kuwa mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 7.35 kati ya Bohari Kuu ya Dawa na wazalishaji mbalimbali wa vifaa vya matibabu ilikuwa imepita muda wake kwa zaidi ya miaka miwili (2019/20 hadi 2021/22) na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 2.52 na shilingi bilioni 4.83 kwa NMB na TCB mtawaliwa bado fedha hizo zilikuwa benki bila kutumiwa na Bohari Kuu ya Dawa.

Ninaamini kuwa, hakuna udhibiti wa kuridhisha juu ya usimamizi wa fedha kwani fedha zilizosalia benki zingeweza kusaidia Bohari

Kuu ya Dawa kutekeleza shughuli zingine za dharula ikiwa ni pamoja na kununua dawa na vifaa vya matibabu.

**Ninapendekeza kuwa Bohari Kuu ya Dawa iondoe fedha zote zilizosalia benki na kuzitumia kusaidia shughuli zingine za Bohari Kuu ya Dawa ikiwa ni pamoja na ununuzi wa dawa na vifaa vya matibabu.**

### 6.2.2 Akaunti za Benki zilizositishwa zenye kiasi cha shilingi bilioni 20.65

Ukaguzi wangu wa usimamizi wa akaunti za benki ulibaini kuwa kuna taasisi nne za umma zenye akaunti zilizositishwa zikiwa na salio la pesa **(Jedwali Na. 12).**

**Jedwali Na. 12: Akaunti zilizositishwa zinazosimamiwa na taasisi za umma.**

| S/N | Jina la Taasisi | Idadi ya namba za akaunti | Fedha zilizomo (Sh. Million) | Haitumiki tangu mwaka |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Bandari Tanzania | 10 | 20,208.00 | 2020/21 |
| 2 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi Wa Mazingira Dar es Salaam | 4 | 417.76 | 2020/21 |
| 3 | Kampuni ya Ndege Tanzania | 1 | 23.26 | 2019/20 |
| 4 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha. | 7 | 1.16 | 2020/21 |
| | **Jumla** | | **20,650.18** | |

***Chanzo:*** *Uchambuzi wa taarifa za fedha zilizokaguliwa, 2021/22*

Zaidi ya hayo, Mamlaka ya Bandari Tanzania ina akaunti moja katika benki ya CRDB yenye Namba 0250800929000 yenye kiasi cha dola za Marekani milioni 20.05 nchini Burundi, ambayo haikutumiwa katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22 kutokana na ukosefu wa watia saini. Hali hiyo ilijitokeza pia katika akaunti za benki za Eco zilizopo Kongo, Zambia, na

Rwanda. Akaunti zisizotumika zinaweza kutumiwa kwa shughuli haramu/udanganyifu. Pia, fedha zilizopo benki zingeweza kutumiwa kwa shughuli za Mamlaka.

**Ninapendekeza kuwa mashirika na taasisi zingine zifanye kila jitihada kuhakikisha kuwa akaunti zote za benki ambazo hazitumiki zinafungwa bila kuchelewa ili kuepuka hatari ya matumizi mabaya ya fedha na gharama zisizo za lazima za benki.**

### 6.2.3 Watumishi waliohamishwa waliendelea kuwa waidhinishaji wa fedha katika akaunti za benki za Mamlaka ya Bandari Tanzania

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022, Mamlaka ya Bandari Tanzania ilikuwa na waidhinishaji wa akaunti zake 12 za benki, ambao hawakuwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Bandari baada ya kuhamishiwa kwenye taasisi zingine za Serikali.

Ni maoni yangu kuwa mapungufu yaliyobainika yanatokana na ukosefu wa mipango ya usimamizi ya kuteua waidhinishaji wa akaunti kwa wakati, hivyo kuongeza hatari ya wafanyakazi wasio wa Mamlaka ya Bandari kutoa fedha bila kujulikana na kuidhishwa na Mamlaka.

**Ninapendekeza kuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania ihakikishe benki zote zina waidhinishaji waliothibitishwa kuwa ni wafanyakazi wa Mamlaka ya Bandari na kuwajulisha benki mara moja kuhusu mabadiliko yanayohusiana na waidhinishaji wa akaunti za benki.**

## 6.3 Udhibiti wa madeni yatokano ya biashara na madeni mengine

Udhibiti wa madeni unajumuisha kufuata udhibiti wa msingi na taratibu za ukusanyaji na makubaliano na wadeni wao. Mapitio yangu yalibainisha udhaifu ufuatao kuhusu udhibiti wa madeni katika mashirika ya umma na taasisi zingine:

### 6.3.1 Madeni yasiyothibitishwa na yasiyoweza kurejeshwa shilingi bilioni 7.51 katika Shirika la Mawasiliano Tanzania

Nilibaini kuwa Shirika la Mawasiliano Tanzania lilikuwa na madeni makubwa yenye thamani ya shilingi bilioni 21 ambayo uongozi haukuweza kutambua wadaiwa husika, katika kiasi hiki Shirika la Mawasiliano Tanzania lilitoa mapendekezo kwa Bodi ya Shirika kufuta deni la shilingi bilioni 7.51.

Ninaamini kuna uwezekano kuwa madeni yasiyothibitishwa yalikuwa ni madeni hewa, hivyo kunauwezekano wa madeni yasiyokuwa na nyaraka yamejumuishwa kwenye kitabu cha mahesabu.

**Ninapendekeza Shirika la Mawasiliano Tanzania liombe kibali kutoka kwa Msajili wa Hazina na Wizara ya Fedha na Mipango ili kufuta madeni ambayo hayawezi kurejeshwa.**

### 6.3.2 Utoaji wa vyeti vya kuhitimu na nakala za matokeo kwa wanafunzi 423 wenye deni la shilingi milioni 456.50

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa Chuo Kikuu cha Dodoma kiliwapa vyeti vya kuhitimu na nakala za matokeo ya masomo wanafunzi 423 ambao bado walikuwa na deni la shilingi milioni 456.50 kwa Chuo. Hii ni kinyume na kifungu namba 20.3 cha kanuni za chuo kwa Programu za Shahada ya kwanza ambazo zinahitaji ofisi inayohusika kutoa vyeti na nakala za matokeo ya masomo kwa wanafunzi baada ya kupata taarifa za kifedha za wanafunzi zilizothibitishwa na mhasibu wa Chuo kuonesha malipo yote ya ada zinazotakiwa kulipwa kwa Chuo kuwa zimelipwa.

**Ninapendekeza kuwa Chuo Kikuu cha Dodoma kihakikishe (a) takwimu za wanafunzi wote katika mfumo wa usimamizi wa rekodi za wanafunzi zinaunganishwa na mfumo wa kifedha ili kuhakikisha hakuna mwanya kwa wanafunzi kupata vyeti na nakala za matokeo ya masomo bila kulipa ada zao, na (b) ifuatilie hatua zote muhimu ili kurejesha fedha zote kutoka**

**kwa wanafunzi waliopewa vyeti na nakala za matokeo ya masomo wakati wakiwa na madeni.**

### 6.3.3 Kiasi kikubwa cha madai yenye thamani ya shilingi trilioni 3.58

Nimepitia malimbikizo ya madai kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022 katika mashirika ya umma na taasisi zingine 206. Nilibaini kuwa taasisi za umma 97 zilikuwa na madai yasiolipwa yaliyofikia shilingi trilioni 3.58 yanayohusiana na huduma zilizotolewa kwa wateja **(Kiambatisho Na VI).** Suala hili niliripoti pia katika ripoti ya fedha ya mwaka 2020/21 ambapo mashirika ya umma na taasisi zigine 93 zilikuwa na ukusanyaji duni wa madai yaliyofikia kiasi cha shilingi trilioni 3.71. Malimbikizo ya madeni yasiyolipwa yanaendelea kuathiri mapato ya taasisi na uwezo wa kutekeleza shughuli zilizopangwa.

(i) Nilibaini kuwa, sehemu kubwa ya madeni ya muda mrefu ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania ya shilingi bilioni 378.09 yalikuwa ni mauzo ya gesi ambayo hayajalipwa na Shirika la Umeme Tanzania, ambayo ni shilingi bilioni 354.99 sawa na asilimia 94 ya deni lote ambalo halijalipwa. Mwenendo wa deni unaonesha kuongezeka kwa deni la Shilika la Umeme Tanzania kila mwaka. Kwa maoni yangu, madai ya muda mrefu ambayo hayajalipwa yanasababishwa na Shilika la Umeme Tanzania kushindwa kulipa ankara zake kwa wakati, hali inayosabisha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kukosa fedha za kuwekeza katika sekta ya gesi na mafuta.

(ii) Kufikia tarehe 30 Juni 2022, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ilikuwa na madai ya shilingi bilioni 611 ambayo yakikuwa yameiva lakini hayajakusanywa. Mikopo iliyoiva haijakusanywa kutokana na kukosekana kwa ufanisi katika ukusanyaji na kutokuwepo kwa mfumo wa kushirikisha wadau muhimu kama vile Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Wakalaka wa Vitambulisho vya Taifa, Wakala wa Mapato Tanzania, Wakala wa Usajili wa Biashara na

Leseni na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi.

(iii) Katika Bohari Kuu ya Dawa, mapitio yangu ya deni linalodaiwa la shilingi bilioni 375.11 nilibaini kuwashilingi bilioni 255.66 zinahusiana na taasisi za Serikali ambazo hazijalipwa kwa miaka minne. Fedha hizi zingeweza kutumiwa kununua vifaa vya matibabu ili kuwezesha utoaji wa huduma za afya.

(iv) Katika Shirika la Nyumba Tanzania, nilibaini kuwa jumla ya shilingi bilioni 19.92 kati ya shilingi bilioni 22.62 zilitokana na wapangaji waliohama.

Nilibaini kuwa malimbikizo ya madeni ya muda mrefu yalisababishwa na juhudi ndogo za ukusanyaji wa madeni, malimbikizo ambayo wateja hawawezi kupatikana, madeni yasiyothibitishwa, na kutolipwa kwa madeni na taasisi za serikali kwa muda mrefu.

**Ninapendekeza kuwa mashirika na taasisi zingine zilizotambuliwa (a) ziboreshe na kudhibiti ukusanyaji wa madai ikiwa ni pamoja na hatua za kisheria kuhakikisha kuwa wadeni wote wanamaliza madeni yao bila kucheleweshwa; na(b) wawasiliane na Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhusu malimbikizo ya madeni ya muda mrefu yanayosababishwa na taasisi za serikali.**



# SURA YA SABA

# USIMAMIZI WA MATUMIZI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

## 7.0 Utangulizi

Matumizi katika mashirika ya umma na taasisi zingine yanapaswa kuzingatia bajeti, sera za ndani na nje ya shirika, nyaraka, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya matumizi. Kwa kiasi kikubwa matumizi hulenga katika kugharamia shughuli za kawaida na za maendeleo kulingana na majukumu ya shirika husika.

Matumizi ya kawaida hujumuisha mishahara ya watumishi, posho na marupurupu mengine; na manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali za uendeshaji na usimamizi wa shirika husika. Matumizi ya maendeleo yanajumuisha ununuzi na ujenzi wa mali za kudumu zinazoshikika na zisizoshikika, mitambo na vifaa.

Ukaguzi wangu katika usimamizi wa matumizi kwenye mashirika ya umma na taasisi zingine ulihusisha tathmini ya kubainisha kama matumizi yanafanyika kwa kuzingatia bajeti, sera, nyaraka, sheria na kanuni mbalimbali za matumizi zilizoidhinishwa.

Katika mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022 nilibaini mapungufu kadhaa na kutoa mapendekezo ili kuboresha na kuimarisha usimamizi wa matumizi katika mashirika ya umma kama nilivyoeleza kwenye aya zinazofuata.

## 7.1 Matumizi yasiyokuwa na tija ya jumla ya shilingi bilioni 63.77

Nilibaini kuwa mashirika ya umma 12 katika ukaguzi wa kawaida na ukaguzi maalumu yamefanya matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 63.77 ambayo hayakuwa na tija na manufaa ya kiuchumi kwa shirika na Serikali kwa sababu gharama hizo zingeweza kuepukwa kwani zinatokana na malimbikizo ya riba na adhabu za malipo ya fedha kwa kuchelewa kulipa madai ya wakandarasi na wadai wengine, hukumu za mahakama zilizoamulu shirika husika kulipa riba na fidia, na mashirika kutokuwa makini kuhakiki na kukata malipo ya awali kwenye ankara kabla ya kulipa madai ya wakandarasi ama wazabuni.

Pia, baadhi ya mashirika yameiingia mikataba yenye masharti yasiyotekelezeka, hivyo kusababisha ongezeko la gharama, kutozwa riba na adhabu zisizo na tija kwa shirika husika na serikali. Hali hii inapelekea upotevu wa rasilimali za umma na kuathiri ufanisi wa mashirika husika katika kutekeleza majukumu yake. Orodha ya mashirika yenye matumizi yasiyokuwa na tija imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 13.**

**Jedwali Na. 13: Mashirika yenye matumizi yasiyokuwa na tija**

| Na. | Jina la Shirika/Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Umeme Tanzania | Adhabu na riba kwenye malipo yaliyocheleweshwa | 37,318.77 |
| 2 | Mamlaka ya Bandari Tanzania | Fidia na riba kwenye malipo yaliyocheleweshwa | 20,100.00 |
| 3 | Bohari Kuu ya Dawa | Malipo kwa vifaa ambavyo havikuletwa na malipo ya kumtafuta mzabuni hewa | 2,022.66 |
| 4 | Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL | Adhabu na gharama za utunzaji kwa kuchelewesha kukamilika kwa taratibu za malipo | 1,777.92 |
| 5 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | Adhabu na riba kwenye malipo yaliyocheleweshwa | 1,773.68 |
| 6 | Shirika la Mawasiliano Tanzania | Malipo ambayo hayajarejeshwa baada ya mkataba kuvunjika | 345.65 |
| 7 | Kampuni ya Mkulazi | Riba kwenye malipo yaliyocheleweshwa ya kodi | 151.48 |
| 8 | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi | Riba kwenye malipo yaliyocheleweshwa ya kodi za ardhi | 132.56 |

| Na. | Jina la Shirika/Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|
| 9 | Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro | Gharama za makontena yaliyocheleweshwa kurudishwa | 117.50 |
| 10 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza | Riba kwenye malipo yaliyocheleweshwa | 21.01 |
| 11 | Shirika la Madini la Taifa | Riba kwenye malipo yaliyocheleweshwa ya kodi | 11.96 |
| 12 | Baraza la Taifa la Ujenzi | Riba kwenye malipo yaliyocheleweshwa ya kodi ya ardhi | 0.83 |
| | | **Jumla kuu** | **63,774.02** |

***Chanzo*:** Taarifa za ukaguzi kwa kila shirika kwa mwaka 2021/22

**Ninapendekeza kuwa mashirika ya umma na taasisi zake yafanye uhakiki na uchambuzi wa kina wa kanuni na masharti ya mikataba na kushirikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri kuhusiana na masuala ya kisheria kwenye mikataba husika; kuandaa na kutekeleza mikakati halisi ya usimamizi wa mtiririko wa fedha ili kuwezesha ulipaji wa madeni yaliyoiva kwa wakati; na vyombo vyenye mamlaka ya usimamizi wa mashirika tajwa kuongeza uangalizi na usimamizi wa malipo ili kuzuia matumizi yasiyo na tija.**

## 7.2 Matumizi yasiyostahili ya shilingi bilioni 77.75

Nilibaini mashirika 21 katika ukaguzi wa kawaida na ukaguzi maalumu yamefanya matumizi yasiyostahili yenye jumla ya shilingi bilioni 77.75 ambayo yalitokana na malipo ya posho kwa watumishi wasiostahili, malipo yasiyokuwa na uthibitisho na vielelezo vya matumizi husika. Orodha ya mashirika ya umma na taasisi zingine zenye matumizi yasiyostahili imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 14.**

**Jedwali Na. 14: Mashirika ya umma yenye matumizi yasiyostahili**

| Na. | Jina la Shirika/Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|
| 1 | Bohari Kuu ya Dawa | Malipo ya utangulizi pasipo kuwa na mkataba, na malipo yasiyokuwa na vithibitisho | 65,337.16 |
| 2 | Shirika la Viwango Tanzania | Malipo zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa, na malipo ya posho ya hatari ambayo hayajaidhinishwa na Msajili wa Hazina | 8,598.58 |

| Na. | Jina la Shirika/Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|
| 3 | Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania | Malipo yasiyokuwa na vithibitisho | 2,426.41 |
| 4 | Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania (Ukaguzi Maalum) | Malipo ya nyongeza ya mshahara kinyume na utaratibu, posho isiyostahiki ya kuhamishwa kituo cha kazi na masurufu yasiyokuwa na vielelezo na viambatisho | 489.63 |
| 5 | Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko | Malipo yasiyokuwa na vithibitisho | 237.75 |
| 6 | Shirika la Nyumba la Taifa | Malipo ya posho ya nyumba na umeme kwa watumishi wasiostahili | 150.30 |
| 7 | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Ukaguzi Maalum) | Matumizi ambayo hayana vielelezo na vithibitisho | 111.25 |
| 8 | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Sekta Binafsi | Malipo ya kodi ya Ardhi kwa kipindi ambacho Mfuko haukuwa na Umiliki | 59.33 |
| 9 | Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba | Malipo yasiyokuwa na vithibitisho | 50.00 |
| 10 | Shirika la Umeme Tanzania | Malipo ya bima ya wakurugenzi ambayo hayajaidhinishwa na Msajili wa Hazina | 48.59 |
| 11 | Chuo cha Uhasibu Arusha | Malipo zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa | 41.10 |
| 12 | Chuo cha Tekinolojia Dar es Salaam | Masurufu yaliyorejeshwa bila vithibitisho | 32.00 |
| 13 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza | Malipo ya posho kwa watumishi wasiostahili | 56.78 |
| 14 | Bodi ya Nyama Tanzania | Malipo yasiyokuwa na vithibitisho | 29.40 |
| 15 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tabora | Malipo yasiyokuwa na vithibitisho | 23.12 |
| 16 | Bodi ya Usajili wa Wahandisi | Malipo yasiyokuwa na vithibitisho | 15.93 |
| 17 | Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo | Malipo yasiyokuwa na vithibitisho | 11.79 |
| 18 | Chuo Kikuu cha Dodoma | Malipo ya posho zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa | 11.52 |
| 19 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | Malipo zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa kwa wazabuni | 6.07 |
| 20 | Chuo cha Diplomasia | Masurufu yaliyorejeshwa bila vithibitisho | 5.50 |
| 21 | Kampuni ya Mbolea Tanzania | Posho zilizolipwa zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa | 4.80 |

| Na. | Jina la Shirika/Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|
| Jumla kuu | | | 77,747.01 |

***Chanzo***: Taarifa za ukaguzi kwa kila shirika kwa mwaka 2021/22

**Ninapendekeza mashirika ya umma na taasisi zingine yahakikishe fedha zilizotumika isivyo stahili kutokana na matumizi haya zinarudishwa kwenye shirika husika, na kuimarisha miongozo ya ndani ili kuhakikisha sera, kanuni na sheria za matumizi zinafuatwa ipasavyo. Pia, ninashauri vyombo vyenye mamlaka ya usimamizi wa mashirika tajwa kuongeza usimamizi wa matumizi ikiwa ni pamoja na kuimarisha udhibiti wa mifumo ya ndani na kuwawajibisha Maafisa Masuuli husika.**

## 7.3 Malimbikizo ya madeni ya jumla ya shilingi trilioni 7.65

Madeni ni madai halali ambayo bado hayajalipwa kwa bidhaa, kazi ama huduma zilizotolewa kwa mashirika ya umma na taasisi zingine.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mashirika  ya umma 99 yana madeni ya jumla ya shilingi trilioni 7.65. Taarifa za kina za madeni ya muda mrefu kwa kila shirika zimeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. VII**

Baadhi ya mashirika hayo yanakabiliwa na changamoto za ukwasi usiojitosheleza kutokana na ukosefu wa fedha za kutosha kulipa kwa wakati madeni yaliyoiva hali ambayo inatokana na aidha ucheleweshwaji wa fedha kutoka serikalini, kutofanya vizuri kwa biashara zao, au kutokuwa na mikakati yenye ufanisi katika usimamizi wa mtiririko wa fedha.

Kuchelewa kulipa kwa wakati madeni yaliyoiva kunashusha hadhi na kuharibu taswira ya mashirika ya umma na Serikali. Pia, wazabuni wanaweza kukataa kutoa huduma au kutoa huduma kwa masharti magumu kwa mashirika husika hivyo kuathiri utendaji wa shughuli za kila siku za mashirika hayo. Aidha, ucheleweshaji wa malipo kwa muda mrefu husababisha riba na

adhabu ambazo zinakuwa na gharama za ziada na zisizokuwa na tija.

**Ninapendekeza kuwa mashirika ya umma na taasisi zingine (a) ziweke na kutekeleza mpango mkakati madhubuti wa usimamizi wa mtiririko wa fedha na utekelezaji wake ili kuhakikisha madeni ya muda mrefu yanalipwa mapema iwezekanavyo na kwa siku zijazo madeni yote yalipwe kwa wakati; na (b) kwa madeni yanayohitaji ruzuku ya Serikali, Serikali ihakikishe fedha zinatengwa na kupelekwa kwa wakati kwenye mashirika ya umma na taasisi husika ili kulipa madeni hayo.**

## 7.4 Masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu ya shilingi bilioni 3.51

Kanuni ya 96 hadi 103 ya Kanuni za Fedha za Umma, (GN/Na.132/2001) inatoa muongozo juu ya usimamizi wa masurufu ambayo pia imeakisiwa katika kanuni za kifedha za mashirika ya umma husika, kama vile masurufu kurejeshwa ndani ya siku saba hadi 14 baada ya kukamilika kwa shughuli husika; na kutotoa masurufu mengine kabla ya kutoa vielelezo vya uthibitisho vya matumizi ya masufuru ya awali; na ikitokea kushindwa kutoa vielelezo vya uthibitisho wa matumizi basi muhusika hutakiwa kurejesha fedha au kukatwa kwenye malipo ya mshahara wake.

Ukaguzi umebaini kwamba mashirika ya umma 31 yalikuwa na masurufu yenye jumla ya shilingi bilioni 3.51 ambazo hazijarejeshwa kwa kipindi cha mwezi mmoja hadi zaidi ya mwaka mmoja kinyume na muongozo tajwa hapo juu. **Jedwali Na. 15** limeorodhesha mashirika hayo na muda wa ucheleweshaji.

Vilevile, nilibaini kwamba, mashirika ya umma tajwa hayakuwa yamechukua hatua madhubuti za urejeshwaji wa masurufu, kama vile kukata marejesho ya masurufu kutoka kwenye mishahara ya watumishi waliopewa masurufu hayo.

**Jedwali Na. 15: Mashirika ya umma yenye masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu**

| Na. | Jina la Shirika/Taasisi | Kiasi (Sh. Milioni) |
|---|---|---|
| 1 | Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania | 844.68 |
| 2 | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 543.47 |
| 3 | Mamlaka ya Udhibiti wa Bima Tanzania | 332.64 |
| 4 | Bohari Kuu ya Dawa | 273.75 |
| 5 | Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania | 256.18 |
| 6 | Shirika la Posta Tanzania | 126.05 |
| 7 | Shirika la Utangazaji Tanzania | 107.9 |
| 8 | Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo | 104.72 |
| 9 | Chuo Kikuu Mzumbe | 92.06 |
| 10 | Chuo cha Sukari cha Taifa | 85.71 |
| 11 | Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Dawa | 84.79 |
| 12 | Kituo cha Kompyuta Chuo Kikuu cha Dar es Salaam | 68.63 |
| 13 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Songea | 62.83 |
| 14 | Chuo Kikuu Huria cha Tanzania | 57.58 |
| 15 | Kampuni ya Mkulazi | 57.02 |
| 16 | Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere | 56.39 |
| 17 | Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka | 45.61 |
| 18 | Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania | 43.35 |
| 19 | Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari | 41.7 |
| 20 | Bodi ya Kahawa Tanzania | 35.53 |
| 21 | Shirika la Umeme Tanzania | 32.8 |
| 22 | Shirika la Viwango Tanzania | 30.43 |
| 23 | Chuo cha Diplomasia | 27.31 |
| 24 | Shirika la Uwekezaji Watumishi Housing | 22.44 |
| 25 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tabora | 18.59 |
| 26 | Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania | 16.41 |
| 27 | Bodi ya Pareto Tanzania | 15.32 |
| 28 | Bodi ya Nyama Tanzania | 12.73 |
| 29 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga | 6.38 |
| 30 | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima | 4.66 |
| 31 | Baraza la Rufaa za Kodi | 2.4 |
| | **Total** | **3,510.06** |

***Chanzo***: *Taarifa za ukaguzi kwa kila shirika kwa mwaka 2021/22*

Kutokurejeshwa kwa masurufu kwa wakati siyo tu kunaweza kusababisha upotevu wa fedha za umma, bali pia inapelekea kupotosha taarifa za fedha kwa kuripoti masurufu ambayo hayajarejeshwa kama madai wakati huenda kazi au matumizi

tayari yamekwisha kamilika na hivyo kuripoti matumizi kidogo tofauti na uhalisia.

**Ninapendekeza mashirika ya umma na taasisi zingine (a) yaimarishe na kuboresha usimamizi wa masurufu na kuhakikisha yanarejeshwa kwa wakati; na (b) kwa masurufu yasiyorejeshwa kwa wakati iwepo mifumo thabiti ya kuhakikisha masurufu hayo yanarejeshwa kwa kukatwa moja kwa moja kwenye mishahara ya watumishi husika.**

## 7.5 Kuchelewa kulipa michango ya kisheria kwa mifuko ya hifadhi za jamii ya shilingi bilioni 131.80

Sehemu hii inaelezea michango ya kisheria iliyocheleweshwa na mashirika ya umma na taasisi zingine kwa mifuko mitatu ambayo ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Michango hiyo inapaswa kuwasilishwa ndani ya mwezi mmoja baada ya siku ya mwisho ya mwezi wa mchango husika.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mashirika ya umma 11 yalichelewa kuwasilisha michango yao ya kila mwezi kwa mifuko hiyo ya hifadhi ya jamii yenye jumla ya shilingi bilioni 131.80 kwa kipindi cha kuanzia mwezi mmoja na zaidi ya mwaka. Taarifa na maelezo zaidi nimezionesha kwenye **Jedwali Na. 16**

**Jedwali Na. 16: Mashirika ya umma yaliyochelewesha michango ya kisheria**

| Na. | Jina la Shirika/Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh. Milioni) | Muda wa kuchelewa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Reli Tanzania | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi | 127,800.00 | Zaidi ya mwezi 1 |
| 2 | Hospitali ya Taifa Muhimbili | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Bima ya Afya | 2,639.03 | Zaidi ya mwezi 1 |
| 3 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tabora | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi na Mfuko wa Bima ya Afya | 708 | Mwezi 1 hadi miezi 84 |
| 4 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma | 203.36 | Zaidi ya mwezi 1 |

| Na. | Jina la Shirika/Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh. Milioni) | Muda wa kuchelewa |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma | 132.81 | Mwezi 1 hadi miezi 3 |
| 6 | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma | 129.69 | Mwezi 1 hadi miezi 15 |
| 7 | Kituo cha Kompyuta Chuo Kikuu cha Dar es Salaam | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma | 80.33 | Mezi 1 hadi miezi 7 |
| 8 | Kampuni ya Mkulazi | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi | 75.58 | Mwezi 1 hadi miezi 5 |
| 9 | Chuo cha Usafirishaji cha Taifa | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma | 32.15 | Miezi zaidi ya 12 |
| 10 | Chuo cha Ufundi Arusha | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma | 1.9 | Mwezi 1 hadi miezi 2 |
| 11 | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma | 1.74 | Mwezi 1 hadi miezi 11 |
| | **Jumla** | | **131,804.59** | |

***Chanzo***: *Taarifa za ukaguzi kwa kila shirika kwa mwaka 2021/22*

Kuchelewa kuwasilisha michango ya kisheria kunatokana na ukosefu wa fedha za kutosha au kutumia fedha za michango kwenye matumizi mengine ya taasisi badala ya kulipia michango hiyo kwa wakati, na pia menejimenti kutoweka kipaumbele cha kuzingatia matakwa ya kisheria.

Ucheleweshwaji huu unasababisha mashirika ya umma husika kutozwa riba na adhabu ambazo zinakuwa matumizi yasiyokuwa na tija. Vilevile, mapungufu haya yanaharibu sifa na taswira ya shirika na Serikali kwa ujumla.

Aidha, michango ya kisheria iliyocheleweshwa kwa muda mrefu inawanyima wanufaika wa huduma za mifuko kupata huduma stahiki kwa wakati na kwa viwango tarajiwa vya ubora.

**Ninapendekeza kuwa mashirika husika yahakikishe yanafuata kikamilifu sheria na kanuni za mifuko husika na kuwasilisha kwa wakati michango ya kisheria kwa mifuko husika.**

## 7.6 Matumizi yasiyofaa ya fedha za Mfuko wa Miundombinu ya Reli Shilingi bilioni 195.99

Kifungu cha 68 (9) cha Sheria ya Reli, Sura 170 kinaeleza kuwa, matumizi ya fedha kutoka Mfuko wa Miundombinu ya Reli yanapaswa kutumika kwa ajili ya matumizi ya kiutawala yanayohusiana moja kwa moja na uendeshaji na usimamizi wa reli, pamoja na kufadhili ukarabati na maendeleo ya miundombinu iliyopo na utoaji wa miundombinu mipya ya reli.

Vilevile, kifungu cha 3 (1) cha Sheria ya Reli, Sura 170 kinafafanua, "miundombinu ya reli" kama vifaa ambavyo vinatumika kuendesha reli, njia za reli na njia zingine na miundo mingine inayohusiana (kama vile, mahandaki, madaraja, vituo, majukwaa, mitaro, matuta), miundombinu ya chini na juu, barabara za huduma, mifumo ya ishara, mfumo wa udhibiti wa hisa, matangazo ya mifumo ya mawasiliano na ishara, mifumo ya usambazaji wa umeme na majengo yanayohusiana, maghala, yadi, mashine na vifaa, lakini haijumuishi mabehewa".

Mapitio ya matumizi ya fedha zilizokusanywa chini ya Mfuko wa Miundombinu ya Reli, nilibaini kuwa Shirika la Reli Tanzania lilipewa kibali na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kununua mabehewa na vipuri vyake vyenye jumla ya shilingi bilioni 195.99. Hata hivyo, vitu hivyo havikupaswa kugharamiwa na fedha za Mfuko kwa sababu siyo sehemu ya miundombinu ya reli kama ilivyofafanuliwa kwenye kifungu cha 3 (1) kikisomwa kwa pamoja na kifungu cha 68 (9) cha Sheria ya Reli, Sura 170.

**Ninapendekeza Shirika la Reli Tanzania lipendekeze marekebisho ya Sheria ya Reli, Sura 170 kama kuna haja ya kuingiza vipengele vingine vinavyotokana na biashara ya reli ili viweze kugharamiwa chini ya fedha za Mfuko wa Miundombinu ya Reli, ili kuimarisha usimamizi mzuri wa lengo kuu la Mfuko.**

## 7.7 Malipo ambayo hayajathibitishwa yaliyofanywa na Hifadhi za Taifa Tanzania shilingi bilioni 1.99

Katika ukaguzi maalumu niliofanya katika Hifadhi za Taifa Tanzania nilibaini mapungufu yafuatayo;

### (i) Kushindwa kuthibitisha uhalali na usahihi wa malipo ya jumla shilingi bilioni 1.95

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Hifadhi za Taifa Tanzania ilibainisha utekelezaji wa majukumu na malipo mbalimbali yenye jumla ya Shilingi bilioni 1.95 yaliyofanyika kupitia hati za malipo 40, lakini usahihi na uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitishwa kutokana na kukosekana kwa nyaraka sahihi za viambatanisho licha ya kuorodhesha majina ya waliolipwa. Mbali na utekelezaji usiothibitishwa wa majukumu hayo, jumla ya Shilingi bilioni 1.34 zilionyeshwa kupokelewa na watumishi mbalimbali kupitia hati za malipo zilizosainiwa, huku jumla ya Shilingi milioni 611.55 zikishindwa kuthibitishwa kuwa zimepokelewa na watumishi husika. Hifadhi za Taifa Tanzania imepata hasara ya Shilingi bilioni 1.95 kama malipo ambayo matumizi yake hayakuweza kuthibitishwa.

**Ninapendekeza menejimenti ya Hifadhi za Taifa Tanzania kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa.**

### (ii) Posho zilizolipwa zaidi na juu ya viwango vilivyoidhinishwa shilingi milioni 38.72

Nilibaini kuwa Hifadhi za Taifa Tanzania imeweka miongozo ya matumizi yenye kumbukumbu Na. BE.38/340/01/01 na Kumbukumbu Na. BE.38/340/01/02 ambayo imeweka viwango vya posho za kazi na posho za honoraria zilizotakiwa kuanza kutumika kuanzia tarehe 1 Mei 2017 na 9 Julai 2018, mtawalia. Pamoja na utoaji wa miongozo hiyo, nilibaini kuwa Hifadhi za Taifa Tanzania ililipa posho mbalimbali za wafanyakazi jumla ya shilingi milioni 38.72

zaidi ya viwango vilivyoainishwa katika miongozo hiyo. Pia nilibaini kuwa malipo haya yalifanyika kwa wafanyakazi mbalimbali kwa fedha taslimu badala ya akaunti za benki katika miaka ya fedha 2019/20 na 2020/21.

**Ninapendekeza menejimenti ya Hifadhi za Taifa Tanzania kuhakikisha udhibiti wa malipo kwa kuzingatia viwango halisi na kama ilivyoainishwa katika miongozo.**




# SURA YA NANE

# USIMAMIZI WA BAJETI KATIKA TAASISI ZA UMMA

## 8.0 Utangulizi

Usimamizi wa bajeti ni muhimu ili kuhakikisha mashirika ya umma na taasisi zingine zinafanya matumizi kwa kufuata sheria ya bajeti na kanuni zake, miongozo na maelekezo kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Lengo kuu la usimamizi wa bajeti ni kusaidia utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na kufikia malengo yaliyowekwa katika Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa taifa 2021/22 hadi 2025/26.

Sura hii inaeleza umuhimu wa usimamizi bora wa bajeti pamoja na ushirikishwaji wa wadau muhimu katika kuandaa na kutekeleza bajeti, utoaji wa ruzuku kutoka serikalini, utoaji sahihi wa taarifa za bajeti na kuhakikisha rasilimali zinatumika kwa ufanisi katika kufanikisha malengo ya taasisi husika.

## 8.1 Utoaji usiotosheleza wa fedha za ruzuku za serikali shilingi bilioni 161.88

Katika mapitio ya taarifa za utekelezaji wa bajeti za mashirika ya umma na taasisi zingine, nilibaini kuwa mashirika 18 kati ya mashirika 184 (bila kujumuisha mashirika ya kibiashara ya serikali) ambayo hutegemea ruzuku ya serikali, yalipokea jumla ya shilingi bilioni 382.43 sawa na asilimia 70 ya fedha zote za bajeti zilizoidhinishwa ambazo ni shilingi bilioni 544.31. Hivyo kusababisha upungufu wa fedha wa jumla ya shilingi bilioni 161.88 sawa na asilimia 30 **(Jedwali Na.17).**

Utoaji hafifu wa ruzuku za serikali unaweza kusababisha taasisi hizi kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, Aidha inaweza kuzorotesha utoaji wa huduma kwa umma. Pia kunaweza kusababisha miradi kuchelewa au kutokamilika hivyo kushindwa kufikia malengo ya shirika.

**Jedwali Na. 17: Kiasi cha ruzuku ya fedha ambacho hakikutolewa na serikali kwa mashirika ya umma**

| Na. | Jina la Taasisi | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.milioni) | Kiasi Kilichotolewa (Sh. Milioni) | Nakisi Ya Bajeti (Sh. Milioni) | Asilimia ya Nakisi ya Bajeti (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Singida | 2,000 | 153 | 1,847 | 92% |
| 2 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kahama Shinyanga | 2,516 | 400 | 2,116 | 84% |
| 3 | Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam | 9,131 | 2,426 | 6,705 | 73% |
| 4 | Chuo Kikuu Ardhi | 51,401 | 16,907 | 34,494 | 67% |
| 5 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mtwara | 8,782 | 3,152 | 5,630 | 64% |
| 6 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga | 2,470 | 1,078 | 1,392 | 56% |
| 7 | Shirika la Viwango Tanzania | 31,348 | 14,332 | 17,016 | 54% |
| 8 | Chuo cha Usafirishaji cha Taifa | 34,201 | 17,856 | 16,345 | 47% |
| 9 | Ofisi ya Taifa ya Takwimu | 226 | 127 | 99 | 44% |
| 10 | Baraza la Michezo Tanzania | 1,427 | 856 | 571 | 40% |
| 11 | Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili | 85,558 | 52,260 | 33,298 | 39% |
| 12 | Hospitali ya Taifa Muhimbili -Mloganzila | 21,402 | 14,660 | 6,742 | 32% |
| 13 | Bodi ya Usajili wa Wahandisi | 1,172 | 860 | 312 | 27% |

| Na. | Jina la Taasisi | Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.milioni) | Kiasi Kilichotolewa (Sh. Milioni) | Nakisi Ya Bajeti (Sh. Milioni) | Asilimia ya Nakisi ya Bajeti (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 14 | Mamlaka ya Udhibiti wa Soko la Mitaji | 708 | 532 | 176 | 25% |
| 15 | Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi | 1,879 | 1,463 | 416 | 22% |
| 16 | Shirika la Habari la Taifa | 24,288 | 19,397 | 4,891 | 20% |
| 17 | Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam | 19,874 | 17,565 | 2,309 | 12% |
| 18 | Hifadhi za Taifa Tanzania | 245,925 | 218,405 | 27,520 | 11% |
| | Jumla | **544,309** | **382,429** | **161,880** | |

**Chanzo:** Taarifa za fedha 2021/22

**Ninapendekeza kuwa, Serikali ihakikishe fedha za ruzuku zilizoidhinishwa katika bajeti zinatolewa kwa ukamilifu ili kuwezesha utekelezaji wa kazi zilizopangwa na kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya mashirika ya umma na taasisi zingine.**

## 8.2 Ukusanyaji pungufu wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani shilingi bilioni 174.63

Mashirika ya umma hukusanya mapato kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani kama vile ada, mauzo, mapato ya uwekezaji, na vyanzo vingine, ambavyo hutumiwa kwa matumizi ya kawaida katika taasisi. Mapato haya yanajulikana kama mapato ya vyanzo vya ndani.

Mapitio ya taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2022, nilibaini kuwa mashirika ya umma 50 kati ya 184 (bila kujumuisha mashirika ya kibiashara) yalikusanya shilingi bilioni 364.49 sawa na asilimia 68 ya fedha zote za bajeti ya mapato ya vyanzo vya ndani ambayo ni shilingi bilioni 539.12.

Aidha, jumla ya shilingi bilioni 174.63 sawa na asilimia 32 ya fedha za bajeti ya mapato ya nyanzo vya ndani, hazikukusanywa **(Kiambatisho Na. VIII).**

Sababu za upungufu katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani ni pamoja na kushindwa kukusanya mapato baada ya kutoa huduma. Kwa mfano mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira zinakabiliwa na changamoto za kukusanya madeni kutoka kwa wateja wao baada ya huduma kutolewa, haswa taasisi za serikali, hii ni kutokana na ukosefu wa mita za malipo ya kabla ya upokeaji huduma. Pia, kukosekana kwa mfumo thabiti kwa mamlaka za udhibiti katika kukusanya ada za kila mwaka kutoka kwa mashirika yanayohusika na mamlaka hizo.

Mapato yasiyokusanywa husababisha upungufu wa fedha ambazo zilipangwa kufanya shughuli zilizokusudiwa.

**Ninapendekeza kuwa, Mashirika ya umma na taasisi zingine zifanye tathimini kamili katika mifumo yao ya ukusanyaji wa mapato ili kuweza kutambua maeneo dhaifu na kukuza mikakati ya kuboresha ukusanyaji wa mapato.**

## 8.3 Mapungufu katika matumizi ya mfumo wa bajeti wa PlanRep katika usimamizi wa bajeti za mashirika ya umma

Katika ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha, nilibaini kuwa mashirika ya umma 13 kati ya 206 hayakutumia/ walitumia kwa kiwango kisichoridhisha cha mfumo wa bajeti wa PlanRep kinyume na Aya 163 na 166 ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mipango na Bajeti ya Mwaka 2021/22 **(Jedwali Na. 18)**. Mfumo wa bajeti wa PlanRep uliundwa kama nyenzo ya kufanya makisio ya mapato na matumizi, tathimini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa bajeti katika mashirika ya umma.

Mapungufu hayo yanasababishwa na kukosekana kwa utengamanishi kati ya mfumo wa bajeti wa PlanRep na mifumo ya uhasibu ya mashirika ya umma. Hata hivyo kukosekana kwa utengamanishi huko pia kuna sababishwa na mageresho (GFS code)

ya kibajeti ya kwenye mfumo wa bajeti wa PlanRep kutofautiana na mageresho yaliyopo kwenye mifumo ya uhasibu ya taasisi. Pia, kukosekana kwa ujuzi juu ya matumizi ya mfumo huo.

**Jedwali Na. 18: Mashirika ya umma yenye mapungufu katika matumizi ya mfumo wa bajeti wa planrep**

| Na. | Jina la taasisi | Hali ya matumizi ya mfumo |
|---|---|---|
| 1. | Kampuni ya Ndege Tanzania | Hawatumii |
| 2. | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati | Hawatumii |
| 3. | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | Haitoshelezi |
| 4. | Bodi ya Bima ya Amana | Hawatumii |
| 5. | Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya | Haitoshelezi |
| 6. | Kampuni ya Mkulanzi | Hawatumii |
| 7. | Taasisi ya Mifupa Muhimbili | Haitoshelezi |
| 8. | Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania | Haitoshelezi |
| 9. | Shirika la Nyumba la Taifa | Haitoshelezi |
| 10. | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma | Haitoshelezi |
| 11. | Shirika la Umeme Tanzania | Hawatumii |
| 12. | Shirika la Mawasiliano Tanzania | Haitoshelezi |
| 13. | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi | Haitoshelezi |

**Chanzo:** Taarifa za ukaguzi 2021/22

Kukosekana kwa utengamanishi wa mifumo hiyo inapelekea mapungufu katika kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha ambazo zinaweza kudhoofisha usahihi na kuaminika kwa taarifa hizo. Hii inaweza pia kusababisha ugumu katika tathimini na udhibiti wa bajeti, ambayo inaweza kuwa na athari kubwa kwa ugawaji wa rasilimali kwa ufanisi.

Kwa mfano, kukosekana kwa utengaminishi wa mifumo kulipelekea Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam kuwa na matumizi ya zaidi ya shilingi bilioni 1.46 ya kiwango cha bajeti kilichoidhinishwa.

**Ninapendekeza kuwa, mashirika ya umma (a) yawasiliane na Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha utengamanishi thabiti kati ya mfumo wa bajeti wa PlanRep na mifumo ya uhasibu ya mashirika ya umma ili kufanya tathmini na**

**usimamizi wa bajeti; na (b) kuhakikisha watumishi wanaohusika na mfumo huo wanapewa mafunzo ili kuongeza ufanisi katika matumizi yake.**

## 8.4 Utekelezaji usioridhisha katika majukumu ya kamati za bajeti

Kamati za bajeti zina wajibu katika kutathmini utekelezaji wa bajeti na mgawanyo wa rasilimali kulingana na vipaumbele vya mpango mkakati na vipaumbele vya Kitaifa kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 17(3) cha Kanuni ya Bajeti ya mwaka 2015. Miongoni mwa changamoto zilizobainishwa katika Mwongozo wa mwaka 2019/20 ni pamoja na kamati za bajeti kutoshiriki kikamilifu katika uandaaji na utekelezaji wa bajeti.

Nilibaini mapungufu katika utendaji wa kamati za bajeti katika mashirika ya umma 13, ambapo baadhi ya mashirika ya umma hayakua na kamati za bajeti kama ilivyoelezewa kwenye **(Jedwali Na.19).** Kutoshirikishwa huko kunatokana na ukosefu wa hatua za uwajibikaji kuhusu kuhusisha au kutokuhusisha kamati ya bajeti katika maamuzi au michakato ya bajeti.

**Jedwali Na. 19: Mashirika ya umma yenye utekelezaji usioridhisha katika majukumu ya kamati za bajeti**

| Na. | Jina la Taasisi | Mapungufu yaliyobainika |
|---|---|---|
| 1. | Taasisi ya Mifupa Muhimbili | Kamati ya bajeti ilikutana mara mbili kwa mwaka 2021/22 na haikufanya tathimini katika taarifa za utekelezaji wa bajeti |
| 2. | Kampuni ya Stamigold | Hakuna kamati ya bajeti |
| 3. | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi | Hakuna kamati ya bajeti |
| 4. | Kampuni ya Uendelezaji wa Joto-ardhi Tanzania | Hakuna kamati ya bajeti |
| 5. | Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania | Hakuna kamati ya bajeti |
| 6. | Chuo cha Diplomasia | Kamati ya bajeti haikukutana kwa mwaka 2021/22 |
| 7. | Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam | Hakuna Kamati ya bajeti |
| 8. | Chuo cha Uhasibu Arusha | Kamati ya bajeti ilikutana mara moja kwa mwaka 2021/22 na haikufanya |

| Na. | Jina la Taasisi | Mapungufu yaliyobainika |
|---|---|---|
| | | tathimini katika taarifa za utekelezaji wa bajeti |
| 9. | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Njombe | Kamati ya bajeti haikukutana kwa mwaka 2021/22 |
| 10. | Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania | Kamati ya bajeti haikukutana kwa mwaka 2021/22 |
| 11. | Bodi ya Utalii Tanzania | Hakuna kamati ya bajeti |
| 12. | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bariadi | Hakuna kamati ya bajeti |
| 13. | Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibaiolojia Tanzania | Hakuna kamati ya bajeti |

***Chanzo***: *Taarifa za ukaguzi 2021/22*

Nina shaka na ufanisi wa kamati za bajeti katika uandaaji wa bajeti ambapo inaweza kupelekea kushindwa kufanya tathimini ya utekelezaji wa bajeti.

**Ninapendekeza mashirika ya umma kuhakikisha kamati za bajeti zinawajibika katika kuhakikisha zinatekeleza majukumu yao ipasavyo.**

## 8.5 Matumizi ya fedha za mashirika ya umma na taasisi zingine zaidi ya kiwango cha bajeti kilichoidhinishwa shilingi bilioni 118.04 bila idhini

Nilipitia taarifa za utekelezaji wa bajeti na kubaini kuwa mashirika ya umma saba yalifanya matumizi ya shilingi bilioni 118.04 **(Jedwali Na. 20)** zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa kwenye bajeti.

Hii inahusishwa na mapungufu katiba kudhibiti matumizi ya fedha zilizopangwa.Kwa mfano mapungufu katika mifumo ya kusimamia na kudhibiti utekelezaji wa bajeti ambapo hupelekea matumizi zaidi ya fedha ambazo zingeweza kutumiwa kwa shughuli zingine.

Matumizi hayo ya zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa katika bajeti yanakwamisha utekelezaji kamili wa shughuli zingine zilizopangwa kufanyika kwa kutumia fedha hizo kwa mwaka husika.

**Jedwali Na. 20: Mashirika ya umma yaliofanya matumizi zaidi ya kiwango cha bajeti kilichoidhinishwa**

| Na. | Jina la Taasisi | Bajeti iliyoidhinishwa (Shilingi milioni) | Matumizi halisi (Shilingi milioni) | Matumizi yaliyozidi (Shilingi milioni) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Umeme Tanzania (Bajeti ya mafuta ya mitambo ya umeme) | 490,537.30 | 594,755 | 104,218.7 |
| 2 | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 143,992.94 | 152,625 | 8,632.06 |
| 3 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi Wa Mazingira Dar es Salaam | 138,451.32 | 139,911 | 1,460.68 |
| 4 | Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila (Matumizi ya utawala) | 1,945.75 | 3,182.36 | 1,236.61 |
| 5 | Shirika la Posta Tanzania (Matumizi ya utawala | 3,746 | 4,961 | 1,214.58 |
| 6 | Mamlaka ya Bandari Tanzania (Kuajiri vibarua wa mkataba) | 903.01 | 1997.59 | 1,094.58 |
| 7 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Nzega(Matumizi ya maendeleo na Utawala) | 1116.82 | 1299.42 | 182.60 |
| | **Jumla** | **780,693.14** | **898,731.37** | **118,038.23** |

**Chanzo:** Taarifa za ukaguzi 2021/22

**Ninapendekeza kuwa mashirika ya umma kuweka udhibiti ambao utahakikisha uzingatiaji wa sheria na miongozo ya bajeti kikamilifu hii ni pamoja na kuandaa sera, taratibu na tathimini za mara kwa mara**




# SURA YA TISA

# USIMAMIZI WA MIKATABA NA UNUNUZI

## 9.0 Utangulizi

Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2011 Sura 410 na kanuni zake inazitaka taasisi na mashirika ya umma kuzizingatia sheria wakati wa kufanya shughuli za ununuzi na usimamizi wa mikataba.

Ili kuhakikisha usimamizi wa mikataba na manunuzi ya umma yanafanyika kwa ufanisi kwa kuzingatia sheria zilizowekwa na kanuni zake, Serikali iliamua kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma na kuipa jukumu la kusimamia, na kudhibiti shughuli za manunuzi ili kukuza uchumi na kuleta ufanisi katika matumizi ya fedha za umma, usawa, haki na uwazi na kupata thamani ya fedha. Ili kuhakikisha uwazi katika manunuzi, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ilianzisha mfumo wa ununuzi (TANePS) ambapo mchakato wa manunuzi wa mashirika na taasisi zingine za umma unatakiwa kufanywa kupitia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki.

Nilifanya ukaguzi wa uzingatiaji wa michakato ya ununuzi wa kazi za ujenzi, bidhaa na huduma katika mashirika na taasisi zingine za umma na kutoa mahitimisho kuhusu kuzingatia na kufuata sheria. Yafuatayo ni mapungufu na mapendekezo yaliyotolewa:

## 9.1 Mapungufu katika usimamizi wa mikataba

Ukaguzi wangu wa usimamizi wa mikataba umebaini madhaifu yafuatao:

## a) Kuchelewa kukamilika kwa miradi yenye thamani ya shilingi bilioni 8.23

Nimepitia miradi mitano yenye thamani ya shilingi bilioni 8.23 na kubaini kuchelewa kukamilika kwa miradi kuanzia miezi mitatu hadi miaka mitano kama inavyooneshwa kwenye **(Jedwali Na. 21).** Ucheleweshaji huo umesababishwa na ukosefu wa fedha, usimamizi hafifu wa mikataba, na ucheleweshaji wa kutoa vibali.

**Jedwali Na. 21: Orodha ya taasisi zilizochelewa kukamilisha miradi**

| Jina la Taasisi | Jina la Mradi | Kiasi cha Mkataba Sh. (Milioni) | Tarehe ya Kukamilisha | Muda wa Kuchelewa |
|---|---|---|---|---|
| Chuo cha Diplomasia | Ujenzi wa kumbi za mihadhara | 3,379.06 | 30-Disemba-20 | Miezi 17 |
| Shirika la Viwango Tanzania | Ujenzi wa ofisi na kivuli cha ukaguzi wa magari | 1,609.83 | 14-Novemba-21 | Miezi 7 |
| Hifadhi za Taifa Tanzania | Kukarabati kilomita 70 kutoka Naabi-Ndutu-Kusini na kilomita 40 kutoka Duma Ranger Post-Vilima Rasta katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. | 1,520.83 | 24-Julai-22 | Miezi 3 |
| Bohari Kuu ya Dawa | Upanuzi wa mpango mkuu wa nishati | 1,074.61 | 24-Juni-16 | Miaka 5 |
| Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro | Ugavi, Ufungaji wa Mfumo wa maegesho ya magari | 647.75 | 16-Novemba-21 | Mienzi 11 |
| | **Jumla** | **8,232.08** | | |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi, 2021/22*

Nina wasiwasi kuwa ucheleweshaji wa kukamilika kwa miradi hiyo kunasababisha kuchelewa kupatikana kwa matokeo yaliyokusudiwa na pia kuna hatari zingine zinazohusiana na ucheleweshaji kama vile migogoro na wakandarasi, kuharibu sifa na kuongezeka kwa gharama.

### b) Kuchelewa kuwasilisha bidhaa zilizonunuliwa zenye thamani ya shilingi bilioni 18.09

Ukaguzi wangu wa mikataba ya ununuzi wa bidhaa na huduma katika mwaka huu wa ukaguzi, ulibaini ucheleweshaji wa bidhaa na utoaji wa huduma kutoka kwa wazabuni wenye thamani ya shilingi bilioni 18.09 katika mashirika ya umma 12 kwa kipindi kati ya siku 22 hadi miezi 16 kinyume na Kanuni ya 114 (b) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 na muda uliokubaliwa katika mikataba iliyosainiwa. Maelezo zaidi yanatolewa katika **Jedwali Na. 22.**

**Jedwali Na. 22: Taasisi zilizochelewa kupokea bidhaa**

| Na | Jina la Taasisi | Idadi ya Mikataba | Ghara za mikataba (Sh. Milioni) | Tarehe ya kumaliza mkataba | Muda Uliochelewa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine | 4 | 54.99 | 04-Februari-2021 hadi 30-Aprili-2022 | Miezi 2 hadi Miezi 16 |
| 2 | Shirika la Umeme Tanzania | 9 | 2,534.47 | 24-Mei-22 | Miezi 7 |
| 3 | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 1 | 7,948.64 | 15-Aprili-2022 | Miezi 6 |
| 4 | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 2 | 154.53 | 30-Juni-22 | Miezi 4 |
| 5 | Chuo Kikuu cha Dodoma | 3 | 71.80 | 23-Januari-2022 | Miezi 4 |
| 6 | Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania | 4 | 13.84 | 17-Machi-22 | Miezi 3 |
| 7 | Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili | 4 | 289.01 | 30-Juni-21 | Mwezi 1 |
| 8 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi Wa Mazingira Mbeya | 2 | 1,961.18 | 18-Aprili-22 | Siku 93 |
| 9 | Shirika la Mawasiliano Tanzania | 5 | 497.79 | 22-Machi-2022 | Siku 56 |
| 10 | Shirika la Posta Tanzania | 10 | 2,349.48 | 05- Juni-2022 | Siku 48 |

| Na | Jina la Taasisi | Idadi ya Mikataba | Ghara za mikataba (Sh. Milioni) | Tarehe ya kumaliza mkataba | Muda Uliochelewa |
|---|---|---|---|---|---|
| 11 | Chuo Kikuu Mzumbe | 11 | 2,186.15 | 02-Novemba-2021 | Siku 42 |
| 12 | Kampuni ya Uendelezaji wa Joto-ardhi Tanzania | 1 | 23.82 | 28-Machi-22 | Siku 22 |
| | Jumla | 56 | 18,085.70 | | |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi, 2021/22*

Nina mashaka juu ya matokeo ya ucheleweshaji katika kufikia malengo au kukidhi mahitaji kutokana na bidhaa zilizonunuliwa. Pia, nilibaini taasisi za umma hazichukui hatua kama kutoza tozo za kushindwa kutimiza mikataba ipasavyo kwa wazabuni ili kurekebisha kasoro zinazotokana na kutofuata vigezo na masharti ya mkataba.

**Napendekeza, mashirika ya umma kuchukua hatua zitakazopelekea miradi iliyotajwa kukamilika na bidhaa na huduma zinazonunuliwa kuwasilishwa na kutekelezwa kwa wakati.**

## 9.2 Kuingia katika mkataba bila kuwa na mtaalamu kulikosababisha kusitishwa kwa mkataba wa shilingi bilioni 1.10

Hospitali ya Taifa Muhimbili iliingia mkataba Na. PA/009/2021-22/HQ/W/54 na kampuni ya Shivani Scientific Industries kwa ajili ya usimikaji wa Vifaa vya kurutubisha vijulikanavyo kama (Invitro fertilization (IVF) tarehe 16 Machi 2022 kwa jumla ya shilingi bilioni 1.10 kuanzia 15 Machi 2022 hadi 10 Agosti 2022.

Ukaguzi wa utekelezaji na usimamizi wa mkataba ulibaini kuwa mzabuni aliongezewa muda wa wiki 21 kutoka tarehe 11 Agosti 2022 hadi tarehe 31 Disemba 2022. Licha ya kuongezwa kwa muda, mradi huo haukutekelezwa. Uongozi ulisitisha utekelezaji wa mkataba kutokana na kutokuwepo kwa fedha na mtaalamu wa kuendesha vifaa hivyo.

Ni maoni yangu kuwa, manufaa yaliyotarajiwa ya mradi ili kuongeza uwezo wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili katika kutoa huduma inayotarajiwa hayajapatikana, lakini pia Hospitali ya Taifa imepata hasara katika gharama za mchakato wa manunuzi ya kumpata mzabuni. Hii imesababishwa na udhaifu katika kuweka mipango ya utekelezaji wa mikataba kwa ufanisi, hali iliyopelekea kuanza mkataba bila ya kuwa na mtaalamu na kutenga fedha za mradi.

**Napendekeza Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ijipange upya kwa kuhakikisha mtaalamu anapatikana kwanza na kutenga fedha ya mradi huu ili kukidhi malengo yanayotakiwa.**

## 9.3 Ucheleweshaji wa uwasilishaji wa magari yaliyonunuliwa na Wakala wa Huduma za Manunuzi ya Serikali yenye thamani ya shilingi bilioni 4.2

Nilitathmini manunuzi ya magari katika taasisi 14, nikabaini kuwa mashirika ya umma yalilipa shilingi bilioni 4.20 kwa Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Serikali kwa ajili ya kununua magari yaliyoagizwa kwa makubaliano ya uwasilishwaji wa magari kuanzia miezi minne hadi sita. Hata hivyo, hadi tarehe 31 Desember 2022 wakati wa ukaguzi nilibaini ucheleweshaji wa wastani ulioanzia mwezi mmoja hadi miezi 28 tangu malipo yafanyike. Orodha ya mashirika ya umma yenye magari ambayo hayajapokelewa ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 23**.

**Jedwali Na. 23: Orodha ya magari yaliyonunuliwa lakini hayajapokelewa**

| Na. | Juina la Taasisi | Idadi ya magari | Kiasi (Sh. Milioni) | Idadi Miezi Kuchelewa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania | 5 | 461.73 | 28 |
| 2 | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 3 | 464.6 | 12 |
| 3 | Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje | 1 | 162.93 | 11 |
| 4 | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira | 2 | 406.03 | 8 |
| 5 | Shirika la Viwango Tanzania | 2 | 962.49 | 5 |
| 6 | Chuo Kikuu Mzumbe | 3 | 277.04 | 5 |
| 7 | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma | 1 | 162.93 | 5 |

| Na. | Juina la Taasisi | Idadi ya magari | Kiasi (Sh. Milioni) | Idadi Miezi Kuchelewa |
|---|---|---|---|---|
| 8 | Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini | 2 | 242.8 | 4 |
| 9 | Taasisi ya Saratani ya Ocean Road | 2 | 186.69 | 3 |
| 10 | Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania | 1 | 92.35 | 3 |
| 11 | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi | 1 | 267.66 | 2 |
| 12 | Bodi ya Usajili wa Wahandisi | 2 | 252.74 | 2 |
| 13 | Chuo Kikuu Huria cha Tanzania | 1 | 162.93 | 1 |
| 14 | Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi | 1 | 92.35 | 1 |
| | Jumla | | 4,195.29 | |

**Chanzo**: Taarifa ya Ukaguzi, 2021/22

Aidha, nilibaini Shirika la Wakala wa Meli Tanzania liliagiza magari matano aina ya Toyota Hilux Pickup Double Cabin na kulipa tarehe 13 Machi 2020 lakini magari hayo hayakuwasilishwa, ijapokuwa Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Serikali ilikuwa ikiwasilisha magari aina hiyo hiyo yaliyoagizwa na taasisi zingine. Hii inaonesha kuwa Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Serikali haina utaratibu wa kushughulikia maagizo kutoka kwa taasisi nunuzi.

Ni maoni yangu kuwa Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Serikali hakuzingatia masharti ya makubaliano yanayosimama kati ya taasisi nunuzi na wakala, hivyo anaweza kushindwa kutekeleza majukumu kutokana na kupanda kwa gharama ya magari jambo ambalo linaweza kuleta mzigo kwa Serikali. Aidha, malengo ya taasisi za umma husika yataathiriwa kwa sababu ya ucheleweshaji wa magari.

**Ninapendekeza taasisi husika zifuatilie kwa Wakala wa Huduma ya Ununuzi wa Serikali ili kuhakikisha magari yanaletwa, na Pia Wakala aboreshe taratibu za ununuzi ili kuwasilisha magari yaliyoagizwa kwa wakati.**

## 9.4 Kampuni ambayo haijasajiliwa imepewa mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 12.78

Nilifanya ukaguzi maalumu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na kubaini kuwa kitengo cha Ushirikiano wa Viwanda

kinachojulikana kama BICO ilianzishwa chini ya kitivo cha uhandisi cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1990 na kusajiliwa na Bodi ya Wakandarasi mnamo tarehe 15 June 1999 kama Mshauri Elekezi wa ndani wa Kihandisi na tarehe 29 Februari 2016 kama Maabara ya Majaribio ya Vifaa vya Kihandisi. Hata hivyo, nilibaini BICO ilitekeleza jumla ya miradi 98 toka mwaka 2017/18 hadi mwaka 2019/20 ya ukarabati wa miundombinu ya chuo kikuu kwa thamani ya shilingi bilioni 12.87, ingawa BICO haikuwa imesajiliwa kufanya kazi za ukandarasi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kinyume na Kifungu cha 10 cha Sheria ya Usajili wa Makandarasi ya mwaka 1997 kama ilivyorekebishwa na Kifungu. (9) na(10) cha Sheria ya Usajili wa Makandarasi (Marekebisho) ya mwaka 2008. Pia hapakuwa na cheti cha malipo ili kuthibitisha kazi zote ziliyofanywa.

**Ninapendekeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kihakikishe (a) kusajili BICO kwa Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ili kufanya kazi kama mkandarasi, na (b) kuhakikisha miradi inatolewa kwa wakandarasi waliosajiliwa, na kazi zote zinazofanyika zinapimwa, zinakaguliwa na kuthibitishwa ubora wake.**

## 9.5 Mikataba iliyosainiwa bila kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Afisa Sheria ya kiasi cha shilingi bilioni 45.71 na dola za Marekani milioni 7.75

Kanuni ya 59 na 60 ya Kanuni za Ununuzi ya Umma za mwaka 2013 zilizofanyiwa marekebisho na kanuni ya 2 na 3 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (Marekebisho) ya mwaka 2016 inaeleza kuwa mkataba wowote rasmi ambao thamani yake ni zaidi ya shilingi bilioni moja na ikiwa ununuzi ni kwa kupitia zabuni ya ushindani wa kimataifa, utahakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya mkataba kusainiwa na wahusika. Zabuni ambazo hazijahakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, zabuni hizo ni batili, na zabuni ambayo thamani yake iko chini ya shilingi bilioni moja itahakikiwa na afisa wa sheria wa taasisi nunuzi.

Katika mapitio ya mchakato wa utoaji wa zabuni na usimamizi wa mikataba katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22,

nilibaini kuwa mashirika ya umma saba yalisaini mikataba bila kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Afisa Sheria yenye thamani ya shilingi bilioni 45.71 na dola za Marekani milioni 7.75 kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 24.**

Kuna ongezeko la mikataba iliyosainiwa ambayo haijahakikiwa, hali inayoweza kuziweka taasisi hizo katika hatari ya migogoro ya kisheria na inaweza kuhatarisha utekelezaji wa mikataba.

**Jedwali Na. 24: Mikataba iliyosainiwa kabla ya kuhakikiwa**

| Jina la Taasisi | Idadi ya Mikataba | Kiasi (Sh. Milioni) |
|---|---|---|
| Mfuko wa Maendeleo ya Pamba | 2 | 21,000.00 |
| Bohari Kuu ya Dawa | 6 | 11,725.81 |
| Shirika la Nyumba la Taifa | 1 | 9,630.40 |
| Hospitali ya Taifa Muhimbili | 1 | 1,069.20 |
| Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga | 1 | 1,013.23 |
| Mfuko wa Maendeleo ya Pamba | 2 | 624.82 |
| Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi- Mtwara RVTC | 14 | 328.27 |
| Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Nzega | 2 | 314.52 |
| Jumla | | 45,706.25 |
| Jina la Taasisi | Idadi ya Mikataba | Dola za Marekani (Milioni) |
| **Bohari Kuu ya Dawa** | **2** | **7.75** |

**Chanzo:** Taarifa ya Ukaguzi, 2021/22

Aidha, nilibaini Mamlaka ya Bandari Tanzania na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga walihakiki mikataba yenye thamani ya shililingi bilioni 1.16 na shilingi milioni 121.82 mtawalia, lakini hawakujumuisha ushauri wa kisheria kutokana na uzembe wa uongozi katika kuzingatia sheria za ununuzi.

**Napendekeza mashirika ya umma yahakikishe mikataba inahakikiwa na ushauri unaotolewa unazingatiwa kwenye mikataba ili kuepusha migogoro ya kisheria na hasara inayoweza kutokea kutokana na kushindwa kwa kesi mahakamani; na pia napendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ichukue hatua stahiki kwa mashirika ya**

**umma yanayosaini mikataba yenye thamani kubwa kabla ya kuhakikiwa.**

## 9.6 Mapungufu yaliyobainika katika dhamana za malipo ya awali na dhamana za utekelezaji

### a) Kutokuwepo kwa dhamana za malipo na kuwepo kwa dhamana zilizoisha muda wake kwa malipo ya awali

Nilikagua mikataba katika mashirika na taasisi zingine za umma 10 na kubaini mapungufu katika malipo ya awali yenye thamani ya shilingi bilioni 3.17 yaliyofanywa wakati wa utekelezaji wa mkataba. Taasisi zinalipa malipo ya awali kabla au bila ya wazabuni kuwasilisha dhamana za malipo ya awali zinazohitajika. Vilevile, dhamana za malipo ya awali zilizowasilishwa zinakwisha muda wake wa dhamana kabla ya kukamilika kwa mahitaji yake ya kimkataba, jambo ambalo ni kinyume na vifungu vya mikataba husika. Maelezo yanaoneshwa **kwenye Jedwali Na. 25.**

**Jedwali Na. 25: Taasisi zenye mapungufu katika malipo ya utangulizi**

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh. Milioni) | Maelezo ya Mapungufu |
|---|---|---|---|
| 1 | Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam | 1,423.41 | Kuisha kwa muda wa dhamana |
| 2 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga | 464.31 | Kuisha kwa muda wa dhamana |
| 3 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza | 361.08 | Kutokuwa na dhamana ya malipo |
| 4 | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 284.85 | Kutokuwa na dhamana ya malipo |
| 5 | Taasisi ya Elimu Tanzania | 244.20 | Kutokuwa na dhamana ya malipo |
| 6 | Kampuni ya Stamigold | 164.26 | Malipo kwamMzabuni kabla ya kuleta bidhaa |
| 7 | Shirika la Viwango Tanzania | 160.98 | Kuisha kwa muda wa dhamana |
| 8 | Ofisi ya Taifa ya Takwimu | 36.00 | Kutokuwa na dhamana ya malipo |

| Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh. Milioni) | Maelezo ya Mapungufu |
|---|---|---|---|
| 9 | Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine | 15.67 | Kutokuwa na dhamana ya malipo |
| 10 | Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi | 10.91 | Kutokuwa na dhamana ya malipo |
| | **Jumla** | **3,165.66** | |

***Chanzo***: *Taarifa ya Ukaguzi, 2021/22*

Kwa maoni yangu, kutokuwepo dhamana za malipo ya awali ama kuwepo kwa dhamana zilizokwisha muda wake kabla ya urejeshaji kamili wa malipo ya awali kunaweka mashirika na taasisi zingine za umma katika hatari ya upotevu wa fedha za umma endapo vipengele vya mkataba vitakiukwa. Zaidi ya hayo, hakukuwa na ufanisi wa usimamizi wa utekelezaji wa mikataba kutoka kwa mameneja wa miradi hali iliyoongeza hatari zaidi. Pia, inaonesha kuwa mashirika ya umma yanatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wazabuni ambao hawana uwezo wa kusambaza bidhaa.

**Ninapendekeza mashirika na taasisi zingine za umma watafute nyongeza ya muda wa dhamana wa matumizi na kuhakikisha dhamana zote za malipo ya awali ambazo hazijawasilishwa zinawasilishwa ili kupunguza hatari ya upotevu wa fedha za umma iwapo wazabuni watakiuka utekelezaji wa vipengele vya mikataba.**

### b) Mikataba imetekelezwa bila dhamana wa utendaji kazi yenye thamani ya shilingi bilioni 46.16

Nilikagua mashirika ya umma nane na kubaini kuwa, mashirika hayo hayakudai dhamana za utendaji kazi kwa mikataba 77 iliyotekelezwa yenye thamani ya shilingi bilioni 46.16 kutoka kwa wazabuni walioshinda zabuni, ambapo ni kinyume na Kanuni ya 29 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 inayomtaka mzabuni aliyeshinda zabuni kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi wake, na Aya ya 11.2 ya Mwongozo wa dhamana wa Februari 2022, uliotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ambao unaelekeza kuwa dhamana za utendaji ziwasilishwe kabla ya kusainiwa kwa mkataba, na atakayekiuka atawajibika kwa

adhabu iliyotanabaishwa katika kifungu cha 104 cha Sheria ya Ununuzi ya Umma, Sura 410.

Orodha ya mashirika ya umma yaliyo na mapungufu katika dhamana za utendaji wa mikataba imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 26.**

**Jedwali Na. 26: Mashirika yenye Mapungufu Katika dhamana za utendaji**

| Na. | Jina la Taasisi | Idadi ya Mikataba | Kiasi cha Mkataba (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|
| 1 | Bohari Kuu ya Dawa | 63 | 42,028.73 |
| 2 | Shirika la Taifa la Madini | 5 | 2,640.05 |
| 3 | Taasisi ya Elimu Tanzania | 1 | 406.99 |
| 4 | Chuo cha Diplomasia | 1 | 334.29 |
| 5 | Shirika la Habari la Taifa | 3 | 268.36 |
| 6 | Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili | 1 | 209.55 |
| 7 | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima | 2 | 169.98 |
| 8 | Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania | 1 | 106.24 |
| | Jumla | 77 | 46,164.19 |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi, 2021/22*

Shirika la Umeme Tanzania, Shirika la Viwango Tanzania na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii walikuwa na dhamana za utendaji kazi zenye thamani ya shilingi bilioni 2.50 zilizokwisha muda wake wakati mikataba bado inaendelea. Pia, nilibaini taasisi nne (Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi Wa Mazingira Tanga, Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini, na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi) ambazo zilipata dhamana za utendaji kazi zenye thamani ya shilingi bilioni 6.46 kutoka kwa wazabuni lakini hazikuthibitisha kutoka kwa mtoa huduma hizo kinyume na matakwa ya kanuni.

Kukosekana kwa dhamana ya utendaji kazi, taasisi za umma zinawekwa katika hatari ya kupoteza rasilimali kwa miradi inayoendelea kutokana na wakandarasi na wazabuni wengine kushindwa kutekeleza majukumu.

**Ninapendekeza mashirika ya umma na taasisi zingine kuhakikisha mikataba yote inawekewa dhamana ili kulinda maslahi ya mashirika ya umma na kuepuka upotevu wa fedha unaoweza kutokea.**

## 9.7 Ukiukwaji wa sheria za manunuzi katika Kampuni ya Magazeti ya Serikali kwa manunuzi yenye thamani ya shilingi bilioni 7.49 na dola za Marekani 48,480

Katika ukaguzi wa mikataba ya ununuzi wa bidhaa (inayojulikana kama LPO) katika Kampuni ya Magazeti Tanzania, nilibaini LPO 13 zenye thamani ya shilingi bilioni 7.49 na LPO moja yenye thamani ya dola za Marekani 48,480 ambazo zilitolewa kwa kampuni ya Muhammad Jahangir freight service bila kufuata taratibu za ununuzi kinyume na kifungu cha 4A (1) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410. Nukuu zote za bei katika LPO hizo zilipatikana kutoka kwa mzabuni mmoja, kinyume na Kanuni ya 164(1) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013. Hii inamaanisha kuwa zabuni zimefanyika bila ushindani au ununuzi kutoka chanzo kimoja, jambo ambalo huongeza hatari ya upendeleo, udanganyifu na inakiuka kanuni na viwango vya msingi vya ushindani wa haki.

**Ninapendekeza Shirika la Magazeti Tanzania kuzingatia matakwa ya Sheria za Ununuzi wa Umma ili kuimarisha uadilifu, ushindani, uwajibikaji, uchumi, ufanisi, uwazi na kufikia thamani ya fedha.**

## 9.8 Manunuzi yaliyofanywa bila mikataba sahihi shilingi bilioni 23.41 na dola za Marekani 79,219.13

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Bohari Kuu ya Dawa na Chuo cha Sukari cha Taifa walifanya michakato ya ununuzi 36 kwa wazabuni yenye thamani ya shilingi bilioni 23.41 na michakato ya ununuzi kwa wazabuni watatu ya dola za Marekani 79,219.13 bila kusaini mikataba rasmi. Kinyume na Kanuni ya 233 (1) za Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 (iliyofanyiwa

marekebisho na Kanuni ya 75 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma (Kama zilivyorekebishwa) za mwaka 2016.

Badala yake, Bohari Kuu ya Dawa na Chuo cha Sukari cha Taifa zilitumia barua zilizosainiwa na Afisa Masuuli kuagiza na kufanya malipo kamili ya bidhaa kabla bidhaa kuwasilishwa kutokana na mahitaji ya dharura.

Kukosekana kwa makubaliano ya mkataba, kunapelekea taasisi nunuzi kukabiliwa na hatari ya hasara kutokana na kukosekana kwa vigezo na masharti yanayohusu malipo ya awali, kutowasilisha bidhaa, na migogoro inayoweza kutokea wakati wa utekelezaji wa ununuzi.

**Ninapendekeza Bohari Kuu ya Dawa na Chuo cha Sukari cha Taifa zihakikishe katika siku zijazo manunuzi yote yanakuwa na mikataba rasmi katika fomu iliyoainishwa na inasainiwa ipasavyo na pande zote mbili.**

## 9.9 Bohari Kuu ya Dawa kukiuka udhibiti uliowekwa katika mchakato wa ununuzi wenye thamani ya shilingi bilioni 10.89

Katika ukaguzi wangu wa mkataba Na. IE-009/2021/2022/HQ/50/02 uliotolewa kwa Kampuni ya Kimataifa ya Viwanda vya Dawa ya Misri ijulikanayo kama EIPICO wenye thamani ya shilingi bilioni 10.89 wa ununuzi wa vifaa tiba kutoka Misri, nilibaini kuwa bodi ya zabuni haikupewa nyaraka muhimu kutoka kitengo cha manunuzi ya umma kama vile nyaraka za zabuni,mialiko ya zabuni, maelezo ya zabuni na taarifa ya tathmini kwa ajili ya kuidhinisha ,kinyume na kanuni ya 55 ya Kanuni ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013. Pia, Afisa Masuuli hakuteua timu ya tathmini hivyo tathmini huru haikufanyika. Zaidi ya hayo, mchakato wa majadiliano na utoaji wa tuzo ya mkataba haukuhusisha Bodi ya Zabuni. Menejimenti ya Bohari Kuu ya Dawa ilikwepa taratibu za udhibiti kutokana na hitaji la dharura la bidhaa zilizoagizwa.

Kwa maoni yangu, kuna uwezekano wa kutoa tuzo kwa wazabuni wasio na uwezo kutokana na kutofuatwa kwa sheria za ununuzi na kusababisha ugavi wa bidhaa zisizokidhi viwango na kupata bei ya juu ya ununuzi wa bidhaa ambazo haziakisi thamani ya fedha.

**Ninapendekeza Bohari Kuu ya Dawa kuzingatia udhibiti wa ununuzi uliowekwa katika sheria za ununuzi ili kuhakikisha kunakuwa na uwazi, ufanisi na kupata thamani ya fedha.**

## 9.10 Mipango ya utekelezaji wa mkataba iliyokuwa kinyume na sheria na kupelekea hasara ya dola za Marekani 821,958.36 sawa na shilingi bilioni 1.89

Tarehe 12 Oktoba 2021 Bohari Kuu ya Dawa iliingia mkataba namba (IE-009/2021-2022/G/50/1) na mzabuni AL Handisiya wenye thamani ya dola za Marekani milioni 3.01 kwa ajili ya ununuzi vifaa tiba.

Hata hivyo nilibaini tarehe 11 Oktoba 2021 Bohari Kuu ya Dawa ilifanya malipo ya awali ya dola za Marekani milioni 1.51 sawa na (shilingi bilioni 3.46) kwa kampuni ya M/s.AL Handsiya ambayo yalifanyika kabla ya kuingia makubaliano ya kimkataba. Aidha nilibaini kuwa malipo ya awali yaliyofanywa hayakuwa na dhamana ya benki na kampuni ya AL Handisiya haikuwasilisha vifaa tiba kwa Bohari Kuu ya Dawa kinyume na makubaliano. Katika hali isiyoeleweka, nilibaini vifaa tiba vilivyoagizwa viliwasilishwa na kampuni ya Egyptian International Pharmaceutical Industries Company (EIPICO) na siyo AL Handsiya, na hapakuwa na mchakato wa manununuzi wala mkataba kati ya Bohari Kuu ya Dawa na kampuni ya EIPICO wa kuleta vifaa tiba hivyo, bali kulikuwa na barua kutoka kwa kampuni ya EIPICO ya tarehe 24 Novemba 2021 ikielezea kushindwa kwa kampuni ya AL Handsiya na hivyo kampuni hiyo kuchukua jukumu la kuleta vifaa hivyo. Hapakuwa na mpangilio wa kimkataba kati ya wazabuni hao wawili ama kwa Bohari Kuu ya Dawa kuhusu mzabuni EIPICO kuchukua majukumu ya mzabuni AL Handisiya. Hivyo, nilishindwa kuthibitisha uhalali wa kisheria wa manunuzi ya vifaa tiba hivyo.

Aidha, nilifanya tathmini ya vifaa tiba vilivyowasilishwa na mzabuni EIPICO na nilibaini vifaa hivyo viligharimu dola za Marekani milioni 1.51, ilihali kama vingewasilishwa na mzabuni AL Handisiya ingegharimu dola za Marekani 683,891.64 tu. Kwa kuchagua pendekezo kutoka kwa mzabuni EIPICO, Bohari Kuu ya Dawa ilipata hasara ya dola za Marekani 821,958.36 sawa na shilingi bilioni 1.89 kwa sababu ya utofauti wa bei wa vifaa hivyo.

Pia, nilibaini Bohari Kuu ya Dawa ilitumia kiasi cha shilingi milioni 111,120,922 kwa malipo ya kujikimu na gharama za usafiri kwa watumishi wawili waliokwenda Misri kumtafuta mzabuni AL Handisiya ambaye alishindwa kutimiza wajibu wake licha ya kulipwa malipo ya awali. Hata hivyo, hakuna ushahidi uliotolewa kuthibitisha kama timu ilifanikiwa kumpata mzabuni AL Handisiya walipomfuatilia Misri.

Ni maoni yangu kuwa, mchakato wa uhakiki kuhusu kutathmini uwezo wa mzabuni haukufanyika ipasavyo.

**Ninapendekeza Bohari Kuu ya Dawa ifanye tathimini ya uhakiki kwa wazabuni wa kimataifa kwa kutumia ofisi zetu za balozi zilizo katika nchi mbalimbali kabla ya kuingia mikataba ili kuepuka hasara. Pia, kuchunguza uhusiano wa kibiashara kati ya wazabuni hao wawili na hatua stahiki kuchukuliwa.**

## 9.11 Ongezeko kubwa la bei kwa kuchelewa kufanya uhakiki - dola za Marekani milioni 3.22 sawa na shilingi bilioni 7.41

Tarehe 8 Juni 2020 Shirika la Umeme Tanzania liliidhinisha ripoti ya majadiliano ya zabuni na tarehe 23 Juni 2020 ilitoa barua ya kukubali kampuni ya TBEA ya kuleta vifaa vya ujenzi wa mradi wa ujenzi wa njia ya kusambaza umeme wenye thamani ya dola za Marekani milioni 9.19. Hata hivyo, nilibaini kuwa uhakiki haukufanywa wakati wa tathmini ya zabuni. Mwezi Mei 2021, Shirika la Umeme Tanzania liliuomba Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini China kufanya uhakiki unaoonesha uhalali, uwezo na uzoefu wa kampuni ya TBEA ili kuingia mkataba.

Kutokana na kuchelewa kutia saini mkataba, kampuni ya TBEA iliwasilisha ombi la marekebisho ya bei ya zabuni na marekebisho ya mkataba Julai 2021. Ombi hilo lilitolewa kutokana na kupanda kwa bei ya vifaa bila kutarajiwa, na kusababisha ongezeko la bei kwa dola za Marekani milioni 3.22 sawa na asilimia 35 ya bei ya awali, hivyo kufanya jumla ya dola za Marekani milioni 12.41.

Pia nilibaini kuwa licha ya mkataba kusainiwa Septemba 2021, haukutekelezwa kwa sababu ya ufinyu wa bajeti ya mwaka 2021/22 na ulipangwa kutekelezwa mwaka 2022/23.

Ni maoni yangu kuwa, kuchelewa kunaweza kusababisha gharama ya ziada kutokana na marekebisho ya bei. Hii ilichangiwa na mapungufu ya Shirika la Umeme Tanzania katika kufanya uhakiki wa mzabuni kwa wakati na ufinyu wa bajeti ya kutekeleza mkataba uliosainiwa.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania ifuate taratibu za ununuzi ili kuepuka mabadiliko ya bei zisizo za lazima; na mkataba kutekelezwa mapema iwezekanavyo ili kuepuka ucheleweshaji zaidi na ongezeko la gharama.**

## 9.12 Manunuzi yaliyofanywa zaidi ya bajeti na mpango wa manunuzi wa mwaka kwa shilingi bilioni 96.06

Kanuni ya 69 (3)(7) ya Kanuni ya Manunuzi wa Umma ya mwaka 2013 inaitaka taasisi nunuzi kuandaa mahitaji yake ya bidhaa, huduma na kazi za ujenzi kwa usahihi kwa kadri inavyowezekana kwa kuzingatia huduma au shughuli ambazo zipo katika mpango kazi wa mwaka na kujumuishwa katika makadirio ya mwaka na kutengeneza mpango wa ununuzi kwa mahitaji ambayo fedha za kutosha zimejumuishwa katika bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha au kama malipo yatalipwa katika mwaka wa fedha unaofuata, malipo hayo yawe yametengewa bajeti.

Nilibaini mikataba 30 ilisainiwa na kutekelezwa katika mashirika na taasisi zingine za umma 10 ikilinganishwa na taasisi saba kwa mwaka 2020/21. Hata hivyo, gharama za mikataba zilizidi kiasi

kilichoidhinishwa katika mpango wa ununuzi kwa kiasi cha shilingi bilioni 4.62 ( **Jedwali Na. 27**). Mchakato wa kuandaa mahitaji na kupanga bajeti haukuzingatia bei za soko na mahitaji halisi ya taasisi.

**Jedwali Na. 27: Ununuzi ambao gharama za mkataba imezidi kiasi kilichopitishwa cha bajeti**

| Na. | Jina la Taasisi | Idadi ya Zabuni | Kiasi cha Bajeti (Sh.milioni) | Kiasi cah Mkataba (Sh. Milioni) | Kiasi Kilichozidi (Sh. Milioni) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kampuni ya Stamigold | 7 | 12,720.00 | 14,721.07 | 2,001.07 |
| 2 | Tume ya Nishati ya Atomiki Tanzania | 1 | 2,000.00 | 3,033.65 | 1,033.65 |
| 3 | Taasisi ya Elimu Tanzania | 8 | 6,147.68 | 6,869.86 | 722.18 |
| 4 | Chuo Kikuu Huria cha Tanzania | 5 | 1,309.62 | 1,777.18 | 467.56 |
| 5 | Shirika la Umeme Tanzania | 1 | 78.00 | 190.02 | 112.02 |
| 6 | Mfuko wa SELF Microfinance | 1 | 86.00 | 186.43 | 100.43 |
| 7 | Shirika la Posta Tanzania | 2 | 2,387.45 | 2,449.09 | 61.64 |
| 8 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Nzega | 1 | 1,526.39 | 1,586.92 | 60.53 |
| 9 | Kampuni ya Mkulazi | 1 | 175.56 | 223.54 | 47.98 |
| 10 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Njombe | 3 | 65.95 | 78.89 | 12.94 |
| | Jumla | 30 | 26,496.65 | 31,116.65 | 4,620.00 |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi, 2021/22*

Aidha, nilibaini Bohari Kuu ya Dawa ilitekeleza zabuni nne zinazohusisha kiasi cha shilingi bilioni 96.06 ambazo hazikuwekwa kwenye bajeti wala kujumuishwa kwenye Mpango wa ununuzi wa mwaka. Mapungufu haya yalichangiwa kwa kiasi kikubwa na mahitaji ya dharura yasiyopangwa na bila kufuata taratibu za udhibiti wa bajeti.

**Ninapendekeza taasisi za umma zihakikishe kuwa manunuzi yote yanayofanywa yanaendana na mpango wa ununuzi wa mwaka ulioidhinishwa kulingana na uhalisia wa bei halisi ili kuepuka matumizi yasiyopangwa na kufikia mafanikio ya malengo ya ununuzi.**

## 9.13 Ucheleweshaji wa malipo ya madai ya wakandarasi na wazabuni wengine ya kiasi cha shilingi bilioni 1.99 na paundi za Uingereza 39,387.20

Katika Ukaguzi wangu nilibaini ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi na wazabuni wengine katika taasisi sita. Ucheleweshaji huo ulikuwa kati ya siku 90 hadi siku 227 kwa jumla ya madai ya shilingi bilioni 1.99 na paundi za Uingereza 39,387.20 ambayo hayajalipwa **(Jedwali Na. 28).** Chanzo cha ucheleweshaji huo kilibainika kuwa ni uhaba wa fedha unaozikabili taasisi hizo.

**Jedwali Na. 28: Orodha ya taasisi zilizochelewa kufanya malipo**

| Na. | Jina la Taasisi | Idadi ya Mikataba | Kiasi (milioni) | Muda ucheleweshaji |
|---|---|---|---|---|
| | **Kiasi kwa Sh.** | | | |
| 1 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi Wa Mazingira Tanga | 1 | 1,064.28 | Siku 101 |
| 2 | Hifadhi za Taifa Tanzania | 2 | 590.34 | Siku 90 |
| 3 | Chuo Kikuu Mzumbe | 2 | 206.17 | Siku 102 |
| 4 | Chuo cha Uhasibu Arusha | 2 | 126.47 | Siku 227 |
| 5 | Shirika la Maendeleo la Taifa | 1 | 9.63 | Siku 153 |
| | **Jumla Sh.** | | **1,996.89** | |
| | **Kiasi kwa Paundi ya Uingereza (GBP)** | | | |
| **6** | Baraza la Mitihani Tanzania | **1** | **39,387.20** | Siku 130 |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi, 2021/22*

Malipo yasiyofanyika kwa wakati yanasababisha ucheleweshaji wa mradi na kuzuia utoaji wa huduma kwa wakati kwa walengwa, na kusababisha gharama za ziada kwa mashirika kutokana na riba na adhabu kutoka kwa ankara ambazo hazijalipwa.

**Ninapendekeza taasisi za umma husika zilipe kwa wakati kulingana na makubaliano ya vigezo na masharti ya mikataba ili kuepuka malipo ya gharama za ziada.**

## 9.14 Taratibu za ununuzi zenye thamani ya shilingi bilioni 80.53, dola za Marekani milioni 51.59, na Yuro milioni 11.54 zimefanyika nje ya mfumo wa ununuzi wa kielekitroniki

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ilianzisha Mfumo wa Ununuzi wa Kielektroniki ujulikanano kama TANePS kwa ajili ya kuwasilisha kwa mtandao mipango ya ununuzi, mialiko ya zabuni na tuzo za mikataba. Katika mwaka unaomalizika, nilibaini mashirika na taasisi zingine 21 zilifanya taratibu za ununuzi nje ya TANePS, jambo ambalo ni kinyume na Kanuni ya 342 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013 na Waraka Na. 4 wa mwaka 2019 wenye Rejea Na. EB/AG/485/01/Vol. XII/26 wa tarehe 23 Novemba 2019, uliotolewa na Hazina. Tazama taasisi husika katika **Jedwali Na. 29**.

**Jedwali Na. 29: Taasisi zilizofanya manunuzi nje ya mfumo wa TANePS**

| Na. | Jina la taasisi | Idadi ya mikataba | Kiasi |
|---|---|---|---|
| | (Sh. Milioni) | | |
| 1 | Shirika la Umeme Tanzania | 1 | 39,118.70 |
| 2 | Bohari Kuu ya Dawa | 8 | 20,444.49 |
| 3 | Shirika la Nyumba la Taifa | 6 | 9,044.49 |
| 4 | Taasisi ya Mifupa Muhimbili | 17 | 2,870.24 |
| 5 | Bodi ya Utalii Tanzania | 44 | 1,870.00 |
| 6 | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi -Tabora, Dar es Salaam na Kipawa | 58 | 1, 523.06 |
| 7 | Chuo Kikuu Ardhi | 9 | 1,108.56 |
| 8 | Chuo cha Sukari cha Taifa | 152 | 888.00 |
| 9 | Chuo cha Usimamizi wa Fedha | 15 | 750.02 |
| 10 | Bodi ya Korosho Tanzania | 6 | 690.17 |
| 11 | Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya | 5 | 531.49 |
| 12 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga | 24 | 491.80 |
| 13 | Chuo Kikuu cha Dodoma | 2 | 345.11 |
| 14 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Karatu | 30 | 282.87 |
| 15 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Same Mwanga | 2 | 148.32 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 16 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Karatu Korogwe | 8 | 137.20 |
| 17 | Mfuko wa Maendeleo ya Pamba | 1 | 71.06 |
| 18 | Shirika la Masoko la Kariakoo | 10 | 65.27 |
| 19 | Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu Katika Ukanda wa Kitropiki | 5 | 64.65 |
| 20 | Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania | 1 | 55.00 |
| 21 | Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania | 1 | 27.38 |
| | **Jumla** | | **80,527.88** |
| **Dola za Marekani (Milioni)** | | | |
| | Shirika la Umeme Tanzania | 1 | 51.49 |
| **Fedha za Yuro (Milioni)** | | | |
| | Shirika la Umeme Tanzania | 1 | 11.54 |

**Chanzo**: *Taarifa ya Ukaguzi, 2021/22*

Aidha, ni muhimu kutambua kwamba taasisi tano, ambazo ni Shirika la Nyumba la Taifa, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Bohari Kuu ya Dawa, Taasisi ya Mifupa Muhimbili na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi zimeonesha mapungufu yaleyale ambayo nilibaini kwenye ripoti yangu ya mwaka uliopita. Hii ina maana kuna uzembe wa usimamizi katika kuzingatia matakwa ya sheria na waraka.

Kwa maoni yangu, utaratibu wa kufanya ununuzi nje ya Mfumo wa Ununuzi wa Kielektroniki unazuia uwazi na kuizuia Serikali kufikia malengo yake katika kutumia mfumo wa ununuzi.

Katika ukaguzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, nilibaini kuwepo kwa kasoro katika mfumo wa TANePS ambazo zilisababisha baadhi ya zabuni kutokamilika kwa wakati au kufutwa bila kujua, jambo ambalo lilisababisha malalamiko kuibuliwa na taasisi tatu za ununuzi kuhusu kasoro za mfumo. Nina wasiwasi kuhusu kasoro za mfumo kwani zinaathiri taratibu za ununuzi kufanyika kama ilivyopangwa na taasisi.

**Ninapendekeza (a) mashirika ya umma kuhakikisha yanazingatia kikamilifu matumizi ya mfumo wa ununuzi wa kielektroniki kama inavyotakiwa na sheria, na (b) Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ifuatilie taasisi nunuzi ili kuimarisha matumizi ya mfumo kikamilifu na (c) Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ifanye tathmini ya mfumo na**

**kurekebisha kasoro za mfumo wa TANePS ili kufikia malengo yaliyokusudiwa katika matumizi ya mfumo.**

## 9.15 Mapungufu yaliyoonekana katika usimamizi wa miradi katika Shirika la Mawasiliano Tanzania na Shirika la Umeme Tanzania

Nilibaini udhaifu katika usimamizi wa miradi katika taasisi mbili: Shirika la Mawasiliano Tanzania na Shirika la Umeme Tanzania. Katika Shirika la Mwasiliano Tanzania, kulikuwa na miradi 464 iliyokamilika yenye thamani ya shilingi bilioni 10.33 ambayo haikufungwa kutokana na ufatiliaji usioridhisha na kuchelewa kuwasilishwa kwa nyaraka muhimu toka kwa mameneja wa miradi. Hii inaleta hatari ya matumizi mabaya ya fedha kutokana na uwezekano wa kutokuwepo kwa miradi hiyo. Katika Shirika la Umeme Tanzania, kulikuwa na miradi 167 yenye thamani shilingi bilioni 39.7 ambayo haikutekelezwa katika mwaka wa ukaguzi 2021/22. Hakuna sababu za msingi zilizotolewa za kutotekelezwa au kutofungwa kwa miradi, ikionesha kukosekana kwa ufuatiliaji na hatari ya kupotoshwa kwa taarifa za fedha endapo miradi hiyo itakuwa imekamilika na inatumika bila kufungwa na kupunguza thamani.

**Ninapendekeza Shirika la Mawasiliano Tanzania na Shirika la Umeme Tanzania watekeleze taratibu sahihi za ufuatiliaji na ufungaji wa miradi kwa wakati ili kupunguza hatari hizi.**

## 9.16 Malipo ya awali kwa wazabuni bila vigezo na masharti katika Bohari Kuu ya Dawa na Hospitali ya Taifa Muhimbili – Mloganzila, shilingi bilioni 61.99

Katika Bohari Kuu ya Dawa nilibaini kuwa malipo ya awali yenye thamani ya Shilingi bilioni 61.81 yalilipwa kwa wazabuni 22 katika mwaka wa fedha 2021/22 bila kuwa na mikataba inayoainisha masharti ya malipo ya awali kinyume na Kanuni ya 164 ya Kanuni za Fedha za Bohari Kuu ya Dawa, 2011.

Zaidi ya hayo, nilibaini Hospitali ya Taifa ya Muhimbili - Mloganzila ilifanya malipo ya awali kwa wazabuni kuanzia Julai

2021 hadi Juni 2022 yenye thamani ya Shilingi milioni 178.21 bila ya mkataba.

Kuna uwezekano kwamba Bohari Kuu ya Dawa na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili -Mloganzila zinatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wazabuni ambao hawana uwezo wa kusambaza bidhaa hizo, zaidi ya hayo, taasisi husika zinakosa faida ya kutumia fedha ambazo zipo kwa wazabuni kama malipo ya awali.

**Ninapendekeza Bohari Kuu ya Dawa na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili -Mloganzila ziimarishe udhibiti na kuhakikisha kuwa hakuna malipo ya awali yatakayofanywa kwa wazabuni bila ya kuwa na mkataba wa kisheria unaoainisha masharti ya malipo ya awali.**

## 9.17 Mkandarasi alianza utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa Hoteli ya Nyota Tatu kabla ya kukamilika kwa mchakato wa ununuzi

Katika ukaguzi wangu maalum wa Hifadhi ya Taifa Tanzania, nimefanya mapitio ya taratibu za ununuzi na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa hoteli ya nyota Tatu katika eneo la Rubambangwe-Chato, pamoja na usahihi wa malipo yanayofikia shilingi bilioni 12.9 zilizotolewa na Hifadhi za Taifa Tanzania. Ukaguzi wangu, umebaini maeneo kadhaa yenye mapungufu. Mnamo Julai 5,2019, Hifadhi za Taifa Tanzania ilisaini Mkataba wa Makubaliano na Kampuni ya SUMA JKT kwa ajili ya ujenzi wa Hoteli ya Nyota Tatu katika eneo la Rubambagwe-Chato, ili mkandarasi akabidhiwe eneo la mradi kabla ya Mkataba kusainiwa. MoU ilibainisha makadirio ya gharama za mradi wa Shilingi Bilioni 1moja kwa kuwa gharama halisi za mradi hazikuanzishwa wakati huo. Kabla ya kuanza kwa mradi huo tarehe 28 Oktoba 2019, TANAPA ilifanya malipo ya awali ya shilingi milioni 500 kwa SUMAJKT tarehe 2 Agosti 2019, na baadaye tarehe 17 Februari 2020 ilifanya malipo

mengine ya shilingi milioni 500, hivyo kufanya jumla kuwa shilingi bilioni 1.

Hifadhi za Taifa Tanzania ilianza mchakato wa ununuzi tarehe 11 Julai 2019 kupitia Fomu ya Ununuzi Na. 2, ambapo bodi ya zabuni ilibadilisha njia ya ununuzi kutoka zabuni ya kitaifa ya ushindani na kuwa njia isiyo ya ushindani kwa mzabuni mmoja. Tathmini ya mkandarasi ilionesha Kampuni ya SUMAJKT ilikuwa na uzoefu wa chini ya miaka mitano na haikuwa na wastani wa mauzo ya ujenzi wa shilingi bilioni moja kila mwaka kama ilivyotakiwa kwenye maelekezo kwa wazabuni.

Pamoja na mapungufu hayo, tarehe 26 Machi 2020, baraza la wadhamini la Hifadhi za Taifa Tanzania iliingia mkataba na. PA/037/2019-20/W/HQ/139 wenye thamani ya shilingi bilioni 11.0 na Kampuni ya SUMA JKT kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo kwa miezi 12 kuanzia tarehe 14 Aprili 2020.

Ripoti ya utekelezaji wa mradi ilionesha kuwa hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2021, Hifadhi za Taifa Tanzania ilikuwa imelipa jumla ya Shilingi bilioni 4.1 (asilimia 37 ya gharama za mradi) na utekelezaji wa asilimia 40, bila kuendelea ilibaki vilevile hadi wakati wa ukaguzi huu tarehe 20 Desemba 2021.

**Ninapendekeza Hifadhi za Taifa Tanzania izingatie sheria, kanuni na taratibu za ununuzi wa umma wakati wa utekelezaji wa miradi ya baadaye.**



# SURA YA KUMI

# TATHIMINI YA UDHIBITI WA MIFUMO YA NDANI, RASILIMALI WATU NA UTAWALA

## 10.0 Utangulizi

Serikali imeanzisha mifumo ya udhibiti wa ndani kwa taasisi zake ili kuhakikisha usimamizi sahihi wa vihatarishi katika kufanikisha malengo ya taasisi. Mifumo hiyo inategemea wafanyakazi wenye ujuzi na uwezo pamoja na muundo mzuri wa utawala na maelekezo sahihi. Hata hivyo, kuna changamoto zinazokabili utekelezaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani, usimamizi wa rasilimali watu na mifumo ya utawala, kama vile ukosefu wa bodi za wakurugenzi kwa mashirika ya umma, maafisa wa umma wanaokaimu kwa muda mrefu zaidi ya miezi sita, na upungufu wa wafanyakazi.

Sura hii inaangazia masuala yaliyoonekana wakati wa ukaguzi wa udhibiti wa ndani, rasilimali watu, na mifumo ya utawala ya mashirika ya umma na taasisi zingine

## 10.1 Mashirika ya umma yasiyokuwa na Bodi za wakurugenzi

Bodi ya Wakurugenzi ina jukumu muhimu katika kuangalia utendaji wa taasisi za umma kwa maslahi ya umma. Bodi hizo zinawajibika kufanya maamuzi kwa maslahi ya umma, ikiwa ni pamoja na kusimamia maamuzi ya kifedha na kupitia mipango ya kibiashara.

Idadi ya mashirika ya umma na taasisi zingine bila Bodi ya Wakurugenzi zimepungua kutoka 31 kwa mwaka 2020/21 hadi 13 mwaka 2021/22, shaka yangu ni kuchelewa kuteuliwa bodi mpya baada bodi iliyopo kuisha muda wake. Kazi ya usimamizi ni

muhimu ili kuhakikisha kuwa shughuli za taasisi zinaongozwa kwa maslahi bora ya umma. **Jedwali Na. 30** linabainisha idadi ya taasisi za umma ambazo hazina Bodi ya Wakurugenzi.

Ni muhimu kuwa Bodi zinateuliwa haraka ili kusimamia mashirika ya umma na kuhakikisha kuwa shughuli zao zinaongozwa kikamilifu kwa maslahi bora ya umma.

**Jedwali Na. 30: Mashirika ya umma yasiyokuwa na bodi za wakurugenzi**

| Na. | Jina la shirika | Tarehe ya mwisho kuwa na Bodi | Miezi ambayo taasisi imekaa bila kuwa na bodi hadi Februari 2023 |
|---|---|---|---|
| **Mashirika ambayo hayana Bodi za wakurugenzi kwa zaidi ya mwaka mmoja** | | | |
| 1 | Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo na Teknolojia | Julai 2015 | 92 |
| 2 | Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania | Oktoba 2019 | 42 |
| 3 | Kampuni ya gesi | Julai 2019 | 36 |
| 4 | Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL | Julai 2019 | 36 |
| 5 | Chama cha Hakimiliki Tanzania | Disemba 2020 | 26 |
| 6 | Chuo cha Sukari cha Taifa | Agosti 2020 | 31 |
| 7 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Same Mwanga | Agosti 2020 | 31 |
| 8 | Baraza la Kiswahili Tanzania | Januari 2021 | 26 |
| 9 | Taasisi ya Mifupa Muhimbili | Oktoba 2021 | 17 |
| 10 | Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibiolojia Tanzania | Septemba 2021 | 17 |
| 11 | Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano | Novemba 2021 | 15 |
| **Mashirika ambayo hayana Bodi za wakurugenzi chini ya mwaka mmoja** | | | |
| 12 | Bodi ya Utalii Tanzania | 23 Aprili 2022 | 10 |
| 13 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Iringa | Januari 2023 | 1 |

**Chanzo:** Taarifa za fedha za mashirika, 2021/22

Nilibaini pia kutokuwepo kwa bodi kamili ya wakurugenzi katika taasisi mbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili na Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo na Teknolojia, ambapo wenyeviti wa bodi wamechaguliwa bila wajumbe wake.

Hii inadhoofisha mifumo ya udhibiti wa ndani na kuchelewesha maamuzi muhimu, ambayo inaathiri uendeshaji wa taasisi.

**Ninapendekeza mamlaka zinazoteua zizingatie utambuzi mapema wa wajumbe wa bodi na kuanza mchakato wa uteuzi ili kupunguza changamoto hizi.**

## 10.2 Changamoto za mashirika ya umma na taasisi zingine katika matumizi ya mfumo wa ulipaji serikalini(MUSE)

Nilipitia utekelezaji wa muongozo wa Hazina Na.5 wa mwaka 2019 ambao uliagiza maafisa masuuli kutumia mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya uhasibu na usimamizi wa fedha, pamoja na agizo kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango iliyotolewa Aprili 2020 ambao ulihitaji taasisi za serikali kutumia MUSE.

Nilibaini kuwa idadi ya mashirika ya umma na taasisi zingine ni 206, kati ya hayo mashirika ya umma 36 wameruhusiwa kutotumia mfumo huo na Wizara ya Fedha na Mipango na mashirika ya umma 174 walitakiwa kutumia MUSE. Kati ya mashirika hayo 174 nimegundua kuwa mashirika 100 (asilimia 57) hayatumii MUSE kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ugumu wa shughuli za taasisi hizo kutumia MUSE.

Aidha, kati ya mashirika 74 ambayo yalitumia MUSE, nilibaini kuwa mashirika 42 (asilimia 56) yalikabiliwa na changamoto mbalimbali katika kutumia MUSE **(Kiambatisho Na. IX)**. Changamoto zilizobainika ni pamoja na mfumo kuzorota au kuzima kabisa, maboresho yanayofanywa na waundaji wa mfumo bila kuwataarifu watumiaji, na kutotoa ushirikiano wa kutosha pale changamoto zinapotokea kwa watumiaji wa mfumo.

Aidha, Baadhi ya moduli zinakosekana kwenye mfumo, kuwepo tofauti katika chati za uhasibu. Kurekodi malipo zaidi ya mara moja, mfumo hauna uwezo wa kuchakata na kutoa taarifa za miradi inayojitegemea. Baadhi ya miamala ya mapato haitokei kwenye taarifa za benki, baadhi ya mageresho ya kibajeti kwenye mfumo wa bajeti wa PlanRep hayaonekani kwenye MUSE.

Maoni yangu ni kuwa changamoto hizi zinapelekea kazi nyingi kufanywa nje ya MUSE hivyo siyo tu kusababisha makosa katika utoaji wa taarifa za fedha lakini pia inaleta changamoto katika utendaji wa taasisi kwa ujumla.

**Ninapendekeza Serikali kuwaagiza wataalamu wa MUSE kwa kushirikiana na mashirika ya umma na taasisi zingine, kuhakikisha kuwa changamoto zote za MUSE zinatatuliwa ili kuboresha utendaji wake.**

## 10.3 Matumizi yasiyoridhisha ya mpango mkakati kama nyenzo katika kuongoza shughuli za mashirika ya umma na idara zake

Aya ya 7.4 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 hadi 2025/26 inaeleza jukumu la utekelezaji wa mpango huo kwa mashirika ya umma kwa kutumia mpango mkakati wa shirika husika katika kufanya tathimini ya uratibu na utekelezaji.

Katika kufanya tathimini ya mpango mkakati wa mashirika ya umma na taasisi zingine nilibaini kuwa mashirika ya umma 15 na taasisi zingine zilikuwa na kasoro zinazoashiria kutokuwa na ufanisi katika mpango wao.

Kasoro hizo zilijumuisha ukosefu wa mpango mkakati, mpango mkakati uliokwisha muda wake, ufuatiliaji na tathmini hafifu, au shughuli ambazo hazijatekelezwa **(Jedwali Na. 31**).

Hii inatokana na kutokuwepo kwa bodi za usimamizi katika kuidhinisha mpango mkakati, Ufinyu wa bajeti katika kutekeleza malengo yaliyopangwa na Tathimini isiyoridhisha ya mpango mkakati.

**Jedwali Na. 31: Mashirika ya umma yenye Matumizi yasiyoridhisha ya mpango mkakati**

| Na. | Jina la shirika | Mapungufu yaliyobainika |
|---|---|---|
| 1. | Bodi ya Amana za Bima | Mpango mkakati uliisha muda wake 30 Juni 2021. Mpango mpya unasubiri idhini ya bodi ya wakurugenzi |
| 2. | Hospitali ya Taifa Muhimbili | Walinunua vifaa vya matibabu 12 kati ya 93 katika mpango mkakati ulioisha 2016/17-2021/22 |
| 3. | Shirika la Umeme Tanzania | Mpango mkakati wa muda mfupi (2021/22-2022/23) haukuendana na mpango wa bajeti |
| 4. | Shirika la Nyumba la Taifa | Mpango mkakati 2015/16-2024/25 hauoneshi muda wa kufanya tathimini ya malengo husika |
| 5. | Chuo Kikuu cha Dodoma | Kushindwa kutekeleza lengo la kuanzisha Kitengo cha ushauri na utafiti mnamo Januari 2022 |
| 6. | Bohari Kuu ya Dawa | Utekelezaji usioridhisha wa malengo ya mwaka 2021/22 chini ya asilimia 50 |
| 7. | Shirika la Reli Tanzania | Hakuna mpango wa kufanya tathimini katika mpango mkakati 2019/20 -2023/24 |
| 8. | Kampuni ya TTCL Pesa | Mpango mkakati uliisha mda wake 30 Juni 2020. Mpango mpya unafanyiwa uchambuzi |
| 9. | Chuo cha Ufundi Arusha | Shughuli sita zilizopangwa hazikutekelezwa chini ya mpango mkakati ulioisha 2017/18-2021/22. |
| 10. | Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam | Ucheleweshaji katika kutekeleza Mpango mkakati mpya wa 2021/21-2024/25 ambao bado unafanyiwa mapitio |
| 11. | Kampuni ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam | Hakuna Mpango mkakati |
| 12. | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima | Tathimini ya mwisho wa mwaka haikufanyika |
| 13. | Bodi ya Tumbaku Tanzania | Tathimini ya mpango mkakati wa 2018/19-2023/24 haikufanyika toka kuanzishwa kwake |
| 14. | Chuo Kikuu Mzumbe | Utekelezaji usioridhisha, kwa mwaka 2021/22 kati ya shughuli 111, shughuli 23 hazikufanyika |
| 15. | Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo na Teknolojia | Hakuna mpango mkakati |

**Chanzo**: Taarifa za ukaguzi 2021/22

Maoni yangu ni kuwa matumizi yasiyoridhisha ya mpango mkakati pamoja na kushindwa kufanya tathimini ya mpango huo husababisha utendaji mbovu uliosababishwa na kutokuwa na mwelekeo, na kuwafanya watumie rasilimali bila tija na bila uhakika wa kufikia malengo ya Taasisi.

**Ninapendekeza mashirika ya umma na taasisi zingine (a)kupanga bajeti ya kutosha ili kutekeleza shughuli zilizopangwa katika mpango mkakati, (b) kuharakisha mchakato wa tathimini wa mpango mkakati ulioisha muda wake, na (c) kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ili kufanikisha malengo ya mpango mkakati uliopo kwa wakati huo.**

## 10.4 Tathimini isiyoridhisha ya vihatarishi katika mashirika ya umma na taasisi zingine

Uongozi Bora, usimamizi wa vihatarishi, na mifumo ya udhibiti wa ndani ni kati ya malengo muhimu katika kutambua na kupunguza vihatarishi katika shughuli za mashirika ya umma. Ili kufikia lengo hili, uongozi hujenga sera, mifumo, na taratibu za kusimamia mchakato wa kutambua vihatarishi. Hii huongeza ufanisi wa shirika katika kutambua, kufuatilia, na kuondoa vihatarishi katika kuhakikisha uendeshaji wa taasisi kwa ufanisi zaidi.

Wakati wa ukaguzi wa 2021/22, nilibaini mashirika ya umma na taasisi zingine tisa hazikuchukua hatua stahiki katika usimamizi wa vihatarishi Kwa mfano; Hii ni pamoja na kukosekana kwa sera ya usimamizi wa vihatarishi ili kutambua na kupunguza vihatarishi kama ilivyoelezwa katika **Jedwali Na. 32**

**Jedwali Na. 32: Mashirika ya umma na Taasisi zingine ambazo hazikufanya tathimini ya vihatarishi ipasavyo**

| Na. | Jina la Taasisi | mapungufu niliyobaini |
|---|---|---|
| 1. | Bodi ya Maziwa Tanzania | Hakuna sera ya usimamizi wa vihatarishi |
| 2. | Chuo Kikuu Mzumbe | Hawakufanya tathimini ya vihatarishi pamoja na kushindwa kuhuisha rejista ya vihatarishi |

| Na. | Jina la Taasisi | mapungufu niliyobaini |
|---|---|---|
| 3. | Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania | Hakuna sera ya usimamizi wa vihatarishi |
| 4. | Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu | Hawakufanya tathimini ya vihatarishi katika mradi wa reli ya kisasa |
| 5. | Kituo cha Pembejeo za Kilimo na Teknolojia Vijijini | Hakuna rejista ya vihatarishi |
| 6. | Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji | Kuna sera ya usimamizi wa vihatarishi lakini hakuna rejista ya vihatarishi |
| 7. | Shirika la Usimamizi wa Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika | Hakuna mfumo wa usimamizi wa vihatarishi |
| 8. | Kampuni ya Mkulanzi | Hakuna sera ya usimamizi wa vihatarishi |
| 9. | Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli | Hakuna sera ya usimamizi wa vihatarishi |

**Chanzo:** Taarifa za ukaguzi 2021/22

Hii inaweza kupelekea kuwepo kwa vihatarishi vitakavyo athiri kazi za taasisi pamoja na vitendo vya udanganyifu bila kubainika na menejimenti.

**Ninapendekeza mashirika ya umma na taasisi zingine kuhakikisha wanafanya tathimini ya vihatarishi kwa kutumia nyenzo za kubaini na kuvifanyia kazi vihatarishi hivyo**

## 10.5 Mashirika ya umma na taasisi zingine zenye mifumo ya ndani isiyoridhisha

### 10.5.1 Mashirika ya umma na taasisi zingine zenye nyenzo za kazi zisizoridhisha

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa mashirika ya umma na taasisi zingine 25 zilikuwa na changamoto katika nyenzo za kazi. Baadhi ya mashirika yalikuwa hayana nyenzo hizo toka kuanzishwa kwa taasisi, wakati mashirika mingine nyenzo zao zilikuwa zimepitwa na wakati hivyo hazikidhi mahitaji ya sasa.Aidha, Nilibaini kuwa baadhi ya mashirika ya umma yalikuwa yanasubiria kuidhinishwa kwa nyenzo katika hatua mbalimbali. Pia nilibaini kuwa baadhi

ya mashirika ya umma yalihuisha nyenzo hizo bila idhini kutoka kwa Ofisi ya Raisi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hii inapingana na matakwa ya aya 4.2 ya muongozo wa sheria ya umma 2017.

Hii inatokana na kutokuwa na bodi za wakurugenzi zinazoidhinisha nyenzo hizo, mapitio na tathimini ya muda mrefu na menejimenti katika nyenzo zilizoisha muda wake na kutowasilisha nyenzo hizo zilizohuishwa katika Ofisi ya Raisi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kuidhinishwa. **Jedwali Na. 33**

**Jedwali Na. 33: Mashirika ya umma na Taasisi zingine ambazo hazina nyaraka za miongozo ya kuendesha kazi zake**

| S/n | Jina la taasisi | Mapungufu yaliyobainika |
|---|---|---|
| 1. | Chuo cha Diplomasia | Kanuni za fedha hazikuidhinishwa. |
| 2. | Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo na Teknolojia | Hakuna kanuni za fedha |
| 3. | Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda | Kanuni za fedha hazikuidhinishwa |
| 4. | Tasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania | Nyenzo zimepitwa na wakati ambazo ni : Sheria ya kuanzishwa kwa taasisi ya utafiti wa misitu; kanuni za utumishi, kanuni za fedha, muundo wa maendeleo wa utumishi na mshahara |
| 5. | Bodi ya Utalii Tanzania | Kanuni za fedha zimepitwa na wakati hivyo hazikidhi mahitaji ya sasa |
| 6. | Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | Kanuni za fedha hazikuidhinishwa |
| 7. | Bodi ya Amana za Bima | Hakuna taratibu za kuendesha shughuli za taasisi |
| 8. | Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro | Hakuna taratibu za kuendesha shughuli za taasisi pamoja na muundo ya maendeleo ya utumishi |
| 9. | Chuo Kikuu Ardhi | Kanuni za fedha zimepitwa na wakati hivyo hazikidhi mahitaji ya sasa |
| 10. | Tume ya Sayansi na Teknolojia | Hawana taratibu na kanuni za sheria ya tume ya sayansi na teknolojia |
| 11. | Kampuni ya MCB | Kanuni za fedha na kanuni za utumishi hazikuidhinishwa |
| 12. | Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini | Kanuni za fedha na kanuni za utumishi hazikuidhinishwa |

| S/n | Jina la taasisi | Mapungufu yaliyobainika |
|---|---|---|
| 13. | Bodi ya Usajili Wa Wakandarasi | kanuni za utumishi,kanuni za fedha, muundo wa maendeleo wa utumishi zimepitwa na wakati hivyo hazikidhi mahitaji ya sasa |
| 14. | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Iringa | Kanuni za fedha zimepitwa na wakati hivyo hazikidhi mahitaji ya sasa |
| 15. | Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania | Kanuni za fedha zimepitwa na wakati hivyo hazikidhi mahitaji ya sasa |
| 16. | Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania | Kanuni za utumishi hazikuidhinishwa |
| 17. | Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori | Kanuni za fedha zimepitwa na wakati hivyo hazikidhi mahitaji ya sasa |
| 18. | Chama cha Hakimiliki Tanzania | Kanuni za fedha zimepitwa na wakati hivyo hazikidhi mahitaji ya sasa |
| 19. | Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam | Kanuni za fedha hazikuidhinishwa |
| 20. | Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania | Kanuni za fedha zimepitwa na wakati hivyo hazikidhi mahitaji ya sasa |
| 21. | Makumbusho ya Taifa | Kanuni za fedha hazikuidhinishwa |
| 22. | Chuo cha Sukari cha Taifa | Kanuni za fedha zimepitwa na wakati hivyo hazikidhi mahitaji ya sasa |
| 23. | Mamlaka ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje | Kanuni za fedha zimepitwa na wakati hivyo hazikidhi mahitaji ya sasa |
| 24. | Baraza la ushindani | Kanuni za fedha zimepitwa na wakati hivyo hazikidhi mahitaji ya sasa |
| 25. | Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo | Hawakufanya mapitio ya sheria ya kuanzishwa kwa shirika pamoja na taratibu zake |

**Chanzo:** Taarifa za ukaguzi 2021/22

Kutokuwepo kwa nyenzo hizo kunaweza kuwa na madhara kwa taasisi ikiwa ni upungufu katika usimamizi wa vihatarishi, kutokuwajibika na kupungua kwa ufanisi katika utoaji wa huduma.

**Ninapendekeza kuwa mashirika ya umma na taasisi zingine (a) kushirikiana na mamlaka ya uteuzi kuteua bodi ya wakurugenzi au baraza (b) kuharakisha mchakato wa mapitio ya nyenzo zilizopitwa na wakati, na (c) kuwasilisha nyenzo hizo zilizohuishwa kwa Ofisi ya Raisi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kuidhinisha.**

### 10.5.2 Kutowasilisha taarifa za fedha na taarifa ya mwaka ya mapato kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni mtawalia

**(i) Mashaka katika usimamizi wa fedha wa Mfuko wa Maendeleo wa Michezo katika Baraza la Michezo Tanzania**

Nilibaini Baraza la Michezo Tanzania halikuandaa na kuwasilisha kwa ukaguzi taarifa za kifedha za Mfuko wa Maendeleo ya Michezo kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022. Mfuko huo ulianza utendaji tangu mwezi Oktoba 2021 na kupokea ruzuku kutoka serikalini ya shilingi bilioni 1.69 toka kuanzishwa kwake.

Hii ni kinyume na Sheria ya Baraza la Michezo Tanzania, Aidha, hali hii inapunguza uwezo wangu wa kuhakikisha kuwa masuala ya mfuko huo yanaratibiwa kwa maslahi bora ya umma na kuwa fedha hazikutumika vibaya.

**Ninapendekeza Baraza la Michezo Tanzania, kupitia Katibu Mkuu wa Baraza kuhakikisha linaandaa na kuwasilisha taarifa za fedha za Mfuko wa maendeleo ya michezo kwa ajili ya ukaguzi.**

**(ii) Kutowasilisha taarifa ya mapato ya mwaka kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni**

Nilibaini kwa miaka minne ya kifedha iliyopita, kampuni tanzu za Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (Kampuni ya gesi na Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL ) hazikuwasilisha taarifa ya mapato ya mwaka kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni kama inavyohitajika na Kifungu cha 128 cha Sheria ya Kampuni (Sura ya 212)

Hii ilitokana na ukosefu wa Bodi ya wakurugenzi kwa ajili ya kuidhinisha taarifa hizo. Kutowasilisha taarifa hizo kunaweza pelekea adhabu na faini kama ilivyoelezwa kwenye sheria ya kampuni na kusababisha matumizi yasiyofaa ya pesa kwa kampuni.

**Ninapendekeza kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kuwasiliana na mamlaka zinazoteua wajumbe wa bodi ili kuhakiksha wajumbe wa Kampuni ya gesi na Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL wanateuliwa.**

## 10.6 Maofisa wanaokaimu nafasi kwa muda wa zaidi ya miezi sita hadi miaka saba

Nilibaini mashirika ya umma na Taasisi zingine 14 walikuwa na maafisa 109 wanaokaimu kwa kipindi cha zaidi ya miezi 6 hadi miaka 7 kinyume na Agizo D.24 (3) la Kanuni za kudumu katika utumishi wa umma za mwaka 2009, kama ilivyoelezwa katika Jedwali 36. Hii ni tatizo linalojirudia ambalo liliripotiwa awali katika Taarifa yangu ya 2019/20 na 2020/21, ambapo mashirika ya umma na Taasisi zingine 33 na 22 walikuwa na maafisa wanaokaimu nafasi zao 175 na 155 zaidi ya miezi sita, mtawalia.

Nimegundua kuwa tatizo hili limetokana na kucheleweshwa kwa mchakato wa idhini kutoka Ofisi ya Rais ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa watu waliopendekezwa katika nafasi hizo.**Jedwali Na. 34**

**Jedwali Na. 34: Maofisa wanaokaimu katika nafasi zao zaidi ya miezi sita**

| Na. | Jina la Shirika | Idadi ya watumishi wanaokaimu | Muda wa kukaimu kuanzia miezi sita hadi |
|---|---|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Njombe | 5 | Miaka 7 |
| 2 | Kampuni ya Ndege Tanzania | 9 | Miaka 5 |
| 3 | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 13 | Miiaka 5 |
| 4 | Shirika la Habari la Taifa | 4 | Miaka 5 |
| 5 | Mamlaka ya Bandari Tanzania | 16 | Miaka 4 |
| 6 | Ofisi ya Taifa ya Takwimu | 9 | Miaka 4 |
| 7 | Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete | 6 | Miaka 4 |
| 8 | Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili | 6 | Miaka 3 |
| 9 | Chuo Kikuu cha Mzumbe | 13 | Miaka 3 |

| Na. | Jina la Shirika | Idadi ya watumishi wanaokaimu | Muda wa kukaimu kuanzia miezi sita hadi |
|---|---|---|---|
| 10 | Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu | 7 | Miaka 2 |
| 11 | Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori | 7 | Miaka 2 |
| 12 | Shirika la Mawasiliano Tanzania | 5 | Mwaka 1 |
| 13 | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima | 7 | Mwaka 1 |
| 14 | Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda | 2 | Mwaka 1 |
| | Jumla | 109 | |

**Chanzo**: Taarifa za ukaguzi 2021/22

Aidha, nilibaini Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Njombe na Kampuni ya Ndege Tanzania walikuwa na maofisa wanaokaimu nafasi zao kwa muda muda kati ya miezi sita hadi miaka saba.

Nilibaini kuwa Kampuni ya Ndege Tanzania, maofisa tisa wanaokaimu nafasi hizo hawakupata idhini ya kukaimu kutoka kwa katibu Mkuu (UTUMISHI). Aidha, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Njombe, maofisa wanaokaimu nafasi mbalimbali hawakuwa na sifa za kukaimu nafasi hizo

Ni maoni yangu kuwa maafisa ambao wanakaimu kwa muda mrefu wanaweza kupoteza hamasa na kujiamini katika utendaji wao, ambapo kwa upande mwingine inaweza kuathiri shughuli za taasisi.

**Ninapendekeza kuwa mashirika ya umma na taasisi zingine kwa kushirikiana na Mamlaka za Uteuzi wapewe kipaumbele kwenye mchakato wa kuidhinisha na / au kuteua wafanyakazi wenye sifa ili kuimarisha mashirika hayo na kutatua tatizo la kuwa na wafanyakazi wanaokaimu nafasi kwa muda mrefu.**

## 10.7 Mashirika ya umma na taasisi zingine 12 zenye upungufu wa wafanyakazi 4,547

Katika mwaka wa fedha 2021/22, nilibaini mashirika ya umma na taasisi zingine 12 zenye upungufu wa wafanyakazi 4,547 sawa na asilimia 43 ya kiwango cha wafanyakazi kilichopendekezwa **(Jedwali Na. 35).** Hii pia iliripotiwa katika ripoti zangu zilizopita za 2019/20 na 2020/21 ambapo kulikuwa na upungufu jumla wa wafanyakazi 4,592 na 8,356 katika mashirika ya umma na taasisi zingine 23 na 29, mtawalia.

**Jedwali Na. 35: Taasisi zenye upungufu wa wafanyakazi**

| Na. | Jina la taasisi | Wanaohitajika | Waliopo | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 4930 | 2734 | 2196 |
| 2. | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 2827 | 1378 | 1,449 |
| 3. | Chuo Kikuu Mzumbe | 926 | 619 | 307 |
| 4. | Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Dawa | 648 | 405 | 243 |
| 5. | Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania | 381 | 302 | 79 |
| 6. | Hifadhi ya Taifa Tanzania-Katavi | 160 | 82 | 78 |
| 7. | Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori | 163 | 99 | 64 |
| 8. | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Shinyanga | 150 | 87 | 63 |
| 9. | Ofisi ya Taifa ya Takwimu | 242 | 206 | 36 |
| 10. | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kigoma/Ujiji | 27 | 7 | 20 |
| 11. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ofisi za kanda) | 79 | 70 | 9 |
| 12. | Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano | 7 | 4 | 3 |
| | Jumla | **10,540** | **5,993** | **4,547** |

**Chanzo:** Taarifa ya Ukaguzi 2021/22

Ni maoni yangu kuwa, upungufu wa watumishi unahusishwa na kuchelewa kupata vibali vya ajira kutoka Ofisi ya Rais,

Menejimenti ya Utumishi wa Umma, na Utawala Bora. Hali hii inaathiri uwezo wa taasisi kutoa huduma bora na kufikia malengo waliyojiwekea.

**Ninapendekeza Serikali ihakikishe Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, na Utawala Bora itoe kipaumbele katika mchakato wa kutoa vibali vya ajira.**

## 10.8 Mashirika ya umma na taasisi zingine zenye mapungufu katika muundo wa taasisi na muundo wa maendeleo wa utumishi

Wakati wa ukaguzi nilibaini mapungufu katika muundo wa taasisi na muundo wa maendeleo wa utumishi katika mashirika ya umma na taasisi zingine nane.

(i) **Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi** waliomba idhini ya muundo mpya wa taasisi tangu Aprili 2018 lakini mpaka Oktoba 2022 bado muundo ulikuwa haujaidhiniswa. Hali hii inakwamisha kuhuisha muundo wa maendeleo wa utumishi.

(ii) **Ofisi ya Taifa ya Takwimu** hawajaanza kutumia muundo wa taasisi ulioidhinishwa tangu Novemba 2018 japokuwa muundo wa maendeleo wa utumishi ulishaidhinishwa toka Machi 2022.

(iii) **Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza** wanatumia muundo wa maendeleo wa utumishi uliouhishwa na mpango wa motisha uliouhishwa bila idhini ya Katibu Mkuu (UTUMISHI).

(iv) **Kampuni ya MCB** inaendesha shughuli zake bila muundo wa maendeleo wa utumishi

(v) Muundo wa taasisi wa **Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori** umepitwa na wakati hivyo muundo mpya unasubiri idhini ya Katibu Mkuu (UTUMISHI)

(vi) **Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati** inatumia muundo wa maendeleo wa utumishi wa Julai 2019 na mpango wa motisha wa Julai 2021 bila idhini ya Katibu Mkuu (UTUMISHI)

(vii) **Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibaiolojia Tanzania** hakijawahi kuwa na muundo wa maendeleo wa utumishi toka kuanzishwa kwa taasisi hiyo 2017.

(viii) Aidha, muundo wa maendeleo wa utumishi wa **kampuni ya Mkulazi** haukuendana na mahitaji ya kanuni za kudumu katika utumishi wa umma za mwaka 2009. Nilibaini Kampuni ya Mkulazi iliajiri watu 46 kwa masharti ya kudumu na ilibadilisha masharti ya ajira ya wafanyakazi sita kutoka mikataba kwenda kudumu bila kupata vibali vya ajira kutoka Ofisi ya Raisi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hii inapingana na matakwa ya Aya ya D.4 (2)(3) ya kanuni za kudumu katika utumishi wa umma za mwaka 2009.

Hii inatokana na juhudi hafifu za menejimenti katika kuhakikisha nyaraka muhimu za utawala zilizoidhinishwa na mamlaka husika zipo na zinatumika ipasavyo.

Ni maoni yangu kuwa kutotekelezwa muundo wa taasisi na muundo wa maendeleo wa utumishi kunaweza kupelekea kushuka kwa ufanisi wa taasisi. Malipo yanayotokana na miongozo ambayo haijaidhinishwa yanakosa uhalali wa kisheria na hayawezi kuthibitishwa.

**Ninapendekeza mashirika ya umma na taasisi zingine (a) kushirikiana na mamlaka za kuidhinisha ili kuhakikisha muundo wa shirika na muundo wa maendeleo wa utumishi inaidhinishwa, na (b) kuhakikisha muundo wa shirika ulioidhinishwa unatekelezwa baada tu ya kuidhinishwa (c) Ninapendekeza kuwa uongozi wa Kampuni ya Mkulazi kufuata taratibu za ajira kama ilivyoelekezwa na Ofisi ya Raisi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.**

## 10.9 Mapungufu katika usimamizi wa mikopo ya wafanyakazi katika mashirika ya umma na taasisi zingine

### 10.9.1 Kiasi kikubwa cha fedha ya mikopo ya wafanyakazi wa NHIF shilingi bilioni 41.42 bila kuwa na mfuko wa kuzungusha fedha

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa hadi tarehe 30 Juni 2022, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulikuwa na mikopo ya wafanyakazi ambao haujalipwa shilingi bilioni 41.42 , ambapo kiasi cha shilingi bilioni 11.18 kilikuwa ni mikopo mipya iliyotolewa wakati wa mwaka 2021/22 bila kuzingatia mahitaji ya Aya 1.4 cha Sera ya Mikopo ya Wafanyakazi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambapo kinahitaji mikopo kutolewa chini ya mfumo wa mfuko wa kukopa na kulipa. Aidha, nilibaini kupungua kwa ukwasi wa fedha wa mfuko huo hata hivyo mfuko uliongeza kikomo cha mikopo ya wafanyakazi.

Hii inatokana na usimamizi usioridhisha katika kutekeleza mahitaji ya sera ya mikopo ya wafanyakazi katika kuanzisha mfumo wa mfuko wa kukopa na kulipa uliosababisha kiasi kikubwa cha fedha kuwa mikopo ya wafanyakazi ambayo inaathiri ukwasi wa mfuko.

**Ninapendekeza Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya utekeleze Sera ya Mikopo ya Wafanyakazi kwa kuweka mfuko wa kurejesha mikopo ya wafanyakazi ili kuepuka kutumia fedha za uendeshaji kufadhili mikopo ya wafanyakazi na hivyo kuepuka kuathiri ukwasi wa mfuko.**

### 10.9.2 Mikopo ambayo haijarejeshwa na wafanyakazi katika Mamlaka ya Elimu Tanzania shilingi milioni 167

Nilibaini kuwa maofisa 10 wanadaiwa shilingi milioni 167 kwa kipindi cha kuanzia mwaka mmoja hadi 10 bila ya mpango madhubuti wa kurejesha mikopo hiyo.

Mikopo hiyo imebaki bila kulipwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo uhamisho na kustaafu kwa maofisa. Uongozi ulieleza

kuwa hatua zaidi zimepangwa kuchukuliwa ili kurejesha mkopo uliobaki ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kisheria. Kwa maoni yangu, ikiwa mikopo haitarudishwa kwa wakati, Mamlaka itapata hasara.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Elimu Tanzania ichukue hatua stahiki katika kukusanya mikopo iliyosalia ya wafanyakazi.**

## 10.10 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kutolipa mtaji wa hisa kwa kampuni tanzu ya kampuni ya gesi na kampuni ya uwekezaji ya TANOIL

Ukaguzi wangu wa kampuni tanzu za Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kwa mwaka wa fedha 2021/22, ulibaini kuwa kampuni ya gesi ina hisa 1,500 za shilingi milioni 1.00 kila moja nakufanya jumla ya thamani za hisa kufikia shilingi bilioni 1.5 zinazomilikiwa kwa asilimia 100 na Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania wakati Kampuni ya uwekezaji TANOIL ina hisa 50,000,000 za kawaida zenye thamani ya Shilingi 100 kila moja na jumla ya thamani za hisa ya Shilingi bilioni 5.00, zinazomilikiwa kwa asilimia 100 na Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania.

Kufikia tarehe 30 Juni 2022, mtaji usiolipwa ulifikia shilingi bilioni 1.50 kwa kampuni ya gesi na shilingi bilioni 5.00 kwa Kampuni ya uwekezaji TANOIL kutokana na kutokuwepo kwa bodi za wakurugenzi katika kampuni tanzu na hivyo kusababisha ufuatiliaji mdogo wa malipo ya mtaji wa hisa kwa kampuni husika. Kutolipwa kwa mtaji wa kampuni kunasababisha kampuni tanzu kutoweza kupata fedha kwa ajili ya kufadhili mtaji wa uendeshaji wa shughuli za uwanzishwaji wa kampuni.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Bodi ya Wakurugenzi wafanyie tathimini upya ya malengo ya kuanzishwa kwa kampuni tanzu hizo ili kukamilisha malipo ya mtaji wa hisa katika kampuni hizo.**

## 10.11 Mapungufu yaliyobainika katika mashirika ya umma katika kutunza rejista ya mali za kudumu kwenye mfumo wa (GAMIS)

Wizara ya Fedha na Mipango ilitoa waraka unaozitaka taasisi za umma zote kuweka takwimu zao kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS) ifikapo tarehe 31 Agosti 2021. Hata hivyo, katika ukaguzi, nilibaini kuwa taasisi za umma 28 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 36** zilikuwa hazitunzi kumbukumbu za mali za taasisi katika Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali, kinyume na maagizo ya Wizara ya Fedha na Mipango. Zaidi ya hayo, baadhi ya taasisi zilizokuwa zikitumia mfumo huo zilikuwa zikitumia sehemu ya mfumo huo kutokana na ukosefu wa namba za utambulisho wa mali pamoja na kushindwa kufanya uhakiki wa mali. Sababu kuu za kutofuata waraka na ukosefu wa uelewa na mafunzo kuhusu matumizi ya mfumo huo.

**Jedwali Na. 36: Orodha ya taasisi ambazo hazitumii GAMIS**

| Na. | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati |
| 2 | Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji |
| 3 | Mamlaka ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje |
| 4 | Chuo cha Usimamizi wa Fedha |
| 5 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Karatu |
| 6 | Shirika la Masoko la Kariakoo |
| 7 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Korogwe |
| 8 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Kyela |
| 9 | Baraza la Usimamizi Watumiaji Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu |
| 10 | Hospitali ya Taifa Muhimbili |
| 11 | Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila |
| 12 | Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili |
| 13 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Muleba |
| 14 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza |
| 15 | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya |
| 16 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Ngara |
| 17 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Nzega |
| 18 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga |
| 19 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tabora |
| 20 | Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania |
| 21 | Bodi ya Pamba Tanzania |
| 22 | Kampuni ya Mbolea Tanzania |

| | |
|---|---|
| 23 | Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania |
| 24 | Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania |
| 25 | Bodi ya Tumbaku Tanzania |
| 26 | Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu Katika Ukanda wa Kitropiki |
| 27 | Kampuni ya Ubungo Plaza |
| 28 | Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam na kampuni tanzu zake |

***Chanzo**: Taarifa za Fedha za Mashirika, 2021/22*

Ni maoni yangu kuwa utumiaji wa mfumo wa GAMIS kama nyenzo ya kutunza mali za kudumu una umuhimu mkubwa wa kutoa taarifa za kuaminika kuhusu utunzaji wa mali za umma tangu upatikanaji hadi uondoshaji wake.

Katika hali hii, kutotekeleza na kutokamilika kwa rekodi ya mali katika mfumo wa GAMIS kunakwamisha juhudi za Serikali kufikia malengo yake ya kutunza kumbukumbu za mali za taasisi zote.

**Ninapendekeza kuwa mashirika ya umma ambayo hayatumii mfumo wa GAMIS kutekeleza maagizo ya Serikali ili kuhakikisha takwimu zinazoripotiwa za mali za kudumu katika taarifa za fedha zinafanana na takwimu za mfumo wa GAMIS. Pia, nashauri Mlipaji Mkuu wa Serikali kutoa msaada wa mafunzo ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.**




# SURA YA KUMI NA MOJA

# USIMAMIZI WA KODI KATIKA MASHIRIKA NA TAASISI ZINGINE ZA UMMA

## 11.0 Utangulizi

Mamlaka ya Mapato Tanzania ina jukumu la kusimamia na kutekeleza sheria za kodi, ikiwa ni pamoja na Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148, na Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa Mamlaka na Taasisi Zingine za Umma zinazingatia sheria hizi za kodi kwa kutathmini, kukusanya, na kurekodi mapato yote ambayo sheria hizi zinatumika. Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi zimepewa mamlaka ya kusikiliza na kuamua masuala yanayohusiana na migogoro au rufaa za sheria za kodi. Kwa hiyo, uhusiano kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na mashirika na taasisi zingine za umma zinazolipa kodi ni moja ya usimamizi na uzingatiaji wa kanuni, ambapo Mamlaka ya Mapato inasimamia sheria za kodi na kutoa njia za kukata rufaa au utatuzi wa migogoro kupitia Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi.

Sura hii inafafanua kwa kina masuala yahusuyo uzingatiaji wa sheria za kodi na mapungufu katika usimamizi wa kesi za kodi katika mashirika ya umma kama ifuatavyo :-

## 11.1 Tozo ya riba na adhabu kutokana na kutofuata sheria za kodi shilingi bilioni 123.32

Mashirika na Taasisi Zingine za Umma sita zilitozwa riba na adhabu kwa kushindwa kuwasilisha marejesho ya kodi na kulipa kodi kwa tarehe zinazotakiwa kisheria kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 37**. Ucheleweshaji wa ulipaji wa kodi

ulisababishwa zaidi na changamoto za kifedha zinazozikabili taasisi na mashirika ya umma husika, hali hii inayoonesha umuhimu wa kusimamia fedha na kuhakikisha fedha za kutosha zinapatikana ili kutimiza wajibu wa kulipa kodi kwa wakati.

**Jedwali Na. 37: Riba na adhabu zilizotozwa kwenye mashirika ya umma**

| Na. | Jina la Taasisi | Tarehe ya Tathmini | Mwaka wa Fedha | Kiasi cha Riba/Adhabu Sh. (Milioni) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Mawasiliano Tanzania | 20-Mei-22 | 2018-2020 | 1,547.71 |
| | | 7-Agosti-22 | 2014-2015 | 170.10 |
| 2 | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma | 5-Mei-22 | 2016-2018 | 19,634.70 |
| | | 5-Mei-22 | 2015-2018 | 24,291.36 |
| | | 24-Mei-22 | 2019-2021 | 77,053.16 |
| 3 | Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine | 2020/21 | 2018-19 na 2019/20 | 20.63 |
| 4 | Shirika la Taifa la Maendeleo | 16 Machi 2022 | Feb 2021 mpaka Mei 2022 | 22.21 |
| 5 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | 2021/22 | 2021/22 | 515.98 |
| 6 | Chuo Kikuu cha Dodoma | 2021/22 | 2021/22 | 68.6 |
| | **Jumla** | | | **123,324.45** |

**Chanzo: Taarifa za ukaguzi za Taasisi husika**

Ucheleweshaji wa malipo ya kodi unaikosesha Serikali fursa ya kukusanya mapato kwa wakati na unasababisha matumizi yasiyo na tija kwa mashirika ya umma kutokana na malipo ya riba na adhabu.

**Ninapendekeza mashirika na taasisi zingine za umma kuainisha mtiririko wa fedha ili kulipa kodi husika na kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani ili kuhakikisha kuwa madai yote ya kodi yanayostahili kulipwa yanalipwa kwa wakati, kuhakikisha uzingatiaji wa sheria na kanuni katika kufanya maamuzi.**

## 11.2 Kodi ambazo hazijalipwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania shilingi bilioni 46.83

Wakati wa ukaguzi na mapitio katika uzingatiaji wa sheria za kodi, nilibaini kuwa Mashirika na Taasisi Zingine za Umma 13 hazikuwasilisha kodi mbalimbali zenye jumla ya shilingi bilioni 46.83 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kipindi kati ya siku 56 hadi miaka tisa kinyume na matakwa ya kifungu 84 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332, ambacho kinaelekeza kwamba kodi za zuio ziwasilishwe ndani ya siku saba. **Jedwali Na. 38** linaonesha mchanganuo wa kodi mbalimbali ambazo hazikuwasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania zikiwemo kodi ya ongezeko la thamani, kodi za zuio, kodi ya mapato na tozo ya mafunzo na maendeleo ya ufundi stadi.

**Jedwali Na. 38: Kodi mbalimbali ambazo hazikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kati ya siku 56 hadi miaka tisa**

| Na. | Jina la Taasisi | Kodi ya mapato (Gratuity) | Kodi ya Ongezeko la Thamani | Kodi ya Zuio | Kodi ya Mapato | Kodi ya ujuzi na maendeleo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Sh (Milioni) | | | | | |
| 1. | Shirika la Reli Tanzania | | | 611 | 22,100 | 15,600 | 38,311 |
| 2. | Hospitali ya Taifa Muhimbili | | | | 6,409 | | 6,409 |
| 3. | Mamlaka ya Bandari Tanzania | | | | 891 | | 891 |
| 4. | Kampuni ya Huduma ya Meli | | | 16.85 | 532.76 | 190 | 739.61 |
| 5. | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tabora | | | 22 | 170 | | 192 |
| 6. | Taasisi ya Ushauri Elekezi ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam | | 77.3 | | | | 77.3 |
| 7. | Shirika la Umeme Tanzania | | | 73.86 | | | 73.86 |
| 8. | Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania | 24.94 | | | 48 | | 72.94 |

| Na. | Jina la Taasisi | Kodi ya mapato (Gratuity) | Kodi ya Ongezeko la Thamani | Kodi ya Zuio | Kodi ya Mapato | Kodi ya ujuzi na maendeleo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Sh (Milioni) | | | | | |
| 9. | Kampuni ya Ubungo Plaza | | | | 25 | | 25 |
| 10. | Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa Tanzania | | | | 18.76 | 2.8 | 21.56 |
| 11. | Chuo cha Sukari cha Taifa | | | | 6.73 | | 6.73 |
| 12. | Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania | | | 5.24 | | | 5.24 |
| 13. | Chuo Kikuu Mzumbe | | 2.6 | 1.44 | | | 4.04 |
| | **Jumla** | **24.94** | **79.9** | **730.39** | **30,201.25** | **15,792.8** | **46,829.28** |

**Chanzo:** Taarifa za ukaguzi za mashirika husika

Kutolipwa kwa kodi kumesababishwa na ukosefu wa fedha katika Taasisi husika. Kutolipa kodi kunasababisha kuongezeka kwa gharama kwa mashirika na taasisi zingine za umma kutokana na uwezekano wa kulipa riba na adhabu zinazoweza kutozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

**Ninapendekeza mashirika na taasisi zingine za umma zizingatie sheria za kodi na kuhakikisha zinalipa kodi husika kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.**

## 11.3 Kodi zilizochelewa kulipwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania shilingi bilioni 5.09

Nilibaini mashirika na taasisi zingine za umma 18 zilichelewa kuwasilisha makato ya kodi ya jumla ya shilingi bilioni 5.09 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kama inavyotakiwa na kifungu cha 84(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332. Sheria ya kodi ya mapato inamtaka kila wakala wa kodi ya zuio kumlipa kamishna ndani ya siku saba baada ya kumalizika kwa kila mwezi

wa kalenda, kiasi chote cha kodi ambacho amekusanya kwa mwezi husika.

Kutolipa kodi kwa wakati kumechangiwa na menejimenti za taasisi husika ama kutozingatia matakwa ya sheria ya kodi au fedha za kodi zilizokusanywa kutumiwa kwa matumizi mengine kabla ya kulipwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

**Jedwali Na. 39** linaonesha mchanganuo wa kodi zilizocheleweshwa kwa siku kuanzia moja hadi siku 1095.

**Jedwali Na. 39: Ucheleweshaji wa kuwasilisha kodi Mamlaka ya Mapato**

| S/N | Jina la Taasisi | Makato ya Kisheria | Siku Zilizochelewa | Kiasi (Sh) (Milioni) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kampuni ya Mbolea Tanzania | Kodi ya Mapato | 365 - 1095 | 285.88 |
| 2. | Shirika la Umeme Tanzania | Kodi ya Zuio | 63 - 727 | 391.73 |
| 3. | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania | Kodi ya Mapato | 30 - 364 | 0.10 |
| 4. | Chuo cha Usafirishaji cha Taifa | Kodi ya Zuio | 131 - 343 | 143.76 |
| 5. | Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa | Kodi ya Mapato | 81 - 324 | 4.74 |
| 6. | Bodi ya Kahawa Tanzania | Kodi ya Zuio | 7 - 240 | 16.64 |
| 7. | Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji | Kodi ya Mapato | 24 - 115 | 54.09 |
| 8. | Chuo cha Ufundi Arusha | Kodi ya Mapato | 4 - 91 | 1.73 |
| 9. | Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania | Kodi ya Mapato | 5 - 81 | 54.29 |
| 10. | Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi | Kodi ya Mapato | 28 - 57 | 20.92 |
| 11. | Kampuni ya Mkulazi | Kodi ya Ujuzi na Maendeleo | 21 - 52 | 27.06 |
| 12. | Ofisi ya Taifa ya Takwimu | Kodi ya Zuio | 3 - 52 | 9.89 |
| 13. | Kituo cha Elimu Kibaha | Kodi ya Zuio | 26 - 36 | 26.93 |
| 14. | Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa Tanzania | Kodi ya Zuio | 8 - 32 | 3,932.13 |
| 15. | Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka | Kodi ya Mapato | 16 - 18 | 7.35 |

| S/N | Jina la Taasisi | Makato ya Kisheria | Siku Zilizochelewa | Kiasi (Sh) (Milioni) |
|---|---|---|---|---|
| 16. | Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo | Kodi ya Mapato | 1 - 15 | 0.45 |
| 17. | Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili | Kodi ya Zuio | 4 - 12 | 113.25 |
| 18. | Shirika la Posta Tanzania | Kodi ya makadirio | 2 - 8 | 0.44 |
| | **Jumla** | | | **5,091.34** |

**Chanzo:** Taarifa za ukaguzi za mashirika

Kuchelewa kuwasilisha kodi kwa Mamlaka ya mapato kunapelekea mashirika na taasisi zingine za umma kutozwa adhabu na riba na kuinyima Serikali fursa ya kukusanya fedha hizo kwa wakati.

**Ninapendekeza Mashirika na Taasisi Zingine za Umma zihakikishe zinawasilisha kodi kwa wakati kwa Mamlaka ya Mapato ili kuepuka kutozwa adhabu na riba.**

## 11.4 Migogoro ya kodi zenye thamani ya shilingi bilioni 126.95

Wakati wa ukaguzi nilibaini migogoro ya kodi kati ya mashirika ya umma na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kodi zenye thamani ya shilingi bilioni 126.95 kwa mwaka wa fedha 2021/22. Migogoro hiyo imepelekwa Bodi ya Rufaa za Kodi, Baraza la Rufaa za Kodi na kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kama inavyoonesha kwenye **Jedwali Na. 40**

**Jedwali Na. 40: Migogoro ya kodi kati mashirika ya umma na Mamlaka ya Mapato**

| Na | Jina la taasisi | Madai | Kiasi Sh. 'Bilioni' |
|---|---|---|---|
| 1 | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi | Rufaa ya Kodi Na. 313/2018 katika Bodi ya Rufaa za Kodi (TRAB) jijini Dar es Salaam. Mfuko umewasilisha rufaa kupinga uamuzi wa kodi ulioleta deni la kodi kwa Mfuko kwa mwaka wa fedha 2015/16 | 53.56 |
| | | Rufaa ya Kodi Na. 314/2018 katika Bodi ya Rufaa za Kodi (TRAB) jijini Dar es Salaam. Mfuko umewasilisha rufaa kupinga uamuzi wa kodi ulioleta deni la kodi kwa Mfuko kwa mwaka wa fedha 2016/17 | 9.90 |

| Na | Jina la taasisi | Madai | Kiasi Sh. 'Bilioni' |
|---|---|---|---|
| | | Rufaa ya Kodi Na. 73/2022 katika Bodi ya Rufaa za Kodi (TRAB) jijini Dar es Salaam. Mfuko umewasilisha rufaa kupinga uamuzi wa kodi ulioleta deni la kodi kwa Mfuko kama mwanahisa wa Kampuni ya Katani kwa kushindwa kwa Kampuni ya Katani na kampuni zake tanzu kulipa deni la kodi lililosemwa. | 33.22 |
| 2 | Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania | Mgogoro huo uliwasilishwa kwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi kwa mujibu wa kifungu 59 ya Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania, Sura ya 415. Wakala wa Meli Tanzania ana mapato yasiyokusanywa kutoka kwa wateja ambayo yana mgogoro, hivyo kuna kodi ya ongezeko la thamani ambayo haijawasilishwa Mamlaka ya mapato | 26.63 |
| 3 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Arusha | Mamlaka ya maji ina deni tarajiwa la kodi ya ongezeko la thamani na Tozo ya mafunzo na maendeleo ya ufundi stadi linalotokana na tathmini iliyofanywa na Mamlaka ya mapato kuanzia 2012/13-2015/16 ambalo bado lipo katika mgogoro. Kamishna amekata rufaa kwenye Baraza la Rufaa za Kodi kupinga uamuzi wa Bodi ya Rufaa za Kodi. | 2.36 |
| 4 | Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme | Rufaa Na. 376 ya 2021<br>Kampuni ilipinga matokeo ya ukaguzi wa kodi uliofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania | 0.03 |
| 5 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tanga | Ombi Na. 15 la mwaka 2021 kwa bodi la tarehe 31 Disemba, 2021. Mamlaka ya maji ilipinga matokeo ya ukaguzi wa kodi uliofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania | 1.25 |
| | **Jumla** | | **126.95** |

**Chanzo:** Taarifa za ukaguzi za taasisi husika kwa mwaka 2021/22

Aidha, nilibaini rufaa za Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi (NSSF) ziliondolewa kwenye Bodi ya Rufaa za Kodi

kwa maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya tarehe 25 Machi 2020, ambaye alielekeza taasisi za umma zisishitakiane katika vyombo vya mahakama bila idhini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kwa sasa rufaa hizo zinashughulikiwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa madhumuni ya upatanishi.

**Ninapendekeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuingilia kati na kuongeza kasi ya utatuzi wa migogoro hiyo.**

## 11.5 Kodi ya mapato na kodi ya zuio hazikukatwa kwenye malipo kiasi cha shilingi bilioni 4.12

Kifungu cha 7 cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332 kinaelekeza kwamba posho zote na malipo mengine yanayofanyika kutokana na ajira yatozwe kodi, hii ni pamoja na marupurupu ya ajira yasiyo ya moja kwa moja.

Wakati wa ukaguzi na mapitio katika uzingatiaji wa sheria za kodi nilibaini kuwa mashirika ya umma 16 hayakutoza kodi yenye thamani ya shilingi bilioni 4.12 kwenye malipo yaliyofanywa kwa wafanyakazi na watoa huduma, kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 41.**

Miongoni mwa sababu za kutotoza kodi ni menejimenti za mashirika husika kutozingatia matakwa ya sheria ya kodi na kukosa uelewa wa kutosha juu ya sheria za kodi.

**Jedwali Na. 41: Kodi ambazo hazikukatwa kwenye malipo**

| Na. | Jina la Taasisi | Aina ya kodi | Kiasi Sh Milioni |
|---|---|---|---|
| 1. | Mfuko wa SELF | Kodi mbalimbali ambazo hazijalipwa | 3,139.61 |
| 2. | Kampuni ya Ranchi za Taifa | Kodi ya zuio kwa malipo ya wasambazaji wa mifugo | 555.55 |
| 3. | Shirika la Posta Tanzania | Kodi ya mapato kwenye posho za masaa ya ziada | 172.39 |
| 4. | Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu | Posho na tuzo | 91.48 |
| 5. | Chuo cha Usimamizi wa Fedha | Kodi ya zuio kwenye posho | 25.90 |

| Na. | Jina la Taasisi | Aina ya kodi | Kiasi Sh Milioni |
|---|---|---|---|
| 6. | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Babati | Kodi ya zuio | 23.71 |
| 7. | Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko | Kodi ya zuio kwenye huduma | 21.16 |
| 8. | Shirika la Taifa la Maendeleo | Malipo kwa huduma za kitaaluma | 19.80 |
| 9. | Chuo Kikuu Mzumbe | Kodi ya zuio | 19.64 |
| 10. | Bodi ya Kahawa Tanzania | Kodi ya zuio | 16.47 |
| 11. | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira | Kodi ya mapato na kodi ya zuio | 13.13 |
| 12. | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi Wa Mazingira Bukoba | Kodi ya mapato na kodi ya mafunzo na maendeleo ya ufundi stadi | 9.17 |
| 13. | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania | Kodi ya zuio kwa ada ya wakurugenzi wasio wa muda wote | 5.33 |
| 14. | Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu Katika Ukanda wa Kitropiki | Kodi ya zuio | 2.68 |
| 15. | Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba | Kodi ya zuio kwenye malipo ya bidhaa na huduma | 0.67 |
| 16. | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania | Kodi ya zuio | 0.18 |
| | **Jumla** | | **4,116.87** |

**Chanzo: Taarifa za ukaguzi za mashirika husika**

Kutotoza kodi kunapelekea mashirika na taasisi zingine za umma kutozwa adhabu na kuinyima Serikali nafasi ya kukusanya fedha kwa njia ya kodi.

**Ninapendekeza mashirika na taasisi zingine za umma kutoza kodi kwenye malipo yanayofanywa kwa wafanyakazi na watoa huduma ambao wanastahili kutozwa kodi hiyo ili kutii sheria ya kodi.**

## 11.6 Mapungufu katika ukokotozi wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT)

Kodi ya Ongezeko la Thamani ni tofauti kati ya kodi inayokatwa kwenye mauzo na kodi inayokatwa kwenye manunuzi.

### (i) Kutofautiana kwa taarifa ya mapato yaliyotumika katika kukokotoa marejesho ya kodi ya ongezeko ya thamani shilingi bilioni 401.54

Katika mapitio yangu ya kodi ya mapato katika Mashirika na Taasisi Zingine za Umma kwa mwaka wa fedha 2021/22, nilibaini mapato yaliyoripotiwa katika marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani yalikuwa kidogo ikilinganishwa na mapato yaliyoripotiwa katika taarifa za fedha kwa shilingi bilioni 401.54 kama invyoonekana kwenye **Jedwali Na. 42**.

**Jedwali Na. 42: Kutofautiana kwa mapato kati ya taarifa za fedha na mrejesho wa kodi ya ongezeko la thamani**

| Jina la Taasisi | Maelezo | Mapato katika taarifa za fedha Sh. 'Bilioni' | Mapato Katika Mrejesho wa Kodi ya Ongezeko la Thamani Sh. ' Bilioni" | Tofauti Sh. 'Bilioni' |
|---|---|---|---|---|
| Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania | Mapato | 1,194.06 | 840.76 | 353.30 |
| Shirika la Taifa la Madini | Mapato | 38.14 | 11.97 | 26.17 |
| Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme | Mapato | 48.74 | 26.67 | 22.07 |
| Jumla | | 1,280.94 | 879.4 | 401.54 |

***Chanzo:*** *Mrejesho wa Kodi ya Ongezeko la Thamani, Taarifa za Fedha za Mashirika*

Katika Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) nilibaini kuwa mapato yaliyorekebishwa kwa mwaka wa fedha na mapato yanayotokana na mikataba ya makubaliano ya kugawana faida hayakujumuishwa kwenye taarifa ya marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani ambayo yalikuwa miongoni mwa sababu za utofauti. Hii inaweza kusababisha upotevu wa fedha za Serikali kwa njia ya kodi, pia inaweza kusababisha adhabu kwa mashirika

ya umma yaliyobainishwa endapo mapato yaliyooneshwa kwenye taarifa za marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani si halisi.

**Ninapendekeza mashirika ya umma yaliyobainika yazingatie sheria za kodi na kuhakikisha mapato yaliyoripotiwa katika taarifa za marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani yanakuwa na halisia, kuepuka kulipa kodi pungufu, na kuepuka adhabu na riba za kulipa kodi pungufu.**

### (ii) Kutofautiana kwa kodi ya mapato katika taarifa za marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani shilingi bilioni 3.52

Nilibaini kuwa kodi ya mapato iliyoripotiwa katika taarifa za fedha za Shirika la Mawasiliano Tanzania, na katika taarifa za marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani kiasi cha shilingi bilioni 36.82, inatofautiana na kodi ya mapato katika mfumo wa Serikali (Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (ERCS)) unaotumika kurekodi mapato yanayohusiana na sekta ya simu (shilingi bilioni 33.30) kwa shilingi bilioni 3.52.

Kasoro hii inatokana na kuchelewa kufanya usuluhisho kati ya kodi iliyopo kwenye taarifa za fedha, ambazo zipo kwenye taarifa za marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani dhidi ya Mfumo Serikali wa Ukusanyaji wa Mapato ya Kielektroniki (ERCS).

Hii inaweza kusababisha kutokuwa sahihi kwa taarifa ya kodi ya ongezeko la thamani iliyoripotiwa katika taarifa ya marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani na inaweza kusababisha kulipwa kwa riba na adhabu kama haitawasilishwa kwa wakati.

**Ninapendekeza Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) lifanye usuluhishi wa taarifa za kodi ya ongezeko la thamani kati ya taarifa ya marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani na Mfumo Serikali wa Ukusanyaji wa Mapato wa Kielektroniki (ERCS).**

## 11.7 Mashirika na Taasisi Zingine za Umma kutodai kodi ya ongezeko la thamani na kodi zingine kwa wakati

### 11.7.1 Deni la kodi ya ongezeko la thamani ambalo Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma unadai kwa muda mrefu shilingi bilioni 6.49

Kifungu cha 71 (1) & (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 kinaeleza kuwa mtu ama taasisi inaweza kuomba kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato kurejeshewa kodi aliyolipa zaidi kwa kuonesha ukokotozi sahihi wa kodi pamoja na kuambatisha ushahidi wa madai.

Wakati wa ukaguzi na mapitio katika uzingatiaji wa sheria za kodi, nilibaini kuwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ulikuwa unadai kodi ya ongezeko la thamani shilingi bilioni 6.49 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022, ambapo Mfuko uliomba kurejeshewa shilingi bilioni 1.38, na kiasi kilichobakia cha shilingi bilioni 5.11 hakikuombwa kurejeshwa, badala yake Mfuko ulipanga kutumia bakaa hiyo kulipia kodi za baadaye. Mfuko uliishirikisha Mamlaka ya Mapato Tanzania katika maombi ya kuweza kutumia bakaa kupunguza kodi ya baadaye.

Kutokana na kuunganishwa kwa mifuko ya hifadhi ya jamii mwaka 2018, Mfuko unaweza kupoteza madai yake ambayo bado haujayakusanya ikiwa mfuko hautatumia bakaa hiyo, kwa sababu madeni hayo yamekaa bila kulipwa kwa miaka minne toka mifuko ilipounganishwa hadi mwezi Juni 2022.

**Ninapendekeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ufanye ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha unatumia bakaa ya madai yake ya kodi bila kuchelewa.**

### 11.7.2 Kodi ya ongezeko la thamani katika manunuzi ambayo haijadaiwa shilingi bilioni 1.48

Kifungu cha 69 (1) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148 kinaeleza kuwa mlipa kodi anaruhusiwa kutoa kodi

aliyoilipa katika manunuzi kwenye kodi aliyoikusanya kwenye mauzo kukokotoa kiasi cha kodi ya ongezeko la thamani kinachotakiwa kulipwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ndani ya miezi sita.

Wakati wa ukaguzi katika Shirika ya Mawasiliano Tanzania, nilibaini kiasi cha kodi cha shilingi bilioni 6.43 ambacho shirika lilipa kwenye malipo ya manunuzi ambacho hakikutolewa kwenye kodi iliyoikusanya kwenye mauzo hadi kufikia Juni 2022. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 6.05 kilikuwa ndani ya miezi sita ambapo shirika linaruhusiwa kuidai kwa kuitoa kwenye kodi iliyoikusanya kwenye mauzo. Hivyo kulikuwa na kodi ya shilingi milioni 375.22 ambayo haikutolewa kwenye kodi ya makusanyo ya mauzo. Mapungufu haya yanasababishwa na kutokurekodi miamala pale inapotokea na kuchelewa kupeleka taarifa ya marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani. Shirika lisipodai kodi ambayo ililipa kwenye manunuzi, litashindwa kupunguza mzigo wa kodi linayotakiwa kuilipa.

Pia, nilibaini kampuni ya TANOIL Investment Ltd ilikuwa na manunuzi yanayostahili kutozwa kodi kiasi cha shilingi bilioni 6, lakini ilitoa taarifa ya manunuzi yanayostahili kutozwa kodi kiasi cha shilingi bilioni 4.9. TANOIL Investment Ltd inaweza kushindwa kudai kodi iliyoilipa kwenye manunuzi ya shilingi bilioni 1.1 ambayo taarifa yake haikuwasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka wa fedha 2021/22.

**Ninapendekeza Mashirika na Taasisi Zingine za Umma zihakikishe zinatoa taarifa ya kodi zilizolipa kwenye manunuzi ndani ya muda ulioainishwa kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani.**

## 11.8 Makadirio ya chini ya uhalisia wa kodi inayotakiwa kulipwa shilingi bilioni 1.82

Ukaguzi wangu wa Shirika la Posta Tanzania ulibaini makadirio ya chini ya kodi inayotakiwa kulipwa, ambapo kodi iliyotakiwa kulipwa kwa mujibu wa mrejesho wa mapato ni shilingi bilioni 1.85, wakati kodi iliyotakiwa kulipwa kwa mujibu wa malipo ya

awamu kwa mwaka wa fedha 2021/22 ni shilingi milioni 30, hivyo kupelekea tofauti ya shilingi bilioni 1.82.

Makadirio ya chini ya uhalisia wa kodi inayotakiwa kulipwa yanasababisha upotevu wa mapato kwa Serikali. Pia, shirika linakuwa katika hatari ya kutozwa riba kwa kukadiria mapato kwa kiwango cha chini ya uhalisia. Nilibaini Shirika lilitozwa riba ya shilingi milioni 120.44 kwa mujibu wa kifungu namba 75 cha Sheria ya usimamizi wa Kodi Sura ya 148 kwa kukadiria mapato chini ya kiwango halisi kwa shilingi bilioni 1.82.

**Ninapendekeza Shirika la Posta liwe na utaratibu wa kukadiria kwa ufasaha kiwango cha kodi kinachotakiwa kulipwa kwa awamu.**

## 11.9 Kutotoza kodi ya jengo kwa wateja 6,188 wa malipo baada ya matumizi na wateja 356,286 wa luku

Mamlaka ya Mapato Tanzania imeweka utaratibu wa kukusanya kodi ya majengo kupitia Shirika la Umeme Tanzania kwa kuingiza tozo za kodi ya majengo katika akaunti ya mita ya mteja kiasi kwamba mteja anaponunua nishati kila mwezi hukatwa shilingi 1,000 na shilingi 5,000 kwa mteja mwenye jengo la kawaida na kwa kila sehemu kwa jengo la ghorofa, mtawalia.

Mapitio yangu ya tozo za kodi ya majengo kwa wateja waliotathminiwa kwa sampuli kutoka mikoa 23 kwa mwaka 2021/22 yalibaini kuwa wateja 6,188 wa malipo baada ya huduma, hawakutozwa kodi ya majengo kwa sababu mfumo wa malipo haujasanidiwa kutoza kodi ya majengo na wateja 356,286 wa LUKU (sawa na asilimia 14 ya wateja wote katika mikoa 23) pia hawakutozwa kodi ya majengo. Serikali inapoteza mapato kwa kutokutoza kodi ya majengo kwa wateja.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme lihakikishe wateja wote wanaostahili ikiwa ni pamoja na wateja wanaolipa baada ya kutumia na wateja wanaolipa kabla ya kutumia wanatozwa kodi ya majengo kwa kusanidi tozo kwenye akaunti.**

## 11.10 Kampuni ya kutengeneza nguzo za zege Tanzania (TCPM) haijasajiliwa kwa ajili ya kukusanya kodi ya ongezeko la thamani

Usajili wa kodi ya ongezeko la thamani ni lazima kwa kila taasisi/kampuni baada ya kufikia kiwango cha usajili cha shilingi milioni 100 kwa mauzo katika kipindi cha miezi kumi na mbili, na shilingi milioni 50 katika kipindi cha miezi sita inayoishia mwishoni mwa miezi iliyopita.

Katika mwaka 2021/22 kampuni ya kutengeneza nguzo za zege Tanzania ilipata mapato yenye thamani ya shilingi milioni 645, hivyo kufikia kiwango cha usajili wa kodi ya ongezeko la thamani. Licha ya kufikia kiwango hicho, kampuni hiyo haikusajiliwa kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani.

Kampuni haiwezi kudai kodi kiasi cha shilingi milioni 109.03 ambayo ilistahili kudaiwa kutoka kwenye manunuzi ya shilingi milioni 605.70 ambayo ndani yake yalikuwa na kodi ya ongezeko la thamani. Pia Kampuni haitaweza kulipa kodi ya ongezeko la thamani ambayo ni tofauti ya kodi kwenye mauzo na kodi kwenye manunuzi.

**Ninapendekeza kuwa kampuni ya kutengeneza nguzo za zege Tanzania (TCPM) ifanye ufuatiliaji katika Ofisi za Mamlaka ya Mapato kwa ajili ya usajili wa Kukusanya Kodi ya Ongezeko la Thamani.**

## 11.11 Kuchelewa na kutowasilisha marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania

Kifungu cha 66(1) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148 kinaeleza kuwa, mtu anayetozwa kodi atawasilisha marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani siku ya 20 ya mwezi baada ya kumalizika kwa kipindi cha kodi kinachohusiana.

Kifungu cha 84 cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332 kinamtaka wakala wa zuio kuwasilisha kwa Kamishna, ndani ya

siku saba za mwezi unaofuata mwezi ambao kodi inahusiana, taarifa ya kodi ya zuio kwa mwezi wa kalenda.

Wakati wa mapitio, nilibaini mashirika na taasisi zingine za umma nne zilichelewa kuwasilisha marejesho ya kodi kwa kipindi cha siku moja hadi 435 kama inavyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 43.**

Katika kampuni ya ujenzi na matengenezo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme kuchelewa kulitokana na mfumo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kushindwa kufanya kazi hivyo Mamlaka ilitoa nyongeza ya muda kuanzia tarehe 20 Juni 2022 hadi tarehe 28 Julai 2022. Licha ya nyongeza iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, kampuni hiyo bado ilichelewa kujaza na kupeleka marejesho ya kodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Kuchelewa kuwasilisha marejesho ya kodi ya ongezeka la thamani hupelekea kutozwa riba ya kucheleweshwa kwa malipo ya kodi na adhabu kwa kutofuata sheria.

**Jedwali Na. 43: Kuchelewa na kutokujaza marejesho ya kodi**

| Na | Jina la Taasisi | Aina ya Kodi | Siku zilizochelewa | Kiasi Sh. (Milioni) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania | Kodi ya Ongezeko la Thamani | 101-435 | 838.03 |
| 2 | Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania | Kodi ya Ongezeko la Thamani | Hakuwasilisha marejesho ya kodi | 120.69 |
| 3 | Shirika la Posta Tanzania | Kodi ya Mapato | 1-61 | 27.14 |
| | | Kodi ya Ongezeko la Thamani | 1-21 | 5.45 |
| 4 | Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme (ETDCO) | Kodi ya Ongezeko la Thamani | 2 | 20.10 |
| | **Jumla** | | | **1,011.41** |

**Chanzo: Taarifa za marejesho ya kodi ya Mamlaka ya Mapato**

**Ninapendekeza Mashirika na Taasisi Zingine za Umma kuhakikisha taarifa za marejesho ya kodi zinajazwa kwa**

**wakati na kuwasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato nchini ili kuepuka adhabu na riba zisizo za lazima.**

## 11.12 Mapato na malipo yasiyoambatanishwa na risiti za kodi za kielektroniki shilingi milioni 556.83

Kanuni ya 28 ya Kanuni za Kifaa cha Kielektroniki za Kodi ya Mapato, 2012 inamtaka kila mnunuzi kudai na kubaki na risiti au ankara katika miliki yake.

Aidha, Kanuni ya 21 hadi 25 ya Kanuni hiyo inaelekeza kuwa mtu yeyote atakayeshindwa kudai, kuhifadhi au kutoa risiti ya fedha au ankara ya fedha anatenda kosa na endapo akikutwa na hatia anawajibika kulipa mara mbili ya kiasi cha kodi kilichokwepwa/kutolipwa.

Ukaguzi wangu ulibaini malipo yaliyofanywa na mashirika na taasisi zingine za umma 11 kununua bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi milioni 556.83, lakini malipo hayakuambatanishwa na risiti ya kodi ya kielektroniki ( **Jedwali Na. 44).**

**Jedwali Na. 44: Malipo yasiyoambatanishwa na risiti za kodi za kielektroniki**

| Na | Jina la Taasisi | Kiasi Sh. (Milioni) |
|---|---|---|
| 1 | Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Dawa | 67.42 |
| 2 | Chuo cha Usafirishaji cha Taifa | 139.59 |
| 3 | Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko | 68.12 |
| 4 | Bodi ya Usajili wa Wahandisi | 15.93 |
| 5 | Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania | 7.26 |
| 6 | Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu katika Ukanda wa Kitropiki | 46.78 |
| 7 | Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo | 57.43 |
| 8 | Bodi ya Korosho Tanzania | 78.61 |
| 9 | Chuo cha Sukari cha Taifa | 11.60 |
| 10 | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania | 53.77 |
| 11 | Bodi ya Mkonge Tanzania | 10.32 |
| | **Jumla** | **556.83** |

Aidha, Katika Baraza la Ujenzi la Taifa nilibaini kuwa Baraza lilitoza shilingi milioni 720.16 kwa wateja bila kutoa risiti kwa kutumia mashine ya kodi ya kielektroniki.

Aidha, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kilifanya malipo ya shilingi milioni 51.79 kwa watoa huduma na malipo hayo yaliambatana na risiti ambazo hazikuonesha jina la mnunuzi na namba ya utambulisho ya mlipa kodi ya mnunuazi. Hivyo risiti hizo hazikuzingatia matakwa ya kanuni za Kifaa cha Kielektroniki za Kodi ya Mapato, 2012.

Mashirika na taasisi zingine za umma zinaweza kutozwa adhabu kwa kushindwa kudai na kubaki na risiti au ankara, pia kodi iliyolipwa kwenye manunuzi haiwezi kudaiwa bila ya risiti ya kodi ya kielektroniki, hivyo kodi hiyo ya manunuzi itakuwa gharama kwa taasisi husika. Pia, Serikali inapoteza mapato ambayo ingeyapata kwa njia ya kukusanya kodi kwa risiti za kifaa cha kielektroniki.

**Ninapendekeza kuwa mashirika na taasisi zingine za umma zizingatie sheria ya usimamizi wa kodi** na **kanuni zake kwa kudai na kuhifadhi risiti ya manunuzi.**




# SURA YA KUMI NA MBILI

## MWENENDO WA BENKI ZINAZOMILIKIWA NA SERIKALI NA TAASISI ZINGINE ZA KIFEDHA

## 12.0 Utangulizi

Nilipitia kwa kina utendaji wa Benki zinazomilikiwa na Serikali, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, na Taasisi zinazojishughulisha na masoko ya mitaji na Dhamana nchini Tanzania. Katika tathmini yangu, nilibaini maeneo yenye mapungufu kadhaa kwenye taasisi hizo, hivyo maboresho katika maeneo yaliyokutwa na mapungufu ni muhimu ili kujihakikishia utendaji bora wa taasisi hizo.

Kwa upande wa Benki zinazomilikiwa na Serikali, nilibaini mapungufu katika usimamizi wa mikopo, ukwasi usiojitosheleza, kupungua kwa faida kwa benki za Serikali, tathmini dhaifu kwenye dhamana za mikopo, mifumo hafifu ya kudhibiti gharama za uendeshaji, na kutozingatia matakwa na taratibu za udhibiti. Masuala haya lazima yashughulikiwe ili kuhakikisha uhai wa benki ili ziendelee kuchangia maendeleo ya uchumi.

Aidha kuhusu mifuko ya hifadhi ya jamii, tathmini yangu ilibaini usimamizi duni wa vitega uchumi, usimamizi usioridhisha wa mikopo inayotolewa kwa Taasisi za Serikali, kutojitangaza vya kutosha kwa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Masuala haya yote lazima yashughulikiwe ili kuhakikisha mifuko inaweza kutoa mafao na malipo ya kutosha kwa wanachama wao na kuchangia ustawi wa jamii kwa ujumla.

Kwa ujumla, ni muhimu Benki na Mifuko ya Hifadhi za Jamii vishughulikie mapungufu yaliyoainishwa ili kuboresha utendaji na utoaji wa huduma bora, hivyo kuhakikisha taasisi zinabaki hai na endelevu kwa muda mrefu. Aidha kuboresha mbinu za

usimamizi, kuendana na matakwa ya udhibiti, na kuimarisha uwazi na uwajibikaji ni muhimu katika kufikia malengo yaliyokusidiwa na taasisi hizi.

## 12.1 Wasiwasi juu ya utendaji wa Benki za Serikali kwenye usimamizi wa mikopo, mikopo chechefu, utoshelevu wa ukwasi na uwiano wa utoshelevu wa mitaji

Nilipitia utendaji wa benki nne za biashara za serikali ambazo ni Benki ya Maendeleo ya TIB, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania, Benki ya Azania, na Benki ya Biashara Tanzania, na kubaini masuala kadhaa yanayohitaji juhudi za kipekee ili kuzikwamua benki hizi kama yalivyoelezwa hapa:

Mwaka 2022 Benki ya Maendeleo ya TIB iliendelea kupata hasara kabla ya kodi ya shilingi bilioni 131.07 (2021: shilingi bilioni 10.57). Huku sababu ikiwa ni hasara ya mikopo isiyokidhi viwango yaani mikopo chechefu. Wakati huo huo mwaka 2022 Benki ya Maendeleo ya Kilimo ilipata faida ya shilingi bilioni 15.64 ikilinganishwa na shilingi bilioni 16.03 iliyopatikana mwaka 2021 upungufu wa shilingi milioni 390.

Aidha, mapitio yangu kuhusu mikopo chechefu kwa benki tatu za biashara za serikali ambazo ni Benki ya Maendeleo ya TIB, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania na Benki ya Azania nilibaini kuwa uwiano wa mikopo chechefu hadi tarehe 31 Desemba 2022 ulikuwa kati ya asilimia 5.86 hadi asilimia 20.32, wakati kwa Benki ya Biashara Tanzania hadi tarehe 31 Desemba 2021 ilikuwa asilimia 9.87 ambayo ni kubwa kuliko kiwango kinachokubalika na Benki Kuu ambacho hakizidi asimia 5. Vilevile, mwaka 2022 mapitio yangu ya Benki ya Maendeleo ya TIB, Benki ya Mendeleo ya Kilimo na Benki ya Azania kwa pamoja zilikuwa na mikopo chechefu ipatayo shilingi bilioni 278.93 ikilinganishwa na shilingi bilioni 430.61 za mwaka 2021. Kupungua kwa mikopo chechefu kulitokana na kutengwa nje ya taarifa za fedha kwa mikopo iliyokuwa haina viwango iliyotolewa ya kiasi cha shilingi bilioni 357.80 kwa benki tatu zilizotajwa hapo. Wakati huo huo Benki ya

Biashara Tanzania ilikuwa na mikopo chechefu ya shilingi bilioni 70.06 kwa mwaka 2021.

Pia, mwaka 2022 Benki ya Maendeleo ya TIB ilikuwa na uwiano wa utoshelevu wa mtaji mkuu na mtaji wote kwa mali zenye uzani wa hatari wa asilimia 1.4 (2021: asilimia 4.4) ukilinganisha na kiwango kinachotakiwa na Benki Kuu cha asilimia isiyopungua 13 kwa uwiano wa utoshelevu wa mtaji mkuu kwa mali zenye uzani wa hatari na asilimia 15 kwa uwiano wa utoshelevu wa mtaji wote kwa mali zenye uzani wa hatari. Wakati huo huo mali za benki zilishuka hadi shilingi bilioni 431.13 kutoka shilingi bilioni 629.08 za mwaka 2021 ambao ni upungufu wa shilingi bilioni 197.95 sawa na asilimia 31.46 na hii ilitokana na kupungua kwa mikopo. Benki ilikuwa na malimbikizo ya hasara ya shilingi bilioni 212.27 (2021: shilingi bilioni 141.88).

**Ninapendekeza kuwa serikali ichukue hatua za haraka kushughulikia masuala yanayozikabili benki hizi, ikiwa ni pamoja na kuongeza mtaji wa ziada, kuboresha udhibiti wa matumizi, na kupunguza uwiano wa mikopo chechefu ufikie kiwango kinachokubalika.**

## 12.2 Mapungufu katika usimamizi wa mikopo na dhamana katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Benki ya Biashara Tanzania

Nilibaini mapungufu kadhaa katika usimamizi wa mikopo na dhamana katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo na Benki ya Biashara Tanzania, ambayo yanaweza kuongeza mikopo isiyolipika, na kusababisha ukiukwaji wa matakwa ya udhibiti.

**(i) Usimamizi duni wa dhamana katika Benki ya Maendeleo ya Kilimo:** Nilibaini baadhi ya dhamana hazikusimamiwa na kufuatiliwa ipasavyo hivyo kusababisha taarifa za tathimini ya dhamana kutohuishwa na rejista za dhamana kutokuwa kamilifu. Kwa mfano, nilikuta dhamana tatu za wateja zenye thamani ya shilingi bilioni 3.91 zikiwa zimepitwa na wakati kwa kati ya mwaka mmoja hadi miwili, ilipofika Desemba 2021. Pia, nilibaini

kulikuwa na dhamana yenye thamani ya shilingi bilioni 1.13 iliyotolewa na mthamini ambaye hakuidhinishwa na Benki Kuu ya Tanzania. Hali hii inaweza kusababisha hasara kwa benki iwapo wakopaji watashindwa kulipa mikopo husika.

**Ninapendekeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania iboreshe taratibu za kutsthmini dhamana ili kuongeza usahihi na kuhakikisha tathmini hazipitwi na wakati, pia benki iwe na rejista za dhamana zilizohuishwa na zenye taarifa kamili.**

(ii) **Mapungufu kwenye usimamizi wa mchakato wa mikopo na ufuatiliaji wake:** Nilibaini tathmini ya mikopo na ufuatiliaji kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo haikujumuisha vipengele muhimu kama vile ukadiriaji wa viashiria vya hatari ilivyojiwekea kwa ajili ya kutoa mikopo, kiwango cha chini cha faida ya miradi husika, na ufuatiliaji wa viashiria vya utendaji wa miradi. Hali hii inaweza kuiweka benki kwenye hatari kubwa ya kuwa na mikopo yenye shida hivyo kusababisha hasara hapo baadaye. **Ninapendekeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo iboreshe mfumo wake wa tathmini na ufuatiliaji wa mikopo ili ujumuishe vipengele muhimu vilivyoainishwa kwenye suala hili.**

(iii) **Tathmini isiyofaa ya mikopo ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo:** Benki ya Maendeleo ya Kilimo haikuwa na ushahidi wa kufanya tathmini juu ya hali ya miradi ya wakopaji, ambacho ni kipimo muhimu katika kuainisha mikopo. Hali hii inaweza kuinyima benki taarifa muhimu kwa ajili ya kufanya maamuzi sahihi kuhusiana na usimamizi wa mikopo.
**Ninapendekeza Benki ya Maendeleo ya Kilimo ijumuishe katika sera yake ya mikopo mambo muhimu kuhusu tathmini ya hali ya miradi ya wakopaji ili kusaidia kufanya maamuzi sahihi.**

(iv) **Mapungufu ya usimamizi wa mikopo katika benki ya biashara Tanzania:** Benki ya Biashara Tanzania haikuzingatia kanuni za benki kuhusiana na viwango vya riba kwa mikopo ya wafanyakazi wake wa zamani, kwani walihama wakiwa na mikopo yenye thamani shilingi milioni 57.2 lakini waliendelea kutozwa viwango vya riba sawa na wafanyakazi wa benki, badala ya kutozwa riba

ya kiwango cha kibiashara. Pia nilibaini riba haikusitishwa kwenye mikopo chechefu na mikopo chechefu ya shilingi bilioni 15.62 haikutengwa nje ya taarifa za fedha . Hii inaweza kuiweka benki kwenye hatari hivyo kupelekea kupata hasara.

**Ninapendekeza Benki ya biashara Tanzania ifuatilie mikopo ya wafanyakazi wa zamani ili ilipwe kwa riba ya kiwango cha biashara, isimamishe riba kwa mikopo chechefu, na kuitenga mikopo chechefu nje ya taarifa za fedha kama inavyotakiwa na Benki kuu ya Tanzania.**

## 12.3 Mapungufu katika utendaji wa Bodi ya Bima ya Amana katika kulinda maslahi ya wenye amana

Ukaguzi wangu wa utendaji kazi wa Bodi ya Bima ya Amana katika kulinda maslahi ya wenye amana ulibaini mapungufu kadhaa kama ilivyoainishwa hapa chini:-

- Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Bodi ya Bima ya Amana inafanya kazi chini ya uwiano unaohitajika wa ukubwa wa mfuko kwa jumla ya amana zenye bima. Kwa sasa Bodi ya Bima ya Amana ina uwiano wa asilimia 3.31 ambao ni kiwango cha chini kinachoathiri mchango wa Bodi kwenye utangamano wa kifedha nchini. Bodi inatakiwa kufikisha uwiano wa asilimia 20 kama ilivyokubaliwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki ifikapo 2025 ili kuweza kuwalinda vya kutosha wenye amana endapo benki zitafilisika.

- Bodi ya Bima ya Amana haina mpango madhubuti wa kukusanya wa mikopo hivyo kupelekea ukusanyaji usioridhisha pamoja na kukabiliwa na jukumu kubwa la kukusanya mikopo kutoka katika benki saba zilizofilisika. Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita (2017 hadi 2022) Bodi ya Bima ya Amana kama mfilisi iliweza kukusanya shilingi bilioni 47.12 tu kati ya shilingi bilioni 206.59 zilizotarajiwa kukusanywa kutoka kutika benki saba zilizofilisika ambayo ni asilimia 23. Upungufu huu unapunguza uwezo wa Bodi ya Bima ya Amana wa kutathmini na kufuatilia shughuli za ukusanyaji. Ninapendekeza kwamba Bodi ya Bima ya Amana

iandae mpango kazi wenye malengo na muda maalumu wa kukusanya mikopo na kuwezesha kuuzwa kwa mali za benki zilizofilisika.

- Gharama kubwa zinazohusu ufilisi wa benki saba zilizofikia shilingi bilioni 5.12 huku kukiwa na wasiwasi wa maslahi ya wadai kutolindwa ipasavyo kwa sababu makusanyo yalikuwa shilingi bilioni 5.30, hivyo kiasi kikubwa cha pesa iliyokusanywa kilichotumika kama gharama za kazi ya kukusanyia mikopo hiyo. Bodi ya Bima ya Amana lazima isimamie na kupunguza gharama za ufilisi ziwe kwenye viwango vya chini vinavyokubalika, pia iangalie uwezekano wa kuwatumia mawakala wa kukusanya madeni ambao watalipwa kulingana na ufanisi wa kazi badala ya kuajiri wafanyakazi wa kudumu wanaolipwa malipo bila kuzingatia ufanisi wao.

**Ninapendekeza Bodi ya Bima ya Amana ichukue hatua za haraka kushughulikia mapungufu haya na kuhakikisha maslahi ya wenye amana yanalindwa ipasavyo.**

## 12.4 Usimamizi na utendaji duni wa mikopo inayotolewa na Mfuko wa SELF

Nilikagua utendaji wa Mfuko wa SELF na kubaini usimamizi na utendaji duni katika mikopo, hususan mikopo chechefu yenye thamani ya shilingi bilioni 5. Mikopo isiyolipika ilivuka ukomo uliowekwa na Mwongozo wa utaratibu wa mikopo ambayo inatakiwa kuwa chini ya asilimia 5, huku nikibaini mikopo kwa taasisi moja moja ilikuwa na kiwango hatarishi cha kati ya asilimia 7.91 hadi 57.84 katika mikoa nane niliyoifanyia tathimini. Hali hii ya mikopo ilisiyolipika inaweza kusababisha hasara na huenda ikakupunguza mtaji wa Mfuko, jambo ambalo ni kinyume na mwongozo wa Mfuko wa SELF.

Aidha, Mfuko wa SELF ulikopesha jumla ya shilingi milioni 550.86 kwa mashirika mawili, ambayo ni Lubala SACCOS; na FINI Financial and Real Estate Agency Services Company Limited, lakini mikopo yote miwili ilishindwa kurejeshwa. Jumla ya fedha

zinazodaiwa kwa taasisi hizi mbili ni shilingi milioni 550.86 , ikiwa ni shilingi milioni 275 za mkopo  na riba ya shilingi milioni 253.66 kwa upande wa Lubaba SACCOS; wakati mkopo na riba kwa FINI Financial and Real Estate Agency Services Company Limited ilikuwa shilingi milioni 22.20.

**Ninapendekeza Mfuko wa SELF (a) kuongeza juhudi za kufatilia wateja ili warejeshe mikopo na kufanya tathmini ya kina kwa maombi  ya mikopo mipya (b) kutathmini kwa kina uhalisia wa biashara na utoshelevu wa dhamana, kuchukua hatua za kisheria kwa wadaiwa ikiwemo kutoa notisi ya kuuza dhamana; (c) kushirikisha vyombo vya serikali kuwatafuta wakopaji waliojificha, na (d) kuimarisha mchakato wa kutathmini maombi ya mikopo, ikijumuisha upembuzi yakinifu.**

## 12.5 Utendaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mifuko ya hifadhi ya jamii ilianzishwa kwa madhumuni ya kutoa mafao ya kijamii kwa wanachama na wananchi kwa ujumla, au kwa sekta fulani za kijamii. Mapitio yangu ya mifuko ya hifadhi ya jamii yalibaini mapungufu kadhaa ambayo yanahitaji kushughulikiwa ili kuboreshwa utendaji wa mifuko hiyo, mapungufu hayo yameainishwa hapa chini:

### 12.5.1 Usimamizi duni wa mikopo na michango ya wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii

- **Mikopo ya muda mrefu kwa Serikali ipatayo shilingi trilioni 1.49:** Katika ripoti yangu ya mwaka wa fedha 2020/21, nilitoa dukuduku kuhusu mikopo ya muda mrefu iliyotolewa na mifuko ya hifadhi ya jamii kwa taasisi za serikali na kupendekeza kuwa Wizara ya Fedha na Mipango ishirikiane na taasisi hizo za serikali ili kuweka mipango mizuri ya marejesho ya mikopo husika, huku mifuko ya hifadhi ya jamii ilitakiwa kuimarisha mifumo ya udhibiti ya ndani kabla ya kutoa mikopo na kuendelea  kufuatilia kwa karibu  ili kuhakikisha mikopo yote iliyochelewa kulipwa inarejeshwa.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Sekta Binafsi na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma ilikuwa haijalipwa mikopo iliyotolewa kwa taasisi za serikali na mashirika mengine, ikiwa ni shilingi trilioni 1.17 kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Sekta Binafsi, wakati Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma ulikuwa na mikopo ya shilingi bilioni 321.45. Mikopo hii haijarejeshwa kwa muda wa kuanzia mwaka mmoja hadi miaka 15. Kwa maoni yangu kwa Taasisi za Serikali kushindwa kurejesha mikopo hii kunaathiri uwezo wa mifuko ya hifadhi ya jamii kutekeleza kwa tija na ufanisi majukumu yao ya msingi.

- **Kutorejeshwa kwa mikopo kutoka vyama vya ushirika wa akiba na mikopo shilingi bilioni 27.30**: Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Sekta Binafsi unadai mikopo shilingi bilioni 27.30 kutoka vyama vya ushirika wa akiba na mikopo na taasisi zinazotoa mikopo midogo, ambayo kuna uwezekano isirejeshwe kama juhudi mahususi hazitachukuliwa.

- **Mapungufu katika usimamizi wa madai ya michango ya wanachama shilingi bilioni 53.46:** Nilibaini mapungufu katika kusimamia michango ya wanachama na madai yanayosimamiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Sekta Binafsi. Kwa mfano, mfuko ulikuwa na michango kutoka kwa wanachama ipatayo shilingi bilioni 52.9 ambayo haijakusanywa kwa zaidi ya miezi 12. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma ulikuwa na madai yasiyosuluhishwa ya shilingi milioni 563. Kuchelewa kukusanya michango huathiri uwezo wa mifuko kutimiza majukumu yake ya kimsingi, ikiwemo kuwalipa wastaafu.

**Ninapendekeza kuwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Umma na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Sekta Binafsi iimarishe ukusanyaji wa madeni, uwajibikaji kwenye makusanyo, na ichukue hatua stahiki ili madeni ya michango yakusanywe bila kuchelewa zaidi.**

### 12.5.2 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi haujajitanabaisha vya kutosha ili kuwafikia walengwa ipasavyo

Mwaka 2021/22, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ulibaini changamoto inazokabiliana nazo wakati wa kutekeleza majukumu yake licha ya kufanya mazoezi kadhaa ya uhamasishaji kwa jamii. Uhamasishaji uliofanywa uliangazia masuala kama: wafanyakazi na waajiri kutokuwa na ufahamu juu ya haki zao kuhusu fidia hasa pale wanapoumwa au kupatwa na magonjwa mahali pa kazi.

Mwaka 2022 Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ulifanya utafiti wa ufahamu na kuridhika kwa wadau wake ambapo utafiti huo ulihusisha wilaya 139 na kuwahoji wadau 2,873 wakiwemo waajiri, waajiriwa na watabibu. Utafiti ulibaini kuwa wafanyakazi wengi hawana ufahamu wa kutosha kuhusiana na mfuko na huduma zake.

Kwa maoni yangu inahitajika mipango madhubuti ya elimu na taarifa kwa umma kuhamasisha mfuko ujulikane vema kwa wadau wote, kwani elimu ya kutosha itawasadia waajiri na watumishi kuelewa haki zao pindi wanapopata majanga wakiwa sehemu ya kazi.

**Ninapendekeza Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (a) uandae programu maalumu za elimu kwa umma ikiwa ni pamoja na kutumia mitandao ya kijamii kuelezea majukumu ya mfuko na faida kwa wadau; na (b) kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia programu hizo maalumu za elimu kwa umma nchini kote.**

### 12.5.3 Changamoto za kiutendaji wa kampuni tanzu na vitega uchumi vya mifuko ya hifadhi ya jamii

Kampuni tanzu na vitega uchumi vya Mifuko zinakabiliwa na changamoto za kiutendaji na kupelekea kufanya kazi chini ya viwango. Taasisi hizo ni kampuni ya Sisalana, Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro na Kampuni ya Mkulazi.

(i) **Kushindwa kuhamisha hati miliki ya mali kwenda kampuni ya Sisalana shilingi bilioni 60.18**: Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Sekta Binafsi umeshindwa kuhamisha mali kwa kampuni yake tanzu ya Sisalana kutoka Kampuni ya Katani Ltd, ambayo ina thamani ya shilingi bilioni 60.18. Mali hizo ziliwekwa kama dhamana baada ya Kampuni ya Katani Ltd kushindwa kulipa mikopo ya Mfuko, mkopo ukiwa ni shilingi bilioni 44.44 na riba ikiwa ni shilingi bilioni 15.73.

(ii) **Mipango duni ya utekelezaji wa mradi wa Mkulazi**: Gharama za uwekezaji wa mradi zimeongezeka kwa dola za Marekani milioni 32.64, na hivyo kusababisha gharama za uwekezaji wa mradi kufikia dola za Marekani milioni 55.08, ambalo ni ongezeko la asilimia 146, hii imetokana na kupitiwa upya kwa mradi. Aidha, nilibaini kuwa mpango wa awali ulitarajia mradi kukamilika ifikapo Disemba 2022 lakini hadi kufikia wakati wa ukaguzi wangu Septemba 2022 ujenzi wa kiwanda ulikuwa bado unaendelea ukiwa umefika asilimia 63 ambayo inaashiria itakuwa vigumu mradi kukamilika katika muda huo. Kuchelewa kukamilika kwa kiwanda kunasababisha miwa iharibike na kuongezeka kwa gharama za utunzaji miwa iliyopita muda wa kuvuna.

Vile vile , kampuni ya Mkulazi inakabiliwa na hasara ya shilingi bilioni 2.92 inayohusiana na uwekezaji katika shamba namba 217/1-217/6 (Ngerengere), ambalo lilichukuliwa na serikali mwaka 2022 kwa sababu kampuni ya Mkulazi ilikosa pesa za kuendeleza shamba hili. Hadi wakati namalizia ukaguzi wangu Disemba 2022, hapakuwa na makubaliano kwamba Serikali itailipa Kampuni ya Mkulazi shilingi bilioni 2.92.

(iii) **Utendaji duni wa Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro**: Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro inayomilikiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa umma na jeshi la magereza haikuweza kutengeneza viatu vilivyoagizwa na wateja kutokana na changamoto za kifedha na mikakati duni ya masoko. Mwaka 2021/22 kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro ilipanga kuuza jozi za viatu

138,566 kwa makadirio ya mapato ya shilingi bilioni 8.02. Hata hivyo, kampuni hii ilifanikiwa kupata mapato ya shilingi bilioni 2.46 sawa na asilimia 31, wakati shilingi bilioni 5.56 sawa na asilimia 69 haikuweza kupatikana kutokana na kushindwa kutengeneza na kuuza viatu vilivyotarajiwa.

### (iv) Kushuka faida kutoka kwenye vitega uchumi vya uwekezaji:

Mapitio ya vitega uchumi vya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Sekta Binafsi nilibaini kuwa kiwango cha mapato yatokanayo na uwekezaji kilikuwa chini na chenye mwelekeo wa kupungua katika kipindi cha miaka mitano mfululizo wakati gharama za uendeshaji zilikuwa kubwa hali ambayo iliendelea kuathiri mapato ya uwekezaji.

**Jedwali Na. 45** linaonesha kiasi kilichowekezwa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa watumishi wa Sekta Binafsi na kiwango cha rejesho kwenye uwekezaji:

**Jedwali Na. 45: Taarifa za rejesho kutokana na uwekezaji**

| Maelezo | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| | Kiasi (Sh. Bilioni) | Kiasi (Sh. Bilioni) | Kiasi (Sh. Bilioni) | Kiasi ( Sh. Bilioni) | Kiasi (Sh. Bilioni) |
| Mapato ya kodi ya pango | 10.97 | 10.07 | 11.60 | 10.14 | 9.10 |
| Gharama za uendeshaji | 6.38 | 8.00 | 8.75 | 7.98 | 6.57 |
| Rejesha halisi | **4.59** | **2.06** | **2.84** | **2.15** | **2.52** |
| **Thamani ya Uwekezaji** | | | | | |
| Makazi | 49.30 | 44.64 | 65.13 | 71.52 | 63.19 |
| Hoteli | 345.80 | 342.76 | 398.66 | 473.58 | 479.00 |
| Maghala | 55.44 | 19.66 | 41.63 | 47.27 | 37.54 |
| Watumishi | 11.12 | 11.13 | 14.00 | 12.30 | 14.37 |
| **Jumla** | **461.65** | **418.19** | **519.37** | **604.67** | **594.10** |
| Kiwango cha mrejesho | 1.0% | 0.5% | 0.5% | 0.4% | 0.4% |

***Chanzo:*** *Taarifa kutoka kwa rejista ya uwekezaji ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya jamii kwa watumishi wa sekta binafsi*

Matokeo haya yasiyoridhisha yanasababishwa na mipango duni ya uwekezaji, kukosekana kwa upembuzi yakinifu, miradi

kuchelewa kukamilika, na kukosa uwezo wa kutosha kutathmini utendaji katika ngazi ya miradi.

**Ninapendekeza** Mifuko Ya Hifadhi Ya Jamii (a) Ihakikishe uwajibikaji kwenye utendaji wa kampuni tanzu na uwekezaji kwa kuwashirikisha watendaji wa taasisi husika ili kuwa na malengo yanayotakayofikiwa (b) iboreshe tathmini na kufanya upembuzi yakinifu baada ya kuanza kazi kwa kampuni tanzu na taasisi za uwekezaji ili kusaidia kuboresha mipango na malengo ya baadae ya uwekezaji wenye tija (c) ihakikishe kampuni tanzu zinajifanyia tathmini na kutelekeleza mipango mkakati ya kuboresha utendaji wa kampuni hizo.



# SURA YA KUMI NA TATU

## MAPITIO KATIKA SEKTA YA UTALII TANZANIA

### 13.0 Utangulizi

Serikali ya Tanzania inalenga kuongeza mchango wa utalii katika kuchangia pato la taifa kutoka asilimia 6 hadi 11 ifikapo mwaka 2025 kupitia Mpango wake wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Lengo ni kuvutia watalii milioni 5 na kuingiza mapato ya dola za Marekani bilioni 6. Hata hivyo, zipo changamoto zinazotakiwa kutatuliwa ili kusaidia kufikia malengo yaliyokusudiwa katika kukuza sekta ya utalii. Changamoto hizo ni kama; kutotumika kwa kituo cha kidijitali kwa ajili ya kutangaza utalii wa Tanzania; kuchelewa kukamilika kwa Kampuni ya Uwekezaji ya TANAPA; kuwepo kwa vivutio vya mali kale ambavyo havitangazwi kuvutia watalii, uwepo wa magugu vamizi yanayoathiri malisho ya wanyama pori, ufadhili hafifu wa mradi wa faru pia kukosekana kwa huduma za uhakika za mtandao wa intaneti. Pia, zipo changamoto za utekelezaji wa miradi ya kuboresha mazingira ya uhifadhi kama vile mradi wa kuwabadilishia makazi jamii za watu wanaoishi ndani ya eneo la hifadhi ya Ngorongoro.

Sura hii inaangazia changamoto zinazokabili mpango wa serikali ya Tanzania wa kukuza na kupanua sekta ya utalii kwa ukuaji endelevu, ikiwa ni pamoja na utangazaji duni wa vivutio vya utalii, changamoto za maji, ucheleweshaji wa uendeshaji wa makampuni ya uwekezaji na masuala ya usimamizi na utangazaji wa urithi wa utamaduni.

## 13.1 Hatari ya kutokamilika kwa mradi wa kuwabadilishia makazi jamii ya watu wanaoishi ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro

Serikali kupitia Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro kwa kushirikiana na taasisi zingine za serikali na wadau mbalimbali, imeanza kutekeleza mradi wa kuwabadilishia makazi watu wanaoishi ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro tangu mwezi Juni 2022. Kwa mujibu wa andiko la tathmini ya awali ya mradi, iliyotolewa Aprili 2022 mradi utahusisha kubadili makazi ya takribani kaya elfu 22,000 zinazokadiriwa kuwa na jumla ya watu 110,000 na wanyama wa kufugwa wanaokadiriwa kuwa 750,000 (ambao ni ng'ombe, mbuzi na kondoo). Mradi huu unatekelezwa kwa lengo la kuhifadhi na kurejesha hali ya uoto wa asili na asili ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kufuatia hatari zinazotishia uhimilivu na uendelevu wa mali asili na vivutio vya kitalii vya eneo hilo.

Kama nilivyobainisha katika ripoti zangu za miaka ya nyuma (Aya ya 17.1.1 2019/20 na Aya ya 12.1 2020/21), uhimilivu, uendelevu na ustawi wa Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro uko hatarini kutoweka kutokana na ongezeko la watu, wanyama wa kufugwa na shughuli za maendeleo ya kibinadamu, ambazo zinasababisha mikakati na juhudi za uhifadhi kuwa ngumu kutekelezwa.

Katika mapitio ya taarifa za utekelezaji wa mradi wa kuwabadilishia makazi jamii za watu wanaoishi ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro nilibaini kuwa tangu mradi kuanza tarehe 6 Juni 2022 hadi 19 Octoba 2022, jumla ya kaya 407 (asilimia 1.85) zenye jumla ya watu 2,125 (asilimia 1.93) na mifugo 11,490 (asilimia 1.53) zilikuwa zimehamishwa na kupewa makazi katika kijiji cha Msomera kilichopo Wilaya ya Handeni Tanga, na jumla ya shilingi bilioni 24.76 zilitumika katika zoezi hilo. Kila kaya ilipewa nyumba iliyojengwa kwenye ardhi yenye ukubwa wa hekta 2.5, shamba lenye ukubwa wa hekta 5 kwa ajili ya kilimo, na fursa ya kulisha mifugo kwenye maeneo ya umma yaliyotengwa kwa ajili ya malisho ya mifugo. Pia, serikali iligawa chakula kwa muda wa miezi mitatu kwa kila kaya baada ya

kukabidhiwa maeneo yao mapya ya makazi. Serikali imeweka miundombinu ya maji na umeme kwa kila kaya, imejenga shule, miundombinu ya afya, na majosho ya kuogeshea mifugo. Kwa kuzingatia taarifa nilizozieleza hapo juu, kwa makadirio kwa njia ya "extrapolation" gharama za mradi zinakadiriwa kuwa shilingi trilioni 1.34 ili kubadilisha makazi ya kaya zote elfu 22,000 ikiwa kila kitu kitakuwa kama kilivyofanyika kwa utaratibu wa awali na kama hakutakuwa na mabadiliko.

Pamoja na jitihada za Serikali, kuna viashiria vya hatari ya kutofanikiwa kwa mradi wa kuwabadilishia makazi jamii za watu wanaoishi ndani ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kutokana na; zoezi kuendeshwa polepole, kiasi kikubwa cha fedha kinachohitajika, mahitaji ya uratibu wa mradi, kutokuwepo kwa ufahamu na uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa mradi kwa wadau mbalimbali, upinzani kutoka kwa baadhi ya watu wa jamii zinazoishi ndani ya eneo la hifadhi na jamii ya kimataifa, na baadhi ya Taasisi za Kimataifa. Hali hii inaashiria kutokuwepo kwa mpango madhubuti wa kina kwa ajili ya kutoa mwongozo, mwelekeo na dira thabiti na imara yenye kuzingatia mambo yote muhimu katika kutekeleza mradi huo wa kuhama kwa hiari kwa kaya zote zinazokadiliwa kuwa 22,000 kutoka katika Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

**Ninapendekeza Serikali kwa kushirikiana na wadau wote kuandaa na kutekeleza mpango wa kina wa utekelezaji wa mradi na kutafuta fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza mradi kikamilifu kwa kutumia mbinu na mikakati yote itakayofaa kuhakikisha utekelezaji wa mradi wa kubadili makazi ya kaya zote 22,000 kwa mafanikio.**

## 13.2 Changamoto za kukuza na kutangaza sekta ya utalii zinazoikabili Bodi ya Utalii Tanzania

### 13.2.1 Kuchelewa kuanza kufanya kazi kwa kituo cha kidijitali cha Bodi ya Utalii Tanzania kwa ajili ya kutangaza utalii

Bodi ya Utalii Tanzania ilianza kujenga Kituo cha kidijitali tangu mwaka 2017/18 na kukikamilisha Aprili 2022. Jumla ya shilingi bilioni 1.06 zilitumika kujenga kituo hicho. Lengo kuu la Kituo hicho ni kupanua wigo wa kutangaza vivutio na utalii wa Tanzania kwa njia ya kisasa zaidi ya kidijitali kwa kuviweka vivutio vya utalii vya Tanzania katika kiwango cha kimataifa ili kuzidi kujulikana kupitia vyombo vya habari kama vile twitter, Facebook n.k.

Hata hivyo, hadi kufikia wakati wa ukaguzi wangu mwezi Desemba 2022, kituo hicho kilikuwa hakijafunguliwa ili kuanza kufanya kazi huku ikiwa ni muda wa miezi nane tangu kukamilika kwake, kwa sababu ya ukosefu wa wafanyakazi tisa wanaohitajika wenye ujuzi na weledi unaohitajika kwa ajili ya kukiendesha kituo hicho. Licha ya Bodi ya Utalii kuomba kibali cha kuajiri kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora mnamo tarehe 9 Juni 2022, hata hivyo kibali hicho kilikuwa hakijatolewa hadi wakati wa ukaguzi wangu ambacho ni kipindi cha miezi sita tangu kibali kuombwa.

Manufaa na matarajio mengine yanayotarajiwa kutoka kwenye kituo hicho hayajapatikana kwa wakati kufuatia kuchelewa kufunguliwa kwa kituo hicho. Hii ni pamoja na kuchelewa kwa utangazaji wa vivutio vya utalii vya Tanzania kulikotarajiwa kuongeza idadi ya watalii watokanao na matangazo ya kituo hicho.

**Ninapendekeza kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuidhinisha kibali cha kuajiri watumishi wa kituo hicho ili kiweze kuanza kazi ya kutangaza utalii kidijitali.**

### 13.2.2 Utekelezaji usioridhisha wa mipango ya shughuli za masoko katika kukuza Utalii

Mwaka 2021/22 Bodi ilitekeleza kazi 32 (asimia 68) kati ya 47 za masoko ilizopanga kutekeleza. Tathmini yangu ilibaini kuwa kazi 15 ambazo hazikutekelezwa ni miongoni mwa kazi muhimu zinazohusiana na utangazaji wa utalii kama vile kuandaa na kushiriki katika maonesho ya utalii nchini Korea Kusini, Hong Kong, Thailand na China hadi Juni 2022. Pia nilibaini kuwa kazi 15 za masoko hazikutekelezwa kwa sababu Bodi ya Utalii ilikuwa inafanyia kazi maagizo na maelekezo kadhaa wa kadhaa ya Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo yalipelekea bajeti ya shilingi bilioni 1.98 za Kurugenzi ya Masoko kuhamishwa ili kusaidia kufanikisha Maonesho ya Utalii ya Kanda ya Afrika Mashariki ambayo hayakuwa kwenye mpango.

Kwa maoni yangu, utekelezaji wa kazi hizo, ungekuwa na matokeo chanya kwa vivutio vya watalii na kuongeza uwezo wa Tanzania kuwa kivutio cha juu zaidi kwenye eneo la utalii.

**Ninapendekeza kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii katika siku zijazo endapo kutakuwa na matukio ambayo hayajapangwa, itafute fedha kutoka Hazina kwa ajili ya kugharamia matukio hayo bila kuathiri kazi zilizopangwa za Bodi ya Utalii.**

## 13.3 Uhaba wa maji kwenye maeneo ya hifadhi utokanao na ukame unaohatarisha uhimilivu, uendelevu na ustawi wa mifumo ya ikolojia na maisha ya wanyamapori.

Mwaka 2021/22, nchi ilikumbwa na ukame wa muda mrefu, na kusababisha uhaba wa maji kwa wanyamapori katika Hifadhi za Taifa na maeneo ya hifadhi. Katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro wanyamapori wapatao 135 walikufa kutokana na ukame na pia wengine kukimbilia katika makazi ya watu kutafuta maji na malisho. Vifo hivyo ni pamoja na nyati 40, nyumbu 30, Pundamilia 60 na Viboko watano.

Aidha, migogoro ya binadamu na wanyamapori iliyohusisha vifo vya binadamu ilifikia rekodi ambayo siyo nzuri huku miaka ya 2020 & 2021 wanyamapori waliua watu 26 na kujeruhi 77 wakati 2019-2020, watu 20 waliuawa na 66 kujeruhiwa hali iliyosababisha kulipiza kisasi huku wanyamapori nao kuuwawa na sababu ikiwa ni kugombania maji na malisho (Mchoro I). Idadi ya migogoro kati ya binadamu na wanyamapori imeongezeka kutoka visa 31 vilivyoripotiwa mwaka 2020/21 hadi visa 42 vilivyoripotiwa mwaka 2021/22.

**Kielelezo I: Picha inayoonesha wanyamapori waliouawawa baada ya kuvamia makazi ya watu**



***Chanzo: Ripoti ya migogoro Ngorongoro***

Vile vile, Hifadhi na Maeneo ya uhifadhi yalikabiliwa na changamoto za usimamizi wa maji kutokana na ukweli kwamba maji yanayotiririka ndani ya hifadhi yanatokea nje ya mipaka ya hifadhi ambapo mamlaka haina mamlaka kuyasimania. Kwa mfano, kiasi cha maji katika mito ya Katuma na Kapapa iliyopo

Hifadhi ya Taifa ya Katavi kina cha maji kilipungua kutokana na uvamizi wa wafugaji na wakulima kwenye vyanzo vya maji.

Kwa maoni yangu mfumo wa ikolojia unaweza kuharibika kwa kiasi kikubwa, wanyamapori wanaweza kuangamia na pia migogoro kati ya wanyamapori na binadamu inaweza kuongezeka hadi kufikia kiwango kisichoweza kudhibitiwa iwapo hatua stahiki hazitachukuliwa ili kuimarisha usimamizi wa maji katika Hifadhi za Taifa za Tanzania ikiwa ni pamoja na kujenga mabwawa ya kuvuna maji ya mvua.

**Ninapendekeza Mamlaka kwa kushirikiana na Serikali (a) kuhakikisha shughuli zote za kibinadamu zinazozunguka hifadhi zinasitishwa kupitia kubuni mafunzo na uhamasishaji kwa jamii inayozunguka hifadhi hizo; na (b) kujenga mabwawa ya maji ili yaweze kutumika wakati unapotokea ukame wa muda mrefu na kuathiri upatikanaji wa maji.**

## 13.4 Kuchelewa kuanza kazi kwa kampuni ya uwekezaji ya TANAPA

Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) inaendesha hifadhi za taifa 22 zenye ukubwa wa takribani kilomita za mraba 104,170 na zina mtandao wa barabara wenye urefu wa kilomita 17,202.60. TANAPA huwa ina mipango endelevu ya kutunza miundombinu yake ikiwa ni pamoja na mtandao wa barabara zake ndani ya hifadhi ambazo huathiriwa mara kwa mara na mvua, hasa nyakati za masika na pia shughuli za utalii. Mwaka 2021/22, Mamlaka ilitumia shilingi bilioni 25.4 kwa ajili ya matengenezo ya barabara. Mamlaka iliamua kujenga uwezo wa ndani ili kuimarisha matengenezo ya miundombinu yake na hivyo kuanzisha kampuni ambayo ilisajiliwa mnamo tarehe 21 Julai 2020 kwa ajili ya kufanya shughuli za Mamlaka na miradi mingine ya kandarasi kwa misingi ya kibiashara.

Hadi wakati wa ukaguzi wangu uliofanyika Disemba 2022, kampuni hiyo ilikuwa haijaanza kufanya kazi na hivyo kuwa imechelewa kwa miezi 30 tangu iliposajiliwa huku sababu ikiwa urasimu katika kufanya maamuzi muhimu. Mamlaka

ilinifahamisha kuwa afisa mtendaji mkuu wa kampuni tayari ameteuliwa na hivyo mamlaka ilikuwa inakamilisha taratibu za ajira ya mtendaji mkuu kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kampuni kuanza kufanya kazi.

**Ninapendekeza Mamlaka iharakishe mchakato wa uendeshaji wa kampuni ili iweze kupata thamani ya fedha kutokana na uanzishwaji wa Kampuni hiyo.**

## 13.5 Maeneo ya utalii yameharibika kutokana na ujenzi wa mahema ya kudumu kwenye kambi maalumu

Maeneo maalumu ya kambi huruhusu wageni kupiga kambi kwa kutumia mahema yasiyo ya kudumu kwa muda wa miezi mitatu hadi tisa. Katika ukaguzi wangu nilitembelea maeneo saba ya kambi maalumu ambayo yako chini ya Mamlaka ya Uhifadhi wa Eneo la Ngorongoro ambayo ni Simba B, Ole Kamwanga, Laandana namba 1, Nyati, Acacia namba 1, Tembo B na Lemala Kubwa ambayo kwa ujumla wake yana uwezo wa kubeba mahema 76 yenye uwezo wa kulaza watalii 168 kwa jumla wao.

Katika ziara yangu ya ukaguzi nilibaini kwamba baadhi ya maeneo ya kambi hizo yalikuwa na mahema na miundombinu ya kudumu kwa hadi misimu 10 jambo ambalo ni kinyume na maelekezo ya maeneo maalumu ya kambi ambayo yanahitaji kambi kuvunjwa baada ya msimu kuisha. Maeneo ya kambi ambayo yamekuwa yakifanya kazi kwa kipindi cha kuanzia miaka minne hadi 10 yameoneshwa kwenye **Jedwali Na. 46.**

**Jedwali Na. 46: Maeneo ya uwekezaji yanayofanya kazi kwa muda mlefu kwa mfululizo**

| Na | Jina la eneo | Mwendeshaji | Uwezo wa watu | Idadi ya Mahema | Idadi ya Miaka katika uendeshaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Simba B | Tyche Limited, East Africa Camps | 22 | 10 | 10 |
| 2. | Ole Kamwanga | African Environment Ltd | 25 | 10 | 5 |

| Na | Jina la eneo | Mwendeshaji | Uwezo wa watu | Idadi ya Mahema | Idadi ya Miaka katika uendeshaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 3. | Laandana No. 1 | Tortilis Tanzania Limited | 22 | 10 | 5 |
| 4. | Nyati | Wildlife Guides of Tanzania | 25 | 10 | 4 |
| 5. | Acacia No. 1 | Grumeti Expeditions Ltd | 22 | 10 | 8 |
| 6. | Tembo B | Abercrombie & Kent (T) Ltd | 22 | 10 | 5 |
| 7. | Lemala Kubwa | Kuhama Camp/TNS Hospitality | 30 | 16 | 5 |

*Chanzo: Uchakataji wa wakaguzi  kutoka kwenye mafaili ya Uwekezaji ya Hifadhi 2021/22*

Kwa maoni yangu, kutohamisha mahema mara kwa mara kutoka kwenye maeneo hayo ya kambi maalumu kuna madhara makubwa kwa wanyamapori na mimea kutokana na uharibifu wa uoto wa asili unaotokana na kuweka mahema kwa muda mrefu.

**Ninapendekeza kuwa Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ya Eneo la Ngorongoro ifuatilie na kutathmini utekelezaji wa miradi ili kuruhusu ufufuaji wa uoto wa asili kwa ajili ya usitawi wa mimea na mazingira bora kwawanyamapori hususani  kwenye maeneo yaliyoathirika.**

## 13.6 Rasilimali za urithi wa utamaduni ambazo hazitumiki ipasavyo

Mwaka 2021/22 TANAPA kwa kushirikiana na wataalam wa mambo ya kale walifanya zoezi ambalo lilibaini nyenzo 600 za ikolojia kama vile kuyeyusha chuma, maeneo ya makaburi ya kitamaduni, na majengo ya kihistoria katika Hifadhi ya Mikumi. Nyenzo hizo zimehifadhiwa katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ili baadaye kuja kutumika kwa madhumuni ya utalii.

Ingawa nyenzo hizo zilikusudiwa kutumiwa kwa madhumuni ya utalii, zimesalia bila kazi kwa sababu hakuna utafiti wa kina wa ikolojia ambao umefanywa na kurekodiwa kupata habari za kina kuhusiana na tamaduni, jamii na ustaarabu wa zamani ambao ulifanywa kwenye nyenzo hizo. Ila kazi kama hizo, zingekuwa muhimu kwa kuhifadhi historia, kuendeleza ujuzi wa kisayansi

kwa kutumia data muhimu kwa ajili ya utafiti wa kisayansi kama vile mifupa ya kale na vinasaba ili kuelewa mabadiliko ya idadi ya watu na magonjwa, na kutoa taswira ya utambulisho na uhusiano za zamani kwa jamii za kisasa na za Kitanzania. Hakuna taarifa na kumbukumbu zilizowekwa kimaandishi kwa ajili ya rejea ya siku zijazo za utambulisho kama sehemu ya urithi wa utamaduni wetu.

Kwa maoni yangu urithi wa kitamaduni ukitambuliwa na kuhifadhiwa unakuwa ni kivutio kimoja wapo cha utalii na kuingizia Mamlaka na taifa kwa ujumla mapato na pia ni kitambulisho cha historia mtambuka kwa vizazi vijazo.

**Ninapendekeza Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) itafute fedha kwa ajili ya kukusanya taarifa zaidi kuhusiana na urithi wa kitamaduni, kuboresha upatikanaji wa tovuti, na kuunda jopo la tafsiri ya nyaraka za masimulizi kutoka kwa wazee wenye uzoefu wa kina ili kuweza kuendeleza rasilimali za urithi wa utamaduni.**

## 13.7 Kukatika kwa mtandao wa intaneti mara kwa mara kwenye maeneo ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)

Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ina mkataba na Shirika la Mawasiliano Tanzania kwa ajili ya kutoa huduma ya mtandao wa intaneti wenye uhakika, madhubuti na wenye tija ili kurahishisha mawasiliano na uendeshwaji wa shughuli za hifadhi. Maeneo yanayohitaji mtandao wa intaneti wa uhakika ni pamoja na malango ya kuingilia hifadhini kulingana na unyeti wa maeneo hayo kuwahudumia watalii katika masuala kama vile uhakiki wa malipo, utoaji wa vibali vya kuingia hifadhini n.k.

Nilibaini kukatika kwa mtandao huo mara kwa mara kwenye malango ya kuingilia hifadhini na ilikuwa inachukua muda mrefu bila marekebisho. Uchambuzi wangu ulibaini kuwa katika mageti ya kuingilia hifadhini Serengeti mtandao wa intaneti ulikuwa ukikatika na kuchukua muda wa saa mbili hadi masaa 192 bila marekebisho. Pia, katika hifadhi ya Tarangire kukatika huko

kulichukua saa mbili hadi masaa 15 bila marekebisho na hivyo kuleta usumbufu katika uendeshaji wa shughuli za Hifadhi.

Mamlaka imeweka mtandao wa intaneti wa mbadala ili kukabili changamoto za kukatika mara kwa mara kwa mtandao wa Shirika la Mawasiliano Tanzania ili kuhakikisha shughuli za hifadhi za kuhudumia watalii zinaendelea bila mkwamo. Pia mtandao huo umezingatia mageti yenye shughuli nyingi ili kurahisisha utoaji wa huduma za malipo. Aidha Mamlaka inaendelea na mapitio ya mkataba wa huduma ya mtandao wa intaneti na ubora na uhakika wa mtandao wa intaneti itakuwa ni mojawapo ya vigezo vitakavyoangaliwa.

Kwa maoni yangu Mamlaka haipati thamani ya fedha inayotakiwa kutoka kwenye mkataba wa Huduma za Mtandao wa Intaneti kutokana na mtandao wa intaneti usio wa uhakika unaosababishwa na kukatika kwa mara kwa mara. Pia, hupelekea kukatizwa kwa shughuli za kihifadhi na huleta picha mbaya kwa watalii na inaweza pelekea kuathiri sekta ya utalii.

**Ninapendekeza kuwa Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (a) ihakikishe mageti na hifadhi zote yana mtandao wa intaneti wa uhakika ili kurahisisha shughuli za hifadhi za kuhudumia watalii kwa ufanisi; na (b) kukusanya taarifa zote zinazoonesha kukatika kwa huduma ya intaneti kwa Mwaka wa Fedha wa 2021/2022 na kuchukua hatua zinazostahiki kwa mtoa hutuma.**

## 13.8 Usimamizi na ufuatiliaji usioridhisha wa Mradi wa Faru

Kifungu cha IV cha Mkataba wa Makubaliano ulioingiwa mwaka 2015 kati ya Serikali na Mfuko wa Hifadhi ya Wanyamapori kinaupa Mfuko kazi ya kutafuta ufadhili wa mradi wa faru uliopo kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na kutakiwa kuorodhesha wafadhili wote kwenye jarida la kila mwaka. Hata hivyo, niliomba menejimenti ya Mfuko kunipatia orodha ya wafadhili wa mradi huo lakini orodha hiyo haikutolewa kwa ajili ya tathmini ya ukaguzi, ikiwa na maana kuwa kwa mwaka husika

mradi ulifadhiliwa na Serikali kupitia Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa TANAPA peke yake.

Katika utekelezaji wa bajeti ya 2021/22, mradi wa faru ulikuwa na upungufu wa shilingi milioni 297.50 (28%) ikilinganishwa na bajeti yake ya shilingi bilioni 1.08 iliyoidhinishwa na kupelekea kuathiri shughuli zilizopangwa kama vile kuweka alama ya utambulisho kwenye faru waliokuwa wamezaliwa.

Kwa maoni yangu mradi wa faru unaweza kupata changamoto za uendeshaji kutokana na kutopata fedha za kutosha kujiendesha kutoka Serekalini.

**Ninapendekeza Serikali kuhakikisha inaupatia mradi wa faru bajeti ya kujiendesha katika Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi.**

## 13.9 Kusambaa na kuongezeka kwa mimea vamizi zaidi ya uwezo wa Hifadhi kuyadhibiti.

Katika Ripoti zangu za mwaka 2019/20 na 2020/21, nilipendekeza kuwa Serikali ifikirie kutangaza tatizo la mimea vamizi kuwa suala la kitaifa na kuhakikisha wadau katika ngazi zote wanahusishwa ili kuchukua hatua stahiki kuondoa, kudhibiti na kuzuia kuwapo kwa mimea hiyo ndani ya Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, kwenye hifadhi za taifa, na katika maeneo mengine nchini.

Mbali na hilo, huu ni mwaka wa tatu mtawalia nikiendelea kuripoti kuhusu tatizo la mimea vamizi lakini hakuna jitihada mahususi zilizochukuliwa na Serikali kutokomeza tatizo la mimea vamizi. Kwa mfano, katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire ukaguzi wangu umeshuhudia eneo la hekta 120 jirani na hoteli ya Sopa likiwa limevamiwa na mimea vamizi, hata hivyo Mamlaka ya Uhifadhi iliweza kudhibiti hekta 20 tu kati ya hizo 120. Aidha menejimenti ya Mamlaka ilinielezea kuwa katika mwaka 2018/19 hifadhi ilifanya utafiti na kubaini takribani hekta 879 ambazo

zilishambuliwa na mimea vamizi katika maeneo ya Kuro na Sangaiwe ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Tarangire.

Kukosekana kwa jitihada na uratibu jumuishi kutoka kwa wadau wote ikiwa pamoja na Serikali za kupambana na mimea vamizi, malisho ya wanyamapori yako hatarini kutoweka hivyo kusababisha wanyamapori kupotea kutokana na kukosa malisho.

**Kwa hiyo, ninarudia pendekezo langu kuwa Serikali ifikirie kutangaza tatizo la mimea vamizi kuwa suala la kitaifa na kuhakikisha wadau wa ngazi zote wanahusishwa ili kuchukua hatua za kuondoa, kudhibiti na kuzuia kuwapo kwa mimea hiyo ndani ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, katika hifadhi zingine za taifa, na katika maeneo mengine kote nchini.**



# SURA YA KUMI NA NNE

# UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI

## 14.0 Utangulizi

Utendaji wa mamlaka ya huduma za maji na usafi wa mazingira unapimwa kupitia malengo yaliyobainishwa katika makubaliano na Wizara ya Maji. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji inasimamia masuala ya kiufundi na kiuchumi ya shughuli za mamlaka za maji.

Viashiria muhimu vya utendaji kwa mamlaka za maji ni pamoja na kulinda maslahi ya wateja, uhimilivu na uendelevu wa huduma za maji, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na gharama za uendeshaji. Viashiria vingine ni uhimilivu na ustawi wa miundombinu na mazingira, kusimamia upotevu wa maji na kuongeza vyanzo vya maji.

Licha ya jitihada za serikali za kuboresha upatikanaji wa maji kwa maendeleo ya jamii na ukuaji wa uchumi, kumekuwa na kasoro kadhaa zinazokwamisha huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama na huduma ya usafi wa mazingira, pamoja na kuchelewa kukamilishwa kwa miradi ya miundombinu ya maji.

Sura hii inaangazia mapungufu katika utendaji wa mamlaka za maji na masuala mengine yanayohusiana:

## 14.1 Mapungufu katika utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira yenye thamani ya shilingi bilioni 56.27

Katika utekelezaji wa miradi ya maji kwa mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira, Wizara hutoa mwongozo na ufadhili

kupitia bajeti ya serikali na mamlaka za maji hutumia mapato ya ndani na fedha za wahisani kutekeleza miradi ya maendeleo ya maji. Hatahivyo, ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maji ulibaini mapungufu yafuatayo; Mradi wa DAWASA wa kuchimba visima 20 Kigamboni, Dar es Salaam, ulichelewa kwa miaka nane kutokana na uchelewashaji wa ruzuku kutoka Wizara ya Maji pamoja na mkandarasi kutotekeleza wajibu wake kama ulivyoainishwa kwenye mkataba. Hali hiyo ilisababisha kuongezeka kwa gharama za mradi kwa shilingi bilioni 7.97 na kufanya jumla ya gharama za mradi kufikia shilingi bilioni 26.45. Pia, nilibaini miradi sita ya maji ya DAWASA yenye thamani ya shilingi bilioni 20.18 haikutekelezwa kabisa kwa mwaka 2021/22 kutokana na kukosekana kwa fedha. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji taka Jangwani, Dar es Salaam. Hii inatokana na uanzishwaji wa miradi bila kuhakiki uwepo wa ufadhili na kutohakiki kukubalika kwa dhana na malengo ya miradi hiyo kutoka kwa wadau wakuu wa mradi.

Pia nilibaini mradi wa maji katika mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira Musoma haukukamilika kwa wakati kutokana na ucheleweshwaji wa fedha za ruzuku kutoka Wizara ya Maji na kusababisha ongezeko la gharama ya mradi kwa shilingi milioni 113.41 na kufanya jumla ya gharama za mradi kufikia shilingi bilioni 8.17. Mradi wa visima vya maji wa (Kiranyi na Olasiti) katika Mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira Arusha ulitelekezwa tangu mwezi Novemba 2017 kutokana na maelezo ya ukosefu wa maji. Hata hivyo mamlaka haikuweza kutoa tathmini ya kiufundi kuthibitisha hilo pamoja na kuwa mradi ulishagharimu Mamlaka jumla ya shilingi milioni 661.42. Pia nilibaini uchelewaji wa asilimia 50 kukamilika kwa mradi wa kupanua ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji wa Nyankanga katika Mamlaka ya maji na usafi wa mazingira Geita wenye thamani ya shilingi milioni 812.14 ambao ilitokana na ucheleweshaji malipo kwa mkandarasi kwa sababu fedha za mradi kutoka wizarani hazikupelekwa kwa wakati.

Ni maoni yangu endapo Serikali itatoa fedha za kutosha na kwa wakati kwa mamlaka husika itawezesha utekelezaji wa miradi kwa wakati kulingana na bajeti iliyopangwa.

**Ninapendekezakuwa Serikali kupitia Wizara ya Maji iingilie kati na kuchukua hatua kuhakikisha kuwa miradi yote ya maji inakamilishwa kwa wakati ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za maji safi na majitaka kwa umma Aidha, mamlaka za maji zinapaswa kuhakikisha kuwa miradi inaanzishwa baada ya kuthibitishwa na kukubalika kwa malengo na dhana za miradi yao, na baada ya kuwa na uhakika wa upatikanajii wa fedha ili kuepuka ucheleweshwaji wa miradi.**

## 14.2 Mwendelezo wa hasara kutokana na upotevu wa maji shilingi bilioni 162.14

Upotevu wa maji ni kipimo muhimu cha ufanisi na utendaji wa mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira. Kwa kutathmini kiasi cha maji kinachozalishwa au kununuliwa lakini hupotea kabla ya kufikia wateja. Upotevu wa maji huwasilishwa kwa asilimia na hutathminiwa kwa kutoa kiasi cha maji kilichouzwa kwa watumiaji kutoka kwenye jumla ya kiasi kilichozalishwa au kununuliwa. Sababu zinazochangia upotevu wa maji ni pamoja na uchakavu wa miundombinu ya zamani inayosababisha uvujaji wa maji; na uunganishaji haramu unaopelekea kupotea kwa mapato. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji imeweka kiwango cha upotevu wa maji kinachokubalika kuwa kisizidi asilimia 20.

Kwa miaka minne mfululizo, nilibaini kiwango cha upotevu wa maji kwa mamlaka 23 za Maji Safi na Usafi wa Mazingira kinachozidi kiwango cha asilimia 20 kinachokubalika (**Jedwali Na. 47).** Mwaka 2021/22 upotevu wa maji ulikuwa jumla ya shilingi bilioni 162.14. Ikiwa tatizo la upotevu wa maji halitashughulikiwa ipasavyo, mamlaka za maji zitaendelea kupata hasara zisizo za lazima.

**Jedwali Na. 47: Mwenendo wa upotevu wa maji**

| Na. | Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira | Kiasi cha Upotevu wa Maji 2018/19 (Asilimia) | Kiasi cha Upotevu wa Maji 2019/20 (Asilimia) | Kiasi cha Upotevu wa Maji 2020/21 (Asilimia) | Kiasi cha Upotevu wa Maji 2021/22 (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bukoba | 44.00 | 44.00 | 44.00 | 43.00 |
| 2. | Morogoro | 33.50 | 43.05 | 43.50 | 40.48 |
| 3. | Musoma | 57.50 | 49.70 | 43.10 | 39.90 |
| 4. | Dar es Salaam | 49.20 | 41.25 | 38.89 | 39.03 |
| 5. | Njombe | 35.00 | 29.30 | 29.30 | 39.00 |
| 6. | Korogwe | | 42.00 | 41.00 | 38.00 |
| 7. | Arusha | 43.00 | 47.80 | 50.00 | 37.00 |
| 8. | Mwanza | 36.61 | 37.40 | 36.60 | 36.10 |
| 9. | Lindi | 33.20 | 33.23 | 37.28 | 35.20 |
| 10. | Dodoma | 26.60 | 26.00 | 34.70 | 33.60 |
| 11. | Tabora | 36.70 | 34.68 | 33.00 | 31.84 |
| 12. | Sumbawanga | 31.00 | 31.00 | 31.00 | 31.00 |
| 13. | Tanga | 27.94 | 35.83 | 33.05 | 30.70 |
| 14. | Kigoma | 30.00 | 30.00 | 30.00 | 30.00 |
| 15. | Mtwara | 22.00 | 21.00 | 26.20 | 29.13 |
| 16. | Singida | 26.00 | 33.00 | 31.00 | 29.00 |
| 17. | Mbeya | 30.00 | 30.00 | 28.00 | 28.00 |
| 18. | Bariadi | 28.00 | 28.00 | 28.00 | 27.50 |
| 19. | Moshi | 20.30 | 22.00 | 20.22 | 27.35 |
| 20. | Babati | 38.90 | 31.92 | 30.90 | 25.20 |
| 21. | Shinyanga | 23.29 | 23.29 | 21.00 | 24.00 |
| 22. | Iringa | 25.60 | 24.40 | 24.40 | 23.00 |
| 23. | Kahama | 11.00 | 17.44 | 22.91 | 23.00 |

***Chanzo***: *Ripoti za ukaguzi za mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira,*

**Ninapendekeza Serikali iendelee kuingilia kati kwa kupitia upya miundombinu ya usimamizi wa maji katika Mamlaka za Maji na kuandaa mipango ya kuboresha miundombinu hiyo kwa ajili ya kupunguza upotevu wa maji.**

## 14.3 Mapungufu katika usimamizi na udhibiti wa miundombinu ya maji

Kanuni RP0285-2002 kipengele Na 21030 cha Chama cha Kimataifa cha Wahandisi wa ufumbuzi wa kudhibiti kutu kimeainisha taratibu za kudhibiti kutu katika mabomba ya chuma. Kanuni hiyo imependekeza kutumia mfumo wa kulinda mabomba ya vyuma yanayolazwa ardhini au ndani ya maji dhidi ya kutu.

Katika kutembelea mitambo ya uzalishaji maji ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam ilioyopo Ruvu , nilibaini kuwa mabomba yote yaliyopo chini hayakuwa yametengenezwa kuzuia kutu.

Pia, nilibaini kuwa bomba kuu la kuleta maji Dar es Salaam kutoka katika chanzo cha Ruvu chini, na moja kutoka katika chanzo cha Ruvu juu hayakuwa yametengenezwa kuzuia kutu.

Uharibifu unaotokana na kutu katika mabomba unaweza kuhatarisha ubora wa maji na usalama, kusababisha uharibifu wa vifaa na kuongezeka gharama za matengenezo, na hivyo kuongezeka kwa upotevu wa maji, kupungua kwa ufanisi wa usambazaji na kusababisha kuharibika kwa vifaa na kusimamisha huduma ya upatikanaji wa maji.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam itekeleze mpango wa kina na madhubuti wa udhibiti wa kutu na kuhakikisha mabomba yote ya chuma ya usambazaji na usafirishaji wa maji yanakingwa dhidi ya kutu.**

## 14.4 Kutofanyika kwa uhakiki wa mita za maji na Wakala wa Vipimo

Kanuni ya 10 (2) za Kanuni za Uzito na Vipimo (Kudhibiti vipimo vya Mita za Maji) za Mwaka 2014 kinaelekeza kuwa mita za maji lazima zihakikiwe upya katika mwaka ambao muda wake wa matumizi umefikia ukomo. Pia, kifungu cha 13 (4) cha kanuni hizo kinahitaji mita yoyote ya maji ambayo imebadilishwa au kurekebishwa ni lazima ihakikiwe upya na Wakala Uzito na Vipimo kabla ya kuanza kutumiwa tena.

Hata hivyo, nilibaini kwa mwaka 2021/22 mita za maji zilizofanyiwa matengenezo hazikuhakikiwa na Wakala wa Uzito na Vipimo katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam. Pia, nilibani mita 60 za maji zilizofanyiwa matengenezo hazikuhakikiwa na Wakala wa Uzito na Vipimo

kabla ya kuanza kutumiwa na wateja wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mwanza.

Uhakiki wa mita ni muhimu kwa usomaji sahihi wa vipimo vya viwango vya maji yaliyotumika, lakini Mamlaka hizi hazikutoa kipaumbele katika mipango yao, hali inayoweza kusababisha makosa katika usomaji wa mita na hivyo kuleta mashaka na uhakika wa utozaji bili kwa wateja.

**Ninapendekeza kuwa mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira Dar es Salaam na Mwanza zihakikishe kuwa mita zilizofanyiwa matengenezo zinahakikiwa upya na Wakala wa Uzito na Vipimo.**

## 14.5 Idadi kubwa ya wateja wenye Mita za maji ndani ya majengo

Kanuni ya 47 za Kanuni za Huduma ya Maji ya Mwaka 2019 zinaelekeza kuwa, mita ya maji inapaswa kuwekwa katika eneo ambalo limeamuliwa na afisa aliyeidhinishwa kwa kushauriana na mmiliki wa jengo. Mita hiyo inapaswa kuwekwa karibu iwezekanavyo na mpaka wa nje wa jengo na katika eneo rahisi kwa ukaguzi wa afisa aliyeidhinishwa.

Katika mapitio yangu ya mwaka 2021/22 nilibaini ugumu katika ufikiaji wa mita za wateja katika Mamlaka za maji za Dar es salaam na Tanga. Katika eneo la Kinondoni-Dar es Salaam, wateja 3,893 (asilimia 20) kati ya wateja 19,043, walikuwa na mita ndani ya majengo. Katika Mamlaka ya Maji Tanga nilibaini uwepo wa wateja 982 (asilimia 2.2) kati ya wateja 43,923 wenye mita ndani ya majengo.

Ugumu katika ufikiaji wa kusoma mita, husababisha utoaji bili za makadirio kwa wateja, hivyo kupelekea kuwatoza wateja aidha makadirio ya juu au ya chini. Pia, kunaweza kupelekea upotevu wa mapato kutokana na uunganishaji wa maji kwa njia isiyo halali.

**Ninapendekeza mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira Dar es Salaam na Tanga kuhamisha mita zote zilizoko ndani ya majengo.**

## 14.6 Mwendelezo wa upungufu wa uzalishaji maji katika mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira

Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira,Sura 272 inaelekeza mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira kutoa huduma ya maji safi na majitaka katika miji. Hata hivyo, katika ukaguzi wa mwaka 2021/22 nilibaini mamlaka za maji 25 zilikuwa na upungufu wa uzalishaji na usambazaji wa maji kiasi cha kuanzia asilimia 10 hadi asilimia 80 kwa siku **(Jedwali Na. 48)**. Katika mwaka 2020/21 niliripoti tatizo la upungufu maji katika mamlaka 23 za maji.

**Jedwali Na. 48: Upungufu wa uzalishaji maji katika miji**

| NA. | Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira | Kiasi cha Maji Kinachohitajika ($M^3$ kwa Siku) | Maji Yanayozalishwa ($M^3$ kwa Siku) | Mapungufu ya Maji ($M^3$ kwa Siku) | Mapungufu ya Maji (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Bariadi | 7,116 | 1,395 | 5,721 | 80.40% |
| 2 | Karatu | 5,393 | 1,094 | 4,299 | 79.71% |
| 3 | Geita | 18,885 | 5,330 | 13,555 | 71.78% |
| 4 | Babati | 25,710 | 9,769 | 15,941 | 62.00% |
| 5 | Sumbawanga | 16,800 | 6,826 | 9,974 | 59.37% |
| 6 | Morogoro | 73,748 | 32,687 | 41,061 | 55.68% |
| 7 | Njombe | 8,310 | 3,694 | 4,616 | 55.55% |
| 8 | Lindi | 4,960 | 2,444 | 2,516 | 50.72% |
| 9 | Songea | 20,336 | 10,513 | 9,823 | 48.30% |
| 10 | Mwanza | 172,444 | 91,775 | 80,669 | 46.78% |
| 11 | Arusha | 109,689 | 59,291 | 50,398 | 45.95% |
| 12 | Mtwara | 22,202 | 13,047 | 9,155 | 41.24% |
| 13 | Dodoma | 103,609 | 61,500 | 42,109 | 40.64% |
| 14 | Moshi | 71,392 | 43,230 | 28,162 | 39.45% |
| 15 | Singida | 14,410 | 8,755 | 5,655 | 39.24% |
| 16 | Ngara | 2,828 | 1,798 | 1,030 | 36.42% |
| 17 | Muleba | 1,717 | 1,200 | 517 | 30.11% |
| 18 | Mbeya | 90,000 | 66,500 | 23,500 | 26.11% |
| 19 | Shinyanga | 18,446 | 14,345 | 4,101 | 22.23% |
| 20 | Nzega | 3,979 | 3,130 | 849 | 21.34% |
| 21 | Tanga | 41,072 | 32,464 | 8,608 | 20.96% |
| 22 | Musoma | 24,000 | 19,000 | 5,000 | 20.83% |
| 23 | Masasi Nachingwea | 15,432 | 12,724 | 2,708 | 17.55% |
| 24 | Kahama | 17,500 | 14,900 | 2,600 | 14.86% |

| NA. | Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira | Kiasi cha Maji Kinachohitajika ($M^3$ kwa Siku) | Maji Yanayozalishwa ($M^3$ kwa Siku) | Mapungufu ya Maji ($M^3$ kwa Siku) | Mapungufu ya Maji (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|
| 25 | Tabora | 19,000 | 16,906 | 2,094 | 11.02% |

***Chanzo***: *Ripoti za ukaguzi za mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira*

Sababu kubwa ya upungufu huo ulitokana na kuchelewa kukamilika kwa utekelezaji wa miradi na usimamizi duni unaotokana na upungufu wa fedha zinazotolewa na Wizara ya Maji na hivyo kusababisha mgao wa maji katika miji. Hali hii imesababisha kuwepo kwa mgao wa maji katika miji.

**Kama nilivyopendekeza katika ripoti yangu ya mwaka uliopita, Serikali kupitia Wizara ya Maji, ihakikishe uzalishaji wa maji safi unaongezeka na usambazaji unaimarika kwa kuwezesha kutoa fedha kwa wakati pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa miradi ambayo haijakamilika.**

## 14.7 Mipango hafifu katika ukusanyaji wa madeni katika mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira shilingi bilioni 127.07

Ili kuboresha ukusanyaji wa mapato, mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira zinatekeleza sera ya mikopo inayotaka bili kulipwa ndani ya mwezi mmoja na kusitisha huduma kwa wateja ambao hawajalipa bili kwa zaidi ya siku 90. Hata hivyo, licha ya kuwepo kwa sera hii, mamlaka za maji bado zinakumbana na ongezeko la madeni yanayozidi kipindi cha ukusanyaji madeni kilichowekwa.

Katika ukaguzi wa mamlaka za maji 28 nilibaini mwenendo usioridhisha wa ukusanyaji wa madeni kwa miaka mitatu mfululizo kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 49.** Mwaka 2021/22, Mamlaka za maji zilikuwa na madai ya deni la shilingi bilioni 127.07 kwa kutoa huduma za maji safi kwa ofisi za serikali, taasisi zingine, pamoja na wateja binafsi. Pia, nilibaini kuwa taasisi za serikali zinadaiwa kiwango cha deni cha shilingi bilioni 38.35 sawa na asilimia 30 ya madai ya mamlaka za maji.

**Jedwali Na. 49: Madai ya Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira**

| Na | Mamlaka za Maji | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|
| | | (Sh.Milioni) | (Sh.Milioni) | (Sh.Milioni) |
| 1 | Dar es Salaam | 58,165.64 | 69,643.53 | 62,285.22 |
| 2 | Kahama-Shinyanga | 3,818.42 | 5,355.51 | 11,068.79 |
| 3 | Mwanza | 6,705.41 | 7,039.29 | 7,097.50 |
| 4 | Dodoma | 6,596.58 | 6,757.49 | 6,062.27 |
| 5 | Tanga | 5,460.36 | 5,579.85 | 5,639.37 |
| 6 | Mbeya | 5,863.61 | 6,263.26 | 5,565.19 |
| 7 | Moshi | 4,572.02 | 5,003.53 | 5,166.74 |
| 8 | Arusha | 1,714.52 | 4,040.01 | 4,458.07 |
| 9 | Morogoro | 2,748.14 | 2,832.71 | 2,954.89 |
| 10 | Iringa | 1,492.71 | 1,815.64 | 2,145.12 |
| 11 | Tabora | 1,971.13 | 1,930.08 | 2,058.73 |
| 12 | Mtwara | 1,860.82 | 1,783.66 | 2,017.54 |
| 13 | Musoma | 2,167.94 | 2,353.91 | 1,641.16 |
| 14 | Kahama | 1,552.79 | 1590.47 | 1,592.61 |
| 15 | Shinyanga | 1,886.69 | 1,625.01 | 1,455.15 |
| 16 | Songea | 1,692.80 | 1,412.78 | 1,139.43 |
| 17 | Bukoba | 768.41 | 834.27 | 836.37 |
| 18 | Lindi | 786.21 | 776.27 | 797.71 |
| 19 | Masasi Nachingwea | 672.79 | 587.84 | 725.14 |
| 20 | Singida | 606.65 | 706.49 | 677.31 |
| 21 | Babati | 446.52 | 522.04 | 522.24 |
| 22 | Sumbawanga | 557.84 | 529.12 | 466.88 |
| 23 | Njombe | 273.8 | 337.71 | 334.7 |
| 24 | Ngara | 75.03 | 43.08 | 334.7 |
| 25 | Geita | 105.77 | 90.44 | 131.73 |
| 26 | Bariadi | 69.97 | 65.18 | 92.32 |
| 27 | Karatu | 21.41 | 40.17 | 56.94 |
| 28 | Muleba | 11.34 | 25.54 | 13.7 |
| | **Total** | **112,665.32** | **129,584.88** | **127,066.19** |

***Chanzo:*** *Ripoti za ukaguzi za mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira*

Hali hii inaonesha kuwa hatua zilizochukuliwa na mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira ili kuhakikisha fedha zinakusanywa kwa wakati hazikutosheleza. Kushindwa kukusanya madeni kwa wakati kunaathiri ukwasi na hivyo kusababisha matatizo ya kifedha katika kukidhi mahitaji mengine ya uendeshaji.

**Kama nilivyopendekeza katika ripoti yangu ya mwaka uliopita, Serikali izisaidie mamlaka za maji kuhakikisha zinachukua hatua fanisi zaidi katika ukusanyaji wa madeni, na kuweka**

**katika mita za maji za kulipia kabla ya kutumia huduma ya maji kwa wateja wenye historia ya kuwa na madeni chechefu.**

## 14.8 Makosa katika usomaji wa mita za maji na mfumo wa bili za maji za mamlaka za maji

Miongozo ya huduma kwa wateja wa maji katika mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira inataka mamlaka kusoma mita na kutoa bili kwa wateja kila mwezi. Hata hivyo nilibaini makosa katika usomaji wa mita na utozaji wa bili za maji za Mamlaka ya maji Dar es Salaam, Mwanza na Morogoro.

Katika Mamlaka ya Maji Dar es Salaam, nilibaini uwepo wa wateja 15,311 ambao taarifa za mfumo zilionesha hawakupata maji kwa muda wa miezi 12. Katika Mamlaka ya Maji Mwanza, nilibaini wateja 144 ambao hawakutozwa bili katika kipindi cha kuanzia mwezi mmoja hadi miezi minne.

Pia nilibaini ucheleweshaji mkubwa katika utoaji bili kwa wateja wapya waliounganishwa na huduma za maji katika Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Morogoro. Jumla ya wateja 13 waliounganishiwa maji hawakutozwa bili kwa kipindi cha kuanzia mwezi mmoja hadi miezi nane baada ya kuwekewa mita na kuingizwa kwenye mfumo.

Mapungufu haya yanaweza kupelekea wateja kutumia huduma ya maji bila kulipia aidha kwa kukusudia au kwa kutokujua.

**Ninapendekeza kuwa mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira Dar es Salaam, Mwanza na Morogoro ziimarishe udhibiti wa mfumo wa utoaji bili za maji ili kuhakikisha kuwa wateja wote wanapokea bili zao kwa usahihi na kwa wakati.**



# SURA YA KUMI NA TANO

## TATHMINI YA UTENDAJI WA TAASISI ZA MAFUNZO, UTAFITI NA ELIMU YA JUU

## 15.0 Utangulizi

Taasisi zinazohusika na mafunzo, utafiti na elimu ya juu nchini Tanzania ni pamoja na vyuo vikuu, vyuo vya elimu ya juu, taasisi za kielimu, vituo vya elimu, vituo vya utafiti na taasisi za mafunzo ya ufundi. Taasisi hizi hupokea fedha kutoka Serikalini ili kufidia gharama zao za uendeshaji na maendeleo. Hata hivyo, kuna upungufu katika uongozi na utendaji wa taasisi hizi, ambao unazuia kufikia malengo muhimu kama vile kufundisha, utafiti, maendeleo ya miundombinu, ustawi wa wanafunzi, na matumizi ya teknolojia.

Sura hii inaainisha mapungufu, vizuizi na tathmini ya juhudi zilizofanywa na Serikali na taasisi hizi katika kukuza elimu.

## 15.1 Mapungufu yaliyobainika katika shughuli za utafiti na ushauri katika taasisi za kitaaluma

Nilibaini mapungufu kadhaa katika shughuli za utafiti na ushauri katika taasisi mbalimbali za kitaaluma nchini Tanzania. Upungufu huu unajumuisha kutokuwepo kwa idara ya utafiti na mifumo ya ufuatiliaji, ugawaji hafifu wa rasilimali kwa ajili ya utafiti na ushauri, na huduma duni za machapisho na ushauri.

- Katika **Chuo Kikuu cha Dodoma**, mpango wa kuanzishwa kwa kituo cha utafiti na ushauri haukutekelezwa, ambapo kimepelekea ukusanyaji wa asilimia 12.5 tu ya mapato yaliyotarajiwa kutoka kwenye shughuli za utafiti na ushauri (shilingi milioni 343 kati ya lengo la mwaka la shilingi milioni

2,750). Zaidi ya hayo, hakuna mfumo wa ufuatiliaji wa shughuli za utafiti na ushauri, hivyo kuongeza hatari ya utendaji usiyoridhisha na kupoteza sifa ya chuo kikuu.

- Katika **Chuo Kikuu cha Mzumbe**, hakuna mfumo wa usimamizi wa utafiti na uchapishaji ambao umesababisha ugumu katika kusimamia utafiti na machapisho, hivyo kupelekea changamoto katika kutambua mwelekeo, kupima maendeleo, na kutathmini ufanisi wa shughuli za utafiti na ushauri. Licha ya utafiti wote kuwa unatakiwa kusajiliwa chini ya idara ya utafiti na ushauri lakini hakuna mikataba ya makubaliano ambayo inahifadhiwa na idara hiyo kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini shughuli za utafiti. Wakati wa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022, tafiti 12 zilisajiliwa.

- Zaidi ya hayo, katika **Chuo cha Diplomasia**, bajeti haikukasimiwa kwa ajili ya mfuko maalumu wa utafiti ulioundwa, na Jarida la Ushauri wa Kidiplomasia la Kimataifa halijachapishwa kwa zaidi ya miaka miwili, hivyo kuzuia kazi za utafiti na uchapishaji katika kituo hicho. Vivyo hivyo, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori Afrika, Mweka, hakikufikia malengo yake ya utafiti, ushauri, na uchapishaji kutokana na motisha duni na ukosefu wa mpango mzuri wa kazi.

Mapungufu haya yanaweza kuzuia kusambaa kwa maendeleo ya maarifa nchini na kupunguza kupata matokeo ya uwekezaji katika elimu ya juu. Kutokuweza kupata takwimu za utendaji katika tafiti pia kunaweza kufanya iwe ngumu kutambua mwelekeo, kupima maendeleo, na kutathmini ufanisi wa shughuli za utafiti na ushauri.

**Ninapendekeza vyuo vikuu vianzishe ofisi za utafiti na ushauri ili kuwezesha utekelezaji madhubuti wa shughuli za utafiti na ushauri na kutengeneza mfumo kamili wa kufuatilia usimamizi wa utafiti na ushauri. Vyuo vikuu pia vinapaswa kutenga rasilimali za kifedha za kutosha ili kuharakisha uchapishaji wa majarida ya kitaaluma na kupeleka fedha kwenye mfuko maalumu wa utafiti. Pia, taasisi hizi zinapaswa kuhamasisha**

**wafanyakazi wa kada za kitaaluma kufanya utafiti na ushauri zaidi kwa kuanzisha mpango kazi ambao unahakikisha utekelezaji wa shughuli zote kwa wakati.**

## 15.2 Kupungua kwa mapato yanayotokana na kazi za ushauri

Chuo cha Usimamizi wa Fedha kina wafanyakazi 212 wa kitaaluma wa kudumu ila ni 17 (asilimia 8) tu ndiyo wanaoshiriki katika kazi za tafiti kuanzia Julai 2019 hadi Juni 2022, ambapo ni kinyume na Kanuni 2.1 (a) (i-ii) ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Kanuni na Miongozo ya Utafiti na Uchapishaji, 2021. Kanuni inahitaji wafanyakazi wa kitaaluma kufanya kazi za tafiti pamoja na majukumu ya kufundisha na utawala. Vile vile, nilibaini idadi ya kazi za ushauri katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha zilipungua kutoka 21 mnamo 2020/21 hadi 10 mnamo 2021/22, nakupelekea mapato yanayotokana na kazi za ushauri kupungua kutoka shilingi milioni 713.80 mnamo 2020/21 hadi shilingi milioni 466.60 kwa mwaka 2021/22.

**Ninapendekeza kuwa Chuo cha Usimamizi wa Fedha kiongeze juhudi katika kuhamasisha wafanyakazi wa kitaaluma kushiriki zaidi katika shughuli za utafiti na ushauri.**

## 15.3 Usimamizi usio na ufanisi katika ufundishaji

### 15.3.1 Kutokuwepo kwa uwiano unaotakiwa wa walimu dhidi ya wanafunzi katika Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Stadi

Nilibaini kuwa uwiano wa walimu wa ufundi sanifu na wanafunzi katika baadhi ya programu zinazofanywa na vituo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Dodoma, Dar es Salaam na Mbeya haukidhi viwango vinavyohitajika. Uwiano ulikuwa kati ya 1:28 hadi 1:100 wakati uwiano unaokubalika kulingana na aina ya vituo ni 1:20.

Pia, nilibaini kuwa kuna vituo vingi vya mafunzo ya ufundi stadi nchini Tanzania, ikiwa ni pamoja na vituo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Namtumbo, Ileje, Nkasi, Kitangali,

Ruagwa, na Mabalanga ambavyo havina walimu wa somo mtambuka na uwiano wa walimu wa somo hili ni mdogo mno ukilinganisha na idadi ya wanafunzi. Uwiano huo upo kati ya 1:250 hadi 1:897, wakati uwiano unaokubalika kulingana na aina ya vituo hivyo ni 1:20. Hii imetokana na idadi ndogo ya walimu wa ufundi stadi wa masomo mtambuka kutokana na kukosa kibali cha ajira kutoka Serikalini. Walimu waliopo wanafanya kazi kupita kiasi, hali hii inaweza kudhoofisha ubora wa mafunzo ya ufundi stadi yanayotolewa kwa wanafunzi.

Licha ya upungufu wa walimu, niligundua kuwa baadhi ya walimu waliteuliwa kwa muda kama wasimamizi na wahandisi wa miradi ya ujenzi iliyokuwa inatekelezwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

**Ninapendekeza: (a) Serikali iiapatie Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kibali cha ajira ya walimu ili kupunguza pengo kati ya walimu na wanafunzi; na (b) Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi iondoe walimu kutoka kusimamia miradi ya ujenzi inayoendelea na miradi inayokuja ili kuwapa walimu muda wa kutosha kufundisha.**

### 15.3.2 Usimamizi wa mafunzo usioridhisha

(i) **Kupungua kwa idadi ya kozi fupi zinazotolewa na Chuo cha Usimamizi wa Fedha:** Nilibaini kupungua kwa idadi kozi za mafunzo ya muda mfupi kutoka 33 mwaka wa 2020/21 hadi 19 mwaka wa 2021/22 zilizotolewa katika Chuo cha Usimamizi wa Fedha; hali ambayo imesababisha kupungua kwa kiasi kikubwa kwa mapato ya mafunzo hayo kutoka shilingi milioni 580.1 mwaka wa 2020/21 hadi shilingi milioni 206.8 mwaka wa 2021/22. Kupungua huko kunatokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaosajiliwa na ushindani uliopo kutoka kwa vyuo binafsi vinavyotoa kozi za muda mfupi. Hivyo, jukumu kuu la Chuo la kutoa mafunzo ya muda mfupi halikutimizwa na kusababisha kupungua kwa mapato ya ndani na kuathiri utekelezaji wa majukumu mengine ya muhimu ya Chuo.

**Ninapendekeza Chuo cha Usimamizi wa Fedha kiongeze juhudi katika kuongeza idadi ya kozi za muda mfupi ili kuongeza maarifa kwa jamii na kuzalisha mapato ambayo yanaweza kutumika kusaidia shughuli zingine za taasisi.**

(ii) **Kushindwa kutumia ipasavyo mashine mpya za kufundishia katika Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi:** Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Karagwe ilipatiwa mashine mbalimbali kutoka makao makuu ya Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa matumizi ya kufundishia wakati wa mwaka wa masomo wa 2021/22 zenye thamani ya shilingi milioni 155.33. Kila mashine ilipangwa kutumika kwa madhumuni maalumu. Ukosefu wa mafunzo kwa walimu juu ya mashine hizo, ulipelekea kushindwa kuzitumia kikamilifu mashine hizo kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi, jambo ambalo linasababisha mafunzo hafifu ya vitendo kwa wanafunzi na kusababisha kuzalisha wanafunzi wasio na uwezo kulingana na soko la sasa.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ihakikishe inawapatia walimu mafunzo stahiki juu ya matumizi ya mashine hizo mpya ili mashine ziweze kutumika kikamilifu.**

(iii) **Kuchelewa kutekeleza mpango wa mafunzo unaodhaminiwa na GIZ kwa Wanafunzi 5700:** Programu ya E4D 2021-23 inaendana na makubaliano ya utekelezaji yaliyosainiwa tarehe 15 Juni 2021 kati ya GIZ na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu. Programu ya E4D inalenga kufaidisha watanzania 5,700 wanaokabiliwa na hali ngumu, hasa mabinti na vijana. Mradi huu una vifungu viwili vya vifaa vya Euro milioni 0.4 na mafunzo ya Euro milioni 0.5.

Mnamo tarehe 26 Mei 2022, Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi iliingia mkataba wa kufanya mafunzo kwa wanafunzi, ambapo ni miezi 11 baada ya mkataba wa awali kati ya GIZ na Serikali.

Hadi kufikia mwezi Oktoba 2022 hakukuwa na taarifa yoyote kuhusu wanafunzi waliokuwa wamesajiliwa kupata mafunzo hayo. Mradi huu unapaswa kuwa umekamilika ifikapo Disemba 2023 lakini ulikuwa haujaanza kwa sababu ya kuchelewa kwa serikali kushirikisha Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwenye mradi na kuchelewa kwa ununuzi wa vifaa vya mafunzo ambavyo havikuletwa hadi wakati wa ukaguzi.

Kuchelewa kuanza utekelezaji wa mradi huu kunaweza kusababisha wafadhili kutojitokeza kwa miradi ya baadaye, kutopata fedha kutoka kwa wafadhili kwa ajili ya mradi na jamii kutopata faida yoyote kutokana na mradi huo.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ifuatilie wafadhili juu ya utoaji wa vifaa vya mafunzo na kuhakikisha mafunzo kwa wanafunzi yanafanyika katika kipindi kilichobaki bila kuhatarisha ubora wa mafunzo.**

### 15.3.3 Uchache wa miundombinu, vifaa na zana za kufundishia

Mapitio yangu yalibaini **Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi Simanjiro** haikuwa na jengo la utawala, nyumba za wafanyakazi na karakana ya ufundi uashi. Na katika Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Mwanza nilibaini majengo yaliyoharibika ya nyumba za wafanyakazi na stoo za vifaa. Pia, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Namtumbo ilikuwa na upungufu wa miundombinu kama vile ukosefu wa nyumba za wafanyakazi, hosteli za wanafunzi, gari la ofisi kwa ajili ya usafiri na vifaa kwa ajili ya karakana ya useremala. Pia, kuna upungufu wa zana na vifaa vya karakana katika vituo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Iringa na Kongwa.

Aidha, katika **Chuo Kikuu cha Ardhi**, nilibaini kuna upungufu wa vifaa vya maabara katika Shule ya Uhandisi na Masomo ya Mazingira, Zana na Vifaa vya Jiografia katika Stoo na Karakana ya Upimaji.

Upungufu wa miundombinu ya elimu, zana na vifaa umesababishwa na bajeti ndogo na ikiwa hatua za haraka hazitachukuliwa, hali hii itaenda kuathiri ubora na viwango vya elimu yetu.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (a) ijenge na kurekebishe majengo yaliyochakaa kwa lengo la kurahisisha shughuli za mafunzo; na (b) Chuo Kikuu cha Ardhi kiongeze zana na vifaa katika karakana zote.**

### 15.3.4 Kushindwa kufikia vigezo vya usajili wa vituo vya mafunzo vya Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Nilibaini kuwa, kati ya vituo vipya 16 vya mafunzo ya ufundi vilivyosajili wanafunzi na kuanza mafunzo, ni kituo kimoja tu (asilimia 6.2) ndicho kimepata usajili wa awali, vituo vitatu (asilimia 18.8) viko kwenye mchakato wa kuomba usajili, na vituo 12 (asilimia 75) havijasajiliwa.

Hii imesababishwa na uhaba wa vifaa, karakana na walimu ikiwa ni pamoja na walimu wa masomo mtambuka, wafanyakazi wasio walimu, na timu ya usimamizi kama mahitaji ya usajili yanavyotaka. Ninaamini kuwa wahitimu kutoka vituo vipya vya mafunzo ya ufundi wanapata mafunzo yasiyojitosheleza ambayo yanaweza kuwafanya wasiwe na maarifa, utaalam au weledi wa kutosha hivyo kutokuwa washindani wazuri katika soko la ajira.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ihakikishe (a) vituo vipya vya mafunzo ya ufundi vinatimiza vigezo vya usajili kama vile walimu, miundombinu, na vifaa vya kutosha ili kutoa mafunzo bora; na (b) kusajili vituo vyote vipya kwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.**

### 15.3.5 Kushindwa kufikia malengo ya idadi ya udahili wa wanafunzi wanaojiunga na taasisi za elimu ya juu

Nilibaini kuwa kuna upungufu wa idadi ya wanafunzi katika Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo cha Sukari cha Taifa, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori wa Afrika, Mweka, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Chuo cha Ustawi wa Jamii na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam ambapo malengo hayakufikiwa kwa kiwango cha kati ya asilimia 4 hadi asilimia 72 katika mwaka wa 2021/22. Kutofikiwa kwa malengo ya kuongeza idadi ya wanafunzi kulisababishwa na kukosekana kwa rasilimali kama walimu, miundombinu, zana na vifaa, na kutotangazwa vya kutosha kwa kozi zinazofundishwa katika vyuo hivyo. Hali hii inaathiri ukusanyaji wa mapato ya ndani ya vyuo hivyo na kushindwa kuhudumia umma kwa kiwango kinachoridhisha (**Jedwali Na. 50**).

**Jedwali Na. 50: Malengo ya udahili ya taasisi dhidi ya idadi ya wanafunzi waliodahiliwa**

| Na. | **Taasisi** | **Malengo** | **Uhalisia** | **Tofauti** | **Tofauti katika asilimia** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 500,000 | 141,854 | 358,146 | 72% |
| 2 | Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi | 7,136 | 3,831 | 3,305 | 46% |
| 3 | Chuo Kikuu cha Ardhi | 7,664 | 5,519 | 2,145 | 28% |
| 4 | Chuo Kikuu Huria cha Tanzania | 20,000 | 15,838 | 4,162 | 21% |
| 5 | Chuo cha Sukari cha Taifa | 420 | 342 | 78 | 19% |
| 6 | Chuo Kikuu cha Dodoma | 36,421 | 31,714 | 4,707 | 13% |
| 7 | Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori wa Afrika, Mweka | 950 | 834 | 116 | 12% |

| Na. | Taasisi | Malengo | Uhalisia | Tofauti | Tofauti katika asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 8 | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima | 5,200 | 4,830 | 370 | 7% |
| 9 | Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa | 6,276 | 5,841 | 435 | 7% |
| 10 | Chuo cha Ustawi wa Jamii | 5,000 | 4,628 | 372 | 7% |
| 11 | Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam | 5,978 | 5,724 | 254 | 4% |

***Vyanzo**: Ripoti ya Ukweli na Takwimu; Mpango Mkakati; na Data ya Usajili wa Mwaka wa Sasa, Mkataba wa Utendaji na Daftari la Hazina.*

**Ninapendekeza mashirika ya umma na taasisi zingine kuhakikisha kuwa shughuli zote zilizopangwa zinatekelezwa kama zilivyopangwa kwa kuboresha miundombinu na kuongeza idadi ya wafanyakazi wa kitaaluma. Hii itawasaidia kufikia malengo yao ya kuandikisha wanafunzi.**

### 15.3.6 Kutofanya utafiti wa kutosha wa wahitimu wa elimu ya juu

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania inahitaji vyuo vikuu kufanya utafiti wa kufuatilia wanafunzi baada ya kuhitimu kila baada ya kipindi cha miaka 3 hadi 5 ili kutathmini ufanisi wa mchakato wa kufundisha na kujifunza, na mwelekeo wa soko la ajira wa programu zao. Utafiti wa kufuatilia wanafunzi hutoa ufahamu juu ya utendaji wa wahitimu katika soko la ajira, ambao unaweza kusaidia kuboresha ubora wa elimu unaotolewa na taasisi.

Nilibaini kuwa, Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo cha Diplomasia, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na Chuo cha Sukari cha Taifa havikufanya utafiti wa kufuatilia wanafunzi kwa zaidi ya miaka 10 na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine havikufanya utafiti wa kufuatilia wanafunzi kwa zaidi ya miaka mitano.

Kutofanya utafiti wa kufuatilia wahitimu kwa muda unaohitajika kunatokana na ukosefu wa fedha. Kutofanya utafiti wa mwendelezo wa kufuatilia kazi za wahitimu kunaweza kuwa na

athari mbaya kwenye mitaala ya masomo na ubora wa elimu inayotolewa kwa ujumla.

**Ninapendekeza vyuo vya elimu ya juu kufanya utafiti kamili wa kufuatilia wanafunzi baada ya masomo kwa awamu na kutumia matokeo katika utengenezaji mpya wa mitaala.**

## 15.4 Usimamizi hafifu wa kampuni maalumu na vituo vingine vinavyoendeshwa na Taasisi za Elimu ya Juu

Makampuni maalumu na vituo vingine vilianzishwa kwa madhumuni maalumu kwa lengo la kukidhi malengo fulani yanayohusiana na mafunzo, utafiti, ushauri, na huduma za kijamii. Nilibaini mapungufu mbalimbali katika uendeshaji wa kampuni hizi kama ifuatavyo:

### 15.4.1 Kushindwa kufanya vizuri kwa Kiwanda cha Uchapaji katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Kiwanda cha Uchapaji katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambacho ni kampuni tanzu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kimekuwa na utendaji usioridhisha kwa miaka minne mfululizo kutokana na ufanisi mdogo wa uendeshaji na uhaba wa wafanyakazi. Licha ya kuweka lengo la kuongeza mapato kwa asilimia 20 kila mwaka katika Mpango wa Hatua za Mkakati wa Miaka Mitano 2020/21-2024/25, hakijaweza kufikia lengo hili. Hii imepelekea matatizo ya kifedha na kutokuwa na uhakika kuhusu uwezo wa taasisi hiyo kuendelea kufanya kazi.**Jedwali Na. 51**

**Jedwali Na. 51: Utendaji usioridhisha wa Kiwanda cha Uchapaji katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

| Chanzo cha mapato Mapato | Mapato (Sh. Milioni) | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** |
| Uchapishaji na Uchapishaji wa Vitabu | 56.74 | 28.12 | 28.10 | 12.52 |
| Duka la vitabu | 1.27 | 2.27 | 1.29 | 3.46 |

| Jumla | 58.01 | 30.39 | 29.39 | 15.98 |
|---|---|---|---|---|

***Chanzo:** Uchambuzi wa Wakaguzi wa Hesabu wa Taarifa za Kifedha na Mpango Mkakati wa 2020/21-2024/25 wa Kituo cha Uchapaji katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

**Ninapendekeza Kiwanda cha Uchapaji katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (a) kiongeze uhamasishaji na utangazaji ili kuvutia wateja kwa huduma ya uchapishaji na (b) kufanye mapitio ya ufanisi wa uendeshaji ili kupata njia bora za kuboresha kufikia malengo yaliyowekwa.**

### 15.4.2 Utendaji duni wa Vituo vya Uchapishaji katika Taasisi ya Elimu Tanzania

Vituo vya uchapishaji vinavyomilikiwa na Taasisi ya Elimu Tanzania vimekuwa vikifanya kazi kwa kiwango cha chini kutokana na kukosa mpango wa biashara, mwongozo wa utendaji wa kazi wa kawaida na mashine za uchapishaji zisizotosheleza ambazo husababisha utendaji usioridhisha ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa huduma za uchapishaji zilizokasimishwa kwa wazabuni wa nje kwa shilingi milioni 488.72 (asilimia 156) kutoka shilingi milioni 313.35 katika mwaka wa fedha 2020/21 hadi shilingi milioni 802.07 katika mwaka wa fedha 2021/22.

Kutokuwepo kwa mpango wa uendeshaji wa vituo vya uchapishaji na uchakavu wa mashine kunasababisha kupoteza mapato yanayopatikana kutokana na kutoa huduma za uchapishaji.

**Ninapendekeza Taasisi ya Elimu Tanzania kuandaa mpango wa kibiashara, utaratibu wa kazi wa kawaida na kuongeza vifaa vya uchapishaji katika vituo vya uchapishaji ili kuongeza uzalishaji wa uchapishaji.**

### 15.4.3 Kukosekana kwa taratibu za kukasimisha kazi za huduma na ushauri katika Kampuni ya Ushauri Elekezi ya Mazingira Jengekwa ya Chuo Kikuu cha Ardhi

Kampuni ya Ushauri Elekezi ya Mazingira Jengekwa ya Chuo Kikuu cha Ardhi ilizalisha shilingi bilioni 5.71, ambapo shilingi bilioni

2.78 (asilimia 49) zililipwa kwa washauri watatu wa nje, na kampuni ilibakia na shilingi bilioni 2.93 (asilimia 51) kama sehemu yake ya mapato kama ilivyoripotiwa katika taarifa za kifedha za kampuni. Hata hivyo, sikupata ushahidi wowote juu ya jinsi washauri waliokasimishiwa kazi walivyopatikana na kama sheria za manunuzi zilifuatwa.

Aidha, hakukuwa na taratibu zilizothibitishwa katika taratibu za uendeshaji za Kampuni ya Ushauri Elekezi ya Mazingira Jengekwa kwa ajili ya kutekeleza ushauri na kazi, ambayo ilisababisha fursa ndogo kwa washauri wote na kupungua kwa mapato ya ndani ya kufidia gharama za uendeshaji. Kutokuwepo kwa taratibu zilizothibitishwa katika kukasimisha kazi na upungufu wa rasilimali watu kulipelekea hali hii.

**Ninapendekeza kuwa Kampuni ya Ushauri Elekezi ya Mazingira Jengekwa ya Chuo Kikuu cha Ardhi (a) iongeze uwezo wa rasilimali watu na rasilimali zingine ili kushughulikia huduma za ushauri na kazi ambazo zinakasimishwa kwa washauri wa nje; na (b) iandae taratibu za kukasimisha kazi kwa washauri wa nje zinazozingatia kanuni za manunuzi.**

## 15.5 Mapungufu ya ufanisi wa uendeshaji wa taasisi zinazosimamia na kusaidia elimu ya Juu

### 15.5.1 Kutofikiwa kwa lengo la kutoa mikopo kwenye programu za kipaumbele

Mpango mkakati wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ulilenga kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaosoma programu zenye kipaumbele kwa taifa kwa asilimia 51 ya mikopo yote iliyotolewa kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza kwa mwaka wa fedha 2021/22. Hata hivyo, katika mwaka wa masomo wa 2021/22, asilimia 21 tu ya mikopo, jumla ya shilingi bilioni 33.22 ilitolewa kwa wanafunzi 14,995 katika maeneo ya kipaumbele ya kitaifa, ikiwa ni chini ya lengo la asilimia 51. shilingi bilioni 156.76 zilizobaki zililipwa kwa wanafunzi 57,644 katika maeneo mengine, kinyume na miongozo.

Hii inatokana na idadi ndogo ya waombaji walio na sifa za kusomea masomo yanayohusiana na maeneo muhimu ya kipaumbele ya kitaifa, ambayo inaweza kuzuia kufikia malengo ya maendeleo ya kitaifa katika maeneo hayo kutokana na upungufu wa wataalamu na nguvu kazi.

**Ninapendekeza Serikali iweke misingi sahihi kwa wanafunzi kusoma masomo yanayoendana na vipaumbele vya Taifa .**

### 15.5.2 Mafunzo hafifu ya kudumu kwa wataalam wa utoaji wa elimu na mafunzo yenye misingi ya uwezo katika Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Katika mwaka wa ukaguzi wa 2021/22, Baraza lilifundisha walimu 1,640 katika maeneo ya maendeleo ya mitaala, utoaji wa elimu na tathmini. Hata hivyo hakuna mafunzo endelevu yaliyotolewa kwa wataalam kuhusu falsafa ya Elimu na Mafunzo yenye Misingi ya Uwezo tangu mwaka 2005. Hii inatokana na mipango na mikakati duni kuhusu kuendeleza wataalam wa utoaji wa Elimu na Mafunzo yenye Misingi ya Uwezo ili kukabiliana na changamoto za elimu ya kiufundi ulimwenguni, ikiwa ni pamoja na mabadiliko yanayoendeshwa na soko. Ninaamini kuwa ujuzi wa utoaji wa mitaala unaweza kuwa umepitwa na wakati na unaweza kuathiri uwezo wa wahitimu wa elimu ya kiufundi wa Tanzania ikilinganishwa na wataalamu kutoka nchi za nje.

**Ninapendekeza Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi lianzishe mipango ya mafunzo ya maendeleo endelevu kwa ajili ya mafunzo ya waalimu (wataalamu) ili kuboresha huduma zake kwa wateja wake na kukidhi mahitaji ya kiufundi ya kimataifa.**



# SURA YA KUMI NA SITA

# UFANISI WA MAMLAKA ZA UDHIBITI KATIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAO

## 16.0 Utangulizi

Serikali ya Tanzania ilianzisha mamlaka za udhibiti 57 kusimamia shughuli zinazohusiana na utoaji wa huduma, uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa. Mamlaka hizi zina wajibu wa kubuni na kutekeleza sera, miongozo, na sheria za udhibiti ili kuweka mazingira ya usawa kwa wadau mbalimbali kufanya kazi kwa ushirikiano katika sekta wanazozisimamia. Hata hivyo, katika ripoti yangu ya ukaguzi ya mwaka uliopita, nilibaini kasoro mbalimbali katika mamlaka hizi, kama vile udhaifu katika usimamizi wa michakato ya leseni, kutosimamiwa kwa bei za gesi asilia, usimamizi duni wa ada, na mikakati duni ya kudhibiti shughuli haramu za michezo ya kubahatisha.

Sura hii inaelezea mapungufu mengine ya udhibiti yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa mwaka 2021/22 na mapendekezo kwa serikali na mamlaka husika ili kuboresha ufanisi wa udhibiti;

## 16.1 Mapungufu ya mifumo ya kielektroniki inayotumiwa na mamlaka za udhibiti

Wakati wa ukaguzi wa mwaka wa fedha 2021/22, mapungufu yaliyobainika kwenye mifumo inayotumiwa na mamlaka mbalimbali za udhibiti nchini Tanzania ni kama yanavyoelezwa hapa chini:

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania ilibainika kuwa na udhaifu katika mfumo wake wa usimamizi na udhibiti wa taarifa (RIMS) kama vile kuingiliana kwa nambari zinazotumika kuainisha

bidhaa za usajili na mamlaka zingine, ukosefu wa moduli za kufuatilia bidhaa zisizofaa, na ufuatiliaji hafifu wa bidhaa baada ya kuingizwa sokoni.

Baraza la Mitihani la Tanzania lilibainika kuwa na udhaifu katika mfumo wake wa kutoa huduma za maombi mbalimbali kwa njia ya kielektroniki kama vile mfumo kushindwa kutoa taarifa za ankara zilizolipwa, na kutokuwa na uwezo wa kuwezesha malipo kufanyika moja kwa moja kwa njia ya benki ama kushindwa kuwezesha huduma ya malipo kwa kutumia fedha za kigeni.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji haina mfumo wa kielektroniki wa kukokotoa viwango vya bei za malipo ya huduma ya maji na umeme katika sekta za maji na umeme.

Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania ilibainika kuwa na udhibiti hafifu wa uingizaji wa mifumo ya ndege zisizokuwa na rubani;
Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania ilikuwa na udhaifu katika usimamizi wa kinachofanyika kwenye akaunti za leseni katika shughuli za michezo ya kubahatisha mtandaoni.

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu ilikuwa na udhaifu katika mfumo wake wa usimamizi wa wanachama na mitihani ambayo ni pamoja na kuwepo kwa taarifa za wanachama zilizorudiwa, kurudiwa kwa makampuni yaliyoidhinishwa, kurudiwa kwa taarifa za mawasiliano za wanachama, kurudiwa kwa watumiaji wa mfumo, na kuwepo wanachama wasio na sifa;

Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ilikuwa na udhaifu katika mfumo wake wa usimamizi wa taarifa kwa kutumia kompyuta. Mapungufu hayo ni pamoja na kutokuwepo kwa mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao kwa wakandarasi, hali inayowalazimu kusafiri umbali mrefu kwenda ofisi za kanda; kukosekana utengamanishi na mifumo mingine kama vile mfumo wa Serikali wa kunasa miamala ya mapato, licha ya mapato yote ya bodi kupokelewa kupitia mfumo huo; mfumo hauna uwezo wa kutoa risiti za malipo au taarifa za fedha; na mfumo wake wa usimamizi

wa taarifa kwa kutumia kompyuta hautoshi kuwezesha shughuli zote za Bodi ya Usajili wa Wakandarasi.

Bodi ya Nyama Tanzania haikuwa na mfumo wa kielektroniki katika kuweka kumbukumbu na taarifa za wadau wake; na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ilikuwa na utenguzi usio sahihi wa zabuni kutokana na hitilafu katika Mfumo wa Ununuzi wa Kielektroniki wa Taifa ujulikanao kama TANePS na ukosefu wa moduli ya kutoa taarifa za mapato.

Udhaifu huu ulitokana na usimamizi duni, uboreshaji usio wa kawaida, na mikakati isiyo na ufanisi katika ufuatiliaji na usimamizi wa vikwazo vya teknolojia ya habari na mawasiliano katika mamlaka husika.

**Ninapendekeza mamlaka za udhibiti na serikali zishughulikie mapungufu yaliyobainishwa katika mifumo mbalimbali inayotumiwa na mamlaka hizo; ikiwa ni pamoja na kuboresha mikakati na usimamizi wa teknolojia ya habari na mawasiliano, kukuza na kuwezesha mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kukokotoa bei za huduma, kuimarisha udhibiti na mifumo ya usimamizi wa akaunti za leseni katika shughuli za michezo ya kubahatisha mitandaoni, kusahihisha mapungufu katika mfumo wa usimamizi wa wanachama na mitihani, kutathmini na kusahihisha makosa katika Mfumo wa Ununuzi wa Kielektroniki wa Taifa wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (TANePS), na kutumia teknolojia ya kidijitali ili kuboresha uendeshaji na kupanua wigo wa wateja. Pia, nashauri mapitio ya mara kwa mara ya taarifa katika mifumo ya usimamizi wa habari za kudhibiti ili kubaini na kusahihisha taarifa zinazojirudia na taarifa zinazokosekana, na utumiaji wa mifumo ya huduma za maombi kielektroniki yenye ufanisi.**

## 16.2 Kutokuwepo kwa usimamizi wa kutosha katika utekelezaji wa hatua za kisheria kwa wasiofuata sheria

Mamlaka za udhibiti zina jukumu la kuhakikisha wadau wanaosimamiwa wanatii sheria, kanuni na miongozo inayotawala

sekta zao husika za uendeshaji. Mamlaka hizo hufanya uhakiki, ukaguzi na vipimo vya ufuatiliaji na taratibu zingine ili kubaini iwapo wadau wanatii sheria na kanuni zinazohitajika. Hatua za kisheria za udhibiti zinapaswa kuchukuliwa kwa waliobainika kutokufuata sheria.

Hata hivyo, nilibaini kuna matukio ambapo mamlaka za udhibiti hazitekelezi ipasavyo adhabu zinazohitajika kutolewa kwa wadau wanaoshindwa kufuata sheria. Hali hii inasababisha wadau kurudiarudia kutokufuata sheria na hivyo kuuathiri umma. Hii inatokana na kutokuwepo kwa utaratibu thabiti wa kufuatilia na kusimamia adhabu na faini za kutofuata sheria kwa ajili ya udhibiti. Baadhi ya matukio ya kutofuata utaratibu ambayo hayukuchukuliwa hatua stahiki ni kama yafuatayo.

Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilibaini kasoro katika vituo 306 kati ya vituo 670 vya mnururisho wakati wa ukaguzi wa usalama, ambazo zilihitaji kurekebishwa ili kuimarisha matumizi ya usalama wa vituo hivyo na kupunguza athari za mionzi kwa watumiaji na umma kwa ujumla. Lakini hakukuwa na ushahidi kama Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilifuatilia na kuthibitisha kama mapendekezo yake juu ya upungufu uliobainishwa wakati wa ukaguzi wake yalitekelezwa na hatari zilizobainishwa ziliondolewa au kupunguzwa kwa kiwango kisichokuwa na madhara.

Vilevile, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji haikufuatilia hoja za ukaguzi 103 kama vile mapungufu katika ubora wa usambazaji wa umeme wa kuaminika, gharama za ukarabati na matengenezo, hatua za usalama na zingine katika vituo vya wazabuni wa usambazaji wa nishati wa Shirika la Umeme Tanzania.

Shirika la Viwango Tanzania limekamata bidhaa ambazo zilithibitishwa kutokuwa salama na zilizo chini ya viwango vinavyokubaliwa kwa matumizi ya umma kama vile unga wa mahindi, unga wa ngano, mafuta ya nywele, siagi ya karanga, chai nyeusi, na pilipili ya viwandani hadi kufikia Julai 2022. Hata

hiyo hakuna hatua zilizochukuliwa kwa bidhaa za chakula zilizokuwa chini ya kiwango na zilizoshindwa kukidhi vigezo vya vipimo na haikuteketeza bidhaa zilizokamatwa zisizo salama na zile ambazo ziko chini ya viwango vinavyokubalika kwa matumizi. Bidhaa zilizozuiliwa zipo katika stoo za Shirika la Viwango Tanzania au majengo mengine kwa makubaliano maalum na shirika.

Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli ilikataa gharama za uwekezaji ambazo zimejumuishwa kama gharama zinazoweza kurejeshwa kiasi cha dola za Marekani milioni 53.34 ambazo zilizidishwa na kampuni za mafuta na gesi (PSA holders). Licha ya ukweli huo, hakuna makubaliano au azimio kwa takriban miaka saba na kampuni za mafuta na gesi na gharama hizo hazijarekebishwa na kuzingatiwa kwenye miamala inayoendelea kwani bado zimejumuishwa kama sehemu ya gharama zinazoweza kurejeshwa kwa wamiliki wa kampuni za mafuta na gesi, jambo hili linaiweka serikali katika hatari ya kupoteza mapato.

Hali kadhalika, Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira halikuweza kutambua vituo vyote ambavyo vilitakiwa kulipa ada kwani kanzidata yake haina ukamilifu wa taarifa zinazowezesha kutambua kwa ukamilifu miradi inayoendelea na vituo vinavyoendelea kufanya kazi na vituo ambavyo vimesimama au miradi iliyokamilika. hivyo Baraza limeshindwa kubainisha vituo vilivyochelewa kulipa ada kwa ajili ya kutoza adhabu. Pia Bodi ya Udhibiti wa Stakabadhi Gharani haikutoza adhabu kwa waendeshaji 32 wa maghala ambao wanadaiwa na Bodi.

Masuala haya yanahatarisha usalama wa bidhaa na huduma kwa umma, na yanaongeza hatari ya kupoteza mapato yanayotokana na shughuli za udhibiti.

**Ninapendekeza kuwa mamlaka za udhibiti ziweke na kutekeleza taratibu thabiti za kufuatilia na kuhakikisha hatua za udhibiti zinachukuliwa kwa ukiukwaji wa sheria na miongozo iliyowekwa kwa mujibu wa sheria.**

## 16.3 Mapungufu ya udhibiti katika kushughulikia na kusimamia malalamiko

Malalamiko ni ishara ya kutoridhika, kupinga au kukosoa huduma, bidhaa au hali fulani inayolalamikiwa na watu binafsi, kikundi cha watu au taasisi. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa mamlaka za udhibiti hazina mifumo madhubuti ya kukusanya na kushughulikia malalamiko, ambayo ni vipengele muhimu katika kutathmini ubora wa huduma na bidhaa zinazotolewa na wadau au wasimamizi.

Kwa mfano, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira, kwa pamoja walikuwa na migogoro na malalamiko 199 ambayo hayajashughulikiwa (153 kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira na 46 kwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania) kwa zaidi ya miezi 6 kutokana na kutokuwepo kwa rejista ya malalamiko na kutokuwepo kwa utaratibu wa mawasiliano wenye ufanisi kwa uongozi.

Pia, nilibaini kuwa mamlaka za udhibiti hazina utaratibu wa kiudhibiti wa kuhakikisha wadau au taasisi zinazosimamiwa na mamlaka za udhibiti, zimeweka taratibu sahihi na zenye kujitosheleza katika kukusanya na kushughulikia malalamiko. Hii inaondoa uwezo wa mamlaka za udhibiti wa kusimamia utoaji wa huduma kwa sekta zinazosimamiwa. Hali hii ilibainika kutokana na mamlaka za udhibiti kutokuwa na mipango ya kukagua wala kutoa taarifa juu ya utoshelevu wa taratibu zilizowekwa na taasisi za utoaji huduma na bidhaa ambazo zinasimamiwa , juu ya namza taasisi hizi zinavyoshughulikia malalamiko.

**Ninapendekeza kuwa mamlaka za udhibiti ziweke na kutekeleza taratibu thabiti na zenye ufanisi katika kushughulikia malalamiko dhidi yao au dhidi ya taasisi zinazosimamiwa.**

## 16.4 Udhaifu katika ukaguzi unaofanywa na mamlaka za udhibiti

Wakati wa ukaguzi nilibaini kwamba mamlaka kadhaa za udhibiti zina udhaifu katika taratibu zao za ukaguzi, ikiwa ni pamoja na:

Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu haifanyi ukaguzi wa mara kwa mara kwa mabasi ya shule yaliyopewa leseni ili kuhakikisha yanaendelea kukidhi mahitaji ya usalama wakati wote kwani hakuna utaratibu unaoitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu kufanya ukaguzi tena baada ya ukaguzi wa awali. Hii inaweka usalama wa wanafunzi hatarini.

Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania haikutoa vipimo vya mionzi kwa vituo 207 (asilimia 38) kati ya vituo 549 vya mionzi vilivyokuwa vinafanya kazi mwaka 2021/22 wala kutathmini kipimo cha mionzi ya atomiki kilichopokelewa na wafanyakazi kwa vituo 131 (asilimia 38) kati ya vituo 342 vya mionzi. Hivyo, Tume haijui kiwango cha mionzi kwa vituo 338 (asilimia 62) kati ya vituo 549 vya mionzi .
Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania haikuandaa mpango kazi wa kila mwaka wa kufuatilia na kudhibiti "non-ionizing radiation sources", kama vile minara ya mawasiliano na vituo vya redio. Hali hii inahatarisha usalama wa wafanyakazi na umma kwa ujumla kutokana na mionzi inayozalishwa katika vyanzo hivyo.

Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji haifanyi ukaguzi wa kuzingatia sheria kwa wazabuni wa huduma za umeme 22 na haifuatilii vya kutosha shughuli za wauzaji wakubwa wa gesi asilia Kinyume na Kanuni ya 27(1) ya Kanuni za Umeme (Shughuli za Uzalishaji, Usafirishaji na Usambazaji), 2019. Hii inaweza kusababisha kutozingatia sheria na kusababisha majanga makubwa.

Shirika la Viwango Tanzania linachelewa kufanya ukaguzi wa bidhaa na kuzisajili, na hivyo kusababisha kuongezeka kwa bidhaa zisizoidhinishwa. Kwa mfano, kutoka kwa sampuli ya bidhaa 62 zilizoidhinishwa (chakula na vipodozi) kati ya 1783, bidhaa 51( asilimia 82) hazikutathminiwa kwa wakati ingawa

malipo yalikuwa yamepokelewa. Ucheleweshaji huo ulikuwa kati ya siku 41 hadi 785. Hii inasababishwa na taratibu zisizoridhisha (ufuatiliaji na usimamizi) za kuhakikisha ufanisi katika tathmini, ukaguzi na idhini ya usajili licha ya kuwepo kwa Mfumo wa Maombi ya Mtandaoni (OAS).Hii inaweza kusababisha bidhaa ambazo hazina ubora na zisizokidhi viwango kuingia sokoni na kuwafikia walaji, na pia kusababisha hasara ya mapato kutokana na kukosa ada za usajili wa bidhaa.

Katika Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania sikupata ushahidi ikiwa waendeshaji 10 kati ya 20 wa michezo ya kubahatisha walifanyiwa majaribio na kupata vyeti vya kuthibitishwa vya vifaa vyao, mifumo ya usimamizi, na programu ya mchezo. Hii inaongeza hatari ya kuwepo kwa matokeo yasiyo ya haki ya michezo ya kubahatisha na kuweka umma kwenye hatari ya kufanyiwa udanganyifu.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lilibaini jumla ya miradi 2333 inayoainishwa kuwa na hatari kwani inahusisha shughuli kama zile zinazohusisha kemikali hatari, kuharibu makazi ya maisha ya porini na uchafuzi wa hewa yenye sumu. Hata hivyo, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lilifuatilia asilimia 55 tu ya miradi hiyo, na halikufuatilia vituo vya mafuta licha ya hatari kama vile mlipuko wa moto kwa vituo vya mafuta vilivyojengwa katika maeneo ya makazi na mwenendo wa ongezeko la vituo hivyo. Hii inaweza kusababisha athari mbaya za mazingira na hatari kwa afya ya umma.

Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania haihakikishi kuwa watoa huduma watano wa mawasiliano iliyowapatia leseni wanakidhi mahitaji ya ukaguzi wa usalama wa minara ya mawasiliano na hawasimamii kikamilifu ubora wa huduma za posta, maudhui, huduma za mtandao wa simu kwa umma inayojulikana kama "PSTN Services", na mtandao wa intaneti zinazotolewa na watoa huduma wenye leseni. Hii inaweka watumiaji wa huduma za mawasiliano katika hatari ya kutopata huduma bora zinazoendana na fedha wanazolipa kama vile

kutopatikana kwa mtandao huo au kushindwa kwa mtandao, kiwango cha kushindwa kwa muunganisho wa simu na kadhalika.

**Ninapendekeza kuwa mamlaka za udhibiti ziweke kipaumbele kwenye kuzingatia sheria, kanuni, sera, na miongozo kwa ajili ya kulinda maslahi ya umma kwa kuhakikisha kuwa wadau wanaosimamiwa wanatoa huduma na bidhaa bora kwa umma.**

### 16.5 Kukosekana ufanisi katika michakato ya utoaji wa leseni, usajili na uthibitisho wa bidhaa unaofanywa na mamlaka za udhibiti

Nilibaini kasoro kadhaa katika michakato ya utoaji wa leseni, usajili, na uthibitisho wa mamlaka mbalimbali. Kasoro hizi zina uwezo wa kuhatarisha ufanisi wa mfumo wa udhibiti na kutoa mwanya wa kutengenezwa kwa bidhaa zilizo chini ya viwango na kusambazwa sokoni kwa walaji.

Wakati wa ukaguzi wa mchakato wa uthibitisho wa bidhaa katika Shirika la Viwango Tanzania, nilibaini kuwa shirika lilichelewa kuhuisha leseni za vyeti vya bidhaa ambapo kutokana na sampuli ya maombi 103, ni maombi 12 tu yalifanyika kabla ya kumalizika kwa leseni ya awali na maombi 52 yalifanyika baada ya kumalizika kwa leseni za awali kwa vipindi vya kati ya mwezi mmoja na miaka mitatu kinyume na mwongozo wa utaratibu wa vyeti vya uthibitisho wa bidhaa. Aidha, nilibaini kuwa taarifa muhimu za waombaji kama vile mawasiliano ya wateja na ripoti za ufuatiliaji hazijawekwa kwenye mfumo kwa baadhi ya maombi.

Mapungufu haya yanahatarisha kuwepo kwa hali ya utengenezaji wa bidhaa zisizo na ubora, ama zisizo salama na kuingizwa katika masoko.

**Ninapendekeza Shirika la Viwango Tanzania liimarishe udhibiti wake wa kutambua kwa wakati muda wa kumalizika kwa leseni za uthibitisho wa bidhaa na lichukue hatua za kutuma taarifa moja kwa moja kwa wateja kielektroniki.**

Katika Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania nilibaini ucheleweshaji wa waombaji 23 kati ya 32 wa mbolea walioomba usajili wa mbolea na virutubisho vya mbolea kama ilivyobainishwa wakati wa ziara iliyofanyika tarehe 18 hadi 28 Aprili 2022. Ucheleweshaji huo ulichangiwa na vipimo vya maabara kuchukua muda mrefu. Kipimo cha maabara kwa virutubisho vya mbolea na mbolea ni muhimu kwa uhakikisho wa ubora. Hii imesababisha kuchelewa hadi miezi miwili katika usajili wa mbolea na virutubisho vya mbolea, hivyo kuongeza hatari ya uwepo wa mbolea isiyosajiliwa katika masoko.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania iweke mikakati ya kuboresha mchakato wa upimaji na utoaji wa majibu ya maabara kwa wakati ili kuweza kusajili leseni za uuzaji wa mbolea kwa wafanyabiashara waliomba.**

Bodi ya Nyama Tanzania ina udhaifu katika usimamizi wa usajili wa wadau wake. Nilibaini kuwa Bodi hiyo haina mfumo thabiti wa kuorodhesha na kuweka orodha ya wadau wake, na kwamba namba za usajili zimekuwa zikijirudia kwa wadau 28. Hii inafanya iwe ngumu kwa Bodi kuainisha idadi kamili ya wadau waliosajiliwa na kuhakiki ukamilifu wa mapato yaliyokusanywa.

**Ninapendekeza kuwa Bodi ya Nyama Tanzania iweke namba za usajili wa wadau kwa utaratibu, na kila mdau aliyesajiliwa awe na namba ya usajili ya kipekee kwa utunzaji sahihi wa kumbukumbu na udhibiti wa taarifa za wadau wake.**

Pia, katika Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli, nilibaini hakukuwa na rejista ya wafanyabiashara wa mafuta na gesi yenye taarifa muhimu juu ya mikataba ya mafuta na gesi, leseni, vibali vilivyoidhinishwa, na mabadiliko yanayotokea katika mikataba ya makubaliano ya mafuta na gesi iliyopo, vibali, au leseni. Hii inazuia upatikanaji wa taarifa za sekta ya mafuta na gesi na wadau wa sekta ya mafuta na gesi, ambayo ni muhimu kwa maamuzi.

**Ninapendekeza kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli ihakikishe kuanzishwa na kutumika kwa rejista ya mafuta na gesi na itumike kama inavyotakiwa na kanuni.**



# SURA YA KUMI NA SABA

# UFANISI WA TAASISI ZA UMMA KATIKA SEKTA YA AFYA

## 17.0 Utangulizi

Sekta ya afya inatoa matibabu, vifaa, bima na huduma zingine za afya kwa wagonjwa, na Serikali inalenga kuhakikisha upatikanaji wa huduma yenye ubora kwa wote. Hata hivyo, kutokana na mapungufu katika rasilimali kama vile wafanyakazi na vifaa tiba, si huduma zote za msingi za afya zinakidhi viwango vinavyotakiwa. Kutathmini utendaji wa mashirika ya umma na taasisi zingine katika sekta ya afya ni muhimu ili kuelewa athari zake katika kutoa huduma za afya kwa umma.

Sura hii inaangazia mambo yaliyobainika wakati wa mapitio ya ufanisi wa mashirika ya umma chini ya sekta ya afya ambayo ni Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Bohari Kuu ya Dawa , Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Hospitali ya Mloganzila. Masuala yaliyoainishwa ni pamoja na, wagonjwa kutozwa bei za dawa zisizolingana na bei zilizoidhinishwa, kiasi kikubwa cha madai ya bima ya afya yaliyokataliwa na Mfuko wa Bima ya Afya.

## 17.1 Wagonjwa kutozwa bei ya madawa tofauti na bei iliyoelekezwa katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili na Bohari Kuu ya Dawa Shilingi bilioni 1.23

Katika ukaguzi wa bei za kuuzia dawa na vipandikizi katika duka la dawa la Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili nilibaini dawa na vipandikizi 319 viliuzwa kwa wateja kwa bei ya chini kuliko viwango vilivyoidhinishwa na kusababisha dawa na vipandikizi kuuzwa kwa bei ya chini kwa shilingi milioni 5.28, huku dawa na

vipandikizi 12,105 viliuzwa kwa bei ya juu ya viwango vilivyoidhinishwa, na kusababisha wagonjwa kutozwa zaidi kwa shilingi milioni 224.67. Kwa ujumla, wateja walitozwa jumla ya shilingi milioni 219.39 zaidi ya bei.

Hii ni kwa sababu bei za mauzo zinazotumika katika mfumo wa Duka la Dawa la Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili hazitoki kwenye mfumo wa kielektroniki moja kwa moja, ziliingizwa kwenye mfumo kwa utaratibu usio wa kielektroniki, hivyo kukabiliwa na makosa.

Aidha, Bohari Kuu ya Dawa iliwatoza wateja (vituo vya afya na hospitali) bei kubwa kwenye bidhaa zaidi ya bei iliyoidhinishwa kwa jumla ya shilingi bilioni 1.01, jambo ambalo ni kinyume na bei zilizoidhinishwa. Hii ilisababishwa na usimamizi duni katika kuhakikisha bei zote zinaidhinishwa ipasavyo kabla ya kuingizwa kwenye mfumo. Utozaji wa bei ya juu unapelekea bidhaa nyingi za Bohari Kuu ya Dawa kuonekana zina bei ya juu kuliko bei ya soko, zaidi ya hapo bei za juu zinasababisha matumizi mabaya ya fedha za Serikali katika vituo vya afya na hospitali.

**Ninapendekeza (a) Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili iwasiliane na mtengenezaji wa mfumo ili kurekebisha mfumo wa duka la dawa na kuhakikisha bei sahihi na zilizoidhinishwa zinatozwa kwa wagonjwa, na (b) Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili na Bohari Kuu ya Dawa zihakikishe bei za mauzo katika mifumo hiyo zinaendana na sera ya mauzo.**

## 17.2 Madai ya bima ya afya yaliyokataliwa na mfuko wa bima wa afya shilingi bilioni 8.84

Katika mwaka wa fedha wa 2021/22, vituo vya afya na hospitali zilitoa huduma za matibabu kwa wanachama wa Mfuko wa Bima ya Afya, na kisha kudai gharama za huduma hizo kutoka kwa Mfuko wa Bima ya Afya kulingana na vigezo vilivyowekwa na Mfuko wa Bima ya Afya. Nilibaini kuwa, mashirika na taasisi zingine za umma tano zilipeleka madai yao kwa Mfuko wa Bima ya Afya ya jumla ya shilingi bilioni 92.44, ambapo madai ya

shilingi bilioni 8.84 (10 %) yalikataliwa na Mfuko wa Bima ya Afya kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 52**. Hii inaashiria ongezeko kubwa la madai yanayokataliwa ikilinganishwa na mwaka 2020/21, ambapo madeni yaliyokataliwa yalitokea kwenye mashirika na taasisi zingine za umma mbili yenye thamani ya shilingi bilioni 3.87 (4%). Hali hii inaonesha kuwa idadi ya taasisi na viwango vya madai yanayokataliwa vinaongezeka.

**Jedwali Na. 52: Madai yaliyokataliwa na Mfuko wa Bima wa Afya**

| Na. | Jina la taasisi | Jumla ya madai Sh. (Bilioni) 2021/22 | Madai yaliyokataliwa Sh. (Bilioni) 2021/22 | Asilimia ya madai yaliyokataliwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Hospitali ya Taifa ya Muhimbili | 44.52 | 6.42 | 14 |
| 2 | Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete | 22.26 | 0.13 | 1 |
| 3 | Taasisi ya Mifupa Muhimbili | 14.53 | 1.30 | 9 |
| 4 | Kituo cha Mikutano ya Kimataifa cha Arusha | 1.62 | 0.05 | 3 |
| 5 | Hospitali ya Taifa ya Muhimbili-Mloganzila | 9.51 | 0.94 | 10 |
| | **Jumla** | 92.44 | 8.84 | **10** |

**Chanzo**: Taarifa za ukaguzi za mashirika ya umma

Kwa mujibu wa Mfuko wa Bima ya Afya madai yalikataliwa kutokana na matukio ya kudai mara mbili, matumizi makubwa ya huduma, kutozingatiwa kwa bei elekezi za Mfuko wa Bima ya Afya, utoaji wa huduma ambazo hazijaainishwa na Mfuko wa Bima ya Afya, kukosekana namba za idhinisho, ukosefu wa maelezo katika huduma zinazodaiwa, kughushiwa kwa saini za wagonjwa, huduma ambazo si sehemu ya kifurushi cha Mfuko wa Bima ya Afya, makosa ya kukokotoa, matumizi kupita kiasi ya huduma, na kutofuata Kanuni za Matibabu.

Sababu hizi zinaonesha baadhi ya watumishi wanaohusika katika kutoa huduma za matibabu kwa wanachama wa Mfuko wa Bima

ya Afya hawazingatii taratibu zilizowekwa na zilizokubaliwa kati ya Mfuko wa Bima ya Afya na hospitali au vituo vya afya katika kutoa huduma.

Ongezeko la madai yaliyokataliwa ikilinganishwa na mwaka uliopita linaonesha mwenendo wa kuongezeka kwa madai yanayokataliwa ambayo yanaweza kusababisha kupungua kwa mapato na kuathiri utoaji wa huduma bora za matibabu.

**Ninapendekeza mashirika na taasisi zingine za umma (a) kuhakikisha wafanyakazi wanafuata kanuni na sheria za Mfuko wa Bima ya Afya; (b) kupitia na kusahihisha madai kabla ya kuyawasilisha Mfuko wa Bima ya Afya ili kurejeshewa fedha; na (c) kupitia upya madai yaliyokataliwa na kuwasilisha tena Mfuko wa Bima ya Afya kwa ajili ya kurejeshewa fedha kwa yale ambayo yatapatikana kuwa sahihi au yamethibitishwa ipasavyo.**

## 17.3 Utoaji wa huduma kwa mkopo bila ya mkataba katika Hospitali ya Taifa Muhimbili shilingi bilioni 16.73

Katika ukaguzi wangu wa usimamizi wa mikataba katika Hospitali ya Taifa Muhimbili nilibaini wateja wanne waliopatiwa huduma kwa mkopo kwa jumla ya shilingi bilioni 3.63 bila mikataba.

Mbali na hilo, nilibaini wateja wawili walikuwa na mikataba iliyoisha muda kwa zaidi ya siku 122 kuanzia tarehe ya kuisha mkataba hadi tarehe 30 Juni 2022, ambao huduma zilizotolewa kwao zina jumla ya shilingi bilioni 13.10.

Mapungufu haya yanatokana na hospitali kushindwa kupitia na kuhuisha mikataba na kutokuwepo kwa usimamizi thabiti wa mikataba kuhakikisha huduma za mikopo zinatolewa kwa wateja wenye mikataba.  Pia, hospitali haina ulinzi wa kisheria iwapo ikitokea migogoro.

**Ninapendekeza Hospitali ya Taifa Muhimbili ipitie mikataba yote iliyoisha muda ili kuihuisha, na kuhakikisha huduma za mikopo zinatolewa kwa wateja wenye mikataba.**

## 17.4 Ongezeko la bidhaa zilizopokelewa zenye muda uliobaki chini ya asilimia 80 au miaka miwili kabla ya muda wa matumizi kuisha katika Bohari Kuu ya Dawa shilingi bilioni 295.76

Kifungu cha 7.1.3 cha Mwongozo wa Ghala wa Bohari Kuu ya Dawa wa mwaka 2018 kinamtaka afisa ghala katika kitengo cha kupokea bidhaa kukokotoa muda uliobaki wa bidhaa ili kuhakikisha unazingatia kiwango kilichowekwa cha zaidi ya asilimia 80 au miaka 2 ya jumla ya muda wa matumizi uliobaki wa bidhaa.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa aina 2540 za bidhaa zenye gharama ya shilingi bilioni 295.76 (shilingi bilioni 163.83 kwa mwaka 2019/20) zilipokelewa zikiwa na muda wa chini ya asilimia 80 au miaka miwili ya muda wa matumizi wa bidhaa kuisha, ambayo ni ongezeko la asilimia 81 kutoka mwaka 2019/20.

Hii inasababisha ongezeko la bidhaa zilizokwisha muda wa matumizi, kupita kiwango kilichokusudiwa cha bidhaa zinazotarajiwa kuharibika cha asilimia 1 ya bidhaa zote ghalani kulingana na mpango mkakati. Jumla ya bidhaa zilizoisha muda wake zina thamani ya shilingi bilioni 28.24, kati ya hizo bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 22.67 zinahusiana na miaka iliyopita na shilingi bilioni 5.98 (10% ya jumla ya thamani ya bidhaa zote kwenye ghala za shilingi bilioni 60.38) zinahusiana na mwaka wa fedha 2021/22.

**Ninapendekeza Bohari Kuu ya Dawa ihakikishe bidhaa zote zinazonunuliwa au kutolewa na wafadhili zinakidhi viwango vinavyotakiwa vya zaidi ya asilimia 80 au miaka miwili ya muda wa bidhaa kudumu ili kupunguza wingi wa bidhaa zilizoisha muda wake.**

## 17.5 Ujenzi wa Viwanda Vya Dawa Bila Kuzingatia matakwa ya Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania

Kifungu cha 5 (a) cha Sheria Namba 1 ya Tanzania ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003, kikisomwa pamoja na sheria ya fedha namba 8 ya mwaka 2019, kinaelekeza kuwa Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania (TMDA) kudhibiti masuala yote yanayohusu ubora na usalama wa chakula, dawa, dawa za asili, vifaa vya matibabu, sumu na vipodozi.

Wakati wa tathmini yangu ya ujenzi wa vituo vitatu vya dawa vya Bohari Kuu ya Dawa nilibaini Bohari Kuu ya Dawa ilifanya mashauriano na Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania miezi mitano baada ya kuanza ujenzi wa viwanda mnamo Agosti 2020. Nilibaini Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania ilitoa maelekezo juu ya ujenzi wa majengo ya viwanda ambapo ilielekeza Bohari Kuu ya Dawa aidha kulivunja jengo au kujenga jengo jingine ili kuendana na mahitaji ya Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania. Majengo hayo hayakuwa yamevunjwa wala kuanza ujenzi mpya kipindi nilipotembelea eneo la mradi.

Hii inaweza kuathiri usalama na ubora wa chakula, dawa, dawa za mitishamba, vifaa tiba, sumu, na vipodozi vitakavyozalishwa katika vituo hivi.

Pia inaweza kusababisha upotevu wa fedha za umma katika ujenzi wa vituo vya dawa ambavyo kulingana na tathmini ya Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba Tanzania vinahitaji kuvunjwa au kujengwa majengo mengine.

**Ninapendekeza Bohari Kuu ya Dawa ihakikishe kiwanda hicho kinapitia tathmini za kiufundi na kuthibitishwa kuwa salama kwa madhumuni yaliyokusudiwa na kuzingatia sheria, kanuni na mwongozo.**

## 17.6 Ununuzi wa malighafi ambazo hazipo kwenye bajeti ya manunuzi shilingi bilioni 1.10

Bohari Kuu ya Dawa ilinunua malighafi za kutengeneza glovu mnamo Julai 2021 kwa shilingi bilioni 1.10 huku ujenzi wa viwanda vya kutengeneza dawa za maji (syrup) na glovu vikiwa katika hatua ya awali. Kwa hivyo, vifaa vilibaki ghalani kusubiri ujenzi ukamilike, hii inadhihirisha kulikuwa na vifaa vilivyonunuliwa bila mpango.

Nilifanya ziara ya eneo la mradi mnamo tarehe 28 Julai 2022 na kubaini kuwa ujenzi wa jengo la kiwanda cha glovu ulikuwa umekamilika kwa asilimia 100 na dawa za maji (syrup) ulikuwa kwa asilimia 90, ukisubiri maabara, vyumba vya usafi na mfumo wa maji ukamilike. Malighafi za kutengenezea glovu bado zilikuwa zimehifadhiwa ghalani wakati wa ziara yangu.

Ubora wa malighafi unaweza kufifishwa au kuathirika kutokana na athari za hali ya hewa kwa kuwa zimekaa ghalani kwa zaidi ya miezi 12 bila kutumika.

Ni maoni yangu kuwa kutumia fedha kiasi hicho kwa malighafi ambazo zimekaa muda mrefu bila kutumika siyo jambo lenye tija kwani fedha hizo zingeweza kutumia katika biashara ya dawa na vifaa tiba hivyo kupata thamani ya fedha hiyo.

**Ninapendekeza Bohari Kuu ya Dawa iboreshe mpango kazi katika mradi wowote ili kuhakikisha kuwa thamani ya fedha inafikiwa.**

## 17.7 Wateja 1090 hawakufanya biashara na Bohari Kuu ya Dawa kwa zaidi ya mwaka mmoja

Kwa kuzingatia Taratibu za Kawaida za Uendeshaji (SOP) za Maagizo Jumuishi ya Ugavi wa Vifaa (Mei 2021), kila kituo cha afya/hospitali kinatakiwa kuagiza na kupokea bidhaa mara nne kutoka Bohari Kuu ya Dawa katika kipindi cha mwaka mmoja kwa kipindi cha miezi 3 kati ya shehena moja na nyingine.

Katika mapitio yangu ya taarifa ya wateja kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022 nilibaini kuwa wateja 1090 hawakununua bidhaa yoyote ya afya kutoka Bohari Kuu ya Dawa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022, kati ya wateja 1090, wateja 381 walikuwa wanadaiwa na Bohari Kuu ya Dawa kiasi cha shilingi bilioni 33.86 na wateja 709 walifanya malipo ya awali ya shilingi bilioni 5.34. Kati ya wateja 1,090 wasiofanya biashara, wateja 153 walitengewa fedha zenye thamani ya shilingi bilioni 4.70 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2022. Tatizo hilo lilisababishwa na Bohari Kuu ya Dawa na Wizara ya Afya kutofanya uhakiki wa kutosha juu ya uwepo wa wateja kabla ya kukisia mahitaji na kutenga fedha.

Kuna uwezekano wa upotevu wa fedha kutokana na madeni ya muda mrefu kutoka kwa wateja ambao yawezekana hawapo.

**Ninapendekeza Bohari Kuu ya Dawa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya (a) kufanya uhakiki wa kina wa vituo vyote vya afya ambavyo havifanyi biashara na Bohari Kuu ya Dawa kwa mwaka mmoja au zaidi ili kubaini kama madeni yanayohusu wateja hao ni halisi, (b) kuangalia uwezekano wa kufunga vituo vyote vya afya na hospitali ambavyo havichukui bidhaa, na (c) kuhamisha salio la mikopo lililosalia kwenda kituo kingine cha afya.**

## 17.8 Utendaji usioridhisha wa maduka ya dawa ya Bohari Kuu ya Dawa

Miongoni mwa malengo ya maduka ya dawa ya Bohari Kuu ya Dawa ni kuongeza uhusiano na wateja na vituo vya afya, kuuza bidhaa sokoni na kupanua wigo wa bidhaa na kuongeza idadi ya wateja.

Tathmini yangu ya utendaji kazi wa maduka ya dawa ya Bohari Kuu ya Dawa ilibaini kuwa maduka ya dawa ya Bohari Kuu ya Dawa yalifikia asilimia 6 ya mauzo ya makadilio ya shilingi bilioni 10.35.

Maduka ya dawa ya Bohari Kuu ya Dawa yanakabiliwa na ushindani kutoka kwa maduka ya dawa ya kibinafsi na maduka ya dawa ambayo yanaweza kutoa bei ya chini au dawa mbalimbali zaidi. Pia yanategemea mfumo wa mnyororo wa usambazaji wa usambazaji wa Bohari Kuu ya Dawa, ambao unaweza kuleta ucheleweshaji, bidhaa kuisha ghalani, au masuala ya ubora. Zaidi ya hayo, Baadhi ya maduka ya dawa ya Bohari Kuu ya Dawa yapo katika maeneo yenye uhitaji mdogo ambapo yanapata changamoto kufikia kiasi kikubwa cha mauzo.

Bohari Kuu ya Dawa inakabiliwa na hasara kubwa kutokana na faida ndogo ikilinganishwa na gharama inayotumika katika kudumisha maduka ya dawa na inaweza kusababisha kutotolewa kwa huduma za afya katika maeneo yenye uhitaji.

**Ninapendekeza Bohari Kuu ya Dawa (a) ifanye uchambuzi wa gharama na faida na kuhakikisha utafiti wa soko wa kutosha unafanywa kwa ajili ya kupanua wigo wa wateja, (b) kuhakikisha maduka ya dawa ya Bohari Kuu yapo katika maeneo yenye uhitaji ili kuepuka matumizi mabaya ya rasilimali, na (c) kujenga uhusiano wa wateja na vituo vya afya vinavyojishughulisha na kutoa huduma za bima ya afya, hii itarahisisha utoaji wa huduma.**

## 17.9 Utekelezaji usioridhisha wa mpango wa kurekebisha vifaa tiba katika hospitali za serikali

Tathmini yangu ya mpango wa kina wa matengenezo ya vifaa tiba kutoka idara ya usimamizi wa vifaa tiba ya Hospitali ya Mloganzila kwa mwaka 2021/22 ulibaini kuwa kati ya vifaa 192 vilivyopangwa kufanyiwa matengenezo ni vifaa sita tu vilifanyiwa matengenezo sawa na asilimia 3. Vifaa hivyo sita vilikarabatiwa na wataalamu kutoka nje, ambao wanahitaji kuwa na utaalamu wa hali ya juu. Hospitali ya Mloganzila imekuwa ikifanya matengenezo ya vifaa tiba baada ya tatizo kutokea badala ya kuvifanyia ukarabati kila baada ya muda uliopangwa kabla tatizo halijajitokeza ili kuzuia kukatisha utoaji wa huduma.

Katika Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili, nilibaini kuwa katika mwaka 2021/22 kati ya vifaa vya matibabu 60 vilivyopangwa kwa ajili ya matengenezo, ni vifaa 27 (asilimia 45) tu vilifanyiwa kazi. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa mpango wa matengenezo (kwa baadhi ya mali) ambao Taasisi imeanzisha hauwiani na ratiba ya matengenezo iliyoelezwa na mwongozo wa mashine.

Iwapo vifaa tiba havitakaguliwa na kufanyiwa matengenezo kwa mujibu wa mpango, gharama ya juu ya ukarabati wa dharura wa vifaa inaweza kutokea na kuahirishwa mara kwa mara kwa huduma; kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2021/22, mashine ya uchunguzi wa kina wa mwili (MRI) ya Taasisi ya Mifupa Muhimbili iliharibika na iligharimu shilingi milioni 20 kwenye matengenezo. Iwapo vifaa havitakaguliwa kwa mujibu wa mpango, ubora wa huduma utaathirika.

**Ninapendekeza Taasisi ya Mifupa Muhimbili na Hospitali ya Mloganzila kuhakikisha mpango wa matengenezo unaandaliwa na kujumuisha mali zote muhimu za hospitali na kuhakikisha matengenezo yanafanyika mara kwa mara kama ilivyopangwa.**

## 17.10 Nakisi ya shilingi bilioni 189.65 katika Mfuko wa Bima ya Afya

Mfuko ulipata nakisi ya shilingi bilioni 189.65 kwa mwaka wa fedha 2021/22 kabla ya kodi (2021: shilingi bilioni 93.68). Nakisi ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na mapato ya michango ya wanachama kuwa chini ya gharama zilizotumika kwa wanachama. Gharama za wanachama zimekuwa zikikua kwa kiwango cha juu zaidi kuliko ukuaji wa mapato ya michango ya wanachama kwa miaka mitano iliyopita na kusababisha nakisi ya shilingi bilioni 132.06 (2021: shilingi bilioni 59.03) kutokana na kushughulikia wanachama, ambapo kuanzia mwaka 2021, gharama za wanachama zilikua kwa asilimia 24.6 huku michango ya wanachama ikiongezeka kwa asilimia 12.90. Hii inaonesha mwelekeo wa kupungua kwa mtiririko wa fedha. Ongezeko la matumizi ya huduma miongoni mwa wanufaika lilichangiwa na ongezeko la idadi ya wanachama na walengwa, na athari za janga la Uviko-19 kwa miongoni mwa wanufaika.

Kutokana na hali tajwa hapo juu, faida ghafi iliyokusanywa ya Mfuko imekuwa ikipungua kila mwaka.

Kutokana na ripoti ya watathmini ya mwaka 2021, miongoni mwa mapendekezo ya watathmini kwa Mfuko wa Bima ya Afya ni kuangalia upya na kubadili baadhi ya masharti ya uanachama wa hiari, kuboresha kanzidata na TEHAMA, kuboresha usimamizi wa watoa huduma za afya na kutathmini na kusimamisha baadhi ya uwekezaji kama vile mikopo iliyotolewa kwa taasisi za serikali.

**Ninapendekeza Mfuko wa Bima ya Afya (a) uangalie tena kuhusu mikakati ya jinsi ya kuzalisha ziada kutokana na kushughulika na wanachama na ziada kwa ujumla kwa ajili ya uendelevu wa Mfuko, na (b) kutathmini mapendekezo yaliyotolewa na wataalamu katika ripoti yao na inapowezekana kupitisha mapendekezo ili kurekebisha nakisi inayotokana na kushughulika na wanachama, kama vile kuacha kutoa mikopo na kuboresha usimamizi wa watoa huduma za afya.**

## 17.11 Utendaji usioridhisha wa Hospitali ya Mloganzila

Wakati wa tathmini yangu ya utendaji kazi wa Hospitali ya Mloganzila nilibaini kuwa gharama zilizidi mapato kwa asilimia 7 hadi 19 kutoka 2018/19-2021/22. Aidha, nakisi kwa mwaka iliongezeka kutoka shilingi bilioni 1.92 mwaka 2018/19 hadi shilingi bilioni 5.81 mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 394.

Sababu za hospitali kutofanya vizuri ni mapato yanayopotea kutokana na kuongezeka kwa misamaha ambayo wakati mwingine haidhibitiwi vizuri, kuongezeka kwa madai yanayokataliwa na Mfuko wa Bima ya Afya kutoka kwenye huduma zilizotolewa na Hospitali ya Mloganzila na huduma duni za kibingwa katika Hospitali ya Mloganzila kwa ajili ya kulaza wagonjwa binafsi na wale wa umma.

Utendaji duni unaweza kusababisha kuzorota kwa huduma za afya hospitalini kutokana na mapato duni ambayo hayawezi kukidhi gharama za uendeshaji na ugumu wa kufikia malengo ya kimkakati kutokana na kupungua kwa mapato kulingana na gharama zinazotumika.

**Ninapendekeza kuwa Hospitali ya Mloganzila (a) ihakikishe huduma za kibingwa zinaimarishwa hospitalini hapo ili kuongeza wagonjwa binafsi na wa umma, (b) ihakikishe inaendana na mwongozo wa Mfuko wa Bima ya Afya ili kupunguza idadi ya madai yanayokataliwa, na (c) kuweka misamaha kielektroniki ili kuimarisha udhibiti wa misamaha inayotolewa.**

## 17.12 Kuchelewa kwa kukamilika, kufungwa, kujaribiwa na kutumika kwa mfumo wa usimamizi wa hospitali (IHMS)

Mfuko wa Bima ya Afya uliingia katika makubaliano na kampuni ya Maxcom Africa Limited kwa ajili ya kutengeneza mfumo wa IHMS mnamo tarehe 18 Novemba 2015 kwa ajili ya kufunga, kupima na kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Hospitali na uthibitishaji wa kielektroniki wa kadi ya uanachama kwa muda wa mkataba wa miezi minane kutoka 23 Novemba 2015 hadi 23 Julai 2016. Gharama ya jumla ya makadirio ya mfumo huo ni shilingi bilioni 3.98. Hadi kufika tarehe 30 Juni 2022, jumla ya gharama iliyotumika ilikuwa shilingi bilioni 3.95. Madhumuni ya mfumo huo ni kulenga kudhibiti matumizi ya kughushi ya kadi za bima ya afya.

Mradi haukukamilika hadi Januari 2023, ikiwa ni ucheleweshaji wa zaidi ya miaka sita. Kuchelewa kukamilika kwa mradi kunaunyima Mfuko wa Bima ya Afya nafasi ya kuboresha ufanisi na kuongeza usahihi katika utoaji wa huduma.

**Ninapendekeza kuwa Mfuko wa Bima ya Afya uhakikishe mradi unakamilika ili kuboresha ufanisi wake katika utoaji wa huduma na kuondokana na kughushi matumizi ya kadi za bima.**

## 17.13 Uwezo wa Bohari Kuu ya Dawa wa kutoa huduma unaotiliwa mashaka

Ukaguzi wangu wa uwezo wa Bohari Kuu ya Dawa kufikia malengo ya kimkakati kwa mwaka 2021/22 ulibaini mapungufu yafuatayo.

### 17.13.1 Bidhaa ambazo muda wa matumizi umekwisha shilingi bilioni 30.18

Ukaguzi wangu wa bidhaa zilizopo ghalani zenye thamani ya shilingi bilioni 95.19 ulibaini uwepo wa bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 30.18 ambazo muda wake wa matumizi ulikuwa umekwisha. Bidhaa hizi zinazorotesha hali ya ukwasi wa Bohari Kuu kwasababu haziwezi kuuzika na hivyo kuzuia Bohari Kuu kufikia malengo yake.

### 17.13.2 Ucheleweshwaji wa ununuzi wa dawa na vifaa tiba

Tathmini yangu ya muda wa awali wa manunuzi kwa maombi ya manunuzi 5,936 yaliyotolewa mpaka kufika tarehe 30 Juni 2022 kwa bidhaa za ugonjwa wa mlipuko, bidhaa za kawaida na bidhaa maalum ulibaini ucheleweshaji mkubwa wa uwasilishaji wa bidhaa 354 za kawaida na maalum kati ya siku 30-197 zaidi ya siku 180 zinazohitajika na bidhaa 889 za kawaida na maalum hazikuwasilishwa licha ya ucheleweshaji ambao tayari umetokea kwa muda siku 30-380 zaidi ya siku 180 zinazohitajika.

### 17.13.3 Mapungufu Katika kusambaza bidhaa kwenye kanda

Sehemu ya 11.2(iv) ya Mkataba wa Huduma kwa Wateja wa Bohari Kuu ya Dawa wa mwaka 2021 na kalenda ya usambazaji ya Bohari Kuu ya Dawa 2021/22 kwa ajili ya kusambaza bidhaa kwenye kanda zinahitaji usambazaji wa bidhaa kufanywa ndani ya siku 14 tangu bidhaa zilipoagizwa.

Katika tathmini yangu nilibaini kuwa oda 5,957 (asilimia 14 ya jumla ya oda zote 43,409) zenye kiasi cha bidhaa 6,087,216 zilichelewa kusambazwa kutoka makao makuu ya Bohari Kuu ya Dawa kwenda kanda kwa muda wa siku 30-305. Ukaguzi zaidi

ulibainisha kuwa shehena ya oda 2,114 zenye kiasi cha bidhaa 1,073,464 zilizoombwa zilifikishwa kwenye kanda zikiwa karibu na kuisha muda wake wa matumizi.

### 17.13.4 Kushindwa kufikia kiwango cha chini cha bidhaa kwenye stoo za Bohari ya Dawa

Kiwango cha dawa katika stoo ya Bohari ya Dawa kinapaswa kisivuke kiwango cha chini kianachohitajika katika stoo ili kukidhi usambazaji kwa muda maalumu. Kiwango cha chini katika stoo ya kanda ni kile kinachotosheleza miezi minne na kwa stoo kuu ni miezi miwili.

Wakati wa ukaguzi wangu nilibaini kuwa Bohari Kuu ya Dawa haikufikia hata asilimia 60 ya kiwango cha chini cha bidhaa kinachohitajika kwa bidhaa za kufuatilia kiwango kwa mwezi mmoja (dawa ambazo zinakidhi kikamilifu mahitaji ya afya ya watu na zinapaswa kuwepo kila wakati kuruhusu mfumo wa afya ufanye kazi ipasavyo wakati wote). Mfumo wa udhibiti unahitaji bidhaa ziletwe kila zinaposhuka chini ya kiwango kinachohitajika ghalani. Bohari Kuu ya Dawa ilieleza kuwa bidhaa zilishuka chini ya kiwango cha chini cha bidhaa kutokana na kuongezeka kwa mizunguko ya usambazaji bidhaa kutoka mizunguko minne kwenda sita ya usambazaji na uhaba wa fedha za kununua bidhaa nyingi kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mahitaji ya wateja yanaweza yasitimizwe inavyohitajika ikiwa bidhaa zitashuka chini ya kiwango cha chini cha bidhaa bila kujazwa tena.

### 17.13.5 Bei za juu za dawa zaidi ya bei za mfuko wa bima ya afya kwa asilimia 5 hadi 98

Bei zilizoidhinishwa za Bohari Kuu ya Dawa ni kubwa kwa asilimia 5 hadi 98 kuliko bei zilizoidhinishwa na Mfuko wa Bima wa Afya (bei zitakazotumiwa na hospitali na vituo vya afya vinavyonunua bidhaa kutoka Bohari Kuu ya Dawa na kuwauzia wagonjwa waliokata bima na afya). Kutowiana huku kunaweza kuwa sababu kuu ya kwanini hospitali nyingi na vituo vingine vya afya kutotaka

kuagiza bidhaa Bohari Kuu ya Dawa huku wakijua kuweka oda Bohari Kuu ya Dawa kwa bei ya juu kutapelekea kupata hasara wakati wa kuuza bidhaa hizo kwa wagonjwa wenye bima ya afya.

### 17.13.6 Mapungufu katika kufanya makadirio ya mahitaji ya wateja

Katika kupitia makadirio ya mahitaji ya wateja kwa mwaka 2021/22 nilibaini mapungufu yafuatayo,

- Bidhaa zilizoombwa na wateja (3,813,864,032) zilikuwa asilimia 33 ya mahitaji yote yaliyokadiriwa ya bidhaa 11,712,651,816;
- bidhaa 42,037,840 ziliombwa baada ya kukadiriwa kwa mwaka 2021/22 lakini hazikununuliwa; na
- Bidhaa 710,675 zilinunuliwa na Bohari Kuu ya Dawa baada ya kukadiriwa lakini wateja hawakuweka oda.

Makosa haya yanasababishwa na kutotosheleza kwa mnyororo wa ugavi, bei zisizowiana kati ya Bohari Kuu ya Dawa na Mfuko wa Bima ya Afya na ukwasi usioridhisha unaochangiwa na madeni ya muda mrefu na bidhaa zilizokwisha muda wake.

Hali hii inaweza kusababisha usumbufu mkubwa wa uendeshaji wa Bohari Kuu ya Dawa hivyo kushindwa kutoa huduma zilizokusudiwa, upotevu wa fedha za umma kutokana na thamani kubwa ya bidhaa za ghalani kuisha muda wa matumizi kutokana na makadirio yasiyo sahihi, upotevu wa mapato kutokana na vituo vya afya na hospitali kutokukunua bidhaa kutoka Bohari Kuu ya Dawa kutokana na ukubwa wa bei.

**Ninapendekeza Bohari Kuu ya Dawa (a) iwasiliane na Wizara ya Afya ili kuwezesha ulipaji wa madeni ambayo bado hayajalipwa, (b) kurekebisha mfumo wa ugavi uliopo ili kuongeza ukadiriaji wa uhakika wa mahitaji, na (c) ihakikishe kiwango cha chini cha bidhaa kinapatikana ili kukidhi mizunguko sita ya usambazaji kwenye vituo vya afya na hospitali.**



# SURA YA KUMI NA NANE

# MAZAO NA BODI ZA MAZAO

## 18.0 Utangulizi

Sekta ya kilimo ni muhimu kwa uchumi na ustawi wa Tanzania, na Serikali ilianzisha taasisi na sera mbalimbali kusaidia maendeleo ya sekta ya kilimo. Hata hivyo, sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri kukua kwa sekta na uzalishaji. Changamoto hizo zinajumuisha michakato ya uwezeshaji wa mitaji na uratibu baina ya wadau wa sekta, kulima kwa kutegemea mvua, bei kubwa ya pembejeo, na kukosekana kwa taasisi za uhakika za kutoa mitaji na kuwawezesha wakulima.

Sura hii inaangazia masuala yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa bodi za mazao na majukumu ya bodi hizo, na mapendekezo ya hatua za kufuata kwa ajili ya kuboresha.

## 18.1 Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kushindwa kufanya biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko kwa ushindani na kwa ufanisi

Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilianzishwa ili kuwapa wakulima soko la uhakika la nafaka na mazao mchanganyiko na kuongeza uuzaji wa mazao hayo nje ya nchi ili kupata fedha za kigeni. Majukumu ya msingi ya Bodi ni pamoja na kufanya biashara itakayowezesha ukuaji wa sekta ya kilimo cha nafaka na mazao mengine.

Baada ya kufanya mapitio ya taarifa za fedha na shughuli za uendeshaji wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, nilibaini

kuwa taasisi hii ina changamoto ya kushindwa kufanya biashara ya nafaka na mazao mengine kwa ushindani hapa Tanzania. Uwezo na uhimilivu wa kifedha wa Bodi hii unategemea sana ruzuku ya Serikali ili kuweza kulipa gharama za uendeshaji kutokana na kukosekana kwa ufanisi wa kutumia mali za Bodi kuongeza mapato, kuwa na kiasi kikubwa cha fedha benki bila kuwekeza, na kukosekana mifumo fanisi ya kudhibiti gharama. Pia, Bodi inakabiliwa na changamoto ya ubora wa nafaka na mazao mengine kutoka kwa wakulima kwa sababu hainunui nafaka na mazao yenye kiwango cha chini na kubadilika badilika kwa bei za mazao sokoni.

Pia, nilibaini kuwa mbinu na mikakati ya kibiashara inayotumiwa na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko haina ufanisi wa kutosha kwa kuwa inafanya kazi chini ya uwezo wake na haifanyi tathmini ya kurejesha gharama zote za uendeshaji.

Endapo changamoto hizi hazitatatuliwa, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko haitafanikiwa kufanya biashara kwa ufanisi ili kukua na kutanua wigo wa shughuli zake za biashara na kupata faida inayokusudiwa.

**Ninapendekeza kuwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (a) iwasiliane na Serikali ili kuweka njia bora ya Bodi kuweza kutumia fursa za mikopo ya benki kwa wakati; (b) kuweka mbinu na mikakati ya biashara itakayoiwezesha Bodi kufanya biashara kwa ufanisi na kwa ushindani ili kuweza kupata faida, kukua na kutanua wigo wake wa biashara kimataifa.**

## 18.2 Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko inafanya kazi chini ya uwezo wake wa kuzalisha, kusindika na kuhifadhi bidhaa

Baada ya kuanzishwa na kuanza kazi mwaka 2010, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilikabidhiwa viwanda na vihenge vya lililokuwa Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC) vilivyoko Iringa, Arusha, Mwanza na Dodoma vyenye thamani ya shilingi bilioni 17.6, baada ya kufilisika kwa shirika hilo. Pia Bodi ilikabidhiwa maghala ya kuhifadhia mazao yaliyoko Iringa, Arusha, Mwanza,

Kiteto na Dodoma yenye thamani ya shilingi bilioni 9.35. Baada ya kukabidhiwa, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ilifanya ukarabati na matengenezo ya viwanda, vihenge na maghala hayo kwa gharama ya shilingi milioni 987.54 ili kuendana na teknolojia za kisasa katika kuzalisha na kuhifadhi nafaka na mazao mengine kibiashara. Matengenezo na ukarabati uliofanywa, umeongeza uwezo wa viwanda kuzalisha na kuboresha uwezo wa maghala kuhifadhi.

Hata hivyo, nilibaini kuwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko inazalisha na kuhifadhi kwa kiwango cha chini sana kulinganisha na uwezo wa viwanda na maghala yake, kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 53 na Jedwali Na. 54.** Viwango vilivyoainishwa kwenye majedwali vimejumlishwa kwa mwaka.

**Jedwali Na. 53: Uwezo wa viwanda vya bodi ukilinganisha na uzalishaji halisi**

| Mwaka wa Fedha | Uwezo wa Kiwanda (Mita za ujazo) | Uzalishaji Halisi (Mita za ujazo) | Uzalishaji Halisi kwa % | Uwezo wa uzalishaji ambao hautumiki kwa % |
|---|---|---|---|---|
| 2015/16 | 16,200 | 1,082.80 | 7 | 93 |
| 2016/17 | 16,200 | 2,040.28 | 13 | 87 |
| 2017/18 | 16,200 | 385.50 | 2 | 98 |
| 2018/19 | 16,200 | 3,820.96 | 24 | 76 |
| 2019/20 | 65,700 | 6,833.34 | 10 | 90 |
| 2021/22 | 126,900 | 14,623.93 | 12 | 88 |

***Chanzo:*** *Taarifa za Utekelezaji za Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa mwaka 2021/22*

**Jedwali Na. 54: Uwezo wa maghala kuhifadhi dhidi ya kiwango halisi kilichotumiwa kuhifadhi**

| Mahali pa ghala/Kihenge | Uwezo wa Kuhifadhi | Malengo na Viwango halisi vilivyotumika kuhifadhi kwa mwaka | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021/22 | | | 2020/21 | | |
| | Mita za ujazo | Malengo | Viwango halisi | Viwango halisi kwa asilimia | Malengo | Viwango halisi | Viwango halisi kwa asilimia |
| ARUSHA | | | | | | | |

| Mahali pa ghala/Kihenge | Uwezo wa Kuhifadhi | Malengo na Viwango halisi vilivyotumika kuhifadhi kwa mwaka | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2021/22 | | | 2020/21 | | |
| | Mita za ujazo | Malengo | Viwango halisi | Viwango halisi kwa asilimia | Malengo | Viwango halisi | Viwango halisi kwa asilimia |
| Kihenge | 28,100 | 28,100 | 3,805 | 13.5 | 28,100 | 478 | 1.7 |
| Ghala | 10,000 | 10,000 | 4,033 | 40.3 | 10,000 | 571 | 5.7 |
| **IRINGA** | | | | | | | |
| Kihenge | 13,500 | 13,500 | 25,954 | 192.3 | 13,500 | 18,272 | 135.3 |
| Ghala | 4,000 | 4,000 | 5,000 | 125.0 | 4,000 | 4,500 | 112.5 |
| **MWANZA** | | | | | | | |
| Ghala | 20,000 | 20,000 | 3,506 | 17.5 | 20,000 | 917 | 4.6 |
| **DODOMA** | | | | | | | |
| Ghala | 30,000 | 30,000 | 16,608 | 55.4 | 30,000 | 10,523 | 35.1 |
| KITETO | | | | | | | |
| Ghala | 1,000 | 1,000 | 1,000 | 100.0 | 1,000 | 60 | 6.0 |
| **TOTAL** | **106,600** | **106,600** | **59,906** | **56.2** | **106,600** | **35,321** | **33.1** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Utekelezaji za Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwa mwaka 2021/22*

Matumizi ya chini ya uwezo wa uzalishaji wa viwanda na uwezo wa kuhifadhi wa maghala ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, unatokana na sababu mbalimbali kama vile mtaji mdogo uliowekezwa katika biashara, ufanisi mdogo wa matumizi ya mtaji uliopo, kukosekana kwa malighafi kwa baadhi ya mazao, na ufanisi mdogo wa mbinu na mikakati ya biashara inayotumika. Ikizingatiwa kuwa Bodi ilianzishwa kwa ajili ya kufanya biashara ya nafaka na mazao mengine kwa mujibu wa kifungu cha 6 (1) na kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Na. 19 ya mwaka 2009, ili kuongeza ufanisi wa kazi zake na kuweza kufanya biashara kwa ushindani, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko inatakiwa kuweka mbinu zenye kuweza kubadilika kulingana na uhitaji kama vile kuajiri watumishi kwa haraka, ulipaji wa mishahara kulingana na hali, na kuweza kutumia fursa za kupata mtaji kwa haraka. Bila kufanya maboresho hayo, ni ngumu kwa Bodi kufikia malengo yake na kuwa na manufaa kwa umma.

**Ninapendekeza kuwa, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko iwasiliane na Serikali ili kupata mtaji wa kutosha na kuwekezwa kwenye biashara, na kuweka mbinu na mikakati thabiti ili kuiwezesha bodi kutumia uwezo wake kikamilifu na kwa ufanisi katika biashara.**

## 18.3 Udhaifu katika kupembua na kudhibiti gharama na kutofanya uchambuzi wa kujua wateja halisi wa bidhaa za Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko

Bidhaa zinazozalishwa ama kuuzwa na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko zina ubora mkubwa na zinakidhi vigezo na viwango vilivyowekwa na mamlaka za udhibiti na usimamizi. Kuhakikisha kuwa bidhaa zinakidhi vigezo na viwango vinavyotakiwa, kunasababisha pia kuongezeka kwa gharama za uzalishaji ama uandaaji kwa kila bidhaa. Hata hivyo, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko haina mbinu na mkakati mzuri wa kupanga bei ya kuuzia bidhaa zake kwa namna ambayo inaweza kurejesha gharama za uzalishaji na kupata faida inayokusudiwa kwa kila bidhaa inayouzwa. Bodi haiainishi kiwango cha mauzo mbacho kinarudisha gharama zote kwa ujumla, kabla ya kuanza kupata faida. Pia, mbinu na mikakati yake ya masoko, usambazaji na uuzaji haina ufanisi wa kutosha.

Kukosekana kwa uchakataji, uchambuzi na ufuatiliaji wa kina wa gharama za uzalishaji ama uandaaji wa bidhaa za bodi kunatokana na kukosekana kwa idadi ya kutosha ya wafanyakazi wenye weledi, maarifa na uzoefu wa kutosha. Hali hii inaiweka Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko katika hatari kubwa ya kupata hasara mfululizo na kutofikia mafanikio yaliyokusudiwa kwa umma.

**Ninapendekeza kuwa, Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (a) kuwasiliana na Serikali kuhakikisha kuna idadi ya kutosha ya wafanyakazi wenye weledi,maarifa na uzoefu unaotakiwa kwenye biashara ya nafaka na mazao mengine; (b) kununua, kuweka na kutumia mifumo madhubuti ya kuchakata na kudhibiti gharama, na (c) kufanya upembuzi na uchambuzi wa**

**kina kujua wateja wa bidhaa zake na kuweka na kutekeleza mbinu na mikakati thabiti ya kibiashara (kama vile mbinu na mikakati ya kudhibiti gharama, mauzo,masoko na usambazaji).**

## 18.4 Kupungua kwa mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya biashara

Katika ripoti yangu ya mwaka uliopita (Aya ya 17.1 ya 2020/21), niliripoti mwelekeo wa kupungua kwa uzalishaji wa baadhi ya mazao ya biashara ambayo ni maua ya pareto, crude extract, poda na Marc. Kwa ujumla, uzalishaji wa mazao ya biashara ulipungua kutoka tani milioni 1.06 kwa mwaka wa fedha 2019/20 hadi tani milioni 0.9 mwaka wa 2020/21.

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu nilibaini kuwa, pamoja na kuwepo kwa ongezeko dogo katika uzalishaji wa jumla kutoka tani 898,966.8 kwa mwaka wa fedha 2020/21 hadi tani 938,586.81 mwaka 2021/22, uzalishaji ulipungua kwa mazao ya biashara manne ambayo ni maua ya pareto, chai, kahawa, na mkonge. Hata hivyo, tangu mwaka wa fedha 2017/18, ambapo uzalishaji wa jumla ulikuwa tani milioni 1.01, jumla ya uzalishaji imekuwa ikibadilika-badilika, lakini kwa ujumla kwa miaka mitano iliyopita hakuna ongezeko kubwa la uzalishaji wa mazao ya biashara kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 55**.

**Jedwali Na. 55: Mwenendo wa uzalishaji wa mazao ya biashara kwa tani**

| Jina la Zao | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|---|---|
| Pamba | 222,039 | 348.958 | 348,977 | 122,836 | 144,792 |
| Kahawa | 45,245 | 68,147 | 60,651 | 73,027 | 65,235 |
| Chai | 34,010 | 37,193 | 28,715 | 27,510 | 17,615 |
| Maua ya Pareto | 2,400 | 2,014 | 2,510 | 2,412 | 1,895 |
| Tumbaku | 50,522 | 72,325 | 37,546 | 58,508 | 70,775 |
| Korosho | 313,826 | 225,053 | 232,682 | 210,786 | 238,555.81 |
| Mkonge | 40,635 | 33,271 | 36,379 | 36,169.8 | 29,719 |
| Sukari | 303,752 | 359,219 | 311,358 | 367,718 | 370,000 |
| **Jumla** | **1,012,429** | **797,570.958** | **1,058,818** | **898,966.8** | **938,586.81** |

***Chanzo****: Wizara ya Kilimo (Hotuba ya Waziri katika bajeti ya kilimo ya waka 2022/23)*

Hii inaashiria kwamba juhudi zilizowekwa na Serikali na taasisi zake katika kukabiliana na kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya biashara hazijafikia kiwango cha kumaliza changamoto hiyo.

**Hivyo basi, ninapendekeza tena kuwa Serikali kupitia bodi husika za mazao ya biashara, ichukue hatua zaidi za kuchunguza kwa undani sababu za kupungua kwa uzalishaji wa mazao ya biashara na kuchukua hatua madhubuti za kukabiliana na hali hiyo ili kuongeza uzalishaji wa mazao hayo nchini.**

## 18.5 Bodi za mazao kushindwa kukusanya mapato yanayotokana na utekelezaji wa majukumu yao ya msingi ili kujiendesha

Bodi za mazao zimepewa mamlaka ya kutoza tozo ama ada mbalimbali kama vile ada za usajili, tozo za ukaguzi, ada za vyeti, faini na adhabu kwa wasiofuata sheria kwa ajili ya kazi za usimamizi na udhibiti na kupata mapato ya kuziwezesha kuendesha kazi zao kwa mujibu wa sheria zilizozianzisha, kanuni, maelekezo na miongozo inayotolewa na Serikali. Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa bodi za mazao haziwezi kukusanya mapato ya ndani ya kutosha kutokana na kazi zao za msingi kwa ajili ya kulipa gharama za uendeshaji wa bodi hizo, huku sehemu kubwa ya makusanyo ya mapato ya ndani yakitokana na kazi ambazo si msingi wa kuanzishwa kwa bodi hizo. Hali hii imesababisha mapato ya ndani yanayotokana na kazi za msingi za bodi hizi na hata yakijumlishwa na mapato mengine ya ndani kwa pamoja, hayawezi kukidhi ama kumudu gharama za uendeshaji wa Bodi hizo, kama inavyoonekana **katika Jedwali Na. 56.**

**Jedwali Na. 56: Uwezo wa ukusanyaji wa pato la ndani dhidi ya uwezo wa kulipa gharama za uendeshaji**

| Jina | Jumla ya pato la ndani (Sh. milioni) | Kutoka kwenye kazi za msingi (Sh. milioni) | Asilimia ya pato la ndani la kazi za msingi | Jumla ya matumizi (Sh. Milioni) | Uwezo wa pato la kazi za msingi kugharamia matumizi % |
|---|---|---|---|---|---|
| Bodi ya | 549.76 | 73.23 | 13 | 1,498.29 | 5 |

| Jina | Jumla ya pato la ndani (Sh. milioni) | Kutoka kwenye kazi za msingi (Sh. milioni) | Asilimia ya pato la ndani la kazi za msingi | Jumla ya matumizi (Sh. Milioni) | Uwezo wa pato la kazi za msingi kugharamia matumizi % |
|---|---|---|---|---|---|
| Mkonge | | | | | |
| Bodi ya Pamba | 3,265.75 | 50.35 | 2 | 5,281.56 | 1 |
| Bodi ya Sukari | 10,024.34 | 4,872.15 | 49 | 6,688.53 | 73 |
| Bodi ya Korosho | 3,458.39 | 3,458.39 | 100 | 7,032.23 | 49 |
| Bodi ya Chai | 169.31 | 88.44 | 52 | 828.81 | 11 |
| Bodi ya Pareto | 68.46 | 0 | 0 | 328.41 | 0 |
| Bodi ya Tumbaku | 1,297.51 | 1,240.07 | 96 | 2,364.56 | 52 |
| Bodi ya Kahawa | 7,117.78 | 5,904.47 | 83 | 8,252.74 | 72 |
| **Jumla** | **25,951.30** | **15,687.10** | | **32,275.11** | |

***Chanzo:*** *Taarifa za fedha za bodi kwa miaka husika*

Kwa kuwa Bodi za Mazao zinategemea ruzuku ya Serikali kwa kiasi kikubwa ili kujiendesha, utegemezi wa kazi ambazo si msingi wa kuanzishwa kwa bodi za mazao katika kukusanya mapato ya ndani kama vile kodi za upangishaji majengo na mapato mengine, kunaongeza hatari ya uwezekano wa kupungua kwa juhudi za bodi katika kazi zao za msingi, hivyo kupunguza ubunifu na hamasa katika kutekeleza majukumu ya bodi kama chanzo kikuu cha mapato.

**Ninapendekeza kuwa, serikali izisimamie Boadi za Mazao ya Biashara kuhakikisha zinatekeleza majukumu yao ya msingi kwa ubunifu na ufanisi ili kuwezesha kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato yanayotokana na kazi za msingi**

## 18.6 Kutokuwepo kwa uhakika kama kupanda kwa bei za mazao ya chakula kunawanufaisha wakulima

Ripoti zangu za miaka ya nyuma zimekuwa zikieleza kuwa mazao ya chakula na mazao mengine yamekuwa yakikabiliwa na

kukosekana kwa masoko ya uhakika, hali iliyosababisha wakulima kuuza mazao hayo kwa bei ndogo. Hali hii inawaumiza wakulima kwa kuuza mazao yao kwa bei isiyo nzuri hali iliyowasababishia kupata hasara. Hata hivyo, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto ya kukosekana kwa masoko ya uhakika kwa kuhakikisha upatikanaji wa masoko kwa mazao ya wakulima, hasa mazao ya chakula na mazao mengine. Kwa mfano, baada ya serikali kufanya tathmini ya utoshelevu wa chakula nchini ilifungua mipaka ya nchi kwa wafanyabiashara wa nje kuja kununua mazao kutoka soko la ndani la Tanzania na kusafirisha nje ya nchi. Hatua hii iliongeza uhitaji wa mazao ya chakula yanayozalishwa ndani ya nchi na kuchochea kupanda kwa bei ya mazao hayo kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 57**.

**Jedwali Na. 57: Mwenendo wa mabadiliko ya bei za mazao ya chakula (Bei ya jumla)**

| Zao la Chakula | Shilingi za Tanzania kwa 100Kg | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **2017/18** | **2018/19** | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** |
| Mahindi | 51,760.60 | 47,745.00 | 72,212.40 | 52,427.00 | 57,264.30 |
| Mchele | 182,986.80 | 158,742.40 | 175,175.60 | 141,316.40 | 169,257.40 |
| Mtama | 85,894.00 | 75,527.50 | 104,442.60 | 92,482.70 | 108,534.20 |
| Uwele | 146,681.00 | 134,706.50 | 129,901.20 | 137,718.40 | 162,609.20 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Viwanda na Biashara*

Hata hivyo, hakuna ushahidi wa tathmini unaoonesha kwamba kupanda kwa bei ya mazao ya chakula kunawanufaisha wakulima wa mazao hayo kwa kuwa hakuna tathmini iliyofanyika. Hivyo, kuna hatari na uwezekano mkubwa kuwa kupanda kwa bei ya mazao ya chakula hakuwanufaishi wakulima bali kunawaathiri kwa kuwa wakulima wengi ni wadogo na wanafanya kilimo cha kujikimu, hivyo hawana uwezo wa kuhifadhi mazao ili kuuza baadaye bei zikiwa zimepanda.

**Ninapendekeza kuwa, Serikali ifanye tathmini ili kuhakiki kama kuongezeka kwa bei za mazao ya chakula kunawanufaisha wakulima ama hakuwanufaishi, na kuchukua hatua stahiki kutokana na matokeo ya tathmini itakayofanyika.**

## 18.7 Mapungufu katika mchakato na mifumo ya usimamizi wa mbolea

kujidhatiti kwa Serikali katika kuongeza uzalishaji wa sekta ya kilimo na kuhamasisha matumizi ya mbolea katika kilimo kunadhihirika kwa kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania ili kusimamia uzalishaji, uuzaji, uingizaji na biashara ya mbolea nchini. Lengo kuu ni kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo na kuilinda jamii ya wakulima na umma kwa ujumla dhidi ya athari za kiafya na majanga yanayotokana na matumizi ya mbolea, pamoja na kudhibiti udanganyifu katika soko la mbolea.

Wakati wa ukaguzi nilibaini mapungufu katika mchakato na mfumo wa usimamizi wa mbolea kama ilivyoainishwa katika vipengele vinavyofuata;

### 18.7.1 Uwezo mdogo wa kuzalisha mbolea ndani ya nchi

Uwezo wa kuzalisha mbolea ndani ya Tanzania ni mdogo na kuna kiwanda kimoja tu cha kuzalisha mbolea nchini. Wastani wa uwezo wa kuzalisha mbolea ndani ya nchi ni asilimia 7 tu ukilinganisha na mahitaji kwa miaka mitatu ya 2019/20, 2020/21 na 2021/22 **(Jedwali Na. 58).** Juhudi za Serikali kuanzisha kampuni yake ya kuzalisha mbolea (Tanzania Fertilizer Company) hazijazaa matunda kwa kuwa kwa mwaka 2021/22 Kampuni hiyo haikuzalisha wala kuuza mbolea na wala haikuweza kukusanya mapato yeyote kutokana na shughuli zinazohusu mbolea. Utegemezi wa nchi kwa mbolea inayoagizwa kutoka nje ya nchi ni mkubwa, ambapo asilimia 71 ya mbolea inaagizwa kutoka nchi za nje ili kukidhi mahitaji ya mbolea nchini. Hata hivyo, wastani wa asilimia 22 ya mahitaji ya mbolea nchini hayakutimizwa.

**Jedwali Na. 58: Mwenendo wa hali ya upatikanaji wa mbolea nchini (Mita za ujazo na asilimia)**

| Mwaka | Mahitaji | Mbolea inayozalishwa nchini | | Mbolea inayoagizwa nje | | Upungufu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mita za ujazo | Mita za ujazo | Asilimia | Mita za ujazo | Asilimia | Mita za ujazo | Asilimia |
| 2019/20 | 586,604 | 33,873 | 6 | 524,972 | 89 | 27,758 | 5 |

| Mwaka | Mahitaji | Mbolea inayozalishwa nchini | | Mbolea inayoagizwa nje | | Upungufu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mita za ujazo | Mita za ujazo | Asili mia | Mita za ujazo | Asili mia | Mita za ujazo | Asili mia |
| 2020/21 | 718,051 | 42,695 | 6 | 504,122 | 70 | 171,233 | 24 |
| 2021/22 | 698,260 | 62,724 | 9 | 379,927 | 54 | 255,609 | 37 |
| **Wastani** | **667,638** | **46,431** | **7** | **469,674** | **71** | **151,533** | **22** |

***Chanzo****: Wizara ya Kilimo*

Nchi (hasa wakulima) iko katika hatari ya kukosekana kwa mbolea au kupanda kwa bei za mbolea endapo kutatokea vikwazo vitakavyokwamisha ununuzi na usafirishaji wa mbolea kutoka nje ya nchi kama vile kufungwa kwa mipaka ya nchi zinazozalisha mbolea, kunakoweza kusababishwa na vita, magonjwa ya mlipuko au majanga ya asili. Kwa mfano, athali hizi zimejidhihirisha wakati wa vikwazo vya kusafiri na kusafirisha bidhaa kulikotokana na mlupuko wa ugonjwa wa COVID-19, na vikwazo vinavyotokana na vita ya Urusi na Ukraini vilivyosababisha kupungua kwa uingizaji wa mbolea kutoka nje na kuongezeka kwa bei ya mbolea nchini, hali iliyoilazimu serikali kuanzisha programu ya ruzuku ya mbolea kwa mwaka 2022/23.

Kutokana na juhudi za sasa zinazofanywa na serikali katika kuimarisha na kuikuza sekta ya kilimo, kama vile kujenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, ujenzi wa vihenge na maghala ya kuhifadhia mazao, na juhudi zingine za kuhamasisha kilimo; na kwa kuwa mbolea bora ni muhimu katika kuongeza ufanisi wa kilimo.

**Ninapendekeza kuwa, Serikali itengeneze na kutekeleza mpango wa kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi.**

### 18.7.2 Ucheleweshwaji wa usajili wa mbolea na visaidizi vya mbolea unaofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania

Kanuni ya 7(1) & (2) ya Kanuni za Mbolea za mwaka 2011, zinaitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania ndani ya siku 21, kusajili mbolea na visaidizi vya mbolea na kutoa vyeti vya usajili baada ya kujiridhisha kuwa waombaji wametimiza

masharti na vigezo vya usajili vilivyowekwa na baada ya kuwa wamelipa ada za usajili.

Lakini wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa waombaji 23 kati ya 32 walisajiliwa baada ya mwezi mmoja na wengine hadi miezi miwili zaidi ya muda wa usajili unaotakiwa. Kwa mujibu wa maelezo ya menejimenti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania, ucheleweshwaji huu unatokana na kuchelewa kwa vipimo vya maabara.

Ucheleweshwaji katika mchakato wa usajili wa mbolea na visaidizi vya mbolea, unaweza kusababisha matumizi, kuingizwa sokoni ama kuuzwa kwa mbolea na visaidizi vya mbolea ambavyo havijasajiliwa, hali inayoweza kusababisha matumizi ya mbolea na visaidizi vya mbolea visivyofaa kwa matumizi ya umma.

**Ninapendekeza kuwa, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania ihakikishe inaboresha ufanisi wa mchakato wa usajili wa mbolea na visaidizi vya mbolea kuepuka ucheleweshwaji usiokuwa wa lazima.**



# SURA YA KUMI NA TISA

# UFANISI KATIKA SEKTA YA MADINI, GESI NA MAFUTA

## 19.0 Utangulizi

Uziduaji (uchimbaji wa madini na gesi) ni sekta inayohusisha uchimbaji wa malighafi ili kutumika katika nyanja mbalimbali. Malighafi hizo ni pamoja na madini, gesi asilia na mafuta kutoka ardhini.

Tanzania ina akiba kubwa ya rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia zinazoweza kuchangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa nchi. Sekta ya uziduaji imechangia asilimia 5.2 ya pato la Taifa

Nilipitia utendaji wa mashirika ya umma yanayohusika na uziduaji katika sekta ya uziduaji wa madini, mafuta na gesi. Taasisi zilizokaguliwa ni pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa juu wa Petroli (PURA), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Tume ya Madini, Shirika la Taifa la Madini (STAMICO), na Kampuni ya Stamigold.

## 19.1 Mapitio ya utendaji wa mashirika ya umma yanayohusika na sekta ya gesi asilia na madini

Ukaguzi wa mashirika ya umma yanayohusika na sekta ya uziduaji wa mafuta na gesi ulibaini mapungufu yafuatayo ambayo yanahitaji ufuatiliaji wa Serikali:

### 19.1.1 Kuchelewa kutekeleza mradi wa umeme wa makaa ya mawe ya Kiwira Megawati 200

Shirika la Umeme Tanzania limejiwekea lengo la kuongeza uzalishaji wa umeme kufikia Megawati 1,836 ifikapo Juni 2022 kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Tarehe 10 Agosti 2021, Shirika la Umeme Tanzania na Shirika la Taifa la Madini waliingia kwenye makubaliano ya utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Kiwira ambapo ililenga kuzalisha Megawati 200 hadi kufikia Julai 2027. Katika ukaguzi wa utekelezaji wa mradi huu nilibaini kuwa kazi zilizopangwa kufanyika katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa mradi hazikuwa zimefanyika hadi wakati nahitimisha ukaguzi wangu tarehe 30 Desemba 2022 kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 59**. Pia licha ya kuwepo mkataba wa utekelezaji wa Mradi wa Umeme wa Makaa ya Mawe ya Kiwira, Shirika la Umeme Tanzania halikujumuisha mradi huo kuwa ni miongoni mwa miradi yake ya kimkakati katika Mpango Mkakati wake wa kati (2021/22 - 2022/23), ili kuupa mradi huo kipaumbele na kurahisisha upatikanaji fedha kwa ajili utekelezaji.

**Jedwali Na. 59: Malengo ambayo hayakutekelezwa kama walivyokubaliana kwenye mkataba**

| Na. | Malengo yaliyo pangwa ambayo hayakutekelezwa | Tarehe iliyopangwa |
|---|---|---|
| 1. | Kuwapata Washauri wa kufanya upembuzi ya Mradi | Novemba 2021 |
| 2. | kuwasilisha upembuzi wa kibenki na tathmini ya athari za mazingira | Aprili 2022 |
| 3. | Kumpata Mkandarasi kwa ajili ya uhandisi, manunuzi na ujenzi (EPC) | Juni 2022 |
| 4. | kuwasilisha mkataba wa EPC na mapendekezo ya fedha | Septemba, 2022 |
| 5. | Kujadili mapendekezo ya fedha | Novemba, 2022 |

***Chanzo:** Makubaliano ya utekelezaji mradi kati ya Shirika la Umeme Tanzania na Shirika la Taifa la Madini*

Ni maoni yangu kuwa makaa ya mawe ni rasilimali muhimu nchini ambayo bado hayajatumika kikamilifu katika uzalishaji wa nishati ya umeme.Kutokana na ongezeko la mahitaji makubwa ya nishati nchini, na kutokana na mabadiliko ya tabia nchi yanayoathiri hali ya upatikanaji wa maji yanayotumika kufua umeme. Pamoja na kusuasua kwa uwekezaji kwenye shughuli za utafiti na uchimbaji wa gesi, ni muhimu kwa Shirika la Umeme Tanzania kupanua wigo wa vyanzo vyake vya kuzalisha umeme kwa kuharakisha utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme wa makaa ya mawe ya Kiwira.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania: (a) kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Madini kuchukua hatua za haraka kutekeleza mradi wa makaa ya mawe wa Kiwira bila kuchelewa zaidi, na (b) kuandaa mapendekezo ya fedha zinazohitajika kutekeleza mradi na kuwasilisha Serikalini kupitia Wizara ya Nishati na Wizara ya Fedha na Mipango, ikisisitiza umuhimu wa mradi katika kuzalisha umeme na kukuza uchumi wa nchi.**

### 19.1.2 Kuchelewa kulipia gesi ambayo haijatumika ambayo muda wake wa matumizi unazidi ukomo wa mkataba inayohusisha shilingi bilioni 30.41

Kifungu cha 5.3 cha Mkataba wa mauziano ya gesi (GSA) kati ya Shirika la Umeme Tanzania, Shirika la Maendeleo ya Petroli, na kampuni ya PanAfrican Energy Tanzania (PAET), wa tarehe 17 Juni 2011, kinaelekeza kuwa katika kipindi cha mkataba, muuzaji (PAET) atauza na kufikisha gesi asilia kwa mnunuzi (Shirika la Umeme Tanzania) katika sehemu iliyopendekezwa kulingana na mahitaji yanayotolewa kama ilivyo katika masharti ya mkataba.

Shirika la Umeme Tanzania litapokea na kulipia gesi kama lilivyoomba au italipa kiasi hicho cha gesi asilia pamoja na ile ambayo itakua imeshindwa kuitumia kulingana na masharti ya mkataba. Gesi ambayo itakua hajatumika/kuchukuliwa itakuwa ni gesi ya ziada ambayo mnunuaji atakua na haki ya kuitumia ndani ya miaka mitano baada ya kuilipia.

Ukaguzi wangu ulibaini Shirika la Umeme Tanzania lina ankara mbili ambazo hazikulipiwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 zinazotokana na madai ya gesi ambayo haijatumika kutoka kampuni ya PAET zenye jumla ya thamani ya shilingi bilioni 30.41. Aidha, nilibaini muda wa matumizi ya gesi utaisha Juni 2025 kwa ankara moja, na kwa ankara ya pili muda wa matumizi ya gesi utaisha Juni 2026, hata hivyo muda huu utazidi muda wa ukomo wa mkataba unaotarajiwa ambao ni Juni 2023.

Hadi wakati nahitimisha ukaguzi (Novemba 2022), hakuna malipo yaliyofanywa na Shirika la Umeme Tanzania ili kupata haki ya kutumia gesi hiyo ya ziada **(Jedwali Na. 60).**

**Jedwali Na. 60: Ankara za gesi ambazo muda wake unazidi muda wa ukomo wa mkataba**

| Tarehe ya ankara | Maelezo | Mwisho wa mkataba | Mwisho wa haki za matumizi / kipindi | Kiasi cha ankara (Dola za Marekani) |
|---|---|---|---|---|
| 30-Juni-20 | Ankara au Kuchukua au kulipa | Juni 2023 | 30-Juni 2025 | 6,502,359.27 |
| 30-Juni-21 | | Juni 2023 | 30-Juni 2026 | 6,698,162.28 |
| | | **Jumla ya dola za Marekani** | | **13,200,521.55** |
| | | **Jumla shilingi** | | **30,414,001,651.20** |

***Chanzo:*** *Ankara za gesi ambazo hazijalipiwa*

Kuchelewa kulipiwa kwa ankara hizo na kutotumika kwa gesi inayoendana na ankara hizi kulitokana na Shirika la Umeme Tanzania kutofuata vipengele vya mkataba kwa ukamilifu ikiwemo kuchelewa kuamua kiwango cha gesi inayotakiwa. Kwa kuwa mkataba utafika ukomo Juni 2023 na endapo mkataba huu hautaongezwa muda, basi malipo yatakayofanywa na Shirika la Umeme Tanzania kwa ankara hizi mbili yatakua hasara kwa shirika na nchi.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania (a) liimarishe kitengo cha usimamizi wa mikataba ili kuepuka migogoro ambayo kimsingi imesababisha malipo ya gesi kutofanyika kwa wakati na kuwezesha matumiziyagesi ndani ya muda wa mkataba; (b) lifanye mazungumzo na muuzaji wa gesi ili**

**kupata njia bora zitakazowezesha Shirika kutumia gesi iliyobaki; (c) lihakikishe kuwa ikiwa muda wa mkataba utaongezwa ili Shirika liweze kutumia gesi husika basi Shirika liwasilishe mahitaji ya gesi kwa wakati ili kuepuka bakaa kubwa ya gesi ambayo haijatumika.**

### 19.1.3 Mipango hafifu katika kutekeleza mradi wa kuunganisha umeme Mgodi wa Biharamulo

Shirika la Umeme Tanzania na Kampuni yake tanzu ya kujenga njia za kusafirisha na kusambaza umeme (ETDCO) waliingia mkataba wa huduma tarehe 25 Agosti 2020 kwa ajili ya ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya KV 33 yenye urefu wa kilomita 110 kutoka kituo cha kupoza umeme cha Geita hadi mgodi wa kampuni ya STAMIGOLD Biharamulo kwa gharama ya shilingi bilioni 5.48 kwa kipindi cha miezi minne. Kuunganishwa kwa mgodi kwenye gridi ya taifa kutasaidia kampuni ya Stamigold kupunguza gharama za uendeshaji zinazosababishwa na gharama kubwa za mafuta ya kuendesha majenereta ya umeme hivyo kuongeza mapato kwa Shirika la Umeme Tanzania na Kampuni ya STAMIGOLD.

Mapitio yangu ya taarifa ya utekelezaji wa mradi ya mwezi Juni 2022 nilibaini kuwa mbali na njia maalumu ya kusafirisha umeme kulihitajika kujengwa kituo cha kupoza umeme mgodini ili kuweza kuunganisha umeme. Ukaguzi ulibaini kuwa mkataba wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme ulisainiwa tarehe 06 Mei 2021 kwa kipindi cha miezi nane huku gharama yake ikiwa ni shilingi bilioni 10.53. Taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme, inaonesha hadi Disemba 2022 ujenzi ulikuwa haujakamilika wakati ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Geita hadi Biharamulo ulikuwa umekamilika kwa asilimia 100 na umeme kuwashwa.

Mradi huu umechelewa kwa muda wa mwaka mmoja kutokana na kukosekana kwa ufanisi wa mpango wa kutekeleza mradi na kuchelewa kuanza kwa mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme.

Ikiwa mikataba yote ingeanza kwa wakati mmoja, ingepunguza muda wa kukamilisha mradi huu, hivyo kufanikisha malengo ya mradi kwa wakati. Faida za uwekezaji kwa mradi huu zinachelewa kupatikana kwa sababu Shirika la Umeme Tanzania halijaweza kupata mapato kutoka kwenye mgodi. Pia, kampuni ya STAMIGOLD inaendelea kutumia gharama kubwa za uendeshaji zisizo na tija zinazotokana na gharama kubwa ya mafuta ya kuendesha mgodi.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania (a) kufuatilia kwa karibu mradi huu ili kuhakikisha kituo cha kupoza umeme kinakamilika bila kuchelewa zaidi, ambacho ni muhimu kwa kuunganisha mgodi kwenye gridi ya taifa, na (b) pia kuhakikisha kuwa kwa miradi ijayo kunafanyika mipango thabiti ili miradi ikamilike kwa wakati na kufikiwa malengo yaliyokusudiwa.**

### 19.1.4 Kupungua kwa mauzo ya dhahabu ya mgodi wa STAMIGOLD kwa shilingi bilioni 11.66

Mapitio yangu ya taarifa za fedha za kampuni ya Stamigold kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21 nilibani mauzo ya kampuni yaliongezeka kuendana na kuongezeka kwa uzalishaji wa dhahabu ambao ulionesha utendaji mzuri. Aidha mwaka wa fedha 2021/2022 mauzo yalipungua kwa shilingi bilioni 11.66 sawa na asilimia 23 ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 49.24 ya mwaka 2020/2021. Kupungua kwa mapato kumetokana na kupungua kwa uzalishaji kulikotokana na kupungua kwa uwezo wa mkandarasi katika kuchimba dhahabu kulikosababishwa na ukosefu wa vifaa madhubuti. (Jedwali Na. 61).

**Jedwali Na. 61: Mwenendo wa mauzo na uzalishaji**

| Mwaka wa fedha | Mauzo ya dhahabu (Sh. bilioni) | Tani za mchanga wa dhahabu zilizochimbwa |
|---|---|---|
| 2018/19 | 38.64 | 365,484 |
| 2019/20 | 43.70 | 395,232 |
| 2020/21 | 49.24 | 405,058 |

| Mwaka wa fedha | Mauzo ya dhahabu (Sh. bilioni) | Tani za mchanga wa dhahabu zilizochimbwa |
|---|---|---|
| 2021/22 | 37.59 | 230,445 |

***Chanzo:*** *Taarifa za utekelezaji za kampuni ya STAMIGOLD*

Kwa maoni yangu ufanisi wa Kampuni ya STAMIGOLD unaathiriwa na uzalishaji hafifu wa dhahabu kutokana na uwezo mdogo wa mkandarasi anayefanya kazi ya kuchimba kwa niaba ya kampuni ya STAMIGOLD.

**Ninapendekeza kampuni ya STAMIGOLD (a) ichukue hatua za haraka na stahiki dhidi ya mkandarasi wa uchimbaji madini ili atekeleze kazi kama ilivyokubaliwa katika mkataba ili kuongeza uzalishaji na kuongeza mauzo ya dhahabu, na (b) ifanye uchunguzi wa kutosha kabla ya kuingia mkataba na wakandarasi kwa ajili ya shughuli za uchimbaji madini.**

### 19.1.5 Utekelezaji hafifu wa majukumu ya Shirika la Taifa la Madini katika kuwezesha ufanisi wa kiwanda cha kuchakata dhahabu Mwanza

Mnamo tarehe 19 Disemba 2019 Shirika la Taifa la Madini liliingia makubaliano ya pamoja ya kujenga na kuendesha mradi wa kiwanda cha kuchakata dhahabu Mwanza na wabia ambao ni kampuni ya Rozella General Trading LLC na ACME Consultant Engineering. Majukumu ya wabia ni kujenga na kusimamia shughuli za kiwanda kupitia uwekezaji wa moja kwa moja na kulipa Shirika la Taifa la Madini hisa ya asilimia 25. Makubaliano ya ubia chini ya Kifungu 6.3 (h), yanatoa wajibu kwa Shirika la Taifa la Madini kusaidia na kuandaa vituo vya ukusanyaji vya ndani ili kupata dhahabu ghafi kama malighafi kwa ajili ya kiwanda cha uchakataji.

Mnamo tarehe 29 Agosti 2022 nilitembelea kiwanda hicho ili kuona utendaji wake na kubaini kuwa, kiwanda kilikuwa kinafanya kazi chini ya uwezo wake, pia hakijapata cheti cha ubora cha kimataifa (ISO) kutokana na uzalishaji mdogo. Uwezo wa kiwanda ni kuchakata kilogramu 480 kwa siku, lakini hadi

kufikia tarehe 10 Oktoba 2022 kiwanda kilipata jumla ya malighafi ya kilogramu 170.84 na kuzalisha dhahabu yenye jumla ya kilogramu 43 tangu kiwanda kizinduliwe tarehe 13 Juni 2021.

Kwa maoni yangu, Shirika la Taifa la Madini halijatimiza majukumu yake kwa ufanisi ambayo yangehakikisha kwamba dhahabu ghafi inapatikana kiwandani ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na mradi na malengo ya serikali ya kudhibiti usafirishaji wa dhahabu ghafi, kukuza mapato na kutokomeza masoko ya biashara haramu ya dhahabu.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Taifa la Madini litimize majukumu yake kwa kusaidia na kuandaa vituo vya ukusanyaji wa dhahabu ghafi ili ipatikane ya kutosha kufikia malengo yalikosudiwa kikamilifu.**

### 19.1.6 Jitihada hafifu katika kuendeleza Mgodi wa Dhahabu wa Buhemba

Shirika la Taifa la Madini liliingia mkataba wa ubia (hisa za 30/70) na Kampuni ya Goodfield International DMCC kutoka Falme za Kiarabu tarehe 4 Septemba 2020 kwa ajili ya uendelezaji wa mradi wa dhahabu wa Buhemba Mwamba mgumu chini ya leseni ya utafiti Na. PL 7132/2011 kwa kufanya utafiti wa kina, na kutekeleza shughuli za uchimbaji wa kibiashara kwenye eneo husika.

Mapitio yangu ya taarifa ya utekelezaji wa mradi ya tarehe 28 Agosti 2022 yalibaini kwamba kati ya kazi 13 zilizopangwa kukamilishwa hadi kufikia tarehe 1 Desemba 2022, kazi 3 zilikuwa bado hazijaanza wakati kazi 10 zilikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji **(Jedwali Na. 62).**

**Jedwali Na. 62: Shughuli zilizochelewa kwenye mradi wa Buhemba**

| Na. | Kazi zilizopangwa | Tarehe ya kuanza | Tarehe ya mwisho iliyopangwa | Asilimia za utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Usimamizi wa Mradi katika hatua za awali na Awamu ya Ujenzi | 01-Mei-20 | 01-Oktoba-22 | 35 |

| Na. | Kazi zilizopangwa | Tarehe ya kuanza | Tarehe ya mwisho iliyopangwa | Asilimia za utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Ubunifu wa mgodi | 31-Oktoba-20 | 15-Septemba-22 | 3 |
| 3 | Mipango ya Mgodi na muundo wa uchimbaji | 31-Oktoba-20 | 14-Aprili-22 | 0 |
| 4 | Miundombinu | 13-Februari-21 | 31-Agosti-22 | 6 |
| 5 | Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi | 01-Aprili-21 | 01-Desemba-22 | 50 |
| 6 | Kufanya upembuzi wa bwawa la kuhifadhi matope susu | 12-Aprili-21 | 15-Juni-22 | 0 |
| 7 | Kuthibitisha Rasilimali zilizopo aridhini | 12-Mei-21 | 15-Septa-22 | 10 |
| 8 | Utafutaji na uhakiki / uchimbaji wa visima | 13-Mei-21 | 13-Juni-22 | 40 |
| 9 | Kuandaa vifaa, kutengeneza na kusafirisha | 30-Septemba-21 | 13-Mei-22 | 30 |
| 10 | Kushughulikia sehemu za bomba, jukwaa na usanifu wa vipuri | 30-Septemba-21 | 29-Disemba-21 | 50 |
| 11 | Zabuni ya Shughuli za Uchimbaji Madini (Mining Ore & Waste, Drill and Blast) | 01-Disemba-21 | 15-Februari-22 | 80 |
| 12 | Utafiti wa kijiografia na uchimbaji ili kufafanua miteremko ya jumla | 01-Februari-22 | 03-Machi-22 | 20 |
| **13** | Ujenzi wa Kambi za Muda | 01-Februari-22 | 15-Machi-22 | 0 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya utekelezaji Mradi*

Sababu kubwa ya kuchelewa kwa mradi huu ni kuchelewa kwa shughuli ya kuthibitsha uwepo wa madini. Hali hii ina athari hasi kwa maendeleo ya mgodi.

**Ninapendekeza Shirika la Taifa la Madini lichukue hatua na kuweka mikakati madhubiti kuhakikisha mradi wa kuendeleza mgodi wa dhahabu wa Buhemba unatekelezwa kama ulivyopangwa ili kuanza kwa uzalishaji wa dhahabu.**

### 19.1.7 Kutelekezwa kwa mradi wa vioo wa Nyanza na athari zake kwenye uchimbaji wa madini ya mchanga wa vioo

Mradi wa kiwanda cha vioo Nyanza ulianzishwa mwaka 1978 kwa lengo kuu la kuzalisha vioo ili kupunguza gharama za uagizaji kutoka nje. Malighafi kuu kwa uzalishaji wa bidhaa za kioo ni mchanga wa vioo na chumvi ya sodiamu ambayo inapatikana kwa

wingi katika Wilaya za Bukoba na Monduli mtawalia. Ujenzi wa kiwanda ulianza mwezi wa Februari 1981 na ulikamilika kwa asilimia 83 na ununuzi wa mashine na ufungaji ulikamilika kwa asilimia 98.

Mradi ulisimama kutokana na ukosefu wa fedha na Shirika la Maendeleo la Taifa lilipewa mamlaka na Serikali kupitia Gazeti la Serikali Na.186 la 11 Julai 2003 kuuza mashine zote na vifaa vingine vya mradi, na shirika la maendeleo la taifa liliuza mashine hizo na kubadilisha malengo ya miundo mbinu ya majengo kuwa ya kupangisha.

Ukaguzi wangu wa leseni za uchimbaji madini zinazomilikiwa na Shirika la Maendeleo la Taifa kwa miradi yake mbalimbali kufikia Juni 2022 ulibaini kuwepo kwa leseni nane za uchimbaji wa madini ya mchanga wa vioo huko Bukoba. Leseni hizo zote zilitolewa tarehe 16 Novemba 2012 lengo likiwa ni kufufua kiwanda cha vioo Nyanza. Hadi wakati wa ukaguzi mnamo Disemba 2022, hakuna shughuli za uchimbaji wa madini zilizofanyika katika maeneo yaliyopewa leseni kutokana na kukwama kwa muda mrefu kwa kiwanda cha vioo Nyanza kilichopo Mwanza.

Kwa maoni yangu lengo la kuwa na kiwanda cha vioo Mwanza halijapewa kipaumbele wakati mahitaji ya vioo bado yapo na Shirika linaweza kupata mapato zaidi kutoka kwa mradi huo ikiwa mpango kamili utawekwa na kutekelezwa.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Maendeleo la Taifa (a) lipitie upya lengo la kuwa na mradi wa vioo Mwanza, na (b) litayarishe mpango wa kuendeleza mradi ikiwa matokeo ya tathmini yataonesha kuwepo kwa manufaa ya kuendelea na mradi, au litayarishe mpango wa kina kwa shughuli zingine za kufanywa katika eneo hilo.**

### 19.1.8 Mapungufu yaliyobainika katika matengenezo ya mitambo ya kuzalisha umeme yanayo athiri uzalishaji wa umeme na mauzo ya gesi asilia

Mapitio yangu ya masuala yanayoathiri utendaji kazi wa mitambo ya uzalishaji umeme na hivyo kuathiri uzalishaji wa umeme na mauzo ya gesi kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania nilibaini mapungufu kama ilivyoinishwa hapa chini:

#### a) Changamoto ya kusimama mara kwa mara kwa mitambo ya kuzalisha umeme yanayotokana na kutofanyika kwa matengenezo ya tahadhari

Mapitio yangu ya taarifa ya kituo cha kuzalisha umeme cha Mtwara na ubungo namba moja kwa mwaka 2022 yalibaini injini 13 kati ya 25 zilipata changamoto zisizotarajiwa au hitilafu kwa muda wa masaa 28,641. Hii ikiwa ni tofauti na makadirio ya masaa 421 na hivyo kupelekea masaa ya ziada yapatayo 28,220 kinyume na mipango. Muda wa kusimama kwa injini ulikuwa ni kati ya masaa 7 hadi 8,760.

#### b) Kuchelewesha kwa matengenezo kati ya siku 2 hadi 243

Mapitio yangu ya mipango ya matengenezo na ripoti za utekelezaji wa matengenezo ya mitambo ya umeme zilizotolewa na Shirika la Umeme Tanzania kwa mwaka wa 2021/22 yalibaini ucheleweshaji wa kufanyika matengenezo kati ya siku 2 hadi 243. Kwa maoni yangu kwamba kushindwa kufanya matengenezo kwa wakati kunapelekea uharibifu wa mitambo ambao ungeweza kuepukika. Hivyo kuchelewa kufanya matengezo kwa wakati kunapelekea gharama za matengenezo kuwa kubwa kwa Shirika la Umeme Tanzania kutokana na uharibifu ulitokana na kuchelewa kufanya matengenezo kwa wakati.

### c) Kutotekeleza na kusimamia ipasavyo sera ya matengenezo ya kuzuia hitilafu

Katika mapitio yangu ya ripoti ya uzalishaji ya mtambo wa Ubungo II kwa mwaka wa fedha 2021/22 nilibaini kuwa matengenezo ya marekebisho ya hitilafu yalizidi matengenezo ya kuzuia hitilafu kwa masaa 1,328

Kwa maoni yangu matengenezo ya baada ya tatizo kutokea yataonekana ni gharama nafuu mwanzoni lakini gharama inakuwa kubwa kadiri muda unavoongezeka. Aidha, matengenezo ya kuzuia hitilafu yanafanyika kila baada ya muda uliopangwa au kwa mujibu wa vigezo maalum ,na yanapunguza muda wa kutofanya kazi kwa mitambo na kuboresha utendaji wa mitambo ikiwa ni pamoja na kuiwezesha kuimalisha uhai wa mitambo.matangenezo haya huwa yanaoneka kuwa na gharama kubwa mwanzoni lakini ni gharama nafuu kwa muda mrefu.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania lihakikishe kuna usimamizi wa kutosha katika utekelezaji wa shughuli za matengenezo zilizopangwa ili kuepuka hitilafu zisizotarajiwa za mitambo na kukatika kwa umeme kusikopangwa.**

## 19.1.9 Kuchelewa kukusanywa kwa kodi ya leseni shilingi milioni 472.11

Ukaguzi wangu wa usimamizi wa leseni katika ofisi ya madini Mkoa wa Singida ulibaini kuwepo kwa leseni 553 zilizotolewa kwa waombaji tofauti kati ya mwaka 2014 hadi 2022. Lakini hakuna malipo ya kodi ya kila mwaka na faini hadi wakati wa ukaguzi huu mwezi Desemba 2022, ambao ni sawa na shilingi milioni 472.11 kinyume na Kifungu cha 22 (a) - (b) ya Sheria ya Madini, Sura ya 123.

Kwa maoni yangu kutokukusanya kiasi kikubwa cha kodi na adhabu zake kunainyima Serikali mapato ni ishara ya kutofuata masharti ya leseni, ambayo yanaweza kusababisha leseni kufutwa.

**Ninapendekeza Tume ya Madini (a) iweke usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa leseni zilizotolewa ikiwa ni pamoja na kulipwa kwa wakati kodi na mapato mengine yasiyo ya kodi yanayotakiwa; na (b) ihakikishe leseni zilizotolewa lakini kodi haijalipwa zinafutwa ili kuruhusu wawekezaji wengine kufanya maombi na kuendelea na uzalishaji endapo vitendo vya kutotii kwa wamiliki wa leseni vitaendelea.**

### 19.1.10 Kuwepo kwa zaidi ya vituo vya mitambo 205 ya uchenjuaji madini ambayo haijasajiliwa katika eneo la Geita

Ukaguzi wangu wa shughuli za uchenjuaji madini nilibaini kuwepo kwa vituo vya mitabo 205 visivyo na leseni katika mkoa wa Geita vinayofanya kazi hiyo. Vituo hivyo vimesajiliwa na ofisi ya madini kwa madhumuni ya ukusanyaji wa kodi ya kila mwaka na ya leseni kinyume na Kifungu cha 6(1) ya Sheria ya Madini,Sura 123. Aidha,mitambo hiyo hipo kinyume na kifungu 7(1) cha sheria ya Madini sura 123 Mitambo hiyo imesajiliwa na Ofisi ya Meneja wa Mkoa tu, kwa lengo la kukusanya kodi ya kila mwaka na mirabaha bila kuwa na leseni kutoka kwa Tume ya Madini.

Ni maoni yangu kuwa kuna hatari ya kupotea kwa mapato ya serikali kutokana na ukosefu wa wajibu wa lazima kwa wamiliki na pia kuna hatari kwa watu wanaoishi karibu vituo hiyo kudhurika kutokana na kemikali hatari zinazotumiwa katika shughuli za uchakataji kama hazitadhibitiwa vizuri.

**Ninapendekeza kuwa Tume ya Madini (a) itekeleze utoaji wa leseni za uchenjuaji na kuwaelimisha wananchi katika maeneo ya migodi; na (b) ifanye ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo yaliyopewa leseni ili kubaini shughuli zisizohusiana na masharti ya leseni za uchimbaji na kuchukua hatua stahiki.**

### 19.1.11 Kuchelewa kutolewa kwa leseni kwa ajili ya utafiti wa gesi na mafuta kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania

Katika ukaguzi wangu wa shughuli za Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na hatua zilizochukuliwa kuimarisha maendeleo

ya mkondo wa juu ili kuweza kukidhi ongezeko la mahitaji ya gesi, nilibaini kuwa shirika liliomba leseni ya utafiti kwa ajili ya kitalu cha rasi ya Mnazi kaskazini mwaka 2019 lakini leseni hiyo hadi kufikia muda wa ukaguzi wangu mwezi Novemba 2022 ilikuwa haijatolewa, ambapo ni zaidi ya miaka mitatu tangu ilipoombwa. Aidha, nilibaini kuwa kibali cha uchunguzi wa kijiografia na kiteknolojia eneo la kitalu cha rasi ya Mnazi kilichotolewa tarehe 10 Januari 2019 kilikuwa kimefikia ukomo tangu tarehe 9 Januari 2022 na bado kilikuwa hakijahuishwa.

Kwa maoni yangu, ucheleweshaji wa kutolewa kwa leseni za utafiti unaathiri kufikiwa kwa malengo ya Shirika na pia kushindwa kutumia fursa iliyopo kuongezeka kwa mahitaji ili kuweza kuongezeka uzalishaji wa gesi na kuchochea ukuaji wa uchumi.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania liendelee kuwasiliana na Wizara ya Nishati, Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli kuhakikisha leseni inatolewa bila kuchelewa zaidi.**

### 19.1.12 Mapungufu kwenye usimamizi na uhakiki wa mita za gesi

Kifungu cha 19(2) cha Sheria ya vipimo Sura ya 340 ya mwaka 1982, kinahitaji kuwa kila mzani, kipimo, kipima uzani au kipima kipimo kikaguliwe, kuhakikiwa na mkaguzi. Aidha, kipengele cha 3(A) cha muongozo unaohusiana na vyombo vya vipimo na uzani, Tangazo la Serikali Na. 288 la 2019, kinaeleza kuwa kipima kimiminika kinapaswa kuhakikiwa kila robo mwaka au baada ya ukarabati au kurekebishwa.

Katika usimamizi madhubuti na wa dhati ni muhimu sana kuwepo kwa mita ya kujitegemea ili kuweza kuhakiki upimaji wa gesi unaofanywa na mita nyingine ili kuweza kuwa na taarifa za kuaminika zinazopelekea kufanya malipo. Pia ni muhimu na ni takwa la kisheria mita kuhakikiwa na wakala wa vipimo ili kuweza kutoa uhakikisho wa mita husika. Hii inapelekea mteja kulipa

kulingana na matumizi yake sahihi yaliyotokana na taarifa sahihi iliyohakikiwa na vyombo vilivyokasimiwa kufanya kazi hiyo.

Mapitio yangu ya usimamizi wa vipimo ili kuhakikisha usahihi wa taarifa kwa ajili ya matumizi ya mteja ulibaini mapungufu yafuatayo:-

### a) Kutofanyika kwa uhakiki wa mita za gesi

Mapitio ya ripoti za utendaji na tathmini yalibaini kuwepo kwa mita za gesi 1,555 ambazo hazikuhakikiwa kama inavyotakiwa na sheria ya wakala wa kipimo (WMA). Mita hizo zimefungwa maeneo mbalimbali huku mita moja ikiwa imefungwa Songosongo, mita 8 kwenye viwanda, mita 27 zimeunganishwa kwenye mfumo wa kupunguza shinikizo la gesi (PRMS) na mita 1,520 kutoka kwenye bomba la Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kwenda kwa wateja wa majumbani Mtwara, Lindi, na Dar es Salaam.

### b) Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kutoweka udhibiti katika uhakiki wa gesi kutoka rasi ya Mnazi

Mwezi June 2022 nilitembelea mtambo wa kuchakata gesi wa rasi ya Mnazi na kubaini kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania halikuweka udhibiti kwa kufunga mita yake kwa ajili ya kusoma kiasi cha gesi iliyonunuliwa kutoka kampuni ya Maurel na Prom. Aidha Shirika kama mnunuzi linategemea mita za muuzaji ili kuweza kupima gesi inayonunuliwa na shirika.

Pia, Sheria ya wakala wa vipimo (WMA), inahitaji ukaguzi kufanyika kila robo mwaka, nilibaini mita za Maurel na Prom (M&P) mara ya mwisho kukaguliwa ilikuwa Machi 2021 hadi wakati wa ukaguzi (Agosti 2022) hakuna ukaguzi uliofanyika.

Kwa maoni yangu kutokufanyika kwa uhakiki na kukosekana mita za kuhakiki kunaweza kusababisha hasara ya mapato kwa wateja kupewa ankara pungufu na kwa pande wa ununuzi wa gesi kuna hatari kupewa ankara zaidi ya kiasi kilichopokelelewa.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania lianzishe mfumo wa ukaguzi wa mara kwa mara wa mita za gesi, pia liweke udhibiti wa kutosha kwenye ununuzi wa gesi, kama vile kufunga mita ya kuhakiki gesi inayopokelewa kutoka kwa muuzaji ambaye ni kampuni ya Maurel Prom.**

### 19.1.13 Kutekelezwa kwa mradi bila kuwepo makubaliano kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka

Mradi wa gesi kwa ajili ya matumizi ya mabasi yaendayo haraka Dar-es-salaam ni mradi ambao unafaida mbalimbali ikiwemo faida za kimazigira kwakuwa gesi asilia ni nishati safi ikilinganishwa na dizeli kwa sababu hutoa gesi chache chafuzi na kupunguza gharama kwa kubadilisha mfumo wake kutoka kutumia mfumo wa mafuta na kutumia gesi asilia kwa ajili ya kuendesha mabasi. Gharama ya mafuta ni kubwa tofauti na gesi, hivyo kusaidia kupunguza gharama za uendeshaji kwa mradi huu. Kushuka kwa gharama za undeshaji kunaenda sambamba na kupungua kwa nauli hivyo kuufanya mfumo wa usafiri wa umma uweze kuwa nafuu na wakutegemewa kwa wakazi wa Dar es Salaam.

Mpango mkakati wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kwa kipindi cha 2018/19 -2022/23 umeainisha miongoni mwa malengo yake ni kuongeza wigo wa soko pamoja na ujenzi wa kituo cha kujaza gesi katika kituo cha mabasi ya Mradi wa mabasi yaendayo kasi Dar-es-salaam Ubungo ukilengwa kuwa mmoja wa mteja mkubwa wa mradi.

Mapitio yangu ya utekelezaji wa mradi wa gesi asilia kwa matumizi ya vyombo vya moto nilibaini kuwa katika mwaka wa 2018/19 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania lilianza mazungumzo na Wakala wa mabasi yaendayo kasi Dar-es-salaam kwa ajili ya ujenzi wa kituo maalumu cha kuuzia gesi katika eneo la Ubungo baada ya kupata vyeti vya tathmini ya athari za Mazingira kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Pamoja na mipango mizuri hapakuwepo na

makubaliano ya kisheria kati ya pande hizo juu ya ujenzi wa kituo hicho. Hivyo mnamo tarehe 30 Desemba 2021 ulifanyika mkutano wa pande mbili ambapo Wakala wa Mabasi yaendayo Haraka walitangaza kujiondoa wakieleza sababu kuwa wameishaingia mkataba wa miaka 12 na kituo cha usambazaji wa mafuta (Diseli) kwa mabasi ya mwendo kasi, hivyo mradi ulisita kuendelea.

Katika kutekeleza mradi huo Mnamo tarehe 12 Septemba 2019, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania liliingia mkataba wa huduma za ushauri na ubunifu pamoja usimamizi wa ujenzi wa vituo gesi asilia jijini Dar es salaam, ikiwa ni pamoja na kituo cha gesi asilia Ubungo kwa ajili ya mabasi yaendayo haraka kwa gharama ya mkataba ya shilingi milioni 808.55. Kazi za ubunifu zilikamilika mnamo Septemba 2020 ikijumuisha eneo la kituo cha mabasi ya mwendokasi, ingawa kulikuwa hakuna makubaliano kati ya Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kuhusu matumizi ya eneo huku jumla ya shilingi milioni 323.42 tayari zilikuwa zimeshalipwa kwa Mshauri. Pia Mshauri alilipwa kiasi cha shilingi milioni 34.4 kwa ajili ya kusimamia zabuni Na. PA/031/2020-21/W/23 kwa Mkandarasi wa Uhandisi, Ugavi na Ujenzi, Ufungaji, Majaribio na Uzinduzi wa Kituo cha Kuzalisha gesi Asilia (CNG) kwa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka.

Ni maoni yangu kuwa kutokuwepo kwa Mkataba kati ya pande mbili kulisababisha kukosekana kwa azma ya kutekeleza mradi. Vile vile haya matatizo yote yanaweza kuwa yamesababishwa na kukosekana upembuzi wa kina wa mradi na hivyo yaweza kupelekea shilingi milioni 357.85 zilizotumika kuwa ni hasara.

**Ninapendekeza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (a) Kuishirikisha Wizara mama na Wizara ya Uchukuzi na Miundombinu kufanya mazungumzo na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka ili kutekeleza mradi ambao utaleta nafuu ya gharama za usafiri kwa umma na soko la gesi; na (b) kuhakikisha kuwa mbeleni miradi yote itakayojumusha wabia kunakuwepo na mkataba wa utekelezaji wa mradi.**

### 19.1.14 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kuuza gesi kwa garama ya juu kwa Shirika la Umeme Tanzania

Mnamo tarehe 17 Januari 2019, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji iliandika barua yenye kumbukumbu namba: EWURA/60/TR.1/16/2/019/Vol III/51 kwenda Wizara ya Nishati ikirejea ripoti ya utafiti wa gharama za Shirika la Umeme Tanzania ambayo ilipendekeza mambo mawili ili kupunguza bei ya gesi, na kufanya bei ya umeme kuwa nafuu kwa Watanzania. Pendekezo la kwanza lilikuwa kubadili mikopo ya Serikali kwa Shirika la Umeme Tanzania kuwa Ruzuku na pendekezo la pili lilikuwa kutekeleza pendekezo la kwanza pamoja kubadilisha mkopo wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kwenye bomba la gesi kuwa Ruzuku. Iwapo Serikali itafanyia kazi mapendekezo hayo bei ya gesi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania inaweza kupunguzwa kutoka dola za Marekani 5.19 kwa mmBTU hadi 4.359 kwa mmBTU ambayo itapunguza gharama ya kuzalisha umeme kwa Shirika la Umeme Tanzania.

Ukaguzi wangu wa Mikataba ya mauziano ya gesi pamoja na ankara za madai ya kila mwezi ulibaini kwamba bei iliyotozwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania bado ni kubwa ikilinganishwa na wauzaji wengine wa gesi kama vile kampuni ya PAET licha ya mapendekezo yaliyotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji mwaka 2019.**Jedwali Na. 63**

**Jedwali Na. 63: Bei za gesi zinazotozwa na TPDC na kampuni ya PAET**

| Jina la msambazaji gesi | Bei ya gesi kwa mmBTU katika dola za Marekani |
|---|---|
| Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania | 5.5384 |
| Kampuni ya PAET | 3.8002 |
| Tofauti ya bei | 1.7382 |
| Asilimia za tofauti ya bei | 45.7 |

***Chanzo***: *Mkataba na ankara*

Ni maoni yangu, kwa kuzingatia utegemezi mkubwa wa Shirika la Umeme Tanzania kwenye gesi katika uzalishaji wa umeme, bei ya gesi ni kigezo kikuu cha gharama za uzalishaji wa umeme

ambazo pia huchangia katika vigezo vya kupanga bei ya umeme. Ninafahamu kuwa mwaka 2022, Serikali ilikuwa imetangaza uamuzi wake wa kubadilisha mkopo wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kuwa mtaji na hatimaye kupelekea manufaa kwa jamii.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kuhakikisha kunafanyika mapitio ya bei ya gesi kama ilivyopendekezwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ili kupunguza gharama za uendeshaji umeme hivyo kuleta manufaa kwenye tozo za umeme.**

## 19.2 Ufuatiliaji na usimamizi wa mikataba ya ushirikiano katika uzalishaji (PSA) katika Sekta ya Petroli na Gesi

Tanzania inatumia mikataba ya ushirikiano katika uzalishaji wa gesi (PSA) kama nyenzo ya kusimamia shughuli za gesi asilia. Mikataba hiyo ya uzalishaji wa gesi ndiyo mikataba mama ambayo husimamia uhusiano kati ya nchi na makampuni ya mafuta. Lengo kuu la mikataba hii ni kuhakikisha kuwa nchi inapata manufaa kamili na stahiki kutokana na rasilimali pamoja na kuvutia uwekezaji unaohitajika ili kufaidika na rasilimali hizo. Ili Serikali ipate manufaa katika sekta ya mafuta na gesi asilia, kuzingatia masharti ya mkataba ni muhimu. Mapitio yangu kwenye utekelezaji wa mikataba hii yalibaini mapungufu yafuatayo:

### 19.2.1 Migogoro ya muda mrefu kuhusu gharama zilizotumiwa na makampuni ya gesi kiasi cha dola za Marekani milioni 386.67

Hadi tarehe 30 Juni 2022 kulikuwa na mgogoro kuhusu gharama ambazo kampuni za mafuta zinahitaji kurejeshewa kabla ya kugawana mapato kufuatia maoni yaliyotolewa na ukaguzi. Nilibaini madai yaliyokuwa changamoto kutoka kwa makampuni sita ya mafuta yanayofikia jumla ya dola za Marekani milioni 487.02. Kiasi hiki kinajumuisha dola za Marekani milioni 64.87 zinazohusiana na ukaguzi uliofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa

Mkondo wa juu wa Petroli (PURA) baada ya majukumu hayo kuhamishwa kutoka Shirika la Maendeleo ya Mafuta (TPDC) mwaka 2017.

Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli imefanikiwa kutatua migogoro yenye thamani ya dola za Marekani milioni 11.53 na kushindwa kutatua migogoro yenye dola za Marekani milioni 53.34, pia migogoro inayotokana na ukaguzi uliofanywa na Shirika la Maendeleo ya Petroli na kushindwa kutatuliwa ilikuwa na thamani ya dola za Marekani milioni 333.33 hivyo jumla ya kiasi cha migogoro isiyotatuliwa ni dola za Marekani milioni 386.67. Migogoro hii ina miaka saba bila ya kupata ufumbuzi.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (a) ishirikiane na Shirika la Maendeleo ya Petroli ambao walifanya ukaguzi kabla ya mwaka 2015 na mamlaka husika (kama Wizara ya Nishati na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu) ili kuharakisha ufumbuzi wa gharama za marejesho ya uwekezaji zenye migogoro ya muda mrefu ili kulinda mapato ya serikali; na (b) iongeze jitihada za majadiliano na makampuni ya mafuta na gesi ili kuongeza kasi ya kujibu hoja kuhusu gharama zilizoripotiwa.**

### 19.2.2 Kutofanyika kwa uhakiki wa gharama zilizolipwa na kampuni ya mafuta

Mapitio yangu ya gharama zilizowasilishwa kama makato kwa mwaka wa fedha 2021/22 yalibaini kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania lilipokea ripoti za robo mwaka kutoka kwa kampuni ya uzalishaji wa gesi ya Maurel & Prom ambayo inaonesha kiasi cha shilingi bilioni 5.72 kama gharama zilizowasilishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (Wakaguzi) ikionesha aina ya gharama kulingana na mgawanyo uliokubaliwa. Aidha nilibaini kutokuwepo na hatua zilizochukuliwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kama mbia katika biashara kujiridhisha usahihi wa gharama hizo na

kubaki kutegemea ukaguzi unaofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli.

Ni maoni yangu kuwa, kutokuwepo kwa utaratibu wa kuhakiki gharama zilizoingiwa na makampuni ya uzalishaji kwa wakati kunaongeza uwezekano wa gharama hizo kutokuwa sahihi na kuathiri moja kwa moja mapato ya Serikali.

**Ninapendekeza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania lishirikiane na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petrol kuanzisha mfumo wa kupitia gharama kwa wakati.**

## 19.3 Mapitio ya mfumo wa kisheria katika Sekta ya Uziduaji

Mfumo wa kisheria ni muundo wa kisheria unaosimamia tasnia ya uziduaji. Hii ni pamoja na katiba, sheria, kanuni na mikataba, na mikataba ya kimataifa inayosimamia sekta hiyo. Mfumo wa kisheria unafanya jukumu muhimu katika kuhakikisha utawala bora na maendeleo endelevu, kwani ni uti wa mgongo wa uhusiano kati ya Serikali, kampuni za uchimbaji, Makampuni ya mafuta, na wadau wengine katika tasnia. Mapitio yangu juu ya ufanisi wa mfumo wa kisheria yameonesha mapungufu yafuatao:

### 19.3.1 Kutoanzishwa kwa mfumo na mikakati ya matumizi ya rasilimali za ndani kwa ajili ya kukuza teknolojia kwenye sekta ya mafuta na gesi

Ukaguzi wangu wa usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za ndani nilibaini kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli haijaanzisha mfumo wa ushirikishwaji na ufuatiliaji wa rasilimali za ndani kuendana na tekinolojia katika sekta ya mafuta, pia suala hili halikujumuishwa katika mipango ya utekelezaji ya Mamlaka hii, jambo ambalo ni kinyume na Kifungu 4 (3) cha Kanuni za Ushirikishwaji wa Ndani katika Sekta ya Mafuta za mwaka 2017.

Kwa maoni yangu kutokuwepo kwa mfumo wa ushirikishaji wa ndani na mikakati ya ufuatiliaji na tathmini ya uhamishaji wa

teknolojia kunaweza kusababisha ukosefu wa umakini na mwelekeo wa kuimarisha uhamishaji wa teknolojia. hivyo, sekta inaweza kuwa tegemezi sana kwa bidhaa na huduma zinazoagizwa kutoka nje, hali ambayo hupunguza faida za kiuchumi kwa nchi.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli iunde mfumo wa maudhui ya ndani na mikakati ya kufuatilia na kutathmini mpango wa matumizi ya rasilimali za ndani katika uhamishaji wa teknolojia katika sekta ya mafuta na gesi.**

### 19.3.2 Kutoanzishwa kwa kanzidata ya mafuta

Ukaguzi wangu wa mpango kazi wa utekelezaji wa mikakakati ya mwaka, nilibaini kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli ilipanga kuanzisha kanzidata ya Mafuta ifikapo Juni 2022. Hata hivyo nilibaini kanzidata hiyo bado haijaanzishwa kinyume na Kifungu 84 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) ya 2015, kilichokua kinaeleza ukusanyaji wa taarifa na baadhi ya taarifa zilikuwa bado zipo chini ya Shirika la Maendeleo ya Petroli ikijumuisha mikataba ya mauzo ya gesi.

Kwa maoni yangu kutokuwepo kanzidata ya mafuta kunazuia upatikanaji wa taarifa za sekta ya mafuta kwa wadau, na kufanya iwe ngumu kufanya baadhi ya maamuzi. Ni muhimu kuanzisha na kuendeleza kanzidata ya mafuta ili kukuza uwazi, kuzingatia sheria na kanuni, na kufanikisha uwekezaji katika sekta.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli ifanye kazi kwa karibu na Shirika la Maendeleo ya Petroli na wadau wengine kukusanya habari zote muhimu na kuhakikisha kuwa Kanzidata ya mafuta inakamilishwa kwa wakati kama inavyotakiwa na kanuni.**

### 19.3.3 Ukosefu wa mkataba mfano wa mauzo ya gesi

Mapitio yangu ya Mikataba mitatu ya manunuzi ya gesi kati ya Shirika la Umeme Tanzania na wauzaji wa gesi ambao ni makampuni ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, Kampuni ya PAET na Kampuni ya M&P Exploration Production Tanzania, yalibaini kuwa mikataba hiyo kuwa tofauti kati ya mkataba mmoja hadi mwingine katika muktadha wa vifungu vilivyomo, na kuna changamoto na migogoro kadhaa inayojitokeza kutokana na vifungu vya mikataba ambavyo havilingani na shughuli za biashara na mazingira yake kama vile riba kubwa kwa kuchelewa kulipa,kuwasilisha mahitaji na kulipia gesi ambayo haikutumiwa.

Kwa maoni yangu ni kwamba kuandaliwa kwa mfano wa Mkataba kutapunguza mizozo katika biashara ya gesi na hivyo kusaidia kuleta umoja katika masharti ambayo yatatekelezwa na pande zote mbili kwa urahisi.

**Ninapendekeza mashirika na taasisi zingine zinaoshiriki katika kusimamia biashara ya uuzaji wa gesi kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati kuanzisha mchakato wa kuandaa mfano wa Mkataba wa Uuzaji wa gesi.**

### 19.3.4 kukosekana kwa bei elekezi kwa madini adimu

Ukaguzi wangu ulibaini kuwapo kwa madini ya metali kama vile Neodymium, Lanthanum, Cerium, Scandium, na Europium ambayo hakuna bei elekezi katika masoko ya ndani au kimataifa kinyume naKifungu cha 22(S) cha Sheria ya Madini, Sura 123; Hii inasababishwa na jitihada hafifu za Tume ya Madini katika kutoa bei elekezi za madini.

Ni maoni yangu kuwa kutokuwepo kwa bei elekezi za madini kunaleta hatari ya kupotea mapato ya Serikali kama vile ushuru kwa kutokuwepo thamani ya metali hizo sahihi ya thamani ya madini hayo.

**Ninapendekeza kuwa Kamisheni ya madini ihakikishe utoaji wa bei elekezi za madini metali hizo ili kuboresha tathmini ya madini na kukokotoa mapato ya kodi.**

### 19.3.5 Muingiliano wa majukumu ya kusimamia na utekelezaji wa majukumu ya uwajibikaji wa kijamii wa kampuni unaosababishwa na mkanganyiko wa kisheria

Ukaguzi wangu kuhusiana na usimamizi wa uwajibikaji wa kijamii ulibaini kuwa kuna muingiliano kati ya Kifungu cha 22 na 105 cha Sheria ya Madini, Sura 123 kuhusu ufuatiliaji na usimamizi wenye ufanisi wa programu za majukumu ya uwajibikaji wa kijami. Kamisheni ya Madini, mbali na kupewa jukumu la kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa uwajibikaji wa kijamii na mmiliki wa haki ya madini, jukumu hilo limekabidhiwa pia kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, hivyo kusababisha mgongano juu ya ni nani anayewajibika kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa uwajibikaji wa kijamii.

Ni maoni yangu kuwa hali ya kuweka jukumu kwa taasisi mbili tofauti inaleta hatari ya kukosekana uwajibikaji, jukumu na nia ya kutekeleza majukumu hayo, ambayo kwa upande wake husababisha usimamizi usio na ufanisi wa Uwajibikaji wa Kijamii

**Ninapendekeza uongozi wa Kamisheni ufanye yafuatayo: (a) Kushirikiana na Wizara Mama na mamlaka husika ili kuondoa utata kati ya Kifungu cha 22 na 105 cha Sheria ya Madini kuboresha uwajibikaji na uwazi; na (b) Kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika ili kuhakikisha wamiliki wa haki za madini wanatimiza mahitaji ya Sheria ya Uchimbaji Madini kuhusu kutekeleza jukumu lake la Uwajibikaji wa Kijamii wa Kampuni kwa jamii ili kunufaika na rasilimali zake ikiwa ni pamoja na kukuza mikakati yenye ufanisi kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya jamii katika ngazi za chini.**

### 19.3.6 Kuchelewa kuanza uchimbaji wa madini katika eneo lenye leseni maalumu Na. SML 489/2013

Kifungu na 47(a) cha Sheria ya Madini, Sura ya 123 kinaeleza kuwa mmiliki wa leseni anapaswa kuanza shughuli za uchimbaji ndani ya miezi kumi na nane au kipindi kingine kisichozidi hicho kitakachoruhusiwa na mamlaka ya leseni kuanzia tarehe ya utoaji wa leseni na kuendesha shughuli za uchimbaji kwa kuzingatia kwa kiasi kikubwa mpango wa shughuli za uchimbaji na mpango wa usimamizi wa mazingira.

Pia kifungu Na 6.2 cha makubaliano ya uzalishaji kati ya Kampunii ya MANTRA Tanzania Limited na Wizara ya Madini kwa miaka 15 tangu tarehe 5 Mei 2013 kinaeleza kwamba, mmiliki wa leseni anapaswa kuanza kazi za maendeleo ndani ya miezi mitatu tangu tarehe ya utoaji wa leseni maalumu ya uchimbaji au kipindi kingine kitakachokubaliwa na Waziri, kwa msingi wa mipango, muundo wa jumla wa mgodi na miundombinu inayohusiana, na shughuli za nyongeza zinazolingana na mpango wa uchimbaji ulioidhinishwa.

Nilibaini mnamo tarehe 14 Disemba 2016, Kampuni ya Mantra iliandika barua kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Madini kuomba kusitisha mpango huo kutokana na bei ndogo ya madini kwenye soko la dunia, kama ilivyothibitishwa na Kifungu cha 69(1) cha Sheria ya Madini, Sura 123. Aidha hadi wakati wa ukaguzi wangu Disemba 2022, hakuna taarifa yoyote kuhusu kuanza uzalishaji licha ya kipindi cha miaka sita kupita tangu kazi ziliposimamishwa na miaka tisa kupita tangu leseni hiyo itolewe.

Ni maoni yangu kuwa kusimamishwa kwa maendeleo na uzalishaji kwa kipindi kirefu kunazuia Serikali kupata mapato ya kodi na mapato mengine yasiyo ya kodi kama vile mrabaha. Vile vile viashiria vya kutofuata sheria na masharti ya mkataba yanayoweka hatari ya migogoro inayowezekana kutokea siku za usoni na pia eneo lililopo chini ya leseni limeifugwa kuzuia serikali kushirikiana na wawekezaji wengine wenye uwezo.

**Ninapendekeza Kamisheni ya Madini iingie ifanye mazungumzo na mwekezaji juu ya kuendeleza leseni na ikiwa makubaliano hayakufikiwa, sheria na masharti ya mkataba yanayotakiwa yatekelezwe.**

# VIAMBATANISHO

## Kiambatisho Na. I: Hati za ukaguzi na mahitimisho ya uzingatiaji wa Sheria ya ununuzi na Kanuni zake na Sheria ya bajeti na Kanuni zake kwa mwaka wa fedha 2021/22

| Na | Jina | Hati ya ukaguzi hesabu za fedha | Hitimisho kuhusu Uzingatiaji wa Sheria ya ununuzi na Kanuni zake | Hitimisho kuhusu Uzingatiaji wa Sheria ya bajeti na Kanuni zake |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kampuni ya Ndege Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 2. | Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 3. | Chuo Kikuu Ardhi | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 4. | Jumuiya ya Wahitimu Chuo Kikuu Ardhi | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 5. | Kampuni ya Ushauri Elekezi wa Mazingira Jengekwa ya Chuo Kikuu Ardhi | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 6. | Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 7. | Chuo cha Ufundi Arusha | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 8. | Kampuni ya Ushauri Elekezi wa Uzalishaji Chuo cha Ufundi Arusha - Kikuletwa | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 26. | 2020/21 | Kutofikiwa kwa ujenzi wa laini ya ziada ya kusafirisha umeme kwa asilimia 75 ya kilomita 4,095 na uwezo mpya uliowekwa wa uzalishaji kwa asilimia 94 ya MW 3,428.78<br><br>Nilipendekeza Shirika la Umeme Tanzania liimarishe utaratibu wa upangaji na ufuatiliaji na kuharakisha utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha miradi yote inakamilika kwa wakati | Upangaji wa miradi ya Uzalishaji na Usafirishaji unaongozwa na Mpango Mkuu wa Mfumo wa Umeme (PSMP), ambao unatoa barabara ya uwekezaji ili kukidhi pengo la usambazaji na mahitaji. Serikali inafadhili miradi mikubwa kupitia fedha za bajeti na / au fedha kutoka kwa wa Wafadhili kupitia mikopo ya masharti nafuu. Ili kuziba pengo la rasilimali za mfuko kwa ajili ya utekelezaji wa mradi, Serikali kwa sasa inatathmini njia mbadala za kuhamasisha rasilimali kutekeleza kwa wakati miradi iliyotambuliwa kama vile dhamana za kampuni na mipango ya mfuko binafsi. | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Nitafanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi na ukusanyaji wa rasilimali | Katika hatua ya utekelezaji |
| 27. | 2020/21 | Kushindwa kufikia malengo | Serikali ipo na mpango wa kutekeleza miradi ya | Majibu ya Serikali yamepokelewa. | Katika hatua ya |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | yaliyopangwa ya kuboresha ufanisi wa mtandao na upanuzi kupitia kupeleka BTS 2,200<br><br>Nilipendekeza kuwa (a) Serikali kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iingize fedha za ziada za mtaji kwenye Shirika la Mawasiliano Tanzania ili kuwezesha upanuzi wa mtandao ambao utakwenda sambamba na ongezeko la wateja; na<br>(b) Shirika la Mawasiliano Tanzania linatoa kipaumbele kwa utekelezaji wa malengo ya kimkakati ambayo yana athari za moja kwa moja kwa uendelevu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania katika sekta ya mawasiliano nchini Tanzania | kimkakati ya maendeleo ya mtandao, ambayo italeta matokeo chanya na uendelevu wa biashara. Katika mwaka ujao wa bajeti wa 2022/23, Serikali kupitia Shirika la Mawasiliano Tanzania imepanga kuwekeza Shilingi bilioni 43.2 katika miradi hiyo ya maendeleo ambayo wigo wake utahusisha kupeleka mitandao ya **FTTH** katika maeneo ya Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar. | Nitafanya ufuatiliaji wa utekelezaji katika kaguzi zijazo | utekelezaji |
| 28. | 2020/21 | Kushindwa kurejesha fedha kiasi cha shilingi milioni 712 zilizopo katika akaunti za benki za nje ya nchi za Shirika la Bima la Taifa<br><br>Nilipendekeza Shirika la Bima la Taifa kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Mambo ya Nje, lifuatilie katika | Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania itafanya mipango ya kutathmini akaunti zilizotajwa hapo juu na kuchukua hatua stahiki ipasavyo. | Majibu ya Serikali yamepokelewa Nitaendelea kufuatilia utekelezaji kwenye kaguzi zijazo | Halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | benki husika ili kubadili watia saini au kuzifunga kama hazitumiki tena | | | |
| 29. | 2020/21 | Shaka ya umiliki wa amana za kudumu zenye thamani ya shilingi milioni 432 za Mamlaka ya Bandari Tanzania<br><br>Nilipendekeza Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania na Wizara ya Mambo ya Nje na ushirikiano wa Afrika Mashariki wahakikishe kuwa makubaliano na Benki yanapatikana kuhusu fedha husika ili fedha hizo zirejeshwe Tanzania bila kuchelewa zaidi. | Amana za kudumu tajwa zinatarajiwa kufikia ukomo tarehe 31 Mei 2022 na Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania imeanza kufanya utaratibu na Benki ya Deutsch kuhakikisha mtaji na riba iliyopatikana inawekwa kwenye akaunti ya Mamlaka ya Bandari Tanzania | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Hata hivyo mpaka kufikia Desemba 2022, fedha hizo zilikuwa bado hazijawekwa kwenye akaunti ya Mamlaka ya Bandari Tanzania | Halijatekelezwa |
| 30. | 2020/21 | Matumizi ya matengenezo ya ndege ya shilingi milioni 278.42 yanayoweza kuepukika.<br><br>Nilipendekeza Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ifanye tathmini kuhusu gharama ambazo ndege hii inatumia kisha ifanye maamuzi ya ama kuendelea kuitumia au kufanya utaratibu wa kuiondoa kwenye | Hivi sasa, Ndege CESSNA182P inatumika, hata hivyo Serikali iko katika mchakato wa kuchambua namna bora ya kuiondoa kwenye matumizi. | Majibu ya Serikali yamepokelewa Nitaendelea kufuatilia utekelezaji kwenye ukaguzi ujao. | Katika hatua za utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | matumizi pale itakapoona inafaa. | | | |
| 31. | 2020/21 | Mali zenye thamani ya shilingi bilioni 2.29 ambazo hazitumiki katika Mamlaka ya Bandari Tanzania<br><br>Nilipendekeza Mamlaka ya Bandari Tanzania iombe kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ili kukamilisha mchakato wa uuzaji wa mali hizo. | Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania imeomba kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ili kuziondoa katika vitabu vya hesabu na kuziuza, pia, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango kupitia barua yenye Kumb. Na.EG.110/474/23/146 ya tarehe 26 Agosti 2021. amemteua Mwenyekiti wa Bodi na wajumbe wa bodi ya ukaguzi wa mali zisizotumika<br><br>Timu iliyoteuliwa imekamilisha taarifa ya ukaguzi na mapema Julai 2022 itawasilisha ripoti hiyo kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango. | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Nimejiridhisha kuwa Serikali ipo kwenye hatua ya utekelezaji Nitaendelea kufuatilia utekelezaji huo kwenye ukaguzi ujao. | Katika hatua za utekelezaji |
| 32. | 2020/21 | Muundo usio wazi wa utawala baada ya mabadiliko ya mamlaka ya hifadhi ya eneo la ngorongoro kuwa taasisi ya kijeshi<br><br>Nilipendekeza kuwa Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro iwasiliane na Wizara ya Maliasili na Utalii ili kuharakisha kukamilika kwa muundo wa utawala kwa ajili ya kusimamia vyema shughuli za Mamlaka hiyo. | Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii iliunda kikosi kazi ambacho kilijumuisha wajumbe kutoka Mamlaka ya Hifadhi za Taifa, Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, Wakala wa Misitu Tanzania na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori kukagua Kanuni za Uhifadhi wa Pori la Akiba, 2021 ambazo zilitangazwa kwenye gazeti la serikali GN 589 ya tarehe 9 Julai 2021.<br><br>Kanuni zilizopitiwa zimewasilishwa mbele ya Kamati ya Sheria Tanzu (kamati ya | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Mchakato wa sasa wa kubadilisha muundo wa utawala nimeupitia hata hivyo nitaendelea kufuatilia utekelezaji katika kaguzi zinazofuata. | Katika hatua za utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | kudumu ya Bunge ya Sheria ndogo) kabla ya kuidhinishwa na Bunge. Wizara pia imekamilisha Maagizo ya Jumla ya Huduma za Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu. Maagizo haya yanatoa miongozo ya pamoja ya kufanya kazi za Huduma ya Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu chini ya muundo wa kijeshi. | | |
| 33. | 2020/21 | Mapungufu katika mradi wa ujenzi wa hoteli ya Burigi yenye hadhi ya nyota tatu wa thamani ya shilingi bilioni 11.04<br><br>Nilipendekeza Mamlaka ya Hifadhi za Taifa ihakikishe ina mikakati ya kuwezesha mradi kukamilika bila kuchelewa zaidi. | Thathmini ya athari za mazingira imeshafanyika ikiongozwa na wataalamu wa ndani wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa baada ya kuanza kwa mradi.<br><br>Ucheleweshaji wa kukamilika kwa mradi ulisababishwa na ukosefu wa fedha za kutosha ulioathiri Mamlaka kutokana na janga la UVIKO-19 | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Hata hivyo, naisisitiza Serikali kufanya jitihada zaidi katika kukamilisha hoteli ya hadhi ya nyota tatu ya Burigi Chato. | Katika hatua za utekelezaji |
| 34. | 2020/21 | Shirika la Umeme Tanzania kutotoza kodi ya thamani ya shilingi bilioni 17.40 kwenye posho za watumishi<br><br>Nilipendekeza Shirika la Umeme Tanzania lihakikishe kuwa posho zote wanazostahili kulipwa watumishi zinatozwa kodi husika kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, (kama ilivyorekebishwa Mwaka 2019). | Posho ambazo wakaguzi wa kodi walizirekebisha katika hesabu za mishahara hazitozwi kodi ya mapato kwa mujibu wa kifungu cha 7(3)(i) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, 2004.<br><br>Kwa mujibu wa kifungu cha 7(3)(k) cha Sheria hiyo kinatumika kwa Shirika la Umeme Tanzania kwa sababu kifungu kilichotajwa kinarekebisha kifungu cha 7(3)(i) cha sheria ya kodi ya mapato, 2004 kisomeke kama ifuatavyo" Katika kuhesabu faida ya mtu binafsi au faida kutokana na ajira tutatoa posho ya nyumba, posho ya usafiri, posho ya uwajibikaji, marupurupu | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Hata hivyo, Shirika la umeme Tanzania ni Taasisi ya Biashara ya Serikali ambayo inafanya kazi kwa kutumia bajeti yao wenyewe na serikali inashughulika tu na misaada ya miradi ya maendeleo na hivyo wanatakiwa kutoza kodi kwenye posho za watumishi | Halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | ya ziada, posho ya shida, posho ya muda wa ziada na posho ya heshima inayolipwa kwa mfanyakazi wa Serikali au taasisi yake ambaye bajeti yake inalipwa kikamilifu au kwa kiasi kikubwa nje ya ufadhili wa bajeti ya serikali"<br><br>Kifungu hicho kilithibitishwa kupitia muongozo Na.2 wa mwaka 2011/2012 uliotolewa Septemba 2011 na Wizara ya Fedha, muongozo huu unatoa msamaha kwa baadhi ya posho zilizotajwa hapo juu zinazolipwa kwa wafanyakazi wa Serikali ambao bajeti yao yote au kwa kiasi kikubwa inagharamiwa na Serikali kuu. Shirika la Umeme Tanzania ambalo linamilikiwa na serikali na hufanya kazi chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka1992. Hisa zake zote zinamilikiwa na Serikali ya Tanzania kupitia Msajili wa Hazina, ikiwa chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa Wizara ya Nishati.<br><br>Kwa kuzingatia ufafanuzi huo hapo juu, vifungu vya sheria na miongozo kutoka Wizara ya Fedha, ni wazi kuwa posho zilizotajwa zmesamehewa kodi. | | |
| 35. | 2020/21 | Kushuka kwa uwekezaji na utendaji usioridhisha wa maeneo maalumu ya uzalishaji wa bidhaa za mauzo ya nje | Mamlaka inachambua wawekezaji kupitia mipango yao ya biashara iliyowasilishwa, ambayo inaweza kukabiliwa na mabadiliko zaidi wakati wa utekelezaji. | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Nitaendelea kukagua utekelezaji katika ukaguzi ujao | Katika hatua za utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Nilipendekeza Mamlaka yenye Maeneo Maalumu ya Uzalishaji wa Bidhaa za Mauzo ya Nje kwa kushirikiana na mamlaka husika ihakikishe kuwa wafanyabiashara wenye leseni ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji wa Mauzo ya Nje wanauza bidhaa zao nje ya chini angalau kwa asilimia 80 ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. | Kwa mfano, kabla ya kurejea kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi wenza zilihesabika kama soko la nje, lakini kwa sasa zinahesabika kuwa soko la ndani.<br><br>Hali hii imeathiri sana malengo ya asilimia 80 ya mauzo ya nje. Mamlaka itapitie vigezo vyake ili kujumuisha nchi wenza katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama soko la nje. | | |
| 36. | 2020/21 | Matumizi duni na uvamizi wa maeneo teule ya viwanda na kanda za kiuchumi<br><br>Nilipendekeza kuwa (a) Mamlaka ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji wa Bidhaa za Mauzo ya Nje (EPZA) ichukue hatua zinazofaa ili kulinda eneo lililovamiwa la Ukanda Maalumu wa Kiuchumi Kurasini; na (b) Serikali itenge na kupeleka fedha za kutosha kuwezesha EPZA na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) linaendeleza maeneo ya kiuchumi na viwanda. | Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo imechukua hatua muhimu za kuendeleza na kulinda maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya maeneo maalum ya kiuchumi na kituo cha biashara dhidi ya kuingiliwa na wasshirika wengine.<br><br>Kwa sasa Mamlaka inajenga ukuta wa kulinda eneo hilo dhidi ya uvamizi. | Majibu ya Serikali yamepokelewa<br><br>Nitaendelea kufuatilia utekelezaji kwenye ukaguzi ujao. | Katika hatua za utekelezaji |
| 37. | 2020/21 | Kuchelewa kuanza kwa uzalishaji kwa viwanda vinavyomilikiwa na Mashirika ya Umma. | Serikali imepitia msimamo wake na kuweka kimkakati mradi huo chini ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania ili kuvutia Wawekezaji wengine kwa kuwa | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Hata hivyo, nilibaini kuwa | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (i)Kiwanda cha Bidhaa za Tiba cha Simiyu<br><br>Mifuko ya (PSSSF, WCF, NHIF na NSSF) zinaharakisha kuanza kwa uzalishaji wa viwanda vilivyoanzishwa/vilivyonunuliwa kwa ufuatiliaji wa haraka wa manunuzi ya mitambo na mashine, na Wizara ya Fedha na Mipango ifikirie kutoa kibali cha uendelezaji wa kiwanda kwa Kiwanda cha Simiyu Medical Product.<br><br>(ii)Kiwanda cha Chai cha Mponde<br>Januari 2016, Serikali ilikimilikisha kiwanda cha chai kilichobinafsishwa cha Mponde kilichopo Lushoto-Tanga kutoka Chama cha Wakulima wa Chai Samara (UTEGA) baada ya UTEGA kushindwa kuendesha kiwanda hicho. Nilipendekeza Mifuko (PSSSF, | mradi huo una mtaji mkubwa.<br><br>Utekelezaji wa Mradi wa Bidhaa za Tiba mkoani Simiyu unasubiri kibali cha Katibu Mkuu (Hazina). Hata hivyo, ili kupunguza gharama za uwekezaji, NHIF na WCF wanafikiria kuuingiza mradi huo katika Mradi wa Morogoro Canvas unaotekelezwa kwa pamoja na taasisi nyingine za Hifadhi ya Jamii nchini (PSSSF, NSSF, NHIF, ZSSF na WCF). Kufanikiwa kuunganishwa kwa mradi huo katika mradi wa Morogoro Canvas kungepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uwekezaji wa mradi huo kwani mashine nyingi zinazohitajika zimewekwa katika kiwanda cha Morogoro Canvas.<br><br>Manunuzi yamekamilika. Kazi za ukarabati zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika ifikapo Mei 2022 na uzalishaji kwa majaribio utaanza Juni 2022 na kiwanda kimepangwa kuanza uzalishaji kufikia Desemba 2022. | Kiwanda cha Bidhaa za Tiba cha Simiyu. Kiwanda hakijaanza uzalishaji<br><br>Kiwanda cha Chai cha Mponde. Niligundua kuwa uzalishaji tayari umeanza | |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | WCF, NHIF na NSSF) iharakishe kuanza kwa uzalishaji wa viwanda vilivyoanzishwa/vilivyonunua kwa haraka haraka manunuzi ya mitambo na mashine, na Wizara ya Fedha na Mipango ifikirie kutoa kibali cha uendelezaji wa kiwanda kwa Kiwanda cha Simiyu Medical Product. | | | |
| 38. | 2020/21 | Changamoto zinazokwamisha kuanza kwa kiwanda cha uzalishaji wa nguzo za saruji kinachomilikiwa na Shirika la Umeme Tanzania<br><br>(i) Kutotolewa kwa fedha za ujenzi wa kiwanda Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania liweke mikakati ya kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya ujenzi wa nguzo za zege.<br><br>(ii) Pendekezo la kuanzishwa kwa ubia na kampuni binafsi kwenye uzalishaji wa nguzo za zege<br><br>Nilipendekeza Shirika la Umeme Tanzania lihakikishe utaratibu wake na wazabuni hauathiri uendelezaji wa viwanda saba vya | Serikali imezingatia mapendekezo ya mkaguzi kwa ajili ya utekelezaji, na itatoa fedha kiwandani ipasavyo pale mtililiko wa fedha unaporuhusu.<br><br>Serikali imezingatia mapendekezo ya mkaguzi kwa ajili ya utekelezaji. | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Hata hivyo, Shirika la Umeme halijatoa mtaji wa kutosha kwa Kiwanda cha uzalishaji wa nguzo za Saruji (kiwanda kinachomilikiwa na Shirika la Umeme Tanzania) kuanzisha kiwanda chake cha kutengeneza nguzo za zege kulingana na lengo la awali la uanzishwaji huo ambao ungepunguza gharama za nguzo kwa Shirika la Umeme Tanzania ikiwa ni pamoja na muda wa ukomo ikilinganishwa na nguzo za mbao. | Halijatekelezwa |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | nguzo za zege vilivyopangwa kupitia Kampuni ya Uzalishaji wa Nguzo za Zege. | | | |
| 39. | 2020/21 | Uwekezaji katika hisa zisizoorodheshwa na mali zisizohamishika kwa kuvuka ukomo katika Shirika la Bima la Taifa.<br><br>Nilipendekeza Shirika la Bima la Taifa lihakikishe kuwa linazingatia ukomo wa uwekezaji kwenye hisa zisizoorodheshwa kwenye soko la hisa na mali zisizohamishika, na lichukue hatua zinazofaa ili kupunguza uwiano wa uwekezaji usiotakiwa katika hisa zisizoorodheshwa na mali zisizohamishika. | Serikali imechukua hatua kuhakikisha Shirika la Bima la Taifa haliwekezi katika makampuni yasiyosajiliwa katika soko la mitaji na milki kuu na kuzingatia uwekezaji ulio daraja la kwanza la uwekezaji mpaka uwiano wa makapumi ambayo hayasajiliwa na milki kuu utakaporatibiwa. | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Hata hivyo nilipitia taarifa za fedha za mwaka unaoishia 2021/22 na nilibaini kuwa uongozi ulichukua hatua ya kusitisha uwekezaji katika milki kuu na hivyo kufikia uwiano unaokubalika katika Bima wa asilimia 1.06 na asilimia 14.56 kwa hisa ambazo hazijaorodheshwa (chini au sawa na asilimia 5) na milki kuui (chini au sawa na asilimia 15) mtawalia.<br>Hata hivyo Bima ya Maisha uwiano bado upo juu kwa ailimia 14.19 na asilimia 40.75 kwa hisa ambazo hazijaorodheshwa(chini au sawana asilimia 5) na mali isiyohamishka (chini au saw na asilimia 30) kwa mtiririko huo. | Katika hatua ya utekelezaji |
| 40. | 2020/21 | Mapungufu katika uendelezaji wa mradi wa uwekezaji wa majengo - kawe<br><br>Nilipendekeza Shirika la Nyumba la Taifa lihusishe Serikali ili | Shirika la Nyumba Tanzania bado linaendelea na majadiliano na Al Ghurair kuhusu namna bora zaidi ya kuendeleza mradi wa Kawe kabla ya kukamilisha na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mapitio ya | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Nitaendelea kufuatilia utekelezaji katika ukaguzi ujao. | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kutafuta namna bora ya kutatua masuala ambayo yanachelewesha kukamilika kwa Mradi wa Kawe | makubaliano ya mwanahisa. | | |
| 41. | 2020/21 | Mapungufu katika usimamizi na mwenendo wa mikopo<br><br>(i) Kushindwa kupatikana kwa wateja waliokopa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 225.96 ya uliokuwa Mfuko Mdogo wa Fedha wa Umoja (UTT)<br><br>Nilipendekeza Mfuko wa SELF uimarishe utunzaji wa kumbukumbu za wakopaji na kuzidisha juhudi za urejeshaji wa mikopo.<br><br>(ii) Mfuko wa SELF kushindwa kuzingatia uwiano sahihi wa utoaji mikopo<br><br>Nilipendekeza Mfuko wa Huduma wa SELF uhakikishe unazingatia Sera ya Mikopo ya Mwaka 2019 na uwe unafanya mapitio ya mara kwa mara ili kurekebisha uwiano wa mikopo inayotolewa. | Mfuko unaendelea na jitihada zaidi za kuwatafuta wateja, hadi sasa shilingi milioni 33,049,827 zimekusanywa kutoka kwa wateja 19. Salio kwa sasa ni shilingi milioni 81,816,235.38. Menejimenti inaendelea kuhakikisha; salio lililobaki linakusanywa na katika siku zijazo wateja wa mkopo wa Mshahara huonesha anuani zao za mahali.<br><br>Serikali imehakikisha kuwa Taasisi ya Self Microfinance inafuatilia mchanganyiko wa aina ya mikopo ulioidhinishwa kila robo mwaka na kuhakikisha hatari zinadhibitiwa ili kuboresha utendaji wa Mfuko. | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Nitaendelea kufuatilia utekelezaji katika ukaguzi ujao kuhakiki urejeshaji salio lililobaki.<br><br>Majibu ya Serikali yamepokelewa Nitaendelea kufuatilia utekelezaji katika ukaguzi ujao. | Katika hatua ya utekelezaji |
| 42. | 2020/21 | Bodi ya Bima ya Amana haizingatii sera yake ya uwekezaji | Sera ya Uwekezaji iliyorekebishwa imeandaliwa ambayo inaruhusu mchanganyiko tofauti wa uwekezaji | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Nitaendelea kufuatilia | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Nilipendekeza Bodi ya Bima ya Amana izingatie sera yake ya uwekezaji kwa kuhakikisha kuwa uwekezaji wa juu zaidi katika dhamana za serikali za muda mrefu hauzidi asilimia 70 ya kiwango cha juu cha uwekezaji. | kuwa sawa na asilimia 100 badala ya asilimia 90 kutatua hitilafu ambayo ilibainishwa na Mkaguzi. Sera inasubiri kuidhinishwa kwa utekelezaji. | utekelezaji baada ya kuidhinishwa kwa sera | |
| 43. | 2020/21 | Upungufu wa ukwasi na uhimilivu wa Mfuko wa Hifadhi wa Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF)<br><br>(i)Kiwango cha chini cha uwezo wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma<br><br>Nilipendekeza kuwa Serikali ikamilishe malipo ya deni lote la shilingi trilioni 2.45 la michango ya Serikali ya kabla ya mwaka 1999 ili kuboresha uwezo wa Mfuko kuhusu uwiano wa mafao hadi kiwango kilichopendekezwa cha asilimia 40.<br><br>(ii)Gharama za mafao kuzidi mapato ya michango hivyo kuhatarisha uwezo wa mfuko kulipa mafao<br><br>Nilipendekeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa | Serikali imetoa hatifungani zisizo za fedha taslimu zenye thamani ya shilingi trilioni 2.176 mwezi Desemba 2021 ili kulipa deni la michango iliyofanyika kabla ya mwaka 1999 ambayo iliboresha kiwango cha Ufadhili.<br><br>Makubaliano yaliyoingiwa ni ya shilingi trilioni 4.5. Menejimenti itaendelea kushirikiana na Serikali kwenye salio la shilingi trilioni 2.4 ambalo usuluhishi unaendelea mara tu utakapokamilika utaimarika kwa kiasi kikubwa kiwango bora Fedha. | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Nitaendelea kufuatilia utekelezaji katika ukaguzi ujao. | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Umma (a) uandae mikakati itakayoongeza ukusanyaji wa mapato ya michango ikiwa pamoja, na (b) kushauriana na Serikali kuhusu namna ya kugharamia malipo ya mafao ya wastaafu wa kabla ya mwaka 1999. | | | |
| 44. | 2020/21 | Kutokuwepo kwa kanuni kwenye fao la utengemao katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)<br><br>Nilipendekeza Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi umshauri waziri mwenye dhamana aandae na aidhinishe kanuni za fao la utengemao kwa jamii. | Mfuko tayari umeandaa Mkakati wa Urekebishaji, ambao utatoa njia kwa ajili ya kutoa faida ya Ufundi na Ukarabati wa Kijamii. Mkakati huo unasubiri idhini ya Bodi na kupitishwa na Waziri. | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Nilijiridhisha kuwa mkakati wa urekebishaji wa fao la utengemano umeidhinishwa. Hata hivyo, nilibaini mkakati huo haujafanya kazi kikamilifu kwa kuwa manufaa ya madai hayo hayajatolewa kwa mujibu wa taarifa za fedha za mwaka 2021/22. | Katika hatua ya utekelezaji |
| 45. | 2020/21 | Kutokujulikana kwa mwenendo wa uendeshaji kwa waajiri wenye madeni ya michango ya muda mrefu kwenye Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)<br><br>Nilipendekeza Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), kwa kushirikiana na mamlaka zingine, ubaini kama waajiri ambao hawajalipa ada za michango kwa muda mrefu bado ofisi zao | Mfuko umekuwa ukifanya juhudi mbalimbali, mikakati na ufuatiliaji ili kujua hali ya uendeshaji na kukusanya michango kutoka kwa waajiri ambao hawajachangia kwa muda mrefu.<br><br>Mnamo Februari 2022, Mfuko ulifanya uchanganuzi wa takwimu za waajiri 8,489 ambao hawakuchangia ili kubaini hali yao ya utendakazi. Mchanganuo huo ulichambua taarifa kwa waajiri hao waliopatikana kutoka TRA, NSSF na BRELA. | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Nitaendelea kufuatilia utekelezaji wa hatua zinazofaa kuchukuliwa kwa waajiri ambao hawajachangia kwa muda mrefu. | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | zinafanya kazi au zimefungwa na uchukue hatua zinazofaa. | Matokeo ya uchanganuzi yalionesha kuwa waajiri 3772, sawa na asilimia 44.43, walibainishwa kuwa wanatuma michango hai na malipo ya SDL kwa NSSF na TRA. Zaidi ya hayo, waajiri 4,717, sawa na asilimia 55.57, hawakutuma michango wala malipo ya SDL kwa NSSF na TRA.<br><br>Mfuko umeanza kuwatafuta waajiri 3772 waliobainika kuwa hai ili kukusanya michango ambayo haijalipwa kutoka kwao kwa kutoa barua za matakwa. | | |
| 46. | 2020/21 | Uendeshaji wa shughuli za uchimbaji madini ndani ya hifadhi ya Saadani.<br><br>Nilipendekeza Mamlaka ya Hifadhi za Taifa ishirikiane na Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, na `mamlaka zingine za Serikali ili kutathmini athari za uchimbaji wa madini katika mfumo wa ikolojia wa Hifadhi ya Saadani na kuchukua hatua stahiki. | Menejimenti iliandika barua yenye Kumb. Na. AB. 213/222/01/10 ya tarehe 10 Mei, 2021 kwenda PS-MNRT ikiishauri Wizara kwa kushirikiana na wizara inayohusika na madini kupata msimamo wa Serikali kuhusu uendeshaji na umiliki wa Kampuni ya Seasalt. Ufuatiliaji unafanyika. Zaidi ya hayo, Menejimenti inawasiliana na NEMC ili kuhakikisha kuwa Kampuni ya Seasalt inatekeleza hatua za kukabiliana na athari za mazingira zinazotokana na shughuli za uchimbaji madini kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Nilithibitisha juhudi za Serikali kupitia mawasiliano kati ya MNRT na NEMC. Nitafatilia utekelezaji katika ukaguzi ujao. | Katika hatua ya utekelezaji |
| 47. | 2020/21 | Uwendeshwaji wa shughuli za kilimo cha miwa ndani ya hifadhi ya Saadani.<br><br>Nilipendekeza Serikali na Bodi ya Wadhamini ya Mamlaka ya | Serikali kupitia Menejimenti ya Hifadhi za Taifa ilifanya ufuatiliaji kwa MNRT na kubaini kuwa MNRT iliunda kikosi kazi mwaka 2019 ambacho kilishughulikia suala la migogoro inayohusiana na mipaka kati ya | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Nilithibitisha juhudi za Serikali. Nitaendelea kufuatilia utekelezaji katika ukaguzi ujao. | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Hifadhi za Taifa (TANAPA) kutathmini kwa kina athari za uendeshaji wa mashamba ya miwa ndani ya Hifadhi ya Saadani na kutafuta njia bora ya kukabiliana na hali hiyo, na matokeo ya tathmini hiyo yawe ni maejeo kwa matumizi ya baadae. | Hifadhi ya Taifa ya Saadani na jamii zinazopakana nayo ikiwemo Kampuni ya Sukari Bagamoyo. Kikosi kazi hicho kilipendekeza kuwepo kwa hali ya makubaliano ya pande mbili ambapo umbali wa mita 200 kati ya 500 kutoka ukingo wa mto Wami ubaki kwenye GN ya hifadhi hiyo na Serikali kusalimisha mita 300 ambayo ni sehemu ya Hifadhi ya Taifa ya Saadani ili kutatua mgogoro huo. | | |
| 48. | 2020/21 | Mbinu hafifu katika kupambana na milipuko ya moto hifadhini<br><br>Nilipendekeza Serikali, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) (a) itathmini athari za milipuko ya moto na irejeshe miundombinu na uoto wa asili katika maeneo yaliyoathiriwa na moto;<br>(b) itumie satelaiti katika kubaini matukio ya moto;<br>(c) ianzishe kikosi kazi cha kupambana na majanga ya asili; na<br>(d) itenge bajeti na inunue vifaa vya kisasa vya kuzima moto ikiwa pamoja na helikopta kwa ajili ya kukabiliana na milipuko ya moto, na ambayo itatumika kwa | Serikali ilitoa agizo la kupiga marufuku matumizi ya ukanda wa nusu maili. Menejimenti kwa kushirikiana na Kamati za Usalama za Wilaya kutoka Moshi, Rombo, Siha na Hai imekuwa ikitekeleza maagizo hayo. Pia, uongozi wa Hifadhi za Taifa unaendelea na jitihada za kutenga bajeti ya vifaa vya kisasa vya kuzimia moto. Doria na uokoaji zimeimarishwa. | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Katika mwaka huo niliikuta Serikali kupitia Hifadhi za Taifa ilitumia teknolojia mbalimbali za Satelite. Pia, nilithibitisha vifaa vya kuzima moto vilivyonunuliwa na kuwa kumetengwa kifungu cha bajeti katika Mwaka wa Fedha wa 2022/2023 kwa ajili ya kununua Helikopta. | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | shughuli za doria na uokoaji hifadhini. | | | |
| 49. | 2020/21 | Kuchelewa kwa utekelezaji wa mipango kuhusu upatikanaji wa maji ya uhakika kwa wanyamapori.<br><br>Nilipendekeza Serikali iunge mkono mpango huu wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na ilichukulie suala hili kama kipaumbele ili kuharakisha kukamilika kwa malengo yaliyokusudiwa katika Bonde la Mto Mara na Ghuba ya Speke katika Ziwa Viktoria. | Ufuatiliaji wa karibu uliofanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT) umebaini kuwa Serikali imeamua kulitenga eneo la udhibiti wa pori la akiba la Speke kuwa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Uamuzi huo wa Serikali uliwasilishwa kwa Mamlaka ya Mkoa wa Mara kupitia Kamati nane za kisekta za Wizara tarehe 9 Aprili, 2022. Mamlaka ya Mkoa wa Mara imeagizwa kutekeleza agizo hilo. | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Nitapitia utekelezaji na ukamilishaji wa shughuli zilizopangwa ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji kwenye Hifadhi. | Katika hatua ya utekelezaji |
| 50. | 2020/21 | Uhifadhi wa maeneo ya utalii umezidiwa na shughuli za kibinadamu za maendeleo ndani ya hifadhi.<br><br>Hivyo, Nilipendekeza kuwa Serikali<br>(a) itafute njia mbadala za maendeleo ya binadamu katika maeneo yanayopakana au kuingiliana na maeneo ya hifadhi ili kuboresha programu za uhifadhi kwa jamii ndani na nje ya maeneo ya utalii; na (<br>b) ibainishe mipaka yote ya hifadhi za | Mpango wa matumizi ya ardhi ulitengenezwa kwa vijiji 30 vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa ya Tarangire, lengo kubwa likiwa ni kupata korido, maeneo ya mtawanyiko na mtiririko wa Mto Tarangire. Menejimenti inashirikiana na wadau katika ngazi zote inaendelea kuhakikisha uanzishwaji wa Maeneo mengine ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) ili kuhifadhi na kulinda shoroba za wanyamapori na maeneo ya kutawanyika. | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Nitaendelea kufuatilia utekelezaji wa mikakati iliyowekwa. | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | taifa iliyoingiliwa na iwaondoe wavamizi. | | | |
| 51. | 2020/21 | Kutokuwapo mitambo ya utambuzi kwenye milango ya kuingilia watalii na uwepo wa kamera mbovu kwa masuala ya usalama katika Hifadhi za Taifa za Kilimanjaro.<br><br>Nilipendekeza Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro viweke vifaa vya usalama kama vile mitambo ya utambuzi pamoja na kamera za usalama zinazofanya kazi vizuri katika mageti. | Serikali kupitia Hifadhi za Taifa ilipanga kufunga Kamera za ufuatiliaji na skana kwa ajili ya usalama katika sehemu za kuingia na mageti. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti haikuweza kuupa kipaumbele mpango huu. Uongozi umeomba fedha kutoka kwa Mradi wa ERB (Wizara ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani) ili kuwezesha upataji na usakinishaji wa mifumo ya uchunguzi. Kamera za uchunguzi zinapewa kipaumbele kwa milango mipya ya itakayojengwa.<br><br>Menejimenti imetenga bajeti katika mwaka 2022/2023, ufungaji wa Kamera za Ufuatiliaji na ununuzi wa mtambo wa utambuzi kwa ajili ya usalama katika sehemu za kuingilia na lango. Mchakato wa ununuzi chini ya Mradi wa ERB unaendelea | Majibu ya Serikali yamepokelewa.<br><br>Nitaendelea kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya 2022/23 katika ukaguzi ujao. | Katika hatua ya utekelezaji |
| 52. | 2020/21 | Kutokuwapo kwa Miundombinu ya Majitaka<br><br>Nilipendekeza Serikali kupitia Wizara ya Maji itafute wafadhili au itumie vyanzo vya ndani ili kupata fedha za kuzisaidia mamlaka za maji safi na usafi wa mazingira kujenga mifumo ya majitaka. | Serikali imezingatia mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu na inakusanya fedha kutoka vyanzo vya ndani na wafadhili kama inavyoonyeshwa hapa chini.<br><br>Mamlaka ya Maji DODOMA: Serikali ya Korea Kusini yaunga mkono upanuzi wa mtandao wa majitaka wa Mamlaka ya Majisafi | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Katika mwaka huu nilibaini uboreshaji wa miundombinu ya usafi wa mazingira. Nitaendelea kufuatilia suala hilo katika ukaguzi unaofuata. | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | na Usafi wa Mazingira Dodoma.<br><br>Mamlaka ya Maji ARUSHA: Benki ya Maendeleo ya Afrika inasaidia Mradi Endelevu wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Jijini Arusha<br><br>Mamlakaya Maji BUKOBA: Tumemaliza usanifu na utayarishaji wa nyaraka za zabuni hata hivyo Mamlaka ya ina mabwawa ya kutupa tope kwa Manispaa ya Bukoba kwa ajili ya kutunza maji taka na tupo katika hatua ya manunuzi ya kujenga kituo kimoja Kyaka/Bunazi na Kayanga/Omurushaka. . | | |
| 53. | 2020/21 | Kukosekana kwa hatimiliki na kutowafikishia wakulima teknolojia za kilimo zilizotafitiwa na Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini<br><br>Nilipendekeza Serikali kupitia Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (a) ihakikishe inapata hatimiliki, hakimiliki au hataza kwa vumbuzi zilizofanywa; na (b) iendeleze na kufadhili mpango wa biashara unaosaidia uhamishaji wa teknolojia iliyoundwa kwa watumiaji ili | Kituo cha Zana za Kilimo Vijijini kinajitahidi kuhakikisha kuwa teknolojia iliyotengenezwa ina hakimiliki na hatua zinazofaa zinachukuliwa ili kupeleka teknolojia hiyo kwa umma. Ikumbukwe kwamba sio utafiti wote unaofanywa na Kituo unaoweza kupata Haki Miliki kwani baadhi ya teknolojia hupitishwa au kubadilishwa ili kuendana na hali za ndani, kwa hivyo, hakuna uvumbuzi unaoweza kumilikiwa. | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Nitapitia utekelezaji wa suala hilo katika ukaguzi unaofuata. | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kuwezesha watumiaji kutumia teknolojia husika. | | | |
| 54. | 2020/21 | Usimamizi duni wa ukusanyaji wa mikopo ya wanufaika wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu<br><br>Nilipendekeza Bodi ya Mikopo (a) iweke mikakati ya kuwatafuta wanufaika na waajiri; na (b) iishirikishe Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Balozi za Tanzania ng'ambo ili zisaidie kufuatilia na kurejesha mikopo kutoka kwa wanufaika wanaoishi nje ya Tanzania. | Serikali imezingatia mapendekezo;<br><br>(a) Kwa kuzingatia malengo ya mwaka 2020/21, Serikali inathibitisha kuwa malengo ya kufuatilia wanufaika wa mikopo mwaka 2020/21 yalikuwa 35,000. Idadi halisi ya walengwa waliofuatiliwa walikuwa 31,229 sawa na asilimia 89.2.<br>(b) Kushuka kwa kiwango cha kutekeleza matakwa ya mwajiri kulichangiwa na mchanganyiko wa mienendo ya janga la UVIKO -19 na michakato ya uhamiaji. Menejimenti itahakikisha kwamba miunganisho ya mfumo inaofanywa utaongeza kiwango cha waajiri wanatekeleza. | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2021/22, salio la mkopo ambalo halijafuatiliwa lilibaki shilingi bilioni 249.74 kama ilivyokuwa mwaka uliopita kutoka deni la awali la shilingi trilioni 1.46.<br>Nitaendelea kufuatilia utekelezaji katika ukaguzi ujao. | Katika hatua ya utekelezaji |
| 55. | 2020/21 | Idadi Ndogo ya Waratibu wenye sifa katika Taasisi ya Elimu Tanzania (TET)<br><br>Nilipendekeza Taasisi ya Elimu Tanzania na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuajiri waratibu wa fani husika kwa ajili ya kuandaa mitaala kwa masomo yanayohusika. | Serikali kupitia menejimenti ya Taasisi ya Elimu Tanzania imefanya baadhi ya mikakati ya kukabiliana na upungufu wa wafanyakazi, hadi tarehe 31 Machi, 2022 Taasisi iliweza kuajiri Mkuzaji Mtaala mmoja. Ufuatiliaji wa karibu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora unaendelea kwa lengo la kupunguza kiwango cha upungufu wa watumishi. | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Nitaendelea kufuatilia utekelezaji katika ukaguzi ujao. | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 56. | 2020/21 | Usimamizi duni wa fedha za maendeleo na ujuzi na Mfuko wa Elimu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania.<br><br>Nilipendekeza Mfuko wa Elimu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania na Serikali kutoa rasilimali za kutosha na kushirikisha Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania kwa ufuatiliaji na uhakiki kwa wakati wa miradi.<br><br>Ninapendekeza Mamlaka ya Elimu Tanzania na Ofisi ya Rais TAMISEMI waweke udhibiti utakaowezesha fedha zinazotolewa na Mamlaka ya Elimu Tanzania kupelekwa kwa watekelezaji wa miradi mara moja. | Serikali kupitia Menejimenti ya Mamlaka ya Elimu imetekeleza hatua zifuatazo;<br>(a) Ilifanya ziara za kimazingira kati ya Septemba na Novemba, 2021 kwa Taasisi zote 61 za Mafunzo zilizokuwa zinatekeleza Mpango wa Bursary.<br>(b) Kuajiri maafisa 4 wa Ufuatiliaji na Tathmini kupitia uhamisho. Maafisa hawa wanawajibika kwa shughuli za Usimamizi na Uangalizi wa Mfuko wa Elimu.<br><br>(c) Imenunua magari matatu (3) ya ziada ili kuwezesha shughuli za ufuatiliaji.<br><br>(d) Makubaliano kati ya Mamlaka ya Elimu na Mfuko wa Maendeleo ya jamii Tanzania (TASAF) yalitiwa saini tarehe 24 Novemba 2021 kwa ajili ya ushirikiano katika utekelezaji wa Mpango wa Bursary ikiwa ni pamoja na kutoa msaada katika ufuatiliaji wa shughuli. (e) Mashauriano na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) yamefanyika na fedha zilitolewa kwa miradi yote 24. Hadi tarehe 31 Machi, 2022, miradi 20 kati ya 24 imekamilika.<br><br>Hivi sasa, kuna vituo 48 vinavyomilikiwa na VETA Tanzania Bara. Juhudi zaidi zinaelekezwa katika ujenzi na uanzishaji wa Vituo vipya vya VETA ili kuongeza ufikiaji wa VETA huku ikifikia lengo | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Nitaendelea kufuatilia utekelezaji | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | la serikali la kuwa na angalau Kituo kimoja cha VETA katika kila wilaya.<br><br>Ujenzi wa vituo vinne (5) vya VETA vya Mikoa (Kagera, Rukwa, Geita, Njombe na Simiyu) upo katika hatua tofauti; wakati ujenzi wa vituo vya VETA vya Wilaya 25 nchini kote unatarajiwa kukamilika na kuanza mafunzo ifikapo tarehe 1 Julai, 2022. Kukamilika kwa vituo hivyo kunatarajiwa kuandikisha takribani vijana 15,000 katika medani ya mafunzo ya ufundi stadi. VETA kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itaendelea na ujenzi wa vituo vingine vya VETA nchi nzima katika kila mwaka wa fedha kulingana na upatikanaji wa fedha. | | |
| 57. | 2021/22 | Bei ya gesi ya asili isiyoweza kudhibitiwa na soko la ndani na bei ambayo haijafanyiwa mapitio kwa wauzaji wa maji.<br><br>Nilipendekeza kuwa Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji iangalie kwa kina na kwa wakati unaofaa amri za bei za maji ili kuruhusu Mamlaka za Usambazaji wa Maji kuwa na uwezo wa kujitegemea wakati wa kutoa huduma | Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji itahakikisha bei za soko la ndani za gesi asilia zinatolewa kama inavyotakiwa na sheria ili kulinda soko la ndani. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji itaangalia kwa kina na kwa wakati unaofaa amri za bei za maji ili kuruhusu Mamlaka za Usambazaji wa Maji kuwa na uwezo wa kujitegemea wakati wa kutoa huduma bora kwa wateja wao. | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Nimethibitisha juhudi za Serikali kupitia mawasiliano kati ya Wizara ya Nishati na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kuhusu mapitio ya dhana inayoelekeza bei za petroli, yaani "Sheria ya bei za Gesi Asilia za Petroli za 2020". Pia, nilibaini kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | bora kwa wateja wao. | | Nishati na Maji imefanya mapitio ya amri za bei kwa kuzingatia kesi kwa kesi, ambayo imepunguza idadi ya mamlaka za maji na usafi wa mazingira bila amri za bei hadi 42 kati ya 112. Hata hivyo,suala hilo limesubirishwa kutokana na kuwepo kwa amri ya kusitisha na ukosefu wa utaratibu wa kujulisha Mamlaka za maji juu ya hali ya bei za maji | |
| 58. | 2020/21 | Changamoto za kufanya zoezi la alama za mafuta na Mamlaka ya Viwango Tanzania (TBS).<br><br>Nilipendekeza kuwa Mamlaka ya Viwango Tanzania na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kupitia Wizara husika:<br><br>(a) kuidhinisha uhamisho wa jukumu hili na kuandaa makubaliano rasmi kati ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji na Shirika la Viwango Tanzania kwa kufafanua masharti ya utendaji; na | (a) Makubaliano yalifanywa wakati wa mkutano uliofanyika kuanzia tarehe 27-28 Januari, 2022 Dar es Salaam kati ya Wizara ya Nishati, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Idara ya Kuchambua na Kutunga Sheria za Bunge), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji na Shirika la Viwango Tanzania, kuwa rasimu ya marekebisho ya kanuni za Alama na Udhibiti wa Ubora wa Petroli GN.No.210 ya 2010 itawasilishwa kwa Shirika la Viwango Tanzania kwa maoni zaidi iwapo yatahitajika kabla ya kutunga mkataba wa utendaji. Shirika la viwango tanzania haikupokea rasimu ya marekebisho ya Sheria za Petroli kutoka Mamlaka ya | Majibu ya Serikali yamepokelewa. Naendelea kusisitiza Serikali kuharakisha kuidhinisha mapendekezo. Nitaendelea kufuatilia utekelezaji katika ukaguzi ujao. | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) kuhakikisha mfumo wa usimamizi unaofaa unatengenezwa ili kurahisisha mifumo ya uchunguzi kusambaza matokeo ya vipimo kwa njia ya moja kwa moja kwenye mifumo ya ufuatiliaji wa kati kwenye Mamlaka ya Viwango Tanzania na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji na Shirika la Viwango Tanzania.<br><br>Nilipendekeza kuwa Tume ya Ushindani wa Haki iongeze wafanyakazi katika kitengo cha kupambana na bidhaa bandia kwa kuongeza idadi ya wakaguzi na kuhakikisha kuwa kuna mzunguko wa wakaguzi katika maeneo ya kuingiza bidhaa. | Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji. Shirika la Viwango Tanzania iliuliza hali ya marekebisho hayo kupitia barua yenye kumbukumbu Na. CCA.222/417/01/19 iliyotumwa tarehe 2 Machi, 2022; hakuna majibu yaliyopokelewa kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji.<br>(b) Mfumo, ambao utapeleka matokeo ya vipimo kwa njia ya moja kwa moja kwenye Mfumo wa Ufuatiliaji wa Kati kwenye Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kutoka shirika la viwango tanzania, umepewa kipaumbele kwenye zabuni ya sasa ya muuzaji wa alama ya mafuta. Baada ya kumalizika kwa zabuni ya sasa mwezi Juni 2022, mfumo huo utawekwa na muuzaji mpya atakayeshinda zabuni.<br>(a) Idadi ya wafanyakazi katika Kitengo cha Kupambana na Bidhaa Bandia itaongezwa kulingana na mahitaji kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Utumishi.<br>(b) FCC imeanza kutekeleza Mzunguko wa Kazi ili kuongeza uzoefu wa wafanyakazi, kuwapa mafunzo kwa njia ya msalaba na kuboresha kuridhika kwao na kazi kuanzia Machi 2022.<br>(c) FCC imepata ofisi katika Mwanza na Arusha ili kuanzisha Ofisi mbili za Kanda ambazo zitakuwa na shughuli ifikapo Juni 2022. | | |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 59. | 2020/21 | Ufuatiliaji na uhuhishaji usioridhisha wa ubunifu wa umeme ulioanzishwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania.<br><br>Nilipendekeza kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi (a) iharakishe usanifu wa Sheria ya Usalama wa Barabarani ili kuhakikisha vijipandevya e-Stickers vinajumuishwa; (b) yazingatie marejesho yoyote kutoka kwa kampuni za bima baada ya tarehe 15 Mei 2021 kuwa batili na isiyo na maana na kuanzisha taratibu sahihi za kuandika vipande vya mwili wa vipande vya zamani; na (c) kwa siku za usoni, mabadiliko makubwa yoyote yanapaswa kusaidiwa na mpango wa kutambua faida. | Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Ofisi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi wameandaa rasimu ya kanuni chini ya Sheria ya Usalama Barabarani, Kifungu cha 168 kinachotambua bima ya elektroniki na matumizi ya TIRAMIS kama ushahidi wa bima ya gari. | Majibu ya serikali yamepokelewa. Nilibaini kuwa kwa sasa stika za bima hazitumiki tena. | Limepitwa na wakati |
| 60. | 2020/21 | Mapungufu yaliyobainishwa katika utoaji wa msamaha kwa wagonjwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI).<br><br>Nilipendekeza kuwa | Taasisi hiyo imetoa msamaha kwa Watanzania kulingana na Sera ya Afya ya Taifa ya 2017. Hata hivyo, kutokana na aina ya wagonjwa wanaohudumiwa katika taasisi ya tiba ya mifupa muhimbili, isipokuwa kwa wagonjwa wa hiari, taasisi ya tiba ya mifupa muhimbili pia | Majibu ya serikali yamepokelewa. Mwaka huu nimehakiki huduma ya juu zaidi ya kitaalamu na mapitio ya Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu(SOP) kuhusu usamehevu | Katika hatua ya utekelezaji |

| Na | Mwaka | Mapendekezo ya Ukaguzi | Jibu la Serikali | Maoni ya Mkaguzi | Hali ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (a) Hospitali ya Taifa Muhimbili na taasisi ya tiba ya mifupa muhimbili kuhakikisha msamaha unatolewa kwa wagonjwa wanaostahili tu na wawe na uthibitisho wa kutosha kwa kushirikisha kitengo cha ustawi katika mchakato huo; na<br>(b) Hospitali ya Taifa Muhimbili kushirikiana na Wizara ya Afya kuhusu uwezekano wa kusaidia gharama za wagonjwa wanaopata msamaha na kuhakikisha mchakato wa msamaha unafanywa kwa njia ya kielektroniki. | hushughulikia dharura ambazo zinahitaji utaratibu wa haraka wa kuuokoa maisha, hivyo hakuna wakati wa kupata nyaraka zinazohitajika za msamaha. Baadhi ya wagonjwa ni wasiojulikana, wengine hawana jamaa kabisa lakini huduma lazima zitolewe. | utafanyika katika ukaguzi ujao wa 2022/23. | |
| 61. | 2020/21 | Uzalishaji na udhibiti hafifu wa mbegu/miche bora kwa kuongeza uzalishaji wa mazao.<br><br>Nilipendekeza kuwa Bodi za usimamizi kwa kushirikiana na taasisi za utafiti, zihakikishe kuwa juhudi za kuzalisha mbegu/miche bora zinahamasishwa na kufuatiliwa kwa karibu. | Kuanzia msimu ujao wa 2021/22 serikali itaanzisha mfuko wa maendeleo ya mazao utakaotumika kufadhili shughuli mbalimbali za maendeleo ya kahawa ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa miche. Kuwepo kwa fedha za kutosha, uwezo wa taasisi za utafiti wa kilimo utaongezwa ili kuzalisha mbegu za kahawa na vifaa vingine vya kupandikizia. Hivyo idadi ya miche itakayozalishwa kila mwaka itaongezeka. | Majibu ya serikali yamepokelewa. Nilibaini kwa mwaka 2021/22 uzalishaji ulikuwa Tani 49,962.35 (asilimia 26.68) kati ya mahitaji ya jumla ya tani 187,197 kwa mwaka. Nitaendelea kufuatilia utekelezaji zaidi katika ukaguzi ujao. | Katika hatua ya utekelezaji |
